
Mwongozo wa Tano

# Mafunzo Ya Omega

## *Mafunzo ya Vitendo Kwa wapanda Kanisa*



*Na Muungano wa Kueneza Upandaji kanisa Wakishirikiana na Huduma ya Peter Dayneka wa Urusi*

**Kozi ya Omega:**
**Mafunzo ya Vitendo Kwa Wapanda kanisa**
**Mwongozo wa Tano**

Tafsiri ya asili ilichapishwa na
The Bible League, P.O. Box 28000, Chicago, IL 60625 USA
Tel: (800) 334-7017 E-mail: info@BibleLeague.org www.bibleleague.org

Copyright © 2000,2006 United World Mission.
Machapishwo haya kwa asili yalinukuliwa na *The Alliance for saturation Church Planting* na yaliandaliwa na ushirika huo kwa kushirikiana na huduma ya Peter Deyneka wa Urusi, mradi 250.

Unaruhusiwa na Unashauriwa kuzalisha na kusambaza zana hii katika mfumo wowote endapo kama:
(1) Unampa sifa mwandishi, (2) unaonyesha kama marekebisho yamefanyika, (3) Hulipishi zaidi ya gharama ya kuzalishia tena, na (4) hutengenezi kopi zaidi ya 1000.
Kama utapenda kuweka nakala za nyenzo hii kwenye internet au kama matarajio yako ya matumizi ni tofauti na vichwa vya habari hapo juu tafadhali wasiliana na
United World Mission: Jay Weaver/Omega, 9401-B Southern Pines Blvd.
Charlotte, NC 28273-5596, or omega_course@alliancescp.org

Kutafsiri na kurithi katika lugha yako pia kunashauriwa. Tena, tafadhali wasiliana na omega_course@alliancescp.org ili kwamba tuweze kutia moyo na kuwajulisha wengine wanaoweza pia kuwa wamevutiwa katika lugha yako au matumizi yaliyokusudiwa.

Kwa taarifa zaidi juu ya huduma zao za kuheshimika, tafadhali wasiliana na :

THE ALLIANCE
FOR SATURATION CHURCH PLANTING

(tovoti/rasilimali zinapatikana ila kwa sasa ushirikiano huo haupo tena)
http://www.alliancescp.org/resources/interchanges/2005_aug.html

Peter Deyneka
Russian Ministries

P.O. Box 496
Wheaton, IL , USA 60189
Tel: (630) 462-1739 Fax: (630) 690-2976
info@russian-ministries.org
www.russian-ministries.org

Kwa asili yalipigwa chapa au yalichapishwa katika nchi ya Marekani (USA).

# SHUKURANI

Tunatoa shukurani zetu kwa moyo wa dhati na za pekee kwa wote waliochangia katika matayarisho ya miongozo hii ya mafunzo. Wafuatao ni watu waliojitoa sana kwa kiwango kikubwa kwenye hatua ya kuandika na kutengeneza miongozo hii. Bwana, panda kanisa lako…mpaka miisho ya dunia.

Jay Weaver, Mtengenezaji, Timu ya Ulimwengu

| | |
|---|---|
| Richard Beckham | *Greater Europe Mission* |
| David & Lisa Bromlow | *Christ For Russia* |
| Ron Brunson | *World Witness and United World Mission* |
| Don Crane | *Greater Europe Mission* |
| Bea Crane | *Greater Europe Mission* |
| Hunter Dockery | *World Harvest Mission* |
| Mike Elwood | *Greater Europe Mission* |
| Jeff Geske | *United World Mission* |
| Dave Henderson | *C B International —Project 250 of Peter Deyneka Russian Ministries* |
| Bob Mackey | *United World Mission* |
| Bob Martin | *United World Mission* |
| Paul Michaels | *Grace Brethren Intl. Mission* |
| Norie Roeder | *United World Mission* |
| Ki Sanders | *World Team* |
| Larry Sallee | *UFM International —Project 250 of Peter Deyneka Russian Ministries* |
| Eric Villanueva | *United World Mission* |
| David Westrum | *Interlink Ministries —Project 250 of Peter Deyneka Russian Ministries* |

**SHUKRANI ZA PEKEE KWA AJILI YA MSAADA WAO WA KIUONGOZI NA UTALAAM**

| | |
|---|---|
| Edith Bond | *The Alliance Regional Resource Team* |
| David Gál | *The Alliance Regional Resource Team* |
| Nell Harden | *Retired English Professor* |

# MWONGOZO WA TANO

## Yaliyomo

**DIBAJI** .......... **7**

**KUHUSU MUUNGANO** .......... **9**

**MZUNGUKO WA UPANDAJI KANISA** .......... **10**

**MTAALA** .......... **11**

**MTAZAMO WA UTARATIBU** .......... **13**

**MAONO YA KUM** .......... **19**

**SOMO 13: Maono na Kumlika kwa darubini** .......... **20**

I. Tafsiri ya maono na Kumlika kwa Darubini .......... 20
II. Kuangalia kwa maono ya mavuno ya Mungu .......... 21
III. Kumlika kwa darubini kwa Mavuno Ya Mungu .......... 21
IV. Nguvu za Kiroho na Mamlaka .......... 24

**SOMO 14: Kuhamasisha** .......... **26**

I. Kuhamasisha ni Nini: .......... 26
II. Kwa nini Waumini wahamasishwe? .......... 27
III. Mifano ya Kibiblia ya Wahamasishaji .......... 27
IV. Tabia za Wahamasishaji wafanisi .......... 28
V. Mifano ya Uhamasishaji .......... 29

**SOMO 15: HATUA ZINAZOFATA** .......... **33**

I. Mzunguko wa Upandaji Kanisa .......... 33
II. Wajibu wa Kanisa Mpya: Kuzidisha—Upandaji makanisa—Binti .......... 34
III. Wajibu ya Timu ya Mwanzo yaUpandaji Kanisa: Kuanza Upya—Upandaji Makanisa Mapya .......... 36

**KANISA** .......... **41**

**SOMO 15: Malezi ya Kanisa** .......... **42**

I. Kanuni za Kibiblia za malezi ya Kanisa .......... 43
II. Michanganuo .......... 44

**SOMO 16: Ibada ya Umoja katika kanisa la Mtaa** .......... **46**

I. Kazi ya Ibada .......... 47
II. Jinsi ya Kuonyesha Mifumo Inayofaa ya Ibada .......... 50
III. Ibada ya Umoja na Upandaji Kanisa .......... 50

**SOMO 17: Jinsi ya Kuongoza Ibada ya Pamoja** .......... **52**

I. Wajibu wa Kiongozi wa Ibada .......... 52
II. Sifa za Kiongozi wa Ibada .......... 53
III. Mipaka katika Kuongoza Ibada .......... 54
IV. Zoezi katika Upangaji Huduma ya Ibada .......... 56

**SOMO 18: Kanisa la Mtaa na Mwili Mkubwa wa Kristo ........ 59**

I. Kadhia ya Kushirikiana........ 59
II. Viwango Vya Kujitoa Kwenye Ushirikiano........ 61
III. Sifa Kumi za Ushirikiano Wenye Ufanisi........ 62

**TABIA YA KIROHO ........ 65**

**SOMO 14: Huduma ya Upatanisho ........ 66**

I. Mawazo ya Mwanzo Kuhusu Utatuzi wa Migongono........ 67
II. Utatuzi wa Migogoro ni Swala la Injili ........ 68
III. Mafundisho ya Agano Jipya Juu ya Utatuzi wa Migogoro........ 68
IV. Kuwapenda Wengine ........ 70
V. Msaada wa Kivitendo kwenye Utatuzi wa Migogoro........ 70

**SOMO 15: Unyoofu wa Maadili ya Wapanda Kanisa ........ 72**

I. Matatu ya Kawaida; Pesa, Ngono, Uwezo ........ 73
II. Kanuni za Jumla Kwenye Unyoofu wa Maadili ........ 75
III. Faida za Unyoofu wa Maadili ........ 76
IV. Unyoofu wa Maadili Unaweza Kuwa wa Gharama........ 77

**MAOMBI ........ 79**

**SOMO 10: Maombi ya Kuwezesha kwa Harakati za Upandaaji Kanisa........ 80**

I. Utafiti (Kuchora ramani za Kiroho) ........ 81
II. Kutupa Maono—Ni Nini Mungu Anataka Katika Sehemu Hii?........ 81
III. Funza na Andaa Wa Kuomba Kwa Ajili ya Kueneza Upandaji Kanisa ........ 82
IV. Kutafuta na Kutandaza Viongozi Waombaji ........ 83

**SOMO 11,12: Kongamano la Maombi........ 86**

I. Mshukuru Mungu Kuwa Mungu Mwaminifu........ 86
II. Rejea Baraka za Bwana Zilizopita........ 86
III. Omba kwa Ajili ya Kazi Inayoendelea ya Upandaji Kanisa........ 87
IV. Sherekea Wema wa Bwana kwa wimbo na Kuabudu ........ 87

**UONGOZI ........ 89**

**SOMO 11: Utoaji Viongozi........ 90**

I. Wapanda Kanisa Lazima Watoe Wengine Kwenye Huduma ........ 90
II. Matatizo ya Kutoa ........ 92
III. Kanuni za Kutoa........ 93
IV. Kutunza Mawasiliano na Hao Uliowatoa ........ 95

**SOMO 12: Uongozi wa Harakati........ 96**

***Ziada: Viongozi wa Harakati........ 98***

**VIKUNDI KIINI ........ 101**

**SOMO 12: Viini Vinavyoenea Kupitia Makanisa ya Mtaa........ 102**

I. Tathimini ........ 103
II. Upangaji na Uwekaji........ 104

**SOMO 13: Usimamizi wa Viini ........ 107**

I. Usimamizi wa Vikundi Kiini........ 108
II. Muundo ya Kiusimamizi kwa Vielezo Tofauti vya Huduma ya Vikundi Kiini........ 111
III. Matumzi kwenye Huduma Yako ya Kikundi Kiini ........ 113
***Ziada: Vikundi Kiini: Hatua ya Mwisho ........ 115***

**KUHUBIRI ........119**

**SOMO 1: Kuhubiri Kibiblia I ........ 120**

I. Kujifunza kwa Kufata Neno—Kianzio Imara ........ 121
II. Wazo Kuu la Ujumbe........ 121
III. Muundo wa Ujumbe ........ 123
IV. Aina za Ujumbe........ 125

**SOMO 2: Kuhubiri Kibiblia II ........ 127**

I. Mahubiri ya Agano Jipya ........ 127
II. Kukusudia kwa Watazamaji Wako Unaolenga ........ 129
III. Kusaida wasikilizaji Kugundua ........ 130

**SOMO 3: Kuhubiri Kibiblia III ........ 132**

I. Maswala ya Kiroho........ 132
II. Maswala ya Kihisia........ 134
III. Maswala ya Kimwili ........ 135

**FAMILIA ........ 139**

**SOMO 3: Huduma kwenye Familia ........ 140**

I. Mutiririko Namba Moja—Igor Na Luba ........ 141
II. Mutiririko Namba Mbili—Andrea Na Tibor ........ 142
III. Mutiririko Namba Tatu—Nicu Na Familia Yake ........ 143
IV. Mutiririko Namba Nne—Anicka And Mirek ........ 144
V. Mutiririko Namba Tano—Renata Na Familia Yake ........ 144

# DIBAJI

## KUSUDI LA NYENZO HII

Wapanda kanisa mara nyingi wanafunzwa na kupelekwa nje wakiwa na mafunzo kidogo au bila mafunzo kwa ajili ya kazi iliyo mbele yao. Viongozi wa kanisa ambao wamezidiwa na matatizo ya huduma mara nyingi wanakosa maono wazi ya kile Mungu anachotaka kukamilisha kupitia wao. Wote wapanda kanisa na viongozi wa kanisa wanahitaji mafunzo na maono, lakini shule za Biblia na seminari siyo uchaguzi unaofahamika kwa wengi.

Nyenzo hii imeandaliwa siyo kutoa maono tu kwa wapanda kanisa na viongozi wa kanisa, lakini pia msingi wa kibiblia na ujuzi wa vitendo wa huduma ili kuona maono hayo yanakuwa kitu halisi. Siyo kielimisho cha “maazimio.” Badala yake, inatoa misingi muhimu ya kibiblia na kielimu, vilevile na ujuzi wa vitendo wa huduma, unaohitajika kwa upandaji kanisa. Ingawa kozi ya Omega iliandaliwa kwa ajili ya Ulaya ya mashariki na Kati na Muungano wa Urusi ya zamani, tumetiwa moyo na taarifa ambazo zimeshapatikana kuwa za msaada zinaporithiwa katika mandhali zingine.

Kozi yote hii imeandaliwa kukamilisha malengo mawili:

1. Kutoa mafunzo muhimu kwa makanisa kuweza kupandwa.
2. Kutia moyo uhamasishaji katika mwili mzima wa Kristo kuelekea harakati za upandaji kanisa.

Leo tunaona harakati za upandaji kanisa zikitokea katika nchi nyingi ulimwenguni kote, ikiwemo, Brazil, Roma, Ufilipino, Nigeria, na kwingine. Tunaamini kwamba kanisa la mtaa ni chombo cha msingi cha kuinjilisha ulimwengu, na kwamba upandaji wa kanisa unaotokana na kanuni ya kuongezeka mara dufu ni njia yenye mafanikio zaidi ya kutumia kuelekea kwenye kukamilisha utume mkuu. Makanisa mapya lazima yapandwe kwa maono ya kuongezeka mara dufu na uwezo wa kupanda makanisa mengine mapya. Hili linapotokea, kuna uwezekano wa harakati za makanisa zinazoweza kupangusa kuzunguka taifa na kubadilisha maisha ya watu katika nchi yote.

Harakati za upandaji kanisa zinahitaji watu waliohusika katika ngazi zote za kazi ya upandaji kanisa, kutokea kwa waumini wachanga walio na shauku ya imani yao mpya, hadi kwa viongozi wa madhehebu. Wapanda kanisa peke yao hawawezi kuwa kiungo cha harakati za upandaji kanisa. Nyenzo hii inafaa na ina manufaa makubwa katika ngazi zote za wafanya kazi wa kanisa na viongozi wa kanisa ambao wanaweza kuunga mkono juhudi za wapanda kanisa moja kwa moja au kwa namna nyingine wanapokuwa wanajitahidi kutimiza huduma aliyowaitia Bwana.

## MTAZAMO WA TARATIBU

Mwomngozo huu ni moja ya miongozo mitano, ambayo kila mmoja una wastani wa masomo 26 ya saa moja. Ili kukamilisha malengo yaliyoelezewa hapo juu, kozi yote inatosheleza mapana mbalimbali ya masomo ambayo ni muhimu kwa kazi ya upandaji kanisa. Haya ni pamoja na maono ya KUM, huduma ya kikundi kiini, ufuasishaji, kanisa, uinjilisti, mafunzo ya Biblia kwa kufata neno, uongozi, maombi, tabia ya kiroho na mengine mengi.

Taratibu ziligawanywa katika miongozo mitano ili kutoa njia inayozidi kupanuka kwenye kozi ya mafunzo. Wakati kila mshiriki anapomaliza mwongozo, anatumia mda kabla ya mwongozo unaofuata akiziweka katika matendo kanuni alizojifunza. Kwa hiyo vipindi vingi vya baadaye vinajengwa juu ya kanuni na ujuzi uliojifunzwa na kufanyiwa mazoezi katika masomo ya mwanzoni.

Kwa maneno mengine, taratibu zimeandaliwa kujifunzwa na kutumiwa sambamba na upandaji halisi wa makanisa. Washiriki wanapofanya kazi kwa juhudi kwa ajili ya kuanzisha kanisa jipya, watahitaji kiwango fulani cha ujuzi na ufahamu, na watakutana na matatizo mbalimbali wanapoendelea. Ujuzi na ufahamu unaohitajika mwanzoni mwa upandji kanisa unatolewa katika mwongozo wa kwanza, wakati shughuli na kanuni zinazohitajika baadaye katika upandaji kanisa zinatolewa katika miongozo ya mbeleni. Kila mwongozo umeandaliwa kutoa ujuzi, kujibu maswali, na kujadili matatizo nyeti ambayao yanahusiana na hatua sambamba ya upandaji kanisa ambapo washiriki wanafanya kwa juhudi. Baada ya dibaji hii utaona orodha ya shughuli muhimu za maendeleo au “mapito**”** ambayo wafunzwa wameandaliwa na kutarajiwa kuutumia wakati wa mafunzo ya semina.

Masomo yamegawanywa kwa mada, na kila moja ya miongozo mitano ina masomo kutoka baadhi ya mada. Baadhi ya visa, kama vile “maono” na “kanisa” yote yamo katika miongozo yote mitano. Mengine, kama vile “kufuasa” kunatokea baadaye kwenye kozi, wakati mshiriki anapokuwa kwenye

hatua katika huduma yake ambapo visa hivi ni muhimu. Mtazamo wa kozi yote ulio na orodha ya mada ya somo kwa kila moja ya miongozo mitano imehusishwa baadaye katika hatua hii.

**UTUMIAJI WA NYENZO**

**Ushauri Kwa Washiriki**

Mda wa kutosha, maombi na juhudi yamewezesha utayarishaji wa miongozo yote hii mitano katika kozi yote. Kila mwongozo umeandaliwa kugusia ujuzi maalumu wa huduma na ufahamu unaohitajika wakati wa utaratibu wa kuanzisha kanisa jipya. Kwa hiyo inashauriwa kabisa kwamba unaanza na mwongozo wa kwanza, siyo mwongozo mmojawapo wa baadaye. Kwa heshima hiyohiyo, kila somo limechaguliwa kwa uangalifu na kufanyiwa ufundi ili lifae, kutumika na la lazima katika kazi ya upandaji kanisa. Ni kwa manufaa yako pia kutovuka somo.

Tambua kuwa kusoma halisi kunatokea unapoyatumia mawazo yaliyotolewa katika masaomo haya katika maisha yako binafsi na katika huduma yako. Masomo mengi yana utekelezaji wa azimio mwishoni. Utekelezaji huu wa azimio umeandaliwa kukusaidia wewe kutumia mawazo katika somo na unatakiwa umalizike kabla hujaanza kufanyia kazi mwongozo unaofata. Inaweza kuwa msaada wa hali ya juu kuwa na mshauri wa kukutia moyo na kukushauri unapofanya mwenyewe upandaji kanisa. Mshauri pia anaweza kusaidia hitaji lako la uwajibikaji unapokuwa unayatumia mawzo yaliyojifunzwa katika maisha yako na huduma. Kuwa na mtu anayekuwa nawe bega kwa bega siyo tu maandalizi ua ufanisi, lakini wapanda kanisa wengi wanashuhudia msaada ambao hili linatoa katika maisha yao na katika huduma yao. Kwa hiyo, tunakutia moyo kabisa kwa maombi kutafuta aina fulani ya ushauri kuwezesha na kudumisha huduma yako ya upandaji kanisa.

**Ushauri kwa Wakufunzi**

Nyenzo hii inaweza kutumika kwa aina mbalimbali ya maandalizi kama vile shule ya Biblia, semimari au semina ya kikanisa. Kwa jinsi hiyo hii siyo tu kama nyenzo ya kuanzia ya kuelimishia. Ni nyenzo ya kufundishia. Elimu inayokazia katika ufahamu na habari.Kusudi la nyenzo siyo tu kukuwezesha kupata ujuzi, lakini pia ni kuchochea kuelekea kufikia kuweka huduma inayofanana na ya kibiblia. Mwongozo huu ni kwa ajili ya 'watendaji'.

Ingawa njia unayochagua kufundishia masomo kwa kila mwongozo itategemeana na mandhali yako, kila mwongozo unaweza kufundishwa katika semina ya wiki nzima. Kutokana na maelekezo haya, vituo mbalimbali vya mafunzo vimefanikiwa kwa kutumia mpangilio tofauti unaoendana na mtiririko wa maisha na huduma zilizopo. Wakati mwingine wamechagua siku mbili mfululizo za mapumziko ama vipindi vya kila wiki. Inashauriwa kwamba utekelezaji wa azimio mwishoni mwa kila somo usisitizwe ili kwamba uwe umemalizika kabula ya semina nyingine. Kipindi cha kati ya miezi minne hadi sita ni kipindi kinachofaa kujatarajia kati ya semina na semina. Faida ya njia hii ya ufundishaji ni kwamba inaunganisha kanunu ulizojifunza kwenye semina na ushiriki kwenye semina.

Wakati wa semina siyo lazima kufundisha kila kiini kilichopo kwenye mwongozo kwa sababu washiriki wanaweza kusoma nyenzo wenyewe. Wakati mwingine kufanya wafunzwa kusoma soma na kujadiliana jinsi linavyogusa uzoefu wao ni njia nzuri. Na wakati mwingine, maelezo kutoka kwa mtu ambaye ana uzoefu wa somo lililomalizika inaweza kuwa njia nzuri ya kujenge mawazo. LAKINI USIKALIE NJIA YA MAELEZO. Uwe mbunifu wakati ukijaribu njia mablimbali kujenga kanuni na ujuzi uliomo kwenye masomo. Wakufunzi wengine wamepata mchanganyiko kama vile kujadiliana kwenye makundi, karakana, na inaonekana kufanya kazi na kuwafurahisha.

Umetengwa kwa kutumainiwa, Mungu wa makanisa anahitaji mataifa yafuasishwe, na viongozi wanahitajika.

Una uwezo wa ajabu kusaidia kuandaa wengi watakaoendeleza harakati za upandaji kanisa na kuwezesha wengine katika huduma za kuzaliana kwa kanisa

**Msaada Zaidi**

Usisite kuwasiliana nasi kama tunaweza kuwa msaada zaidi kwako katika kueneza maono ya kueneza upandaji kanisa au kwa vitendo kuandaa wapanda kanisa.

Jay Weaver, General Editor
Budapest, Hungary, January 2000
JayWeaver@compuserve.com

# KUHUSU MUUNGANO

Taratibu hii imetayarishwa na *Muungano wa Kueneza Upandaji Kanisa* wakishirikiana na huduma ya Peter Deyneka wa Urusi, mradi 250. *Muungano* ni ushirikiano wa makanisa na mawakala wa umishenari waliojitoa kuwahamasisha waumini kuenea katka kila nchi zilizopo kati na mashariki ya Ulaya na ushirika wa makanisa ya kiinjili ya Urusi ya zamani. Kueneza upandaji kanisa ni mbinu ambayo inakusudia kuanzisha makanisa katika kila mji, vijiji, na maeneo unayopakana nayo ili kwamba kila atakayemwamini Yesu apate kuwa na kanisa jirani atakaloweza kushiriki na kukua ndani ya Yesu na kujengwa au kuandaliwa kwa huduma. *Muungano* umejengwa juu ya msingi ambao kuunganisha nguvu kutaongeza ufanisi, kupunguza marudio na kuonyesha umoja kati kati ya mwili wa Kristo.

### TUNACHOAMINI

- Kanisa la mtaa ni zana ya msingi ya Mungu anayoitumia kueneza injili na ufuasishaji
- Ushirikiano na makanisa pamoja na mashirika ya kimishenari ni madhubuti kwa ongezeko la makanisa ya mtaa na maendeleo ya harakati za kueneza upandaji kanisa.
- Kuelimisha viongozi ni mhimu kwa upandaji kanisa na ukuuaji wa kanisa.
- Maagano ya Lausanne ni maelezo ya imani ya Muungano (Alliance)

### TUNACHOFANYA

**Kuelimisha na Kushauri Wapanda Kanisa**

*Muungano* unatoa ujuzi unaotokana na mafundisho katika mtindo wa semina pamoja na mazoezi ya huduma yanayolenga kwenye kuanzisha makanisa yanayozaliana.

**Ukusanyaji Bayana wa Taarifa.**

Taarifa makini zinapelekea uamuzi mzuri katika kazi za upandaji kanisa. *Muungano* unaweza kuhusika katika kufundisha na kushauri katika hitaji la kukusanya taarifa zinazohitajika katika eneo la upandaji kanisa na kukua kwa kanisa.

**Harakati za Kuhusisha Maombi**

Harakati za upandaji kanisa zinaanza na maono, ambayo yanagunduliwa na kuandaliwa kwa kutafuta moyo wa Mungu kwa maombi. *Muungano* unaweza kukusaidia kuelewa zaidi nafasi ya harakati za maombi katika kazi ya upandaji kanisa, na namna unavyoweza kuwezesha harakati za maombi katika eneo au sehemu yako.


**Utupaji Maono**

Ni kitu gani Mungu anataka kwa nchi yako? Anataka makanisa kila mahali! *Muungano* unaweza kusaidia kuendeleza maono ya makanisa mapya kwa zana ya semina katika kanuni ya kuendeleza upandaji kanisa.

### KWA TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:

*The Alliance For Saturation Church Planning* (*Muungano wa Kueneza Upandaji wa Kanisa*)
Regional Resource Team
H-1111 Budapest
Budafoki ut 34/B III/2, Hungary
Tel: + (36-1) 466-5978 or 385-8199
Fax: (36-1) 365-4606
E-mail: KUMAAlliance@compuserve.com

# MZUNGUKO WA KUPANDA KANISA




Kupanda kanisa siyo mfuatano wa matukio na shughulu zilizounganishwa bila utaratibu; Ni utaratibu wenye msukumo wa lengo. Utaratibu huu unahitaji ulinganifu wa shughuli, mchanganyiko wa ujuzi, falsafa ya kawaida na ujasili katika uongozi. Maendeleo katika maeneo haya nyeti ndilo lengo la kufundisha wapanda kanisa. "mzunguko wa kupanda kanisa" ni mchoro wa utaratibu wa kupanda kanisa ambao kwa macho unaonyesha, kutoka katika wazo fulani la mtazamo, mwingiliano wa kanuni za ufunguo na kufanya mazoezi ya kazi katika utaratibu huo. Hii inawakilisha 'ramani ya barabara' kwa mpanda kanisa, kuruhusu watu kuonyesha ni wapi wametoka na wapi wanaelekea.

# MITAALA

### Ya Utaratibu wa Upandaji Kanisa kwa Kozi ya Omega

**Mitaala** (vianzio) ni msingi mugumu wa shughuli za huduma ambazo zimeshirikishwa katika utaratibu huu. Kila mtaala unaweza kufikiriwa kama jiwe la kuvukia la mtu binafsi katikati ya utaratibu mkubwa wa kuanzisha kusanyiko jipya. Mitaala inatoa hatua ya utekelezaji imara ambao unaweza kusaidia wafunzwa kuweza kwa vitendo kutumia mawazo yaliyomo kwenye Kozi ya Omega. Zote ni mawe ya mbali ambato yanaonyesha maendeleo, vile vile ubao wa alama ambao unasaidia kutoa mwelekeo zaidi. Zifuatazo ni orodha za mitaala na msisitizo katika Kozi ya Omega

| MWONGOZO WA KWANZA: | Msisitizo juu ya Maono ya KUM, Kusudi la Kanisa, Kujifunza Biblia kwa Kufata Neno na Utafiti |
|---|---|

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kuchunguza kusudi la Kanisa katika mwanga wa Utume Mkuu
- Kuanzisha mkakati wa jumla wa huduma ukizingatia maono ya “Z-kufikiri”
- Kuchunguza “mfumo na kazi” katika Kanisa la kwanza na Kanisa la sasa
- Kujifunza na kufanya majaribio ya Kujifunza Biblia kwa kufata neno
- Kuandika na kushirikisha ushuhuda binafsi
- Kuanzisha vikundi vya kusaidia maombi kwenye uinjilisti na upandaji kanisa
- Kukamilisha mradi wenye mambo mengi wa utafiti katika eneo linalolengwa

| MWONGOZO WA PIL: | Msisitizo Juu ya Uinjilisti na Vikundi Kiini |
|---|---|

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kushirikishana yaliyopatikana katika mradi wa utafiti na wengine katika eneo linalolengwa
- Kuandika maelezo ya kusudi la kanisa
- Kuanzisha falsafa ya huduma ya upandaji kanisa
- Kuanzisha mkakati wa binafsi wa uinjilisti, ikiwemo uinjilisti wa mmoja kwa mmoja
- Kuanzisha vikundi kiini kwa msisitiza juu ya uinjilisti
- Kutumia njia ya kujifunza neno kwa kulifuata binafisi na kwenye vikundi kiini

| MWONGOZO WA TATU: | Msisitizo juu ya Ufuasishaji, Vita Vya kiroho, Vikundi na Kufanya Kazi Kwa Timu |
|---|---|

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kuwatambua na kuwaelimisha viongozi nyeti wa vikundi kiini
- Kutumia muda katika maombi na kufunga
- Kutathimini mtazamo wa dunia wa wapanda kanisa ukilinganishwa na mtazamo wa dunia kibiblia
- Kutumia ukweli wa maandiko kupinga vipingamizi vya kiroho katika maisha na katika huduma ya wapanda kanisa
- Kuunda mpango binafsi wa kufanya ufuasishaji kwa watu wanaojihusisha katka huduma ya upandaji kanisa
- Kufanya maendeleo ya timu na shughuli za kutathimini
- Kuchanganua vipawa vya kiroho vya wapanda kanisa na vya timu ya upandaji kanisa

## MONGOZO WA NNE: Msisitizo Juu ya Uongozi na Uwakili Mwema

**Vitu Maalumuu vya Kutekeleza**

- Kutathimini uwezo na udhaifu wa mtindo wa uongozi wa huduma ya mpanda kanisa, kwa msisitizo juu ya njia za mwingiliano wa mtu binafisi na wengine
- Kushirikisha kanuni za kiongozi mtumishi kwenye maisha na huduma ya mpanda kanisa
- Kufuatilia matumizi ya muda katika maisha na huduma ya mpanda kanisa, kuweka vipao mbele, na kutengeneza ratiba
- Kutathimini utoaji fedha wa mpanda kanisa, vilevile na wa kanisa lenyewe lililopandwa
- Kutazama kwa upya nafasi ya mke na mme kibiblia na wajibu ambao wapanda kanisa wanao kwenye famila zao
- Kuongoza vikundi kiini vilivyopo katika utaratibu wa kuongezeka mara dufu
- Kuandaa mpango wenye mkakati utakaoelekeza kwenye huduma ya kueneza upandaji kanisa

## MWONGOZO WA TANO: Msisitizo Juu ya Kuongezeka Mara Dufu, Kuhamasisha Wengine, na Kuchochea Harakati za KUM

**Vitu Maalumu vya Kutekeleza**

- Kuanzisha Ushirikiano wa huduma na vikundi vingine vya kiinjili katika eneo linalolengwa
- Kupanga na kuweka muundo wa usimamizi kwa vikundi kiini ambao utachochea kukua kunakoendelea na kuongezeka mara dufu
- Kuwafundisha watu kuomba kwa ajili ya Ongezeko la upandaji kanisa; kuhamasisha maombi katika mji, mkoa na hata katika ngazi ya Taifa
- Kuanzisha na kuweka mpango kwa mkufundisha na kushauri wapanda kanisa wapya
- Kuwezesha na kutoa viongozi wapya kwa ajili ya huduma ya upandaji kanisa
- Kuchochea maono katika makanisa mapya kwa wamisionari kujihusisha siyo tu katka eneo lao wanalolenga, bali pia mpaka “miisho ya dunia”

# Kimsingi Inagusia **Awamu ya MISINGI** ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

## MTAZAMO WA MWONGOZO WA KWANZA

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Njia za Kujifunza Biblia (NKB) | Uinjilisti (UI) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 1:**<br>"Z" Kufikiri<br><br>**Somo la 2:**<br>Utume Mkuu na Upandji Kanisa<br><br>**Somo la 3(3A):**<br>Mzunguko wa Upandaji Kanisa 3A: *Vielezo vya Upandaji Kanisa*<br><br>**Somo la 4 (4A, 4B)**<br>Kanuni za Utafiti 4A: *Kulifahamu Eneo unalolenga*<br>*4B: Mifano ya Maswali ya Utafiti* | **Somo la 1:**<br>Misingi ya Kibiblia kwa Ajili ya Kanisa<br><br>**Somo la 2 (2A):**<br>Kusudi la Kanisa<br>2A: *Karatasi ya Mazoezi Kwa Utume Mkuu*<br><br>**Somo la 3 (3A):**Mfumo na Kazi<br>3A: *Mfumo na Kazi Iliyotumika*<br><br>**Somo la 4:** Kutafsiri Maana ya Kanisa la Mtaa | **Somo la 1 (1A)**<br>Kuhesabiwa Haki Kwa Imani<br><br>**Somo la 2:** Kuishi Kufuatana na Injili<br><br>**Somo la 3:**<br>Ukuaji wa Mkristo<br><br>**Somo la 4:**<br>Nguvu ya Injili Inayobadilisha<br><br>**Somo la 5:**<br>Kutunza Kumbukumbu za Maisha ya Kiroho | **Somo la 1, 2:**<br>Kongamano la Maombi:<br>Kuombea Uamsho<br><br>**Somo la 3 (3A):**<br>Jinsi ya Kuwezesha Maombi<br>3A: *Maombi ya Utatu* | **Somo la 1 (1A):**<br>Utangulizi wa Njia za Kujifunza Biblia Kwa Kufata Neno<br>1A: *Jinsi Tulivyopata Biblia*<br><br>**Somo la 2 (2A):**<br>Kulichunguza Neno la Mungu<br>2A: *Lugha ya Biblia*<br><br>**Somo la 3:**<br>Warsha ya Uchunguzi<br><br>**Somo la 4 (4A):**<br>Kufafanua Neno la Mungu<br>4A: *Majedwali ya Biblia*<br><br>**Somo la 5:**<br>Warsha ya Ufafanuzi<br><br>**Somo la 6:**<br>Kulitumia Neno la Mungu<br><br>**Somo la 7 (7A):**<br>Warsha ya Kulitumia Neno la Mungu<br>7A Waefeso-an 1.B.S. | **Somo la 1:**<br>Utangulizi Juu ya Uinjilisti<br><br>**Somo la 2,3:** Kutayarisha Ushuhuda Binafsi |
| **4** | **4** | **5** | **3** | **7** | **3** |

Namba katika mabano (26) zina maanisha mwishoni

# Kimsingi Inagusia **Awamu ya KULETA** ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

## MTAZAMO WA MWONGOZO WA PILI

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Uongozi (UO) | Vikundi Kiini (VK) | Njia za Kujifunza Biblia (NKB) | Uinjilisti (UI) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 5:** Misingi ya Kibiblia ya Kueneza Upandaji Kanisa<br><br>**Somo la 6:** Warsha ya Utafiti<br><br>**Somo la 7:** Kuhamasisha Rasilimali Kupitia Utafiti | **Somo la 5:** Asili ya Kanisa<br><br>**Somo la 6 (6A):** Kazi za Umoja za kanisa<br>*6A: Ubatizo Katika Agano Jpya*<br><br>**Somo la 7:** Kuandaa Maelezo ya Kusudi la Kanisa<br><br>**Somo la 8 (8A):** Falsafa ya Huduma ya Upandji Kanisa<br>*8A: Kuanzisha Falsafa ya Huduma ya Upandaji Kanisa* | **Somo la 6:** Kuishi Kama Wana Badala ya Mayatima<br><br>**Somo la 7 (7A):** Kujifunza Kuwa Wana<br>*7A*: *Yatima Dhidi ya Wana* | **Somo la 4:** Kongamano la Maombi: Kuabudu na Kuritafakari neno | **Somo la 1 (1A):** Misingi ya Kibiblia ya Uongozi *1A: Mchanganuo wa Uongozi*<br><br>**Somo la 2 (2A):** Sura ya kiongozi<br>*2A*: *Hadhi ya Kiongozi* | **Somo la 1:** Kazi na Faida za Vikundi Kiini<br><br>**Somo la 2 (2A, B):** Kanuni za Uongozi wa vikundi Kiini<br>*2A: Vikundi Kiini Vivunja Barafu*<br><br>2B: *Mifano ya Shughuli*<br><br>**Somo la 3 (3A):** Kuanzisha Vikundi Kiini<br>3A: *Karatasi ya Upangaji*<br><br>**Somo la 4 (4A):** Uinjilisti wa Vikundi Kiini<br>4A: *Kuhusu "Oikos"*<br>**Somo la 5:** Kuonyesha Mfano wa Kikundi Kiini<br><br>**Somo la 6**: Falsafa ya Huduma ya Vkundi Kiini | **Somo la 8 (8A):** Njia Tofauti Tofauti za Kutumia Njia ya Kujifunza Biblia Kwa Kulifata Neno<br><br>**Somo la 9 (9A,9B)** Kuongoza Mafunzo ya Biblia Kwa Kulifuata Neno<br>9A: Mafunzo ya Mathayo 20:17-28<br>9B: Kujifunza Juu ya LK 15:1-7<br><br>**Somo la 10, 11 (10A):** Warsha ya Kuongoza Mafunzo ya Biblia Kwa Kufata Neno<br>*10A: Vfungu Kwa Ajili ya IBS* | **Somo la 4 (4A):** Uinjilisti na Upandaji wa Kanisa<br>*4A:Kutathimini Mikakati ya Uinjilisti*<br>**Somo la 5 (5A.5B):** Vizuizi dhidi ya Mafanikio ya Injili<br>*5A: "Kanisa kwa Watu Wote"*<br>*5B: Kujibu Juu ya Kupinga kwa Kawaida*<br>**Somo la 6;7 (6A,6B,6C**)<br>Utaratibu wa kukata Shauri<br>*6A: Sura ya Mtu katika Kuinjilisha*<br>*6B:Kanuni Tatu*<br>*6C: Kuchunguza Njia Aliyotumia Yesu* |
| **3** | **4** | **2** | **1** | **2** | **6** | **4** | **4** |

Namba katika mabano (27) zina maanisha mwishoni

# Kimsingi inagusia **Awamu ya UANZILISHI** ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

## MTAZAMO WA MEONGOZO WA TATU

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Uongozi (UO) | Vikundi Kiini (VK) | Uinjilisti (UI) | Kufuasa (KS) | Vita Vya Kiroho (VK) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 8:** Kusonga Mbele kwa Kwanza<br><br>**Somo la 9:** Asili ya Harakati za Upandaji kanisa | **Somo la 9,10:** Kanisa na Vipawa Vya Kiroho<br><br>**Somo la 11:** Nguvu Za Kijamii za Kanisani | **Somo la 8,9:** Sheria na Injili<br><br>**Somo la 10 (10A):** Toba Kama Njia ya Maisha<br>*10A: Sehemu ya Wenye Dhambi* | **Somo la 5:** Maombi na Kufunga<br><br>**Somo la 6,7:** Kongamano la Maombi: Kuombea Kuenea kwa injli | **Somo la 3:** Mzunguko wa Uongozi<br><br>**Somo la 4:** Utangulizi kwa Kazi ya Timu<br><br>**Somo la 5:** Maendeleo ya Timu | **Somo la 7 (7A)** Nguvu ya Majadiliano ya Vikundi Kiini<br><br>**Somo la 8:** Kutunza Watu Walio Kwenye Vikundi Kiini<br><br>**Somo la 9:** Kufundisha Viongozi Wapya wa Vikundi Kiini | **Somo la 8:** Injili ya Mahusiano | **Somo la 1:** Utangulizi katika kufuasa<br>**Somo la 2 (2A):** Jukumu lako Katika Kufanya Wanafunzi<br>*2A:Tabia ya Upendo wa Kikiristo*<br><br>**Somo la 3 (3A):** Fahamu Lengo Lako, Fahamu Watu Wako<br>*3A:Imani, Tumaini na Upendo*<br><br>**Somo la 4 (4A)**:Kuwasaidia Wanafunzi Kukua Kiroho<br>*4A:Kukua Kiroho Kunahitaji Tathimini*<br><br>**Somo la 5(5A):** Mifumo ya Kufuasa<br>*5A: Kufanya Mpango wa Kufuasa* | **Somo la 1:** Kuelewa Mtazamo wa Kidunia<br><br>**Somo la 2:** Nguvu za Vita vya Kiroho<br>*2A: Mafunzo ya Waefeso 4:17-5:21*<br><br>**Somo la 3: (3A,3B):** Mashambulizi ya Kiroho<br>*3A: Kujifunza Biblia*<br>*3B: Mchanganuo Kutoka Ulimwenguni Kote* |
| **2** | **3** | **3** | **3** | **3** | **3** | **1** | **5** | **3** |

Namba katika mabano (26) zina maanisha mwishoni

# Kimsingi Inagusia **Awamu ya KUFUNDISHA** ya Mzunguko wa Upandaji Kanisa

**MTZAMO WA MWNGOZO WA NNE**

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Uongozi (UO) | Vikundi Kiini (VK) | Kufuasa (KS) | Uwakili Mwema (UM) | Familia (FA) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 10 (10A, 10B):** Vipengele vya Mkakati kwa Harakati za Upandaji Kanisa<br>*10A: Imani na Utii dhidi ya Hofu na Kutokuamini*<br>*10B: Vitu Vinavyoamsha Ukuaji wa Asili*<br><br>**Somo la 11:** Dalili za Harakati<br><br>**Somo la 12:** Uangalizi Kati Kati ya Harakati | **Somo la 12:** Nguvu ya Makanisa yanayoibuka<br><br>**Somo la 13:** Tabia ya Makanisa Yanayokua<br><br>**Somo la 14:** Serikali ya Kanisa na Ofisi za Kanisa: | **Somo la 11:** **U**pendo Kama Msingi kwa Huduma<br><br>**Somo la 12:** **K**uuelewa Moyo wa Baba<br><br>**Somo la 13:** Neema ni Kwa Wanyenye kevu | **Somo la 8, 9:** Kongamano la Maombi Kuomba Kibiblia | **Somo la 6 (6A):** Uongozi wa Kitumishi<br>*6A: Orodha ya Viongozi*<br><br>**Somo la 7:** Nguvu za Uongozi<br>**Somo la 8:** Mitindo ya Mwingiliano<br><br>**Somo la 9:** Mahitaji ya Uongozi<br><br>**Somo la 10 (10A):** Kufunza Viongozi Wapya<br>*10A:Hadhi za Kutia katika Uongozi Mpya* | **Somo la 10:** Majadi-liano ya Maswali na Matatizo ya Vikundi Kiini<br><br>**Somo la 11:** Kuzidisha Kwa Kikundi Kiini | **Somo la 1:** Warsha ya Kufuasa | **Somo la 6:** Utangulizi juu ya Uwakili Mwema<br><br>**Somola 2:** Uwakili mwema Kwenye Fedha<br><br>**Somo la 3:** Matumizi ya Muda<br><br>**Somo la 4:** Utaratibu wa Upangaji Kimikakati<br><br>**Somo la 5:** Warsha juu ya Utaratibu wa Upangaji Kimikakati | **Somo la 1:** Majukumu ya Kibiblia Katika Familia<br><br>**Somo la 2:** Kulea |
| **3** | **3** | **3** | **2** | **5** | **2** | **1** | | |

Namba katika mabano (25) zina maanisha mwishoni

# Kimsingi Inagusia **Awamu ya KUZIDISHA NA HARAKATI** Katika Mzunguko wa Upandaji Kanisa

## MTAZAMO WA MWONGOZO WA TANO

| Maono ya KUM (MO) | Kanisa (KA) | Tabia ya Kiroho (TK) | Maombi (MB) | Uongozi (UO) | Vikundi Kiini (VK) | Kuhubiri (KR) | Familia (FA) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Somo la 13:** Maono na Kupiga Darubini<br><br>**Somo la 14:** Kuhamasisha<br><br>**Somo la 15:** Hatua Inayofuata<br><br>**Somo la 16:** Mafunzo Kama Sehemu ya Harakati za Upandaji Kanisa<br><br>**Somo la 17:** Kuhamasisha Viongozi Kupitia Uanzilishi wa Kitaifa | **Somo la 15:** Malezi ya Kanisa<br><br>**Somo la 16:** Ibada ya Umoja katika Kanisa la Mtaa<br><br>**Somo la 17:** Jinsi ya Kuongoza Ibada ya Pamoja Katika Kanisa la Mtaa<br><br>**Somo la 18:** Kanisa la Mtaa na Mwili Mkubwa wa Kristo<br><br>**Somo la 19:** Mguso wa Kihistoria wa Kanisa __ (Historia ya Kanisa Katika Mandhali ya Nchi) | **Somo la 15:** Huduma ya Upatanishi<br><br>**Somo la 16:** Unyoofu wa Maadili Kwa Wapanda Kanisa | **Somo la 10:** Maombi ya Kuwezesha kwa Harakati za Upandaji Kanisa<br><br>**Somo la 11,12:** Kongamano la Maombi: Kumshukuru Mungu Kwa Ajili ya Uaminifu wake | **Somo la 11:** Kutoa Viongozi<br><br>**Somo la 12:** Uongozi wa Harakati<br>*12A: Viongozi wa Harakati* | **Somo la 12:** Viini Vinavyoenea Kupitia Makanisa ya Mtaa<br><br>**Somo la 13 (13A):** Kusimamia vikundi Kiini<br>*12A: Hatua ya Mwisho* | **Somo la 1:** Mahubiri ya Kibiblia 1: Kuelewa Ujumbe<br><br>**Somo la 2:** Mahubiri ya kibiblia 11: Kuelewa Wasikilizaji<br><br>**Somo la 3:** Mahubiri ya kibiblia 111: Kujielewa Mwenyewe | **Somo la 3:** Huduma Kwa Famila |
| **5** | **5** | **5** | **3** | **2** | **2** | **3** | **1** |

Namba katika mabano (23) zina maanisha mwishoni

**JUMLA YA MASAA YA KOZI YOTE: 127**

# MAONO YA KUM

MAONO YA KUM

SOMO LA 13

# Maono na Kumulika kwa Darubini

## KUICHUKUA INJILI ULIMWENGUNI

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuhamasisha makanisa ya mtaa kufikia nje katika maeneo ya mtaa, mkoa, tamaduni zinazoingiliana na huduma ya ulimwengu mzima.

☞ **Wazo Kuu**

- Wakristo lazima waangalie ulimwengu kwa maono ya mavuno ya Mungu.
- Makanisa yanatakiwa yahusike katika huduma za ndani, kimkoa, kiutamadanu unaoingiliana na kitaifa.

☞ **Matokeo Yanatarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa jinsi ya kuwa na maono ya kibiblia ya kuendeleza injili kuanzia mahali walipo na kwenda mpaka "miisho ya dunia."
- Kujua kanuni ya kutumia kumulika kwa darubini kukuza rasilimali za kanisa katika uinjilishaji wa ulimwengu.
- Kushiriki katika kuweka maono ya kibiblia mahali pao, kimkoa, kiutamaduni unaoingiliana na ulimwengu mzima.

☞ **Ushauri kwa wakufunzi**

Wafanye wafunzwa kuwa na mda wa kujifikilia na kujaza darubini katika kielelezo 13.3 mwishoni mwa somo hili. Hii itawasaidia kuona "Yudea yao, Samaria na miisho ya dunia." Bwana anaweza kutumia somo hili kutia changamoto baadhi ya wafunzwa kwa ajili ya umishenari wa tamaduni zinazoingiliana kufanya kazi wao wenyewe au kuombea wafanyakazi wa tamaduni zinazoingiliana kutumwa kutoka makanisa yao yanayoibuka.

**UTANGULIZI**

Kanisa lazima litii utume mkuu kwa kufanya wanafunzi wa *kwao wenyewe na wa mataifa yote.* Somo hili maalumu litafanya kazi kutokea matendo 1:8 ambayo inaishurutisha kanisa kuwa mashahidi wa Yesu Yerusalemu (ndani), Yudea (mkoa), samaria (tamaduni zinazoingiliana) na miisho ya dunia (tamaduni mpya, lugha na sehemu).

### I. TAFSIRI YA MAONO NA KUPIGA DARUBUNI

Kanisa kufikia wa nje ni kama darubini… inayosogeza kitu zaidi na zaidi mbali kwenye mkazo mkali.

Kwa makanisa ya mtaa kushiriki kiufanisi katika utume mkuu, yanahitaji **maono.** Maono ni uwezo wa kuona mbali ya nini kinaweza kuwa. Maono ya kiroho ya kuufikia ulimwengu kwa ajili ya Yesu Kristo ni uwezo wa kuona mataifa, mikoa, na watu wa ulimwengu kama sehemu na watu ambao injili itaenea kwa njia ya uinjilisti na upandaji makanisa.

Maono ni wazo zuri mpaka linapokuwa kitu halisi. **Kupima darubini** ni methali inayoelezea aina kadhaa ya mpenyo kwenye ulimwengu (kijografia na kiutamaduni) ambayo kanisa lazima lifanye ili kutimiza utume mkuu. Kanisa linalopanuka na kufikia nje ni kama darubini inayopanuka na kukuza, kuleta kitu karibu na karibu mbali kwa mtazamo mkali. Kila aina ya mpenyo utahitaji makanisa ya mtaa kuchukua hatua ngumu za kujitoa na kujitolea kuendeleza injili. Makanisa ya mtaa yanahitaji kuwa yanachukua injili kwa watu katika jumuia zao, mataifa na nje.

## II. KUANGALIA KWA MAONO YA MAVUNO YA MUNGU

Mungu analiita kanisa kuwa na maono ya mavuno yake ya mioyo ya watu Yesu pia alitumia methali ya mavuno katika Mathayo 9:38 kuwaamuru wanafunzi wake kuomba kwamba kuwe na watenda kazi wengi kwa mavuno yeke makuu. Siku ya pentekosti, Waisraeli walisherehekea mavuno ya ngano. Na kuja kwa Roho Mtakatifu siku hiyo, maono ya mavuno yaligeuzwa kanisa lilipozaliwa. Badala ya kufurahia mavuno ya ngano, kanisa lilitangaza utukufu wa Mungu kwa mataifa kwa lugha zao wenyewe, wakivuna mioyo ya watu elfu tatu siku ya kwanza! Watu hawa wakija kwa Kristo, maana mpya ya mavuno ya Mungu, iliwafanywa kuwa sehemu ya kanisa.

Tunaweza kutumia msemo wa upandaji kanisa na kusema Pentekosti ilikuwa ni kanisa mpya lililopandwa la Agano Jipya? Kanisa lililoanza siku ya Pentekosti limezaliana lenyewe zaidi ya milioni kuzidisha kwa kila bara linaloikalia dunia! Mavuno kwa jinsi hiyo lazima yaendelee, kwa kuwa makanisa zaidi ya milioni lazima yapandwe. Jim Montgomery, katika kitabu chake *DAWN 2000*, anasema kwamba karibu makanisa zaidi milioni saba yanahitajika kupandwa kuufikia ulimwengu wote. Maono tuliyonayo ni kuihubiri injili, kupanda makanisa, na kuwaleta watu makanisani kama wafuasi wa Yesu Kristo. Kanisa linachukua maono kwa ajili ya mavuno ya Mungu "kwa kufungua macho yake" na "kuangalia shamba" la ulimwengu. Maono ni mwanzo wa ujasiri wa kanisa kutimiza utume mkuu.

> ... kwa ajili ya Yesu. karibu makanisa milioni saba yaanahitajika kupandwa kuufikia ulimwengu wote.

## III. KUPIGA DARUBINI KWA AJILI YA MAVUNO YA MUNGU


Matendo 1:8 inaelezea kukua kunakoendelea kwa kanisa kutoka Yerusalemu mpaka miisho ya dunia na hata kutoa vidokezo vya kitabu cha Matendo (tazama jedwali 13.1).

**Jedwali 13.1 matendo 1:8**

| MATENDO 1:8: | "Yerusalemu" | "Yudea" | "na Samaria" | Miisho ya dunia |
|---|---|---|---|---|
| **Maana** | mji wa mtaa | mkoa | Eneo linalopakana | ulimwengu |
| **Vidokezo vya Matendo** | Matendo 1-8 (Mdo 5:28) | Matendo 8-12 (Mdo 8:5) | | Matendo 13-28 (Rum 15:19) |
| **Mifano ya kibiblia** | "Wathethalonike" 1 The1:6 | "Masedonia" 1 The1:7 | "na Akia" 1 The1:7 | "kila mahali" 1 The1:8 |

Katika siku za zamani za meli nyingi, nahodha anayeweza angeweza kukaza macho yake mbali kwa kutumia darubini. Anaposogeza darubini yake, sehemu zilikuwa karibu na karibu kwake. Kutumia mfano huu kutimiza Utume Mkuu, inaleta picha ya darubini na sehemu nne zinazokaza (Kielelezo 13.2). Tambua katika kilelezo kwamba kila sehemu ya darubini inahusiana na amri ya Yesu kwa wanafunzi wake katika Matendo 1:8: "…na mtakuwa mashahidi wangu Yerusalemu, na Yudea yote na Samaria, na miisho ya dunia."

**Kielelezo 13.2 kuuingia ulimwengu kwa injili (kupiga darubini)**



**A. Sehemu 1: Huduma ya Mtaa**

Kufungua darubini kwenye sehemu ya kwanza, tunaweza kuangalia huduma ya mtaa ya kanisa. Wanafunzi waliosikia amri hii mara ya kwanza waliitii kimtaa kwa kuijaza Yerusalemu kwa mafunzdisho kuhusu Yesu kristo (Matendo 5:28).

Kama agizo la kwanza katika nyenzo hii ya mafunzo, uligundua "eneo linalokusudiwa" unapotaka kupanda kanisa sasa (Mwongozo wa Kwanza, Maono Ziada 4A "Kuelewa Eneo Lako Unalolenga"). Huduma yako ya kupanda kanisa imekazia kwenye kijiji, mji au ujirani wa mji kwenye eneo linalolengwa. Mara kanisa lako linapoanzishwa, litaendelea kuhudumu kwa watu wa kwenye eneo hilo la kijografia. Hili ni kanisa la mtaa la "Yerusalemu."

> Kuwepo kwa kanisa moja la mtaa katika jiji mara chache kunamaanisha kazi imemalizika.

Asili ya Yerusalemu yako itaonyesha jinsi unavyofika nje kwao. Miji michache ni ya jinsi moja. Miji mingi ina watu wa umri unaopishana, elimu, utamaduni, historia ya kabila, lugha, n.k. haiwezekani kwamba kanisa moja peke yake linaweza kuendana na mahitaji mengi yanayopishana ambayo hali hii imeleta. Vile vile, miji mingi ni mikubwa sana kusafiri humo na kurudi kutoka eneo la kati kati inazuia mahudhurio. Kazi Yetu ni kanisa la mtaa mahali kila mmoja anapoweza kufika. Kuwepo kwa kanisa moja la mtaa katika jiji mara chache sana kunamaanisha kazi imemalizika. Kuzidisha kwa kanisa kuwafikia wengine ni njia bora ya kukamilisha kazi.

Agizo letu ni wazi, tunatakiwa kufikia nje kwa waliopotea. Siyo jukumu la waliopotea kuja kwetu. Kwa msaada wa Mungu, kanisa la mtaa linalokua litaanza kuomba kwa ajili ya waliopotea katika miji yao ambao hawana wa kuwashuhudia, na kwa juhudi kuwa mashahidi kwao.

**B. Sehemu 2: Huduma ya Kimkoa**

> Katika hisia 'tunda' la kweli la kanisa siyo wakata shauri wapya, lakini kanisa jipya.

Kufungua darubini zaidi kwenye sehemu ya pili kunaruhusu kanisa kuona mbali ya mandhali yake mpaka kwenye mapana ya eneo la kijografia. Kanuni hii inaendana na kuwa mashahidi Yudea kama ilivyoelezwa katika Matendo 1:8. Aina hii ya kufikia inahamasisha mwili wa Kristo kupanda kanisa mpya katika eneo la kijografia lililo karibu, mahali amabpo utamaduni na lugha inawezekana kuwa sawa sawa na hiyo ya wajumbe wa kanisa la mtaa. Aina hii ya kufikia itapelekea kanisa "binti" la kwanza.

Kila kanisa tokea mwanzo wake linatakiwa liwe limeshafikiria kwamba kusudi lake ni kuzaliana. Kiasili viumbe hai vyote mapema au baadaye vinainuka, na hata kufa, wakati matunda yake au mzao wake anaendelea kuishi. Kanuni hii ni sawa katika huduma ya kanisa. Katika hisia 'tunda' la kweli la kanisa siyo wakata shauri wapya, lakini kanisa jipya. Njia ya mafanikio zaidi kwa kanisa kuwa na mguso wa kimkoa ni kwa kuzaliana lenyewe, kupanda makanisa binti.

> **Mfano**
>
> Huko Brazili kwa zaidi ya kipindi cha miaka 20 kanisa moja lilijaza eneo la kijografia kwa makusanyiko 200. Mmishenari ambaye makanisa haya yalituma kwenda Albania alikuwa akifundisha juu ya kuzidisha makanisa kwa wapanda kanisa pale na alisema, "Ukuaji wa kanisa letu ulikuwa wa polepole ukilinganishwa na mwingine, lakini hata hivyo, tunapopanda kanisa mpya mara moja ambalo kanisa binti limepanga kupanda makanisa binti mengine upesi iwezekanavyo. Makanisa yetu yanajua kusudi lao ni kupanda makanisa mapya kutokea mwanzoni." Ni aina hii ya kufikiria na kusudi linaloweza kuhamasisha makanisa kutokea mwanzoni mwake kuwa na akili ya huduma kwenye kusanyiko lao wenyewe na zaidi.

Kanisa linapokuwa na haja na imani ya kutimiza maono ya kumlika kwa darubini kwa kupanda makanisa binti itabidi kuchukua baadhi ya hatua za lazima. Inachukua kujitolea kukubwa na kujitoa miongoni mwa wajumbe wa kanisa lililopo kupanda kanisa binti. Hatua hizi zitakuwa ni pamoja na kufundisha wafanya kazi, kuwatuma, kukusanya fedha, na la muhimu zaidi, kuendelea katika maombi kuelekea kukamilisha maono kupitia kupiga darubini.

### C. Sehemu 3: Huduma yaTamaduni Zinazoingiliana

Kufunguliwa kwa darubini kwenye sehemu yake ya tatu inaweza kulinganishwa na kushuhudia katika Samaria. Hii inaelezea kuendeleza injili ki- tamaduni zinazotofautiana. Ingawa Wasamaria wema hawakuwa mbali kijografia kutoka kwa waumi Wayahudi Yerusalemu na Yudea walikuwa na makundi ya tamaduni tofauti na makabila tofauti. Walikuwa na mila nyingi tofauti na mapokeo vile vile na mazoea tofauti ya dini zao. Ingawa Wayahudi walikuwa na uadui na Wasamaria, Yesu aliwapenda wote! Wanafunzi wa kwanza, Philipo hasa, katika kutimiza Utume Mkuu, alichukua injili mpaka Samaria (Mdo 8:4-25).

Kanisa linawajibika kufikia tamaduni zinazoingiliana kwa makundi tofauti ya watu. Tunaweza kufikia nje karibu na makundi ya kabila kwa ajili ya Yesu, hata unapokuwepo mvutono wa kisiasa na kikabila. Hili mara nyingi litahitaji kwamba hao ambao kanisa linatuma nje wanachukua mafunzo ya mwingiliano wa tamaduni, kujifunza lugha, na kujifunza utamaduni wa watu mahali watakapopanda kanisa. Ni juhudi hizi za ziada ambazo mara nyingi zitasababisha kazi mpya kukua na kuzaliana.

### D. Sehemu 4: Huduma ya kimataifa

Kufungua darubini kwa kiwango cha urefu wake inamaanisha kwenye miisho ya dunia iliyotajwa katika Matendo1:8. Hii inapanua huduma ya kanisa kwa watu walio mbali kijografia, kiutamaduni na kilugha. Mfano bora wa kanisa la kwanza wa utii kwenye amri hii unapatikana katika Matendo 13 na kufuatia wakati Paulo na Barnabas (baadaye wengine) walitumwa nje kuwa na huduma ya kupanda kanisa ya mchanganyiko wa tamaduni na za kimataifa.

Kwa kuomba, kutoa, na kutuma wamishenari miisho ya dunia, kanisa la mtaa linakamilisha utaratibu wote wa kupiga darubini. Linakuwa na huduma inayotokea katika ngazo zote—“Yerusalemu, Yudea. Samaria na miisho ya dunia.”

Kazi yetu haijaisha mpaka injili imepenya dunia yote, ikitoa habari ya wokovu kwa kila mtu. Siyo “kawaida” kujali hali ya waliopotea usiowajua. Kwa jinsi hiyo, hii ni haja ya Mungu, na jukumu letu. Kundi jipya linapobadilishwa kuwa kanisa, halijamaliza kazi yake. Badala yake, imeanza tu kuchukua hatua yake ya kwanza katika safari inayoamsha na yenye malipo kwa Bwana.

Ni muhinu na ya kiblia kuomba kwa ajili ya makundi ya watu (Rum 10:1; 1Tim 2:1-2; Efe 6:19) na makanisa yanatakiwa kuomba tokea mwanzoni kwa ajili ya kuenea kwa injili kwa “mataifa yote” (Mt 28:18-20) na wafanyakazi wa mavuno. Watu katika kanisa lako wana maono haya? Kuna watu wanaoomba kwa ajili ya mataifa?

Kutoka katika maono haya ya misheni inawezekana pia kupiga darubini kupitia utoaji wa fedha kwenye misheni. Kanisa la Wafilipi walitoa kifedha kwenye huduma ya Paulo ya umishenari na kufikia nje kwa kupanda kanisa (Flp 4:17-19). Kwa njia hii kanisa linaweza kupiga darubini kupitia misaada kifedha ya wamishenari wanaofanya kazi sehemu za mbali hata kama hawatoki katika kusanyiko hilo.

**Mfano**

Luis Bush (aliyeendesha harakati za Latino ya Amerika za makanisa kutuma wamishenari), na wengine walisafiri Latino ya Amerika yote wakitangaza maono ya umisheri kama sehemu ya harakati za COMIBAM (kifupi cha, Shirika la Amerika la Ibero katika misheni). Kilio kilitoka nje, “Latino ya Amerika, kutokea umishenarini kwenda nguvu ya umishenari!” Wakati huo, nchi za Latino ya Amerika zilikuwa zikipita katika wakati mgumu kiuchumi na wengi hawakweza kuona jinsi ambavyo ingewezekana kutuma wamishenari nchi zingine kama walikuwa wakihangaika kifedha. Luis alitumia mfano wa Ibrahimu, ambaye mwili wake ulikuwa mzuri kama wa aliyekufa lakini imani yake ilikuwa hai. Ilikuwa imani yake ambayo ilileta ahadi ya kijana wake. Kwa njia hii alilinganisha kukosekana kwa fedha na mwili wa Ibrahimu akisema, “Katika Latino ya Amerika hatuna pesa- LAKINI TUNA IMANI!” Kanisa hadi kanisa walikubali wito wa umishenari na tangu COMIBAM katika 1987, maelfu ya wamishenari wametumwa na makanisa ya Latino ya Amerika. Wamekuwa na imani na Mungu ametoa fedha!

Ni uzoefu wa hali ya juu na wa kufurahisha wakati kanisa linapotuma wamishenari ulimwenguni kutoka kwao wenyewe na kwa uwezo wao. Kusanyiko kwa undani zaidi linamiliki na linajilinganisha na upendo wa Mungu kwa mataifa wanapotuma mtu nje ambaye ni mpendwa kwao. Siyo kila kanisa linaweza kusaidia wamishenari lenyewe. Kwa jinsi hiyo, inawezekana kushirikiana na makanisa mengine ya mtaa kutuma nje wamishenari kutoka katika kusanyiko lao. Kwa kutuma nje wamishenari wake, wajumbe wa kanisa la mtaa wanaweza kujisikia yote furaha na ugumu wa kuendeleza injili miongoni mwa watu wasiofikiwa.

## IV. NGUVU YA KIROHO NA MAMLAKA

Kutokana na upandaji kanisa katika eneo la mtaa linalolengwa mpaka kupanda jingine miisho ya dunia. Kanisa linafanya hivyo chini ya mamlaka ya Kristo na kwa nguvu za Roho Mtakatifu. Wakati Yesu alipotoa Utume Mkuu kwa wanafunzi wake, alianza kwa kusema, “Mamlaka yote mbinguni na duniani mmepewa” (Mt 28:18). Aliishia kwa kuwahakikishia kuwa, “niko pamoja nanyi wakati wote, mpaka miisho ya vizazi” (Mt 28:18). Kutiwa katikati ya ahahdi hizi ni kazi ya wanafunzi—kufanya wafuasi wa mataifa yote.

> Kwa ujasiri tunaweza kufika nje kwa majirani zetu na zaidi tukijua kuwa Mungu atatupatia kila tunachohitaji kufuasa mataifa.

Mda mfupi kabla ya kurudi mbinguni, Yesu aliwaahidi wanafunzi wake, “Lakini mtapokea nguvu akisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu” (Mdo 1:8). Matokeo ya kupokea nguvu hizi ilikuwa kwamba wanafunzi wangekuwa mashahidi wa Kristo mpaka miisho ya dunia. Yote mamlaka na nguvu za Mungu zimetolewa kwa watoto wake kuwawezesha kufanya wanafunzi mpaka miisho ya dunia. Yaliyobaki katika kitabu cha Matendo yanaonyesha jinsi waumini walivyokwenda nje chini ya mamlaka haya bila kujali kutahadharishwa wasifanye hivyo na mamlaka ya kidunia. Walikuwa wameamua kumtii Mungu badala ya mtu. Walipofanya hivyo, chini ya nguvu za Roho Mtakatifu, neno la Mungu lilienea kwenye eneo lote.

Kama waumini, tuna mamlaka pia ya Kristo anayeishi ndani yetu. Tuna nguvu za Roho Mtakatifu. Tunaweza kufika nje kiujasiri kwa majirani zetu na zaidi, tukijua kuwa Mungu atatupatia kila tunachohitaji kufuasa mataifa.

## SULUHU

Maono na kupiga darubini ni tabia za kanisa linalotii. Maono yanaangalia wakati ujao kukamilisha kazi kubwa Bwana aliyopatia kanisa lake kupanua injili mpaka miisho ya dunia. Kupiga darubini ni picha ya kanisa linalotii, kiutii likipenya ulimwengu. Ni picha ya kanisa la mtaa kuchukua hatua nzito (kuomba, kutoa, kwenda) kufikia nje yote kijografia na kiutamaduni kuona “utukufu wa Mungu juu ya dunia” (Isa 11:92:14). Kanisa la mtaa halihitaji kuufikia ujirani kabisa kabisa kabla halijawa linaomba na kufanyia kazi kuelekea kupanda makanisa mengine na kutuma nje wamishenari upande mwingine wa ulimwengu. Hii inatakiwa itokee sawia katika maisha ya kanisa la mtaa. Kwa kuongeza, ni muhimu kwamba kanisa binti mpya lililopandwa la kusanyiko, kama ilivyoelekezwa na kanisa mama, linatakiwa pia liwe limepanda ndani yake haja ya kupenya ulimwengu kwa injili. Kutoka katika uelekeo mmoja inawezekana kwa kanisa kufanya mguso wa hali ya juu na kuchangia kwenye harakati ambazo zitatimiza ahadi ya Matendo 1:8.


## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Nini vizuizi kwenye maono na jinsi gani unaweza kuvishinda?
- Jinsi gani unaweza kuhamasisha maono na kupiga darubini katika makanisa yako mapya?
- Kwa nini kanisa moja halitoshi sana kufikia mji wote kwa ajili ya Kristo?
- Jinsi gani darubini yako ni pana? Darubini ya kanisa lako?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Kwa kutumia darubini iliyoonyeshwa katika kielelezo 13.2, anza kushirikisha maono yako kanisa (ma) kuhusu kufikia nje zaidi na zaidi kwa injili.
- Angalia kwenye darubini katika kielelezo 13.3 chini. Kwa kila sehemu ya darubini, andika ni nini "Yerusalemu" yako, Yudea, Samaria na miisho ya dunia." Ni katika sehemu ipi kanisa lako linafanya kazi kijuhudi? Kama kuna sehemu ya darubini ambayo kanisa lako mpya halijahusika, nini unachoweza kufanya kuhamasisha hilo?

**Kielelezo 13.3 Kupiga Darubini kwa ajili ya Kanisa la Mtaa**




## VYANZO SOURCES

Montgomery, Jim. *DAWN 2000*: *7 Million More Churches To Go*. Pasadena, CA: William Carey Library, 1989.

MAONO YA KUM

SOMO LA 14

# Kuhamasisha

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wapanda kanisa kuelewa jukumu la kimkakati la kuhamasisha katika harakati za kupanda kanisa.

☞ **Wazo Kuu**

- "Kuhamasisha" kwa kifupi ina maana kuwaweka tayari watu katika utayari wa kushiriki mahali wanapoweza kuchangia vizuri kwenye sababu ya wote
- Waumini wanatakiwa wahamasishwe ili kupambana kikamilifu.
- Wahamasishaji wafanisi wana tabia ya maono, imani na kutia moyo, na kugusa.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa umuhimu wa kuhamasisha.
- Kujua tabia za wahamasishaji wafanisi.
- Kushiriki katika kuhamasisha mmoja mmoja na makanisa ya mtaa kwa upandaji wa kanisa

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili linaweza kufundishwa kama majadiliano. Chukua mda kujadili tafsiri ya kuhamasisha, angalia kwenye mifano ya kibiblia, na jadili jinsi uhamasishaji unavyoweza kufanywa kivitendo katika makanisa ya mtaa. Jiandae kwa masimulizi, mawazo na rasilimali kuhusiana na uhamasishaji unaoweza kushirikishwa kwa wafunzwa.

## UTANGULIZI

Wakati wa vita, hali ya uharaka na hitaji la kupona linatawala kila kitu watu wanachosema na kufanya. Hata kama watu wako mstari wa mbele kwenye moto wa vita au nyumbani, mbali kutoka kwenye vita, vita inaathiri uhusiano wao wa mwingiliano, mawazo yao, na matumizi ya mda wao na raslimali. Kilio wakati wa vita ni KUHAMASISHA! "Kuhamasisha" *kwa kifupi kunamaanisha kuwaweka watu tayari katika utayari wa kushiriki mahali wanapochangia vizuri katika kazi ya wote na malengo ya wote*.

Kanisa linapokazana kukua, mwisho wa milele wa mamilioni uko mashakani. Wahamasishaji wanaona kupanuka kwa kanisa kama kweli kweli ni—vita ya kiroho. Pamoja na jeshi (nguvu)-kama jitihada wanalia kwa ajili ya kuhamasisha. Katika somo hili tutajadili umuhimu wa kuhamasisha vilevile na baadhi ya njia za kivitendo ambazo kuhamasisha kunaweza kutia moyo makanisa kuwa ya ufanisi zaidi katika kutimiza Utume Mkuu.

## I. NINI MAANA YA KUHAMASISHA? KUHAMASISHA NI PAMOJA NA:

### A. Maono ya Wote

Kuhamasisha hakuwezekani bila maono ya wote. Kwa nini watu wafanye kazi pamoja wakati hawajaribu kutimiza vitu sawa? Bila maono, watu wanahamasisha nini hapo?

Maono ya wote yanatoa mkazo wa kuhamasisha. Maono ya pamoja yanaweza kutoka kwa Mungu tu—maono kutoka kwa Bwana peke yake yanaweza kuwaweka watu pamoja kwa kuungana katika vita vya kiroho. Kama ilivyokwisha kusemwa kwa kurudiwa katika mfuatano

huu wote, kwa maombi yakiuliza “nini Mungu anataka?” Ni njia pengine nzuri ya kuamsha maono kwenye kuhamasisha.

### B. Mafunzo

Maono ya wote hayatokezi mara moja  katika kuhamasisha. Watu lazima wafunzwe na kuandaliwa kwa ajili ya ukamilishaji wa maono. Mafunzo kikawaida yanafuatia maono. Watu wangapi hawainjilishi kwa sababu hawajawahi kamwe kufunzwa jinsi ya kushirikisha imani yao? Watu wanapokuwa hawakufunzwa kumtumikia Mungu kama inavyowapasa, kisha hawajahamasishwa. Kuhamasisha kunaweza kutokea tu wakati watu wanapokuwa wamefunzwa.

### C. Raslimali

Wanagapi wangependa kumtumikia Mungu kama wamishenari lakini hawana msaada wa fedha? Wangapi wengine wangeshirikisha Kristo kwa majirani zao kama wangekuwa tu na zana sahihi? Watu wanapokosa rasilimali kufanya kile Mungu alichowaitia kufanya, hawajahamasishwa. Rasilimali zinakuja kwa mifumo mingi. Mwanamke anatoa baiskeli yake kwa mpanda kanisa ili kwamba aweze kusafiri kwenda sehemu za mji ambazo hazina ushuhuda wa injili. Hii ni kutoa rasilimali. Wakala wa misheni ya kimataifa anawapatia wapanda kanisa filamu ya Yesu, na vyombo vya kuendeshea. Hii ni kutoa rasilimali.

Ni rasilimali gani unaweza kufikiria ambazo zinahitajika kuanzisha na kuendeleza harakati za upandaji kanisa? Chukua wakati na orodhesha baadhi yake sasa.

### D. Uwekaji Kimkakati

Jeshi halijahamasishwa wakati linapokuwa na maagizo (maono), linapokuwa limefunzwa na kupewa (rasilimali). Badala, kuhamasisha kunaweza kutokea tu wakati mtaalamu aliyefunzwa yuko kwenye nafasi ya kufanya maagizo. Wakati watu wanapokuwa wamehamasishwa wanafanyakazi katika sehemu tofauti tofauti katika njia tofauti lakini kuelekea kwenye lengo moja. Kama makanisa yote katika eneo wanafuatisha juhudi za mmoja kwa mwingine na kuweka watu na raslimali katika mfereji kuelekea uinjilisti wa kundi la watu maalumu kwenye kutoa kundi jingine, kuliko makanisa kuhamasishwa kihafifu. Utafiti unaweza kuonyesha wapi kanisa lilipo,  na lisipo, kuweka juhudi zao kudhihirisha mahitaji zaidi ya kimkakati.

## II. KWA NINI WAUMINI WAHAMASISHWE?

Yesu aliomba kwamba wafuasi wake wawe umoja (Yohana 17). Alikusudia kanisa kufanya kazi pamoja kama mwili (1Kor 12, Rum 12). Mungu ameita kanisa lote kuchukua injili ulimwenguni kote. Kwa hiyo, Mungu anamwezesha kila muumini kwa vipawa vya kiroho kwa kusudi la kuhamasisha.

> Hakuna sehemu ya mwili inayoweza kushindana na vita vya kiroho peke yake. Bila kuhamasisha makanisa yanashindania kutoka kwenye nafasi ya udhaifu.

Kuhamasisha kwa hiyo kwa kifupi siyo wazo zuri, ni la lazima. Hakuna sehemu ya mwili inayoweza kushindana vita vya kiroho peke yake. Kanisa linafanya kazi vyema wakati kila sehemu imehamasishwa kuelekea kulipata lengo. Bila aina hii ya kuhamasisha, kanisa linashindana kutokea kwenye nafasi ya udhaifu bila kutumia wajumbe wote kama Mungu anavyokusudia.

Kanisa ni wakala wa Mungu wa kuhamasisha. Wakati mwili wote wa Kristo utahamasishwa kiuangalifu kwenye kusudi  kushuhudia kwa ajili ya Kristo, Mungu atasererekesha kanisa kuelekea  kufikia lengo la kufanya wanafunzi, kote katika taifa lao na pia nje ya mataifa mengine! Kila sehemu ya mwili lazima ielewe jukumu lake na kila kipawa lazima kigundue kupanuka kwake. Katika hili wajumbe wote wa mwili wanaungana kwenye tendo na kufuatia lengo.

## III. MFANO WA KIBIBLIA WA WAHAMASISHAJI

### A. Nehemia

Nehemia aliwahamasisha Wayahudi baada ya kufukuzwa kujenga ukuta wa Yerusalemu. Alifanya hili kwa kutoa maono, kutoa rasilimali vilevile na kuwaweka watu katika nafasi za kimkakati ili kwamba waweze kutumia kujaliwa kwo vipawa. Maono ya Nehemia na lengo  la kujenga upya ukuta wa Yerusalemu yalikuja kwake kama matokeo ya taarifa (utafiti), akiwa amesikia hali katika Yerusalemu,  na kwa kupitia maombi (Ne. 1:2-4).  Aliokoa rasilimali kwa

ajili ya mradi kutoka kwa mfalme Artashasta (Ne. 2:7-9). Kihekima alifanya watu kujenga upya sehemu ya ukuta karibu sana na nyumbani kwao (Ne. 4:22-23).

Kuhamasisha Wayahudi Yerusalemu kuliletea tendo la zaidi ya mtu mmoja na kwamba matokeo yalikuwa zaidi ya jumla ya sehemu. Ukuta ulikamilishwa katika siku 52, kiharaka vya kushangaza, kuweka hofu ndani ya hao wa mataifa wanaowazunguka (Ne. 6:15-16). Watu wa Mungu wanapoungana na kufanya kazi kimkakati kukamilisha mpango wa Mungu, Mungu anabariki katika njia ya kushangaza.

### B. Barnabas

Jina la Barnabas ilikuwa Yusufu, lakini kwa sababu alitumia kipawa chake cha kutia moyo kiufanisi sana, mitume walimwita "Barnmaba", ikiwa na maana "mwana wa faraja." Pia alikuwa mkarimu na kutoa kifedha kwa kazi ya Bwana huko Yerusalemu (Matendo 4:36-7). Barnabas alikuwa na haja kuona injili ikiendelea ulimwenguni kote. Alihudumu kwenye kanisa la Antiokia na kisha kufanya kazi kama mpanda kanisa Kipro na Asia ndogo.

Mchango wa Barnabas mkubwa kwenye kuendelea kwa injili ilikuwa kuhamasisha kwake kwa mtume Paulo kwenye huduma yenye ufanisi. Baada ya kukata shauri kwa Paulo njiani dameski, Paulo alikwenda Yerusalemu na kujaribu kujiunga na wanafunzi, ambao, walikuwa na mashaka kama alikuwa mwanafunzi kweli, tunamuogopa. Lakini Barnabas aliamini katika nguvu ya Mungu inayobadilisha katika maisha ya Paulo. Akihatarisha heshima yake mwenyewe na umaarufu, usalama wa waumini Yerusalemu, Barnabas alimleta Paulo kwa mitume. Barnabas alielezea jinsi Bwana alivyomtokea Paulo na jinsi Paulo alivyohubiri injili bila hofu Dameski (Mdo 9:26-31). Kufuatana na kudhihirisha kwa Barnabas, Paulo alikubalika kwa mitume.

Baada ya kanisa kuanzishwa Antiokia, Barnabas, akiona nafasi kubwa na kuhitaji vipawa vya Paulo, alikwenda Tursis na kumrjeza kwenye kanisa la Antiokia. Paulo akawa mmoja wa viongozi wa kanisa hilo na kutoka kule akavurumisha huduma yake ya kupanda kanisa kote Kipro na Asia Ndogo (mdo 13:1-30. katika yote haya, Barnabas alimhamasisha Paulo ili kwamba Paulo afanye sehemu yake katika kuendeleza ufalme. Fikiria kama Barnabas asingechukua jukumu la mhamasishaji. Makanisa mengi yasingekuwa yamepandwa, nyaraka nyingi za Agano Jipya zisingekuwa zimeandikwa. Unajua Paulo anayehitaji kutiwa moyo na kuhamasishwa?

### C. Paulo

Wazi wazi mtume Paulo alikuwa na kujitolea kwa hali ya juu kwenye kuhamasisha kanisa. Paulo alihamasisha makanisa mengi ya Masedonia, na Akia kutoa kwenye kanisa la Yerusalemu wakati wa mda wa kuhitaji (Rum 15:25-27). Katika nyaraka zake, Paulo mara nyingi alifundisha juu ya vipawa vya kiroho (Rum 12, 1Co 12, Efe 4) na kuyafanya makanisa kuwa macho kwenye umaarufu waliokuwa nao wenyewe kufanya kile Mungu anachotaka (1Kor 1:4-9, Rum 15:14).

Paulo alihamasisha wengine wengi katika kufanya wito wa Mungu kwake. Paulo alimfunza Timotheo, alimtia changamoto kiujasiri kufanyia kazi vipawa vyake vya kiroho na kumuelekeza kuwahamasisha wengine (2Tim 2:2). Timotheo, angekuwa, ndiye ambaye angehamasishwa na Paulo. Safari ya mwisho ya kimishenari ya Paulo inaonekana kuwa safari ya kufundisha/kufuasa/kuhamasisha ambayo tunasoma watu saba waliosafiri na Paulo, wengi wao wakijifunza kutoka kwake (Mdo 20:4). Katika nyaraka zake, Paulo anamtaja Epafura, Dema, Achipas, Tito, Foibe na wengine wengi. Katika Warumi 16, Paulo anasalimia watu 27, wengi wao aliowavuta au kwa njia fulani kuwawezesha katika huduma, akitoa udhihirisho zaidi kwa mtandao wa watu aliowahamasisha Paulo katika kusafiri kwake.

## IV. TABIA ZA MHAMASISHAJI MFANISI

Kuhamasisha hakutokei kama ajali. Kunachukua watu ambao hasa ni wazuri katika kuhamasisha wengine. Watu hawa, wahamasishaji, wanaunda hali ili kwamba kanisa kiasili litakubali maono, kuyaombea yatokee, kufunza na kutoa viongozi na wafanya kazi. Wanakuwa na tabia zifuatazo:

### A. Maono

Wahamasishaji wana maono kwa ulimwengu. Wanasaidia watu wengine wanaoweza kuona ugumu kuangalia katika mahitaji yaliyopo yanayoonekana, kuwatia moyo kuamini kwamba Mungu ana mipango mikubwa kuliko ambavyo wanaweza kudhani. Baadhi ya maeneo hayajahamasishwa kwa sababu makanisa ya mtaa yanakosa maono. Katika hali kama hiyo, mara maono ya Mungu yanapotangazwa inaweza kuwa kilio cha kujirudi au wito kwenye utendeji unaopelekea kwenye kuhamasisha.

### B. Imani na Kutia Moyo

Wahamasishaji ni watu wa imani. Imani maana yake ni kuangalia kupita hali halisi iliyopo kwa kile Mungu anachoweza kufanya. Kama imani inahamisha milima, haiwezi tena kuamsha mwili wa Kristo kujiunga na mwendo wa Matendo 1:8 na kufanya lengo la Mathayo 28:18-20? Imani inamwamini Yesu aliposema kwamba angelijenga kanisa lake. Mtu wa imani atakuwa na shauku kwa ajili ya kanisa.

Imani ya mhamasishaji inagusa njia anayowatenda wengine. Kama Barnabas, “Mwana wa kutia moyo”, wahamasishaji wengi wana vipawa vya kutia moyo. Wanaweza kuona kupitia vipingamizi na kukatishwa tamaa na kukazania kwenye vitu vya juhudi. Wahamasishaji wanawasaidia wakristo kutambua kuwa wao ni maalumu kwa sababu ni wa Mungu, kwamba Mungu amewajalia vipawa kwa ajili ya huduma kwa wengiene, na wanaweza, kwa neema ya Mungu na kupitia nguvu zake kufanya tofauti katika ulimwengu.

### C. Mguso

Wahamasishaji ni watu wa mvuto na wanawekeza mvuto huu kuona kusudi la Mungu linaendelea. Watu wanawasikiliza na kuwaitikia wao kwa sababu wanasadikika—wana sifa njema kanisani, moyo wa kitumishi na uzoefu wa huduma. Wahamasishaji wengi ni watu wa watu na wana uwezo wa kipekee kukumbuka majina, nyuso na uwezo wa watu waliokutana nao kwa mda mfupi tu. Kwa hiyo wanaweza kuunganisha watu kwenye rasilimali na nafasi ambazo zinaweza kusaidia kuendeleza ufalme wa Mungu.

> Wahamasishaji ni watu wa mvuto na wanawekeza mvuto huu kuona kusudi la Mungu linaendelea.

## V. MIFANO YA UHAMASISHAJI

Kanisa la mtaa linahamasishwa wakati watu katika kanisa hilo wanakamata maono kwa ajili ya kuinjilisha waliopotea na kisha kutendea katika maono hayo. Kuhamasisha kunakusudia katika mioyo ya watu—kuwasaidia kuona ulimwengu katika macho ya Mungu. Kuhamasisha kwingi kunatokea kwenye ngazi ya –mzizi, miongoni mwa wajumbe wa kusanyiko.

Hapo chini ni baadhi ya mawazo rahisi ya kuhamasisha wajumbe wa kusanyiko la mtaa kuwasaidia kukamata maono ya kufikia ulimwengu kwa injili. Haya hayachoshi, lakini badala yake, yameorodheshwa kutia moyo kufikiri kwako. Unaweza kupata mawazo mengine yako mwenyewe.

### A. Maombi ya Umoja

Moja ya njia muhimu za kuhamasisha watu kwa ajili ya kuinjilisha ulimwengu ni kuwafanya kuomba pamoja. Takwimu za ramani za utafiti zinaweza kutia moyo maombi maalumu kwa watu wasiofikiwa na maeneo katika taifa lako mwenyewe na ulimwenguni kote. Watu wanapoanza kuomba na kujifunza kuhusu waliopotea, watataka kuhusika katika kuwafikia watu waliopotea. Kama ilivyotajwa katika masomo mengine, maombi ya kutembea na maombi ya pamoja vinaweza pia kuwa zana yenye manufaa katika kufata Roho wa Mungu kugusa mioyo ya watu na kuwapa mzigo kwa waliopotea.

**Mfano**

Kila wiki katika mkutano wa maombi, mtu mmoja angeweza kushirikisha taarifa ndogo kuhusu nchi maalumu au kundi la watu na wanaweza kutumia mda kuombea injili kupenya kwenye mioyo na akili za watu hao. Wangeweza kuomba kwa ajili ya wamishenari kutumwa sehemu hizi kwa watu wasiofikiwa na kwa makanisa kupandwa miongoni mwao. Kundi hili la maombi linaombea kwamba Bwana angeweza kutuma kutoka wajumbe wa kanisa lao timu ya kupanda kanisa kufanya kazi miongoni mwa kundi la watu wasiofikiwa. Walipoomba kwa ajili ya makundi ya watu wasiofikiwa, Bwana alilipa kundi hili mzigo maalumu kwa watu wa Kezaki wa Asia ya Kati. Kati kati ya mda wa kipindi cha miaka miwili, wajumbe watatu wa kikundi hicho cha maombi waligeuka kuwa wamishenari huko Kezaki. Wajumbe wa kusanyiko kisha waliririthi watu wa Kezaki kama mkazo maalumu wa kufikia na kuanza kutuma timu za mda mfupi za wafanya kazi madaktari, wafanya kazi wa ujenzi, wafanyakazi wa watoto, wanamziki na wafanya biashara Kazakstani. Hatimaye, kanisa lilituma timu ya upandaji kanisa kufanya kazi Kazakstani ya magharibi. Kundi la maombi la mwanzo limeshayeyuka na kundi kubwa la watu sasa linakutana kila mwezi kuomba kwa ajili ya watu wa Kazaki.

### B. Shule ya Jimapili ya Watoto/Vipindi vya Vijana

Kama tunataka watoto wetu kuwa na moyo kwa ulimwengu na kuhusika katika kazi ya ufalme wa Mungu, tunatakiwa kuwapa nafasi ya uzoefu wa hilo wakiwa bado watoto. Watoto ni kitu muhimu cha kuhamasisha makanisa kwa kuinjilisha ulimwengu. Mara nyingi wanakuwa kiungo cha familia ambazo hazijaokoka. Watoto wanaokua wakiwa wameimarika katika kujitoa kwa Bwana mara nyingi wanatumiwa naye kwa njia za ajabu wakiwa wakubwa.

Mziki, maigizo, kutembelea wamishenari, kushika jukumu, na huduma za jumuia zote zinaweza kutumika kufundisha watoto kuhusu ulimwengu na upendo wa Mungu kwake na haja ya kuwafikia watu waliopotea. Wahamasishaji na viongozi wa kanisa wanatakiwa wapeleke walimu wao wa shule ya jumapili na wafanya kazi wa watoto kwenye mikutano na semina wanapoweza kupata rasilimali na mafunzo ya kufundisha watoto kuhusu kuinjilisha ulimwengu. Mara nyigi, kurithi familia ya kimishenari ya kuombea, kuwasiliana nao, na kukusanya pesa kwa ajili ya mradi maalumu kunaweza kusaidia watoto kuhusika katika kuinjilisha ulimwengu vilevile kupata kuonja kidogo maisha ya umishenari.

Moja ya njia bora za kuwapa vijana moyo kwa ulimwengu ni kuwafanya kuhusika katika huduma kivitendo. Viongozi wa kanisa wanaweza kutoa nafasi kwao kuhusika kwenye huduma za jumuia, kama vile kufanya kazi katika kituo cha kulea watoto yatima, kuwasaidia wazee, wasiojiweza, wakimbizi wa ndani, au aina nyingine ya huduma za jumuia. Nafasi hizi zinawapa vijana nafasi ya kuangalia mbali na mahitaji yao wenyewe na matakwa na kukuza moyo kwa watu wengine. Timu za vijana zinaweza kiumaarufu kusaidia timu za kupanda kanisa kupitia mziki, ngoma na kutumia tu mda kushirikisha injili kwa vijana wasiookoka katika eneo ambapo kanisa lako linajaribu kupanda kanisa binti. Mikutano ya vijana kuombea shule zao na wanafunzi wenzao wasiookoka pia ni njia yenye ufanisi ya kuwasaidia kuona kwamba Mungu anaweza kuwatumia kama mawakili wake shuleni.

**Mfano**

Mfano wa hili ulitokea mwaka 1992. Kikundi cha maigizo kutoka Uholanzi kilikuja Hungari kusaidia timu ya uinjilisti wa mda mfupi waliokuwa wanasaidia kanisa la Baptisti kwa uinjilisti. Kwenye timu ya uinjilisti kulikuwa na wanafunzi wawili kutoka kwenye chuo cha mageuzi cha walimu waliokamata maono ya kuanzisha kundi lao la maigizo. Walifundisha wengine saba na kuanza kuigiza katika makanisa yao. Kupitia huduma yao watu kadhaa waliokoka na kujiunga na kikundi. Katima miaka mitatu iliyofata, 20 walifundishwa na kushiriki kwenye kikundi cha maigizo. Wote hawa 20 sasa ni wajumbe hai wa makanisa ya mtaa na watano wanahusika katika kazi ya umishenari kikamilifu.

### C. Uhamasishaji Watu Wazima

Katika mwaka 1722 Moraviani Brethren, kwenye ukingo wa kumalizika kutokana na mateso makali, walipata uhuru wa kuabudu na kukua kwa mali ya kata ya Ujerumani iliyoitwa Nicolaus Zinzendorf. Kwenye msingi wa mapatano yanayosisitizia umoja, maombi, umuhimu wa kukubalika na kusamehe miongoni mwa waumini na kipaombele cha uinjilisti, Roho wa Mungu alilitia nguvu kundi katika mwaka 1727 kwenye harakati za kwanza za maisha ya wakati huo. Kufikia 1800 harakati hizi zilikuwa zimetuma wamishenari karibu 1,000 kwenye kila bara la ulimwengu wakiunda makusanyiko kila mahali walipokwenda. Ilikuwa mfano wao ambao ndio uliomumwagia William Carey mwaka 1791 maono ya kuchukua ujumbe wa injili Mashariki ya Mbali, akiongoza harakati za misheni za nguvu katika karne ya kumi na nne.

Kumbuka kwamba kuhamasisha maana yake ni *kuweka wazi na kuandaa watu katika utayari wa kushiriki mahali ambapo wanaweza kuchangia vema zaidi kwenye tendo la wote na lengo la wote.* Watu wazima lazima washawishike juu ya umuhimu wa kuinjilisha ulimwengu (tendo la wote) na lazima waone jinsi wanavyofaa katika picha hiyo. Uhamasishaji unatakiwa uwe kwa njia ya mafundisho ya kibiblia kwenye asili na kusudi la kanisa, Utume Mkuu, na jukumu la waumini katika kuinjilisha ulimwengu. Kwa nyongeza, historia za wamishenari na masimulizi ya kuenea kwa injili ulimwenguni yanaweza kuvutia na kutia hamasa watu kushiriki katika uinjilisti na upandaji kanisa.

La mwisho, kuwaelekeza watu nafasi za kushiriki katika uinjilisti na shughuli za upandaji kanisa kunaweza kuwasaidia kutafuta nafasi yao katika mavuno ya Mungu.

> **Mfano**
>
> Kanisa moja la mtaa lilimsaidia mkimbizi mmoja wa Kambodia kutafuta nyumba, vifaa vya ndani, na kazi. Mkambodia alipouliza alipe kwa ajili ya wema wao, kanisa lilisema, "njoo kwenye ibada yetu." Mkambodia alikwenda, lakini kulikuwa na tatizo—kutokujua lugha, kwa upole alikaa kwenye viti, bila kuelewa chochote. Katika kuitikia kwenye tatizo hili, kanisa lilianda tafsri ya wakati uleule ili kwamba mkambodia aweze kushiriki kwenye ibada. Wanaoongea kivitenamu, kichina, kisipanishi pia waliomba na wakapata tafsiri. Wakati viziwi walipohudhuria ibada kanisa liliandaa kutafsiri kwa lugha ya vitendo. Kupitia mwingiliano wa watu wa tamaduni kadhaa, wajumbe wa kusanyiko walipata moyo kwa ulimwengu. Leo, kanisa hili limetuma zaidi ya familia zaidi ya ishirini kwenye umishenari wa ulimwengu na kuchangia kwa nguvu kwenye msaada wao wa kifedha!

## SULUHU

Kuhamasisha ni kazi ya kiroho. Wahamasishaji wafanisi wana maono, imani, mvuto. Kuna watia moyo wanaosaidia watu kutambua umaarufu wao waliopewa na Mungu. Wanatamani kuona utukufu wa Mungu ukiijaza dunia. Wanaendeleza sababu ya Kristo ulimwenguni na siyo mambo yao waliyoandaa.

Harakati za kupanda kanisa hazitafanikiwa bila uhamasishaji wa ufanisi. Unasaidia kukazania na kutoa rasilimali zilizopo kwenye kazi ya kuinjilsiha ulimwengu—kuanzisha makanisa mapya miongoni mwa watu ambao hawajafikiwa katika taifa na pia katika mataifa mengine. Wakati mwili wa Kristo unapokuwa haukuhamasishwa—hauwezi kushindana kwa nguvu zote.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kwa nini kuhamasisha ni muhimu?
- Unafanyia kazi vipawa vyako vya kiroho kama alivyofanya kwa shauku Barnabas?
- Unamjua yeyote anayetaka kumtumikia Bwana ambaye anaweza kuhamasishwa?
- Unamjua yeyote anayeweza kuwa muhamishaji mfanisi?
- Ni baadhi ya njia zipi zingine maalumu ambazo unaweza kusaidi kuhamasisha watu katika kanisa lako kwenye uinjilisti na upandaji kanisa?
- Ni sifa zipi za muhamasishaji unazokamilisha vema? Ni ipi ni ngumu zaidi kwako?
- Jinsi gani unaweza kuhamasisha kanisa lako kuendeleza injili, kuzaliana kwa kupanda makanisa mapya?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Anza kumtumikia Mungu katika kujaliwa kwako vipawa kuelekea kuendeleza injili.
- Muulize Mungu kuweka yeyote katika moyo wako anayetaka kumtumikia Bwana na anza kufanya nao urafiki na kuwahamasisha.
- Orodhesha hatua tatu unazoweza kuchukua kwenye kuhamasisha kanisa lako kwa ajili ya uinjilisti na upandaji kanisa.

MAONO YA KUM

SOMO LA 15

# Hatua Zinazofata

## UPANDAJI MAKANISA MAPYA

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kusaidia mpanda kanisa kufikiria juu ya maamzi kuhusiana na huduma ya mbeleni inayomkabili, timu ya upandaji kanisa na kanisa mpya lililopandwa.

☞ **Wazo Kuu**

- Wakati kanisa linapokuwa limepandwa viongozi wanatakiwa kufikiria upya jukumu lao katika harakati za upandaji kanisa.
- Makanisa mapya yaliyoundwa yanatakiwa kuelewa majukumu yao kwenye harakati za upandaji kanisa.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshirikli anatakiwa…

- Kuelewa uchaguzi kwa ajili ya huduma ya mbeleni kwa ajili yake, timu ya upandaji kanisa, na kanisa mpya lililopandwa.
- Kufanya kazi na timu ya kupanda kanisa kuhamia katika hatua nyingine inayofata ya huduma.
- Kushiriki katika kusaidia kanisa jipya lililopandwa kutambua jukumu lake la kutuma nje wapanda kanisa kupanda makanisa binti.
- Fikiria kushiriki kuwezesha wengine kuelekea harakati za upandaji kanisa katika mji wake au mkoa.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili ni bora likifundishwa kama kipindi cha majadiliano. Shirikisha kutoka katika uzoefu wako jinsi ulivyokabidhi huduma kwenye kanisa lililopandwa. Ruhusu wafunzwa kuuliza maswali na kushirikisha yanayowatinga wanayokabiliana nayo katika hali yao ya huduma.

### UTANGULIZI


Umefikia sasa mwisho wa mafunzo ya mpanda kanisa. Pengine kwa sasa kanisa limeshaanzishwa au mara moja litaanzishwa. Hii ina maana lengo muhimu limefikiwa. Kwa jinsi hiyo, hii ni hatua moja katika utaratibu. Lengo la Utume Mkuu siyo upandaji wa *kanisa moja,* lakini badala yake *kuzidishwa kwa makanisa* ulimwenguni kote, kwa kila mmoja wao akifanya wafuasi ambao ni wakamilifu katika kumtii Bwana.

Somo hili linajadili yote jukumu la kanisa mpya lililopandwa kwenye harakati za upandaji kanisa na vilevile uchaguzi wa huduma ambapo timu ya upandaji kanisa inahitaji kufikiria kama sehemu ya hatua ya huduma inayofata katika kufanyia kazi kuelekea harakati za upandaji kanisa kwenye mji huo wa timu au mkoa.

### I. MZUNGUKO WA UPANDAJI KANISA

Mzunguko wa upandji kanisa (Kielelezo 15.1) kinaelezea kuendelea kwa asili kwa kazi yetu. Wakati mtu pekee anapoamini katika Kristo, au kutarajiwa kuwaleta wengine kwa Bwana. Kanisa linapokuwa limepandwa, vile vile linatarajiwa kupanda makanisa mengine. Kazi haitamalizika mpaka wote wafikiwe.

**Kielelezo 15.1 Mzunguko wa Upandaji Kanisa**




## II. WAJIBU WA KANISA MPYA: KUZIDISHA—UPANDAJI MAKANISA BINTI

Kanisa linapofikia lengo lake la kwanza la kuanzishwa, linakuwa na maamzi ya bila mzaha ya kufanya. La kwanza linahusu jinsi kanisa mpya litakavyofikia nje na kuanzisha kanisa moja au makanisa mengine. Kutumaini, kupitia kazi yako, kanisa mpya lililopandwa lina "mamba"—liko tayari kufanya kazi ya kupanda makanisa mengine. Tunapoelewa kusudi la Mungu, maono yanatakiwa yawe harakati za mbali kwa upandaji wa kanisa yakipanuka katika maeneo ya kijografia na /kwa makundi yote ya watu.

Kanisa jipya lililopandwa lina jukumu la nafasi ya kushika katika kutimiza Utume Mkuu katika jumuia yake, jumuia za karibu ambazo hazijafikiwa, na katika sehemu nyingine za ulimwengu (angalia Somo la Maono ya KUM la 13, "Maono na Kupiga Darubini"). Hili linahitaji uongozi wa kanisa mpya lililopandwa kuandaa kusanyiko kwa upandaji wa kanisa, kuinua, na kutuma wapanda kanisa na wamishenari kutoka katika wajumbe wake, na kufanya kazi na makanisa mengine ya mtaa kuwasaidia kutimiza agizo lao walilopewa na Mungu la kuinjilisha waliopotea.

### A. Weka Maono Kuwa Hai

Maono yaliyoshawishi kanisa mpya lililopandwa yanaweza kufa nalo mara kanisa mpya lililopandwa linaporidhika. Lakini kuuliza swali hilo tena "Nini Mungu anataka kufanya miongoni mwa kundi la watu hawa au katika eneo hili?" kunaweza kuamshaha haja ya makanisa mengi. Tunajua kuwa Mungu anataka wote kusikia injili. Makanisa yanayojua wito wao wanajitolea katika upandaji makanisa miongoni mwa eneo lote, mataifa, na makundi ya watu.

Unapoangalia zaidi ya kanisa la mtaa unaona picha kubwa. Maono ya Paulo kufikia jimbo la Asia yalikuwa ya kijografia (Matendo 19:10). Unaweza pia kuwa na maono ya kuwafikia watu, kundi la kabila. Katika Wagalatia 2:7-8, tunaona kwamba Petro alifanya kazi na Wayahudi na Paulo na Mataifa. Katika Warumi 11:13 paulo kwa ujasiri anatangaza, "Ni mtume kwa Mataifa." Ni eneo gani Mungu amekuita kulifikia? Ni makundi gani ya watu wanaoishi katika eneo hilo lazima wafikiwe kwa injili?

Uongozi wa kanisa unahitaji kuendelea kuweka kusudi la kanisa mbele ya watu, na nafasi na jukumu la kanisa katika kutimiza Utume Mkuu. Uongozi wa kanisa unapoandaa waumini kwa kazi ya huduma watakua kiroho na kivitendo, wakiendeleza ujuzi wa huduma na maono. Hii inatakiwa ipelekee kwenye huduma za kufikia miongoni mwa wasioinjilishwa.

Injili itakuwa na mguso, kwa mda mrefu, wakati mwili wote unaposonga mbele pamoja. Baadhi ya watu wanashika maono kwa haraka zaidi kuliko wengine. Hao walio na maono wanatakiwa kuendelea kutia moyo wengine kuendelea kusonga mbele. Hao wanaosonga mbele polepole wanaweza kuongeza usitahimilivu kwenye harakati. Wanapoelewa umuhimu wa upandaji kanisa katika kuona Utume Mkuu unatimizwa, hawa "wanaofikiria utaratibu" wanaweza kusaidia kuhakikisha kwamba kila hatua ya mbele ni ya bila mzaha na yenye mshindo. Inatakiwa aina zote za watu wanaofanya kazi pamoja ili kanisa kuendelea kufikia nje katika maeneo mapya kwa injili.

Fanya kazi na kusanyiko lako kufikiria jukumu la kanisa lako ulimwenguni. Tafsiri Yerusalemu yako, Yudea, na Samaria na miisho ya dunia (tazama Somo la Maono la 13, "Maono na Kupiga Darubini"). Tia moyo wajumbe wa kusanyiko kujifunza kuhusu sehemu tofauti za ulimwengu, hitaji la uinjilisti, na upandaji wa kanisa, na kazi ya wamishenari. Kama una darasa la jumapili, watie moyo walimu kuhusisha masomo kuhusu ulimwengu na maisha ya umishenari kama sehemu ya mtaala.

### B. Tuma Nje Timu za Upandaji Kanisa

Mitindo wa upandaji kanisa unaotumia kupanda makanisa mengine utaonyesha jinsi utakavyofundisha wafanya kazi, kufadhili mradi, kutayarisha msaada wa nje, n.k. maono ya KUM ziada 3A, "Mitindo ya Upandaji Kanisa" katika Mwongozo wa kwanza inafupisha njia kadhaa ambazo kusanyiko lako linaweza kupanda makanisa mengine,

Kama umekuwa ukitumia mtindo wa kikundi kiini, kisha upandaji wa kanisa binti ni rahisi. Kikundi kiini kinapozidi, kinaweza kutuma nje kundi jipya lenye nguvu ambalo linaweza, chini ya uangalizi wa uongozi, mpito kwenye kanisa jipya ambao unafikia watu katika eneo tofauti linalolengwa. Baadhi ya makanisa yanakuwa na karibu vikundi kiini 15 hai na kila mara vikundi kiini vipya vitano vinapoanza wanavitumwa nje chini ya uongozi wa kikundi kiini (ikiwemo kiongozi wa kanda) kama kanisa jipya.

*Mapendekezo yafuatayo yanaweza kusaidia karibu mtindo wowote:*

1. *Ombea na Tafuta hao ambao Mungu anawaita kwenye upandaji kanisa.*

   Maombi ni zana mojawapo yenye nguvu Mungu atakayotumia kuamsha maono miongoni mwa watu wake kwa ajili ya huduma kwa ulimwengu. Kanisa mpya linatakiwa kuomba kwa ajili ya kuinjilisha ulimwengu na hasa hasa kwamba Mungu atainua watenda kazi kwa ajili ya mavuno kwa kazi ya upandaji kanisa.

   Kanisa ni chombo cha msingi cha Mungu kwa kuinjilisha ulimwengu na upandaji kanisa ni kazi inayohusu kanisa lote. Kwa hiyo, Tunaweza kutarajia kwamba Mungu atataka kutenga wajumbe kutoka katika kusanyiko letu wenyewe kwa kazi ya upandaji kanisa kama alivyofanya tu katika kanisa la kwanza (Matendo 13:1-3). Tafuta watu kanisani kwako wanaohisi kuwa Mungu anawataka kuhusika katika upandaji wa kanisa. Mtume Paulo mara nyingi alizungumzia juu ya wito wake (Rum 1:1, 1Kor 1:1,, 2Kor 1:1, Gal 1:1, 15-16). Ufahamu huu " wa kuitwa" na Mungu kunamfanya mtu kuendelea kuhudumu wakati kunapokuwa hakuna sababu ya makusudio ya kuendelea au wakati hisia zinaposema "ninaacha!"

   "Wito" huu kwenye huduma ni pamoja:

   - Maono yanayokua kwa ajili ya huduma;
   - Kujaribiwa kwa tabia ya mtu, maono na huduma;
   - Kuthibitishwa kwa mtu na kanisa la mtaa, wazee wa mtu, timu ya mtu, na wapanda kanisa;
   - Kuwezesha kwa Roho Mtakatifu kuweka wito kwenye kutenda (1Tim 4:15, Efe 3:7, Kol 1:28-29).

Kwa kuongeza juu ya sifa za hapo juu, angalia kwenye utayari wa kijitoa kwa ajili ya injili. Upandaji kanisa ni kazi ya mstari wa mbele wa mapambano kwa ajili ya ufalme wa Mungu. Wengi wa mitume wa kwanza walikufa kama wafia imani. Wapanda kanisa watafanya kujitoa. Hili halimaanishi mara zote kufa kifo cha kufia imani, kuvunjika kwa jahazi au kufungwa, lakini ingeweza kumaanisha kama kueleweka vibaya, kuachilia faraja za mtu binafsi, n.k. Mtume Paulo alizungumzia juu ya utayari wa kuachana na haki za mtu ili kuwafikia watu kwa ajili ya Yesu (1Kor 9).

2. *Onyesdha mahali pa kutuma nje timu ya upandaji kanisa.*

   Omba na tafuta uongozi wa Bwana wapi unatakiwa upeleke wapanda kanisa na timu ya upandaji kanisa. Tafiti yote eneo la kijografia na makundi ya watu wanaoishi katika eneo linalolengwa. (Tazama somo la maono ya KUM la 4, "Kanuni za Utafiti (kupiga ramani ya kiroho)" katika Mwongozo wa Kwanza.) Tumia matokeo ya utafiti wako kuonyesha mahitaji ya mafunzo ya wajumbe ya timu ya wapanda kanisa, ukihamasisha kusanyiko kwa ajili ya maombi, msaada wa kifedha, na kuanzisha uinjilisti na mikakati ya upandaji kanisa kwenye eneo hilo linalolengwa.

3. *Hamasisha rasilimali za kanisa kwenye kuhusika katika upandaji wa kanisa.*

   Upandaji makanisa unatokea vyema wakati rasilimali za kanisa zimehamasishwa kwa ajili ya tendo hilo. Rasilimali hizi ni pamoja na watu watakaokuwa katika timu ya upandaji kanisa, fedha za kusaidia timu ya upandaji kanisa, vifaa, na usafiri unaohitajika kwenye huduma ya upandaji kanisa, na wasaidizi wa mda mfupi. Pata watu wenye bidii kwenye jengo la kanisa iwezekanavyo, hata kwa mda wa vipindi vifupi. Wajumbe wa kusanyiko wanaweza kuhudumia timu ya upandaji kanisa kwa maombi ya kutembea, mziki, shughuli za kiuinjilisti na huduma za kijamii. Hii haitasaidia tu kubeba mzigo wa timu ya kupanda kanisa, lakini itasaidia kukuza maono ya upandaji kanisa na kuwafikia waliopotea miongoni mwa wajumbe wa kanisa linalotuma.

4. *Funza, linda na shauri timu ya upandaji kanisa.*

   Onyesha mahitaji ya ufundishaji wa timu ya upandaji kanisa. Wanahitaji mafunzo ya wapanda kanisa, mafundisho ya mwingiliano wa tamaduni, au mafunzo ya kilivu? Mengi ya mafunzo yanayohitajika yanaweza kupatikana si kawaida, lakini baadhi ya mafunzo ya kawaida yanaweza pia kuhitajika kutegemeana na mahitaji ya watu kwenye eneo linalolengwa. Mara timu inapokuwa imepelekwa kwenye mazoezi, ni muhimu kwamba wanakuwa na wa kuwatembelea kila mara kutoka kwenye uongozi wa kanisa wenye vipawa vya uchungaji. Hii itasaidia kuifanya kanisa na timu ya upandaji kanisa kubakia ikiwajibika kwa kila mmoja. Hii itaipatia timu msaada wa kiroho na wa kivitendo katika kufanyia kazi maswala kati ya watu na yanayowasumbua ambayo yataibuka timu inapohudumu na kufanya kazi pamoja. Kwa nyongeza ya uangalizi wa kichungaji, Ni muhimu kwamba timu ya upandaji kanisa inakuwa na mshauri au washauri kadhaa wanaoweza kuisaidia timu kufanya kazi katika hatua tofauti za utaratibu wa upandaji kanisa.


## III. WAJIBU WA TIMU YA MWANZO YA UPANDAJI KANISA: KUANZA UPYA—UPANDAJI MAKANISA MAPYA

Mpanda kanisa aendelee kufanya kazi kama "mtume" au "mpelelezi" mpanda kanisa kwa kuendelea kupanda kanisa jingine, au aendelee kukaa na kuchunga kanisa mpya? Jibu litategemeana kisehemu na vipawa vyake. Ameitwa kuwa mchungaji au mtume/mpelelezi mpanda kanisa? Huduma ya kichungaji inajizinga yenyewe kiufalme kwa kazi na watu wa kanisa moja la mtaa. Mitume/wapelelezi wapanda kanisa ni wainjilisti wa mstari wa mbele wanaohama kutoka sehemu hadi sehemu na wanaweza kuanzisha makanisa kadhaa wakati wa maisha yao. Uamzi huu kuhusiana na huduma ya mbeleni vile vile inategemeana na kuhisi mapenzi ya Mungu kwake. Hii inaonyeshwa kupitia maombi.

Fikiria uwezekano ufuatao:

### A. Timu ya Upandaji kanisa Inasonga Mbele

*Wapanda kanisa wanakabidhi uongozi wa kanisa kwa wengine na kisha kurudi kwenye kanisa linalotuma au kuendelea kwenda kupanda kanisa kwenye eneo jingine.*




Wakati wapanda kanisa wanapokuwa na kipawa cha utume watataka kupanda makanisa zaidi. Wanatakiwa watiwe moyo kufanya hivyo kama ni mapenzi ya Bwana. Mpelelezi mpanda kanisa, kama mzazi wa kiroho, anashirikisha katika wajibu kwa maisha ya kiroho ya hao walio sehemu ya kanisa jipya na kwa hiyo lazima akuchukulie kuondoka bila mzaha. Kuanzisha kanisa na kuliacha kabla halijakomaa ni kama mzazi anayetelekeza mtoto mchanga. Mtume Paulo alikuwa na uhusiano uliokuwa unaendelea kwa makanisa aliyopanda—akiyaandikia barua, na kutoa ushauri wakati matatizo yalipoinuka. Pia mwishowe aliteua wazee walioongoza makanisa hayo mapya yaliyopandwa akihakikisha kwamba kulikuwa na uangalizi wa kuendelea wa kanisa. Hili linatakiwa liwe moja ya kufikria unapoamua hatua ya huduma inayofata kwa kundi.

Swali la utata kwenye uchaguzi huu "ni kwa nani uongozi wa kanisa utatolewa?" wapanda kanisa lazima waaandae kanisa kwa ajili ya uongozi ujao. Uongozi unaweza kupatikana pale pale kwenye kusanyiko jipya. Ni busara kwa kanisa mpya lililoanzishwa kuendeleza na kuandaa viongozi kutoka kwa hao waliowahi kuwa na sehemu fulani katika maisha ya kanisa kutokea mwanzoni. Au, kama mchungaji au kiongozi amechaguliwa kutoka nje ya kanisa, anatakiwa awe na kipawa kizuri cha uchungaji, vile vile na maono sawa na imani ambayo umeipandikiza kanisani.

Watu hawabadili utii unaowapasa kirahisi au kwa haraka. Lazima kuwe na kifungo kati ya uongozi uliochaguliwa na watu. Ni vizuri kuwa na mpango wa taratibu kupitishia uongozi mpya kwenye uhusiano ulioshikamana kuliko kusababisha mabadiliko ya ghafla ambayo yanaweza kuwa kama kuwatumbukiza ndani ya maji ya barafu ya baridi.

### B. Timu ya Upandaji kanisa Inabakia Kuchunga Kanisa Mpya Lililopandwa

*Mpanda kanisa anakaa katika kanisa mpya na kuwa mchungaji wa kanisa mpya.*

La msingi la kufikiri hapa ni "Mpanda kanisa ana vipawa vya kiuchungaji?" Kama aina ya kiongozi mvumbuzi anakaa kama mchungaji asiye na vipawa vya kiuchungaji, wajumbe wa kanisa wanaweza kushindwa kupokea virutubisho na kulishwa neno wanalohitaji.

Katika hali yoyote mara mlishaji anapompata kiongozi mvumbuzi anaweza kuendelea kukaa katika kanisa kusaidia kupangilia, kufunza na kuongoza timu mpya za upandaji kanisa kwenda nje ya kanisa. Kama kiongozi mpya mvumbuzi anaweza pia kwa usitadi kuchunga kanisa mpya vile vile, nafasi kuu zipo kuendeleza injili kupitia upandaji mwingine wa kanisa. Aina hii ya uchungaji kawaida haitachunga kanisa jipya tu lakini utaendeleza wapanda kanisa wengine na huduma ya upandaji kanisa kutoka humo humo kwenye kanisa mpya.

### C. Timu ya Upandaji Kanisa Inageuka Kuwa Timu ya Kuwezesha

*Wapanda Kanisa wanawezesha wengine kwa ajili ya upandaji kanisa katika eneo.*

> Kuwezesha maana yake kuwasaidia watu kuona wajibu wao katika kujaza miji, jiji, na mataifa kwa makanisa, na kuwaonyesha kwamba wanaweza kufanya hilo kadiri Mungu anavyowaonyesha ni kwa jinsi gani.

Kuwezesha kuna maana kuwasaidia watu kuona wajibu wao katika kujaza miji, jiji, na mataifa kwa makanisa, na kuwaonyesha kwamba *wanaweza kufanya hilo* kadiri Mungu anavyowaonyesha ni kwa jinsi gani. Kuwawezesha wengine ni mkakati wa lazima katika kuendeleza injili katika eneo lote. Hili ni pamoja na kutoa maono kwa upandaji kanisa na kisha kufunza, kuandaa, na kuhamasisha hao wanaowazia. Timu ya kuwezesha ni kundi la watu wanaofanya kazi pamoja kuwapa watu maono ya nini Mungu anataka kufanya kupitia wao na kisha kuwasaidia hao waliowazia katika kutimiza maono hayo.

1. *Chochea Maono*

   Nafasi ya timu ya kuwezesha ni kuendelea kushirikisha maono ya "Nini Mungu anataka katika eneno hili, mji, taifa au kundi la watu Kuchochea maono (au kutupa maono) ni pamoja na kuhubiri na kufundisha kwenye kusudi la kanisa, nafsi ya uongozi katika kanisa, na asili ya kazi ya Utume Mkuu. Makanisa na waumini wanatakiwa kuendelea kukumbushwa kuhusu vipaombele vya Mungu, haja na kiu ya kupatanisha watu waliopotea kwake mwenyewe. Watu wanapoitikia kwenye maono haya, timu ya kuwezesha kisha inahitaji kuweza kuwasaidia kutendea maono yao.

2. *Anzisha Juhudi za Maombi Zilizoandaliwa*

   Maombi yanaunga juhudi zetu kwenye juhudi za Mungu. Kazi ya kupanda kanisa ni kazi ya kiroho na inahitaji nguvu ya kiroho. Watu wanapoitikia kwenye maono ya kuona taifa lao, mkoa au mji ukijawa na makanisa, timu ya kuwezesha inaweza kuanza kuita watu hawa pamoja kuomba kwa ajili ya kutimizwa kwa maono haya. Hili linaweza kuwa watu wawili au watatu pekee au kundi katikati ya kanisa, watu kutoka makanisa tofauti walio na maono sawa au kanisa lote kuomba pamoja. Lengo ni kuwa na mzunguko uliopanuka wa watu wanaoomba kwa ajili ya upandaji kanisa.

3. *Funza na Shauri Watu kwa Ajili ya Huduma ya Upandaji Kanisa*

   Moja ya njia nzuri za kuwezesha upandaji kanisa miongoni mwa makanisa mengine ni kwa kanisa mpya lililopandwa kuwa kituo cha mafunzo kwenye eneo. Kwa kuendesha mafunzo, uongozi wa kanisa una nafasi ya kuvuta wengine kuelekea kwenye harakati za upandaji kanisa. (Tazama Maono ya KUM Somo la 16, "Mafunzo Kama Sehemu ya Harakati za Upandaji Kanisa.") Wapanda kanisa waliofunzwa wanatumwa nje na makanisa na madhehebu wanakotoka.

4. *Endeleza Upandaji kanisa wa Ushirikiano*

   Mara nyingi, makanisa ya mtaa yanajisikia kana kwamba hayana rasilimali za kuweza kufunza kikamilifu na kusaidia wapanda kanisa wenyewe. Lakini bado wanakuwa na jukumu na kuhitaji kushiriki katika kutimiza Utume Mkuu. Timu ya kuwezesha inaweza kusaidia makanisa kuunda ushirikiano na kwa pamoja kusaidia na kutuma wamishenari nje na wapanda kanisa kufanya kazi miongoni mwa kundi la watu maalumu au katika eneo maalumu. Hii inaruhusu hasa makanisa madogo kushiriki kikamilifu zaidi kwenye Utume mkuu kuliko ambavyo wangeweza peke yao.

## SULUHU

Mara kanisa mpya lililopandwa linapoanzishwa, lazima lifahamu nafasi yake kwenye harakati za upandaji kanisa. Linatakiwa liwe na haja ya kuzaliana lenyewe kupitia kufunza na kutuma nje wapanda kanisa kutoka kati kati yake, kupitia maombi kwa ajili ya kuinjilisha ulimwengu. Timu ya upandaji kanisa inapaswa kufanya uamzi kuhusiana na nafasi ya wakati wake ujao na mpito wa uongozi katika kanisa mpya lililopandwa. Ukuaji na Kuzidisha kwa kanisa mpya na kuhusika kwa timu kwenye harakati za upandaji kanisa ni fikira muhimu kwenye timu ya upandaji kanisa kuamua hatua yao ijayo ya huduma.

Kuwezesha ni njia ya ufunguo ya kusaidia kutia moyo harakati za upandaji kanisa. Timu ya kuwezesha ni kundi la watu wanaofanya kazi pamoja kuwapa watu maono ya kile Mungu anachotaka kufanya kupitia wao na kisha kuwasaidia hao wanaowazia kutimizwa kwa maono hayo. Nafasi yake ni kutupa maono, rasilimali, kufunza na kutia moyo waumini kwa kila njia kuweza kuhusika katika harakati za upandaji kanisa. Kuwezesha ni muhimu kwa upana wa eneo au upana wa taifa kwa harakati za upandaji kanisa kutokea.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni nafasi ipi katika kazi ya upandaji kanisa utaweza kuchukua?
- Je kanisa unalopanda lina maono ya kanisa binti? Kama siyo, ni hatua zipi utachukua kupitisha maono hayo?
- Elezea tofauti kati ya mpanda kanisa wa kitume/mvumbuzi na mchunguji kwa kuangalia wito na kujaliwa vipawa.

- Ni kujitoa gani utatakiwa kufanya kuona makanisa yameazishwa?
- Jinsi gani unaweza kusaidia wengine au katika utumaji wa kanisa lako au katika kanisa mpya kuwa wapanda kanisa?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Pamoja na timu yako ya upandaji kanisa na mshauri, omba na fikiria nini itakuwa hatua yako inayofata katika huduma.
- Gundua mmoja au wawili wapanda kanisa maarufu katika kanisa lako mpya lililopandwa. Tumia mda kuzungumza nao kuhusu maono yao na kuwashauri katika maandalizi ya kazi ya upandaji kanisa kama sehemu ya timu ya upandaji kanisa.

# KANISA

KANISA

SOMO LA 15

# Malezi ya Kanisa

## TOBA NA KUREJESHWA

**Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuweka mbele kanuni za kibiblia ambazo zinalinda malezi katika kanisa la mtaa.

**Wazo Kuu**

- Ingawa malezi ya timu ya kanisa hayapatikani katika Biblia, wazo limejadiliwa kiuwazi, na kanisa linatarajiwa kufata mipaka ya kiroho.
- Kusudi la malezi ya kanisa *kawaida* ni toba na kurejeshwa kwa muumini anayetenda dhambi.

**Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa kanuni za kibiblia zinazohusiana na malezi ya kanisa la mtaa
- Kujua jinsi ya kutumia kwa vitendo vifaa katika kuweka malezi ya kanisa.

**Ushauri kwa Wakufunzi**

Tambulisha somo hili kwa kuwafanya wafunzwa kushirikisha mashauri ya malezi ya au utaratibu amabao wanaufahamu. Epuka majadiliano ya mifano iliyotajwa hasa hasa ya malezi ya kanisa na dhehebu ya kimadhehebu au viongozi wa kanisa wanaoshughulikia maswala ya malezi. Acha mda mwishoni kujadili mchanganuo wa mambo mengi.

**UTANGULIZI**

Ingawa malezi katika kanisa ni wazo muhinu la kiroho, ni somo kuhusu nini kidogo kinachojulikana na hata hivo kidogo hicho kinatumika. Shuhuda zifuatazo kutoka kwa Mchungaji wa Kirumi zinaelezea hili:

> *"Kwa mara ya kwanza nilipoanza kufikiria somo “MALEZI KATIKA KANISA” ilionekana kwangu kama somo rahisi sana kwa sababu kanisa lilikuwa na uzoefu zaidi katika eneo hili. Lakini ilikuwa isiwe hivyo. Nilikuwa nikichukua Biblia yangu kiuhaba na kuanza kujifunza bila mzaha niligundua matatizo kadhaa kuhusiana na kisa hiki.*
>
> *Nilihisi kuwepo kwa hangaiko kati ya utamaduni wa dini yangu, na ujumbe wa maandiko; kati ya utamaduni wa kidini wa kanisa langu na mtindo wa kweli wa kibiblia. Nilihisi hangaiko katika kuanzishwa kwa maono ya wote kuhusu utaratibu wa malezi.*
>
> *Wakati nikijifunza maandiko, nilikusanya vifaa vya kutosha ambavyo vinagusia kisa hiki. La kunishangaza sikupata vifaa vyovyote ambayo kipekee viligusia malezi ya kanisa.*
>
> *Niliongea na wachungaji wengi na viongozi wa kanisa kujua falsafa yao katika eneno hili lakini nikakuta kanisa moja tu ambalo lilikuwa na falsafa yake iliyoandikwa. Makanisa mengi hayajisikii kama wako kwenye msimamo halisi wanapotakiwa kutumia kanuni za malezi na kushughulikia tatizo bila kuwa na hakika au kwa juu juu tu.”*

Kama anavyoelezea kaka yetu, kama malezi ya kanisa hayakugusiwa hasa hasa kwenye Biblia, kisha maswali kadhaa lazima yaulizwe:

- Malezi ya kanisa ni ya kibiblia?
- Nini malezi ya kanisa?

- Nini hatua za kibiblia ambazo kanisa lazima lichukue katika kutoa malezi kwa wajumbe?
- Nini malengo ya malezi ya kanisa?

## I. KANUNI ZA KIBIBLIA ZA MALEZI YA KANISA

Ingawa neno *malezi ya kanisa* halijatumika katika Biblia, ni agizo angalau katika vifungu vitatu vya Agano Jipya; 1Wakorintho 5, Mathayo 18, na 2Wakorintho 2. Vifungu hivi vinafundisha kanuni fulani kuhusiana na kufanya malezi ya kanisa ambayo yanatumika katika maisha ya kanisa la sasa.

### A. Malezi ya Kanisa ni Agizo la Kibiblia (1Wakorintho 5)

Kwa mfano, kanisa la Korintho kulikuwa na jambo la mwenzao aliyekuwa amehusika katika kuvunja maadili la ngono (v.1). Mtume Paulo aliliandikia kanisa, akitoa maelekezo juu ya jinsi ya kushughulika na mwenzao huyo:

- Kumuweka nje ya ushirika wao (v.2)
- Kumkabidhi kwa Shetani(v.5)
- Usikaribiane au kula naye au makaka wengine wowote waliokuwa amevunja maadili kingono, uchoyo, ukahaba, ulevi, au wadhalimu (v.11)
- Mfukuze mtu mbaya miongoni mwao (v.13)

Paulo pia anawaambia kusudi la vipimo hivi vya kimaadili: "…ili kwamba asili ya dhambi iweze kuharibiwa na roho yake iokolewe siku ya Bwana" (v.5).

### B. Malezi ya Kanisa Lazima Yafate Hatua Fulani (Mathayo 18)

Yesu alisema kwamba wakati mwenzetu anapotenda dhambi, tunatakiwa tufanyie kazi taratibu zifuatazo:

- Ya kwanza, nenda kwake kisiri na muonyeshe kosa lake. Kama anasikiliza, uhusiano umerejeshwa (v.15).
- Kama hasikilizi, chukua mashahidi wawili au watatu pamoja nawe na mkabiri (v.16).
- Kama bado hatasikiliza, liambie kanisa (v.17).
- Kama bado hatasikiliza kanisa, mfanye kama mtu wa nje (v.17).

*Tambua: baadhi ya tafsiri za Biblia zinaonyesha kwamba hii ni "dhambi dhidi yako." Lakini iwe dhambi iko kinyume na wewe kibinafsi au ni dhambi unayoijua, kanuni zile zile zitatumika.*


### C. Kurejeshwa kwa Kaka Anayetubu ni Lengo la Malezi ya Kanisa (2 Wakorintho 2)

Katika barua hii ya pili kwa kanisa la Korintho, Paulo anaandika kuhusu nini cha kufanya wakati mtu mwenye dhambi anapoungama baada ya kuonywa:

- Msamehe na kumfariji (v.7)
- Thibtisha upendo wako kwake upya (v.8)

Sababu ambayo Paulo anatoa kwa hili ni kwamba "Shetani anaweza asiturubuni" (v. 11). Msamaha na kurejezwa ni tabia ya Mungu, anayepatanisha mtu mwenye dhambi na yeye mwenyewe kupitia Yesu Kristo. Wakati kanisa linapokataa kuonyesha sifa za tabia kama hizi za Kristo, Shetani anapata ushindi dhidi ya kanisa. "Tunarubuniwa" na Shetani kwa kusamehe na kurejeza mwenye dhambi anayetubu.

**Kielelezo 15.1 Mchoro wa Mtiririko wa Malezi**




## II. MICHANGANUO

### A. Mchanganuo wa Kwanza

Geoge ni kijana tu aliyempenda Bwana na kijuhudi alikuwa akimtumikia kama kiongozi wa vijana katika kanisa lake na kiongozi wa kujifunza Biblia kiuinjilisti kwenye ujirani wake. Kanisa lake, mara ushuhuda wa juhudi wa kufikia nje kwenye jumuia, hivi karibuni umeshuka kutoka wajumbe 200 mpaka 30. Akiwa amesumbuliwa na hili, alianza kuuliza maswali.

Wazee walikwazwa na kumtaka akutane nao. Bila kupata nafasi ya kuelezea yanayomsumbua, aliamriwa asiulize maswali mengine zaidi na wasijadili hilo zaidi na mtu yeyote. Zaidi ya hayo, aliambiwa hataongoza tena vijana hata vikundi vidogo.

Akijisikia kwamba wazee hawakufanya haki katika matakwa yao, George aliendeleza kikundi chake kidogo. Wazee walimwamuru kukutana na kanisa lote na aliwekwa nje ya kanisa. Barua zilitumwa kwa viongozi wa kanisa katika eneo wakimlaumu kwa kuasi na kutotii mamlaka.

***Maswali ya Kufikiri***

- Kuuliza kwa Goerge ilikuwa dhambi?
- Kuitikia kwa wazee kwenye kuuliza kwake kulikuwa sahihi?
- Jinsi gani ambavyo wangelichukulia hili kwa njia ya kibiblia zaidi?

### B. Mchanganuo wa Pili

Samweli alikuwa mzee wa kanisa katika kanisa lake. Alikuwa na tabia isiyofaa ya kuwaendea wanawake kanisani, mengi yake yakiwa ya kuwadharirisha. Ingawa hakuwa anajisikia hatia ya uzinzi, wazee wengine walijisikia kwamba vitendo vyake havikuwa vya kufaa kwa mzee. Walipomtia changamoto, alitubu dhambi yake kwa kanisa zima na alitolewa kwenye uongozi. Hakukuwa na jaribio lililofanywa la kumrejesha.

***Maswali ya Kufikiri***

- Wazee wengine walikuwa sawa kumtia changamoto Samweli kwa matendo yake? Kwa misingi ipi?
- Walikuwa sahihi kumuondoa kwenye uongozi?
- Ni mpango upi wa kurujesha ambao wangetakiwa kuwa nao?

**C. Mchanganuo wa Tatu**

Jemusi alikuwa mchungaji aliyeshukuriwa sana na kanisa lake. Ilipotambulika kwamba binti yake ambaye hajaolewa alikuwa na mimba, viongozi waligawanyika kuhusu uamzi gani wangechukua. Baadhi walisema haikuwa dhambi yake; alikuwa tayari anaugua kutokana na kuaibishwa pia na kumfikiria binti yake na kwa hiyo alitakiwa kuchukuliwa kwa neema. Wengine walisema kwamba hakuwa anatimiza matakwa ya kibiblia kwa mzee kutawala nyumba yake na kwa hiyo alitakiwa kuonywa. Lakini kwa kuwa hawakuwa na wa kushika nafasi yake na kwa sababu alikuwa anapendwa na watu, waliamua kutokufanya chochote.

***Maswali ya Kufikiri***

- Wazee walikuwa sawa kutolijali tatizo?
- Jinsi gani mabavyo wangeitikia kwenye tatizo hili yote kwa neema na ukweli?

**SULUHU**

Malezi ya kanisa si ya kibiblia tu lakini ni sehemu ya lazima katika maisha ya kanisa. Sababu ya hili siyo ya kuadhibu, lakini kurejesha afya ya kiroho kwa mtu pekee na kanisa la mtaa. Kila kanisa la mtaa linatakiwa kimaombi na kiuangalifu kuanzisha sheria ya malezi.

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Soma 1 Wakorintho 11:29-32 na jibu maswali haya:
    1. Kwa nini kulikuwa na wadhaifu na wagonjwa miongoni mwa waumini?
    2. Nini ilikuwa adhabu ya mwisho?
    3. Kwa nini Bwana anawaonya watoto wake?
- Soma Wagalatia 6:1-5 na jibu maswali haya:
    1. Nini baadhi ya sifa Paulo anazoorodhesha za kumejeza ndugu?
    2. Nini “sheria za Kristo” ambazo Paulo anataja?
    3. Jinsi gani sheria hizi zinatakiwa zitumike katika kumrejeza ndugu?
- Na timu yako, anzisha sheria ya malezi ya kanisa kwa kanisa lako mpya.

KANISA

SOMO LA 16

# Ibada ya Umoja Kwenye Kanisa la Mtaa

## MFUMO NA KAZI KATIKA IBADA

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wapanda kanisa kufikiria jinsi mfumo na kazi zinavyohusiana na ibada ya pamoja.

☞ **Wazo Kuu**

- Ibada lazima ifanyike katika roho (moyo) na katika kweli (akili).
- Mungu ni mshuhudiaji wa ibada

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa...

- Kuelewa tofauti kati ya kazi za kuabudu na mifumo ya kuabudu katika ibada ya pamoja ya kanisa la mtaa.
- Elewa jinsi ya kufanya ibada ya kanisa mpya lililopandwa kuendana na kiutamaduni.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Kipindi hiki kinatakiwa kitolewe kwa njia ambayo kunakuwa na mwingiliano. Anza somo kwa kuwafanya wafunzwa kushirikisha aina kadhaa za ibada ambazo wamewahi kushiriki. Ni mifumo ipi ya ibada wamewahi kukutana nayo na jinsi gani walijisikia kuhusu kutumia mifumo hiyo? Kiasi gani cha kushiriki kwa kusanyiko kilikuwa pale? Maswali mwishoni mwa somo yanaweza kutumika katika majadiliano vilevile.

**UTANGULIZI**

Fikiria juu ya baadhi ya mchanganyiko wa ibada ambazo umewahi kukutana nazo. Fikiria nini kilitokea katika ibada hizi—aina ya mziki, maombi, mahubiri, usomaji wa maandiko, matukio muhimu, n.k. Ni kwa njia zipi ibada hizi zilikusaidia au kukuzuia katika kumwabudu Mungu?

> Ulimwenguni kote, makanisa yanayokua na kuzidisha ni hayo ambayo watu wanataka kuja humo kwenye ibada ya kuabudu kwa sababu yanawasaidia kuwa na kukutana na Mungu na watu wake kwenye maana.

Moja ya maswala ya kimugawanyo zaidi kanisani leo ni swala la mifumo ya kuabudu katika ibada ya pamoja ya makanisa ya mtaa. Baadhi ya makanisa yanapendelea mtindo wa ukimya wa kizamani; mengine yanapendelea mtindo wa kusisimua. Baadhi hayatumii vifaa; mengine yanatumia tu ogani au piano. Bado mengine yanatumia mchanganyiko wa vyombo, kama vile kibodi ya umeme, gita, tarumbeta, violini, fluti. Ngoma. Matoazi, na aina nyingine za vyombo vya mziki. Baadhi ya makanisa yana kwaya au bendi ya kuabudu. Mengine yana kiongozi mmoja wa kuabudu.

Hata hivyo, kwa watu wengi, ibada za hadharani ni kawaida za dini na mujibu kufanyika na kudumu, badala tu ya kuvutwa na uzoefu. Ulimwenguni kote, makanisa yanayokua na kuzidisha ni hayo ambayo watu wanataka kuja humo kwenye ibada kwa sababu yanawasaidia kuwa na kukutana na Mungu na watu wake kwenye maana. Ukuaji mdogo wa kanisa unatokea wakati watu wanapohudhuria ibada nje ya kujisikia kudumu au kwa sababu wanamfanyia Mungu upendeleo.

Ibada ya pamoja ni wakati wajumbe wote wa kanisa wanapokuja pamoja kumwabudu Mungu. Mara kanisa lako mpya lililopandwa linapoanza kufanya ibada ya pamoja, ni muhimu kuelewa kazi za ibada na kisha kuweza kuchagua mifumo inayoendana ya ibada ambayo inakamilisha kazi hizo na kuwavuta watu kwenye kukutana na Mungu aliye hai. (Rejea Somo la Kanisa la 3, "Mfumo na Kazi" katika Mwongozo wa kwanza).

Ni muhimu kuanzisha falsafa ya ibada ambayo inaongoza upangaji na maandalizi ya ibada yako ya kuabudu. Falsafa ya kuabudu kwa kifupi ni maelezo ya kwa nini na jinsi gani kanisa lako au kikundi kiini kinapanga kuendesha ibada. Inatakiwa itokane na kanuni za kibiblia na kuhusisha kazi muhimu za kibiblia ambazo zinaendana na kuabudu. Itasaidia kama kiongozi katika kuwasaidia kuandaa nyakati za kweli zinazoinua za ibada na zinazomtukuza Mungu na za kimaandiko. Itawazuia kutokana na kuchukua iliyopita ya kimapokeo ambayo inaweza kuwa kuu kuu na isiyovutia.

Falsafa ya kuabudu itasaidia kama kiongozi katika kuwasaidia kuandaa nyakati za kweli zinazoinua za ibada na zinazomtukuza Mungu na za kimaandiko.

## I. KAZI YA KUABUDU

Ibada ya pamoja inasherehekea ukati wa Mungu katika maisha ya kanisa. Mungu anastahili kuabudiawa. Yuko kwenye utawala wa mwisho wa anga. Ana upendo hakika kwenye uumbaji wake na kwa viumbe wake. Pia ametuita kuwa sehemu ya familia yake hapa duniani. Mambo yote haya ni sababu ya kutosha kuwa na furaha kuu na kusherehekea. Kuabudu kwa hiyo, ni furaha yetu, kuwa na shukurani, ya kukubali ukuu wa Mungu ulio wa hakika na maadili mema. Katika kuabudu tunatumia uwepo wetu wote—akili, utayari, hisia, na mwili—kuleta kitu fulani cha furaha hiyo ambayo haielezeki kwa mazungumzo ya kawaida lakini kinaweza kuwezekana kwa sehemu ya kiroho tulivyo.

### A. Kumpa Mungu Utukufu na Shukurani

Katika maandiko yote, watu wa Mungu wameamriwa kumpa Mungu utukufu na shukurani kwa Mungu. Tunaona pia mifano mingi ya wahusika wa kibiblia wanaotoa heshima kuu kwa muumbaji wao, kutoka kwa Ibrahimu katika kitabu cha Mwanzo mpaka kwa mtume Yohana kwenye kisiwa cha Patimo. Misemo kadhaa tofauti ilitumika kwa lugha zote ya Kiebrania na Kigiriki kuelezea utukufu kwa Mungu. Kwa kuangalia baadhi ya misemo hii tunaweza kupata picha yenye mambo mengi ya kiasili, halisi na asili ya kuabudu.

1. *Misemo ya Kiebrania*

- *halal*[1] *and tehillah*[2] - *Halal ni* neno lililotumika kila mara zaidi sana kwenye Agano la Kale kwenye kutukuza. Inatokea mara 88. Maana yake ya msingi ni "kuzalisha mvumo wazi." Inamaanisha pia "kujigamba, kusherehekea, kunenea, kujitukuzia…" kutukuza kwa kweli kunatakiwa kuwa na mvumo wazi na wa tofauti. Kunatakiwa kusiwe na kuchanganywa na nini kinachokusudiwa. *Tehillah* (Lililotolewa kutoka halal) linasisitizia kuimba. Tunamwimbia Mungu nymbo wazi za kutukuza. Wakati mwingine nyimbo za kuabudu na sifa si dhahiri na za hila. Nyimbo za kuabudu zinatakiwa wazi wazi na bila makosa kuwa na kumtukuza Mungu (2Nya 20:21-22a, Za 71:8; 107:32).
- *zamar*[3] – maana yake ni "Kugusa au kucheza kamba." Ina hisia pia za kuimba utukufu kwa kusindikiza vyombo vya mziki" (Zab 9:2; 33:2; 149:3).
- *yadah*[4] *and todah*[5] – Kustahi au kuabudu kwa mikono iliyonyooshwa. Kutukuza au kushukuru. Kutoa heshima kwa mikono iliyonyooka (1Nya16:8, Zab 97:12; 99:3).
- *shachah*[6] – Kuinama, kuanguka chini mbele, kujilaza kifudi fudi kimwili kwa hesima mbele ya mtu ambaye anatolewa heshima (Mwa 23:12, ni 60:14a, Zab 29:2b).

---

[1] הלל
[2] תהלה
[3] זמר
[4] ידה
[5] תודה
[6] שחה

2. *Misemo ya Kigiriki*

- *proskuneo*[7]– Kuanguka chini na kubusu miguu ya yule anayestahili heshima (Mt 2:11, 1Kor 14:25,Uf 19:4).
- *aineo*[8] *and epaineo*[9] – kuhimidi au kutukuza Mungu (Lk 19:37, Mdo 2:47, Uf 19:5).
- *eucharisteo*[10] – Shukurani zinazotolewa kwa Mungu kuonyesha shukurani (Lk 17:16, 1The 5:18; Uf 7:12, 11:17).
- *humneo*[11] – Kuimba nyimbo za sifa (Mt 26:30).
- *psallo*[12] – Kupiga chombo na kuimba (Efe 5:19, Yak 5:13).
- *doxazo*[13] - Kuinua (Yn 17:1b, 1KoR 6:20b, Mt 9:8).
- *Eulogeo*[14] – Kubariki na kutukuza (Mt 5:44, Mk 10:16, Lk 24:53).

Maneno haya ya Kieburania na Kigiriki yanaonyesha kwamba kuabudu kwa kweli ni hali ya kweli ya hisia kutoka moyoni na zinaelekezwa kwa Mungu kwa kutukuzwa kwake na shukurani. Ni wazi pia kwamba kuna lazima kuwe na mchanganyiko wa kuabudu—katika mziki, vyombo, na mifumo mingine.

**B. Kumtolea Mungu Huduma**

Ibada ya kweli haiwezekani mbali na kujitoa kikamilifu kwa maisha ya mtu kwa Mungu na kuishi kwa kuonyesha kujitoa huko katika matendo ya ibada na huduma. Neno lililotumika kuelezea kazi hii ya kuabudu kwenye Biblia ni


- *abad*[15] (Waebrania) – Kumfanyia kazi Mungu; kumtumikia Mungu; kuwa mtiifu kwenye amri zake (Kut 7:16, Kum 10:12, 1Isa 7:3, 2Nya 33:16, Zab 100:2).
- *latreuo*[16] (Kiyunani)– Kumwabudu au kumtumikia (Mt 4:10, Mdoc 27:23, Uf 7:15).
- *latreia* [17] (Kiyunani) – Kumtumikia Mungu; Kukaa mbele za Mungu (Rum 9:4b; 12:1).

**C. Mtazamo wa Yesu Juu ya Kuabudu**

Katika mazungumzo yake na mwanamke Msamaria (Yohana 4), Yesu alidhihirisha ukweli mwingine kuhusu kumwabudu Mungu. Alieleza kwamba Mungu hasumbuliwi sana kuhusu *wapi* tunapomwabudia (sehemu), lakini jinsi tunavyomwabudu (tabia)—*katika roho na kweli.* Kwa jinsi gani, Yesu hakuwa anarejea kwenye *mifumo* ya kuabudu. Alikuwa akionyesha umuhimu wa hisia zetu na kushiriki kiakili kwenye utaratibu, badala ya kutumainia sehemu au kawaida za dini kama Wasamaria na Wayahudi walivyofanya siku hizo.

[7] προσκυνεω
[8] αινεω
[9] επαινεω
[10] ευχαριστεω
[11] υμνεω
[12] ψαλλω
[13] δοξαζω
[14] ευλογεω
[15] עבד
[16] λατρευω
[17] λατρεια

**Kielelezo 15.1 Ibada ya Kweli**




Kuabudu kunakokubaliwa lazima kuwe na vipengele vyote. Kama tunaabudu katika roho tu, tunakimbilia hatari ya kuabudu miungu au kumuwakilisha vibaya Mungu wa kweli kwa sababu hatujui kitu kuhusiana naye. Hili halimpendezi Mungu. Kwa upande mwingine, Kama tunaabudu katika kweli tu, kuabudu kwetu ku baridi na kukosa hisia za upendo na ukaribu na Mungu. Aina hii ya kuabudu haimfurahishi pia. Badala, Mungu anatutaka kuelewa ukweli kwa akili zetu na kumwabudu kwa hisia kutoka kwenye undani wa mioyo yetu.

> Mungu anatutaka kuelewa ukweli kwa akili zetu na kumwabudu kwa hisia kutoka kwenye undani wa mioyo yetu.

**D. Vipengele vya Ibada ya Kuabudu ya Pamoja**

Katika historia yote ya kanisa, ibada ya kuabudu ya pamoja ya makanisa ya mtaa imeonyesha kuabudu kibiblia kupitia vipengele vifuatavyo:

- Nyimbo, sifa na mziki—kuimba neno, na nyingi za kusherehekea, kutukuza na kutoa shukurani ( kukazia hisia zetu na utu wa ndani kwa Mungui).
- Mahubiri—Kulihubiri neno (Kukazia ibada yetu kwa Mungu, kwa kutuita sisi tumtii).
- Kusoma Biblia – Kusoma neno la Mungu hadharani (Kukazia akili zetu kwa Mungu kwa kuzichovya katika ukweli).
- Maombi – mawasiliano na Mungu (maombi ya kutukuza, kuinua, toba, maombezi).
- Ushirika – Meza ya Bwana, Ubatizo.
- Zaka na sadaka – kutoa vitu ulivyonavyo kwa Bwana.
- Matukio muhimu – mziki maalumu, kusoma tungo, maigizo, kushirikisha shuhuda, n.k.

Mifumo ya vipengele hivi inatofautiana sana kutoka kanisa mpaka kanisa, kulingana na kawaida za kidhehebu na utamaduni wa ndani. Kwa mfano, baadhi ya makanisa yanasherehekea meza ya Bwana kila juma; wengiene wanaisherehekea kila jumapili ya kwanza ya mwezi. Baadhi ya makanisa yanakutana jumapili asubuhi kwa ibada ya pamoja; wengine wanakutana kila jioni au mara mbili kwa mwaka. Mziki wa kuabudu unatofautiana kwa mapana. Kuonyesha mifumo inayofaa kwa ibada ya pamoja imejadiliwa hapo chini.

## II. JINSI YA KUONYESHA MIFUMO INAYOFAA YA KUABUDU

> Hata katika mji mmoja, watu kutoka katika umri tofauti, kielimu, kabila, utamaduni na historia ya kidhehebu kutaonyesha ibada yao ya pamoja kwa Mungu kwa njia tofauti.

Kama tulivyojadili mwanzoni mwa somo hili, na kuona katika maandiko yote, kuna mifumo mchanganyiko ya kuabudu. Ni vigezo gani unatakiwa kufikiria unapopanga ibada yako ya kuabudu ya pamojao? Hili ni swala muhimu kwako na kwa uongozi wako unaoibuka kulifikiria. Mifumo ya kuabudu unayochagua itatofautiana sana kutoka eneo moja la kijografia au utamaduni mpaka lingine. Hata katika mji mmoja, watu kutoka katika umri tofauti, kielimu, kabila, utamaduni na historia ya kidhehebu kutaonyesha ibada yao ya pamoja kwa Mungu kwa njia tofauti. Mifumo ya kuabudu inatakiwa iwaruhusu watu kuonyesha yote ukweli wa imani zao kwa Mungu (ukweli) na hisia na kujisikia kwenye uhusiano wao na Bwana (roho).

Mifumo inatakiwa iwaruhusu watu kumsogelea Mungu. Ufunguo wa kupanga ibada ya kuabudu, kwa hiyo, ni kutafuta kujua jinsi gani watu katika eneo lako linalolengwa zaidi kikawaida wanaonyesha upendo, furaha, ujasiri, na uhusiano wa ndani. Hizi ni dalili za kuabudu kwa kweli. Kuabudu kamwe hakutakiwi kuwa kwa kujivuna, baridi au kuonyeshwa kwa njia iliyo kinyume na asili na kujisikia kwa muumini. Inatakiwa kiukweli na kiuwazi kuonyesha kujisikia kwetu kwa Bwana, na mawazo yetu kuelekea kwake.

## III. KUABUDU KWA UMOJA NA UPANDAJI KANISA

> Mungu ni mtazamaji wa kuabudu kwetu.

Kama tulivyoona mapema kwenye zana hii, moja ya makusudi ya kanisa ni kumwinua Bwana. Kwa hiyo, kuabudu kwa pamoja ni kazi muhimu ya kanisa. Kuabudu hadharani ni zaidi ya kuabudu kwa siri kunakofanyika sehemu za hadharani. Agano la Kale na hasa hasa Zaburi imejaa mifano ya watu wa Mungu wanaomwabudu pamoja. Katika Agano Jipya, mengi ya matatizo yaliyogusiwa katika nyaraka yalikuwa yanahusiana na kufanya ibada ya pamoja (Mf. 1 na 2 Wakorintho). Waumini wanahimizwa kutokuacha tabia ya kukutana pamoja (Ebr 10:25). Kuabudu kwa pamoja siyo burudani. *Wajumbe wa kusanyiko siyo watazamaji—ni washiriki*. Baadhi ya makanisa yanafanya makosa ya kufanya ibada ya kuabudu ya pamoja kana kwamba imekuwa ukumbi wa kufanyia maonyesho yanayofanywa na wataalamu. Kusanyiko ni "watazamaji" kiongozi wa kuabudu na mchungaji ni "waigizaji wa jukwani." Kuabudu kwa pamoja kunatakiwa kuingiwa na kusanyiko lote.

Kuabudu kwa pamoja kunamtukuza Mungu, kunatoa baraza la kuonyeshea umoja katika mwili wa Kristo (Yoh 17, Mdo 2), na kuimarisha mwili wa Kristo kupitia kufanyia mazoezi vipawa vya kiroho (1Kor 12:7ff, Efe 4:12,13). Huu ni ushuhuda kwa ulimwengu kwa uwepo wa Mungu katikati ya watu wake. Katika kuhudhuria ibada ya kuabudu siyo njia ya msingi ya uinjilisti, Mungu anatumia kuabudu pamoja kama njia mojawapo ya kuwavuta watu wenye dhambi kwenda kwake. Kwa jinsi hiyo, kuabudu huku lazima kuwe kwa kweli kutoka myoni, na siyo kitu cha kawaida au kawaida ya ibada.

> Matokeo ya uchunguzi yalionyesha kuwa ufunguo wa tabia ya makanisa yanayokua ilikuwa ibada ya kuabudu inayovutia watu na yenye furaha.

Thamani ya ibada ya kuabudu inaonekana kuwa na mguso kwenye ukuaji wa kanisa. Kati ya 1994-1996 Idara ya maendeleo ya kanisa la Ujerumani ilifanya uchunguzi wa dunia nzima wa tabia ya ukuaji wa makanisa (Maendeleo ya Kawaida ya kanisa, 1996). Walikagua zaidi ya makanisa 1000 katika nchi 32 kwenye mabara matano. Moja ya matokeo ya uchunguzi yalionyesha kuwa ufunguo wa tabia ya makanisa yanayokua ilikuwa ibada ya kuabudu inayovutia watu na yenye furaha. Washiriki katika makanisa haya walitazamia katika kuhudhuria ibada kwa sababu walikuwa na kukutana na Mungu na watu wake kwenye maana na walikuwa wametiwa moyo na kujengwa katika imani zao. Walitoka nje ya ibada wakiwa na shauku zaidi ya kumtii Mungu—kumpenda na kumtumikia yeye kwa undani zaidi na kumshirikisha kwa wengine.

## SULUHU

Kuabudu kwa pamoja kwa Mungu ni moja ya kazi ya msingi ya kanisa. Mungu anastahili kuabudiwa. Yesu alielezea kwamba waabudu wa kweli wanamwabudu Mungu katika roho na kweli. Katika historia nzima ya kanisa, waumini wanapokutanika kipamoja, vipengele kadhaa vya ibada ya kuabudu vimeanzishwa ili kumwabudu Mungu "katika roho na kweli." Vipengele hivi ni pamoja na kuimba na mziki, maombi, kusoma Biblia. Kushiriki meza, na matukio muhimu. Vipengele hivi vinaweza kuonyeshwa kwa mifumo mchanganyiko inayofaa, kulingana na mapokokeo ya kidhehebu na matendo ya kiutamaduni. Kudhihirika kwa majaribio kunaonyesha kwamba ibada ya kuabudu inayovutia ni tabia ya makanisa yanayokua.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kwa nini ni muhimu kwa watu wa Mungu Kukusanyika pamoja kwa ajili ya kuabudu pamoja? Ni nini dhumuni la Kuabudu pamoja?
- Ni baadhi ya sababu zipi "zinazovuta" ibada ya kuabudu kuchangia kwenye ukuaji? Ni nini asili ya "ibada ya kuabudu inayosisimua?
- Ina maana gani kumwabudu Bwana katika kutanda kwa utukufu wake? (1Nya 16:29).
- Kulingana na kanisa lako au dhehebu, kuinama chini na kupiga magoti ni kazi au mifumo ya kuabudu? (Zab 95:6). Kama ni mfumo, kazi ni ipi?
- Kulingana na kanisa lako au dhehebu kuinua mikono katika kuabudu ni kazi au mfumo? (1Tim 2:8). Kama ni mfumo, Ni ipi ni kazi?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Fanya mafunzo ya kuabudu kwa kufata katika Ufunuo 4:8-11 na 5:9-14. Uwe na hakika kujibu maswali ya "nani", "Nini", "Lini", "Wapi", "kwa Nini" na Jinsi gani?"
- Fanya orodha ya uchunguzi wa njia ambazo watu wengi katika eneno lako linalolengwa zaidi kiasili wanaonyesha upendo, furaha na uhusiano wa ndani.
- Fikiria jengo lako jipya la kanisa. Ni ipi kati ya mifumo hii inafaa kuonyesha kuabudu kwa Mungu katika ibada yako ya pamoja ya kuabudu? Ni mifumo ipi kutoka katika kawaida ya kidhehebu ambayo inaweza kufaa pia? Ni upi unaweza ukawa haufai kwa kundi la watu wako wanaolengwa? Jadili uliyopata na mkufunzi wako au mshauri.

## VYANZO


- Robinson, Martin and David Spriggs. *Church Planting: The Training Manual.* Oxford, England: Lynx Communications, 1995.
- Rowlands, Gerald. *Build My Church! (Volume Two).* Singapore: I.C.M. Publications, 1995.
- Schwartz, Christian A. *Natural Church Development.* Emmelsbüll, Germany: C&P Verlags-GmbH, 1996. (Note this book is available in Croatian, French, German, English, Portuguese, Russian and Spanish. www. CundP.de/international).

KANISA

SOMO LA 17

# Jinsi ya Kuongoza Ibada ya Umoja

## KUPANGA NA KUANDAA IBADA YA KUABUDU

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwaandaa wafunzwa kuwezesha kuabudu kwenye kanisa la mtaa.

☞ **Wazo Kuu**

- Ibada ni muhimu kupangwa kabla ya mda.
- Ibada ya kuabudu inatakiwa ifate kisa.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa vipengele vya ibada ya kuabudu na nafasi ya kiongozi wa ibada kwenye kanisa la mtaa.
- Kujua jinsi ya kuongoza ibada kiufanisi.
- Kuweza kuongoza ibada ya kuabudu yenye ufanisi kwenye kanisa mpya lililopandwa.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Somo hili linatakiwa kuwa majadiliano ya kimsingi. Uwe na kiongozi yeyote wa ibada mwenye uzoefu kwenye mafunzo ashirikishe jinsi wanavyoongoza ibada. Kama inawezekana, karibisha viongozi wenye uzoefu kutoka nje ya mafunzo kuja na kushirikisha wafunzwa jinsi wanavyofanya kazi na wachungaji kwenye makanisa yao na jinsi gani wanapanga na kuandaa kwa ajili ya ibada ya kuabudu.

Wafunzwa wagawanyike katika makundi na hasa wafanyie kazi zoezi katika kupanga ibada ya kuabudu. Makundi yashirikishe mipango yao kwa kundi lote.

### UTANGULIZI

Moja ya makusudi ya msingi ya kanisa la mtaa ni kumwinua Bwana. Ibada ya umoja imeamriwa na kuonyeshwa na watu wa Mungu kwenye Biblia. Ni ushuhuda kwa ulimwengu kwa uhalisi wa Mungu kati kati yetu. Somo lililopita limajadili kazi za kuabudu, vipengele vya ibada ya kuabudu ya pamoja na jinsi ya kuonyesha mifumo inayofaa ya kuabudu.

Somo hili linajadili nafasi ya kiongozi wa ibada, sifa za kiongozi wa ibada, mipaka ya kuongoza ibada ya kuabudu na jinsi ya kupanga na kuandaa ibada ya kuabudu.

### I. WAJIBU WA KIONGOZI WA IBADA

Jukumu la kiongozi wa ibada ni kufanya kazi na uongozi wa kanisa katika kupanga ibada ya kuabudu ya pamoja. Kwa kuongeza, kiongozi wa ibada anawajibika kuongoza ibada halisi ya kuabudu. Hii ni pamoja na kuongoza au kuita watu watakaoongoza vipengele kadhaa vya ibada ya kuabudu, mf. Uimbaji/mziki, maombi, zaka/sadaka, mahubiri, kushirikisha meza ya Bwana n.k.

Katika makanisa mengine kiongozi wa ibada na mchungaji ni mtu yule yule. Katika makanisa mengine ni mjumbe wa timu ya uongozi wa kanisa na anafanya kazi kwa ukaribu na mchungaji katika maandalizi na matayarisho ya ibada ya kuabudu ya pamoja. Katika hali hii, mchungaji kawaida anaandaa na kuongoza mahubiri na vipengele vya ibada ya ushirika wa meza ya Bwana, na kiongozi wa ibada mara nyingi anaandaa na kuongoza vipengele vingine (uimbaji, maombi, sadaka, matukio maalumu, n.k.). Anapokuwa mtu yule yule, mchungaji atawajibika kwa vipengele

vyote vya ibada ya kuabudu. Hii inafaa zaidi kwenye makanisa madogo, lakini kanisa linapokua Mungu atakuwa ameweka viongozi wa ibada waliojaliwa vipawa kanisani na mchungaji atafanya vizuri kushirikisha uongozi kwa watu hawa waliojaliwa vipawa. Hii inamfanya mchungaji kutokujilemeza na vile vile inatoa nafasi kwa uongozi kuendelea kati kati ya kanisa.

Kanuni hizo hizo zinatumika katika makanisa mapya yaliyopandwa. Mpanda kanisa anaweza kuchagua kuongoza ibada kwa mda, lakini mara mwenye kipawa cha kuongoza anapogunduliwa, wanatakiwa wafunzwe na kutolewa kwenye huduma hii. Kwa njia hii, pia, wajumbe wa kanisa wanaanza kuchukua umiliki katika wajibu wa kanisa hilo mpya lililopandwa.

## II. SIFA ZA KIONGOZI WA IBADA

Viongozi wa ibada wanatakiwa wawe na kiwango cha chini cha sifa za kiroho za kiongozi yeyote anayetambulika katika kanisa (mf. Mwalimu wa darasa la jumapili, kiongozi wa kikundi kiini, n.k.); Hakika, baadhi ya makanisa yanataka kiongozi wa ibada kuwa na sifa za kiroho za mzee wa kanisa. Viongozi wa ibada wanatakiwa kuwa na ufahamu wa asili ya kile wanachofanya. Kusudi lao ni kuongoza ibada katika namna kwamba hawajivutii wao wenyewe isipokuwa Mungu. Wanatakiwa wawe watu wanaoelekeza kusanyiko kuelekea kwa Mungu badala ya kuelekeza kwao wenyewe.

Kwa kuongeza kwenye sifa za kiroho za kiongozi anayetambulika kanisani, baadhi ya sifa zingine za kiongozi wa ibada mzuri ni pamoja na zifuatazo:

### A. Mwabudu

Mtu aliyeitwa kuwaongoza wengine kwenye kuabudu anatakiwa awe mwenye mujuzi wa kuabudu na stadi katika kumwabudu Mungu. Haiwazekani kuwaongoza wengine katika kitu fulani isipokuwa kiongozi awe ameshajifunza yanayotakiwa na ujuzi wa kuabudu. Mtu huyu anatakiwa awe na maisha mazuri ya kuabudu kwa mtu binafsi.

### B. Uwezo wa Kimziki

Kiongozi mzuri wa kuabudu lazima awe na ujuzi katika eneo la mziki. Wanahitaji hasa kuwa na ujuzi katika kuwaongoza wengine kwa kutumia mziki—kuongoza uimbaji na upigaji wa vyombo, kutumia mziki wa awali, n.k. Katika Agano la Kale, wanamziki wenye ujuzi waliongoza watu katika kumwabudu Mungu kwa pamoja (1Nya 15:16-21).

### C. Hisia kiroho

Kiongozi mzuri anakuwa na hisia kwenye uongozi wa Roho Mtakatifu. Ibada inatakiwa iongozwe na Roho Mtakatifu. Kiongozi wa ibada anatakiwa kuweza kutambua uongozi wa Roho Mtakatifu, na kisha kuweza kuelekeza ibada kufuatana na maelekezo ya Roho Mtakatifu.

### D. Utu wa Unyenyekevu

Kiongozi mzuri kawaida atataka “kujificha nyuma ya Kristo.” Anatakiwa awe anaweza kudhibiti mawazo ya binafsi, kujisikia na hisia ili kwamba visiingilie kwenye mkutano. Hakuna kinachopotosha kiwango cha kiroho cha ibada ya kuabudu kwa haraka zaidi kuliko kiongozi mwenye majivuno anayejiweka yeye mwenyewe kwenye mkutano. Kiongozi wakati wote lazima atafute kukazia usikivu wake wa kuabudu kwa Mungu.

### E. Uwezo wa Kuongoza Wengine kwenye Kuabudu

Viongozi wazuri wa kuabudu wanatakiwa waepuke kujiingiza kwenye “kupotea katika kuabudu.” Moja ya mifano ya kawaida ya hili ni kiongozi wa kuabudu anayefunga macho na kuonekana kusahau nini kinachotokea kwake. Kiongozi wa ibada anatakiwa kuwa macho juu ya kinachotokea kwenye kusanyiko na kuwa anawatia moyo kusanyiko lote kushiriki katika ibada ya kuabudu. Inawezekana kushiriki katika kuabudu kikamilifu na bado ukawa na ufahamu na kuwa macho kwa watu. Kiongozi anatakiwa awe na hisia kwa Roho Mtakatifu na wakati huo huo akiwa anafanyia mazoezi taratibu mvuto katika ibada.

## III. MIPAKA YA KUONGOZA KUABUDU

Kuabudu kwa undani na kwa nguvu kunahitaji kujaliwa vipawa, hisia kwa Roho Mtakatifu na uzoefu. Umbo la ibada yako ya kuabudu bila mashaka itavutwa na mapokeo yako mwenyewe ya kidini na uzoefu wako wa mwanzoni. Kwa jinsi hiyo, kuna baadhi ya mipaka ya msingi ambayo inaweza kusaidia ibada yoyote ya kuabudu kuwa uzoefu ambao unawavuta waumini karibu zaidi na Mungu na kumpendeza.

### A. Kisa

Ibada itasaidiwa zaidi kwa kuchagua kisa cha msingi ambacho kisha kitaangaliwa kwenye vipengele vyote vya ibada—mziki, mahubiri, maombi, n.k. Ibada ya kuabudu inayotokea kwa kubahatisha itakosa nguvu sawa na kukamilisha kidogo kuliko ile iliyopangwa kukazia kwenye kisa maalumu. Mara nyingi tabia ya “ngoja tumwachie Roho Mtakatifu aongoze” ni udhuru wa kutokufanya juhudi za kujiandaa kabla ya mda—na matokeo yake ibada kupata shida.

### B. Mpito

Muunganiko kati kati ya vipengele vya ibada ni muhimu. Fungu la maelezo au mawili ambayo yanakusudia kuongoza mawazo ya kusanyiko yanaweza kusaidia kulainisha mpito kutoka kushiriki kwenda kwenye kusikiliza kwa bidii, kutoka kuangalia kwenda kwenye utendaji. Kiongozi wa kuabudu atahitaji kuweza kuhisi nini Mungu anachofanya na ikiwezekana kufanya marekebisho kidogo wakati wakiendelea. Kutumia mziki kusaidia kufanya mpito kati ya vipengele tofauti tofauti vya ibada inasaidia kwenye mtiririko wa ibada vile vile.

> Ibada itasaidiwa zaidi kwa kuchagua kisa cha msingi ambacho kisha kitaangaliwa kwenye vipengele vyote vya ibada—mziki, mahubiri, maombi, n.k.

Kwa mfano, baada ya kuimba nyimbo za sifa kwa Mungu za kupaza sauti mwanamziki msindikizaji anaweza kupiga mziki kidogo wa kitulizo kusaidia kusanyiko kutoka kwenye sifa za ushindi kwenda kwa ule wa utulivu wa kutafakari katika kujiandaa kwa ajili ya uimbaji zaidi wa pole pole au kuhamia kwenye maombi au kwenye vipengele vingine vya kuabudu.

### C. Mfuatano wa Vipengele

Mfuatano wa vipengele katika ibada unaleta maana? Kwa mfano, mahubiri yaje baada au kabla ya mda wa maombi? Meza ya Bwana isherehekewe mwanzoni, kati kati au mwishoni mwa ibada? Kuna uwiano kati ya kukaa na kusimama, kati ya kusikiliza na kushiriki, n.k.? Tambua kwamba baadhi ya mapokeo ya kidhehebu yana vipande vya kuabudu ambavyo kiumuhimu vinaonyesha utaratibu wa ibada ya kuabudu.

### D. Nyimbo na Mziki

Mziki na kuimba ni mifumo mikuu ya kuabudu ambayo inawaruhusu watu kumwabudu Mungu kwa hisia zao na kujisikia kwao. Kuna aina pana ya mziki “uliowekwa wakfu”—yote mapokeo na wa kisasa. Baadhi ya vitu vya kufikiria wakati unapochagua mziki kwa ajili ya kuabudu pamoja ni:

1. *Urahisi wa Uimbaji*

Chagua nyimbo ambazo ni rahisi kuimba na ambazo ni rahisi kujifunza. Zinatakiwa ziwe zile ambazo timu ya upandaji kanisa inazijua vyema. Unapotambulisha nyimbo mpya kwenye kusanyiko, zitumie kwenye ibada kadhaa zenye mafanikio, ili kwamba kusanyiko liwe na nafasi ya kujifunza vizuri. Pia, kwa ibada moja ya kuabudu, tambulisha si zaidi ya wimbo mmoja au mbili. Inakuwa vigumu kwa watu kuingia kwenye kumwabudu Mungu kama wanakuwa wanakatishwa sana na mziki usiofahamika. Uwe na maneno ya wimbo kwenye vitabu vya nyimbo za sifa au kwenye karatasi zilinakiriwa au kwenye ubao wa umeme. Hii hasa inasaidia zaidi watu kushiriki kwenye ibada ya kuabudu.

2. *Mchanganyiko*

Jaribu kuchanganya mchanganyiko wa nyimbo za kisasa na za kimapokeo na mziki, kama inawezekana kabisa. Wakati moja ya madhehebu makubwa ya Estonia yaliyorekebisha kitabu chao cha sifa mwanzoni mwa mwaka 1990, baraza lililochaguliwa kwa kazi hii kushirikisha nyimbo za sifa bora zaidi za mapokeo vile vile na kuongeza sifa za kisasa ambazo zimekuwa sehemu ya ibada ya kuabudu kwa makanisa mapya ya

Babtisti yaliyopandwa. Hii imesaidia kuweka daraja kwenye tofauti ya mitindo ya kuabudu kati ya ya zamani, makanisa ya mapokeo na makanisa mapya.

3. *Anavyoonekana*

Jaribu kuwa na mpishano wa mounekano kwenye nyimbo za sifa. Wimbo wa kusherehekea wa kufungua na wimbo wa shangwe wa kufungia unaweza kutofautiana na mwingine, nyimbno za sifa za kurejesha zaidi wakati wa mda uliobaki wa ibada. Mziki wa vyombo unaweza kutumika kiufanisi hasa kwenye mpito kutoka kwenye kusherehekea kwenda kwenye fikira na kurudi kwenye kusherehekea. Hii mara nyingi inaweza kusaidia ibada kutoka kujisikia "kusuka suka" au kuvunjika.

4. *Mziki wa Vyombo*

> Mziki wa vyombo tunaouona katika Agano la kale vilikuwa ni vyombo vya kawaida kwa watu wa siku hizo.

Mziki wa vyombo ulitumika mara kwa mara kwenye maandiko kuonyesha utukufu na kuabudu na kumtukuza Mungu. Mziki wa vyombo tunaouona katika Agano la kale (kinubi, tarumbeta, zeze, n.k.) vilikuwa ni vyombo vya kawaida kwa watu wa siku hizo. Hakuna kilichowakfu kuhusu ogani, piano, au gita. Kanisa moja dogo la Bosenia-Herzegovina lilikuwa limepewa ogani sita na makanisa kutoka Magharibi, ambao walijisikia kwamba kanisa hili lazima liwe na ogani ili kuweza kumwabudu Mungu "kisawasawa". Hata hivyo, hakuna anayeipiga ogani, na kwa hiyo zimewekwa tu, zikikusanya vumbi. Ogani siyo chombo cha kawaida kwenye eneo hilo na kwa hiyo haitumiwi na waumini kwenye kuabudu kwao. Wanamziki wanaohusika kwenye kuabudu wanatakiwa "wapige kiujuzi" kwenye vyombo vyao (Zab 33:3). Nani katika kanisa lako ana ujuzi wa mziki? Ni vyombo gani ni vya kawaida kwa watu katika eneo unalolenga?

Mkazo wa mziki unatakiwa usiwe kwenye ujuzi na vipaji vya wanamziki wenyewe, lakini badala yake kwenye ukuu na enzi ya Mungu. Miziki yote kwenye ibada ya kuabudu inatakiwa ihudumu kuwavuta watu karibu kwa Mungu.

**E. Vifaa**

Vyombo vitakavyotumika wakati wa ibada ya kuabudu vimeandaliwa kisawasawa na vinafanya kazi? Kuja mapema kwenye ibada na kuangalia kama vyombo vimeandaliwa kisawasawa na kufanya kazi ni msaada mkubwa wa kuwezesha hadhi ya ibada ya kuabudu. Vyombo vya kimakosa vinaweza kuwa kizuizi katika kuwaruhusu watu kushiriki kwenye kuabudu na mara kwa mara vinakatisha mkazo wa watu kutoka kwa Mungu.

**F. Mazoezi**

Wazo la kufanya mazoezi kwa ajili ya ibada ni kitu fulani ambacho kinazalisha hisia ya kutopenda. Kwa jinsi hiyo, kuabudu ni sadaka kwa Mungu, na tunatakiwa kuwa tayari kutoa kilicho bora kwa Mungu kwenye kuabudu kwa pamoja. Vile vile, Mziki uliofanyiwa mazoezi, maigizo, shuhuda, n.k., hasa hasa inawaruhusu watu kumwabudu Mungu kiufanisi. Usikivu wa watu haukatishwi kwa kutafuna maneno na mziki uliopigwa vibaya. Vilevile, mazoezi yanasaida kutathimini mtiririko wa ibada na kuhakikisha kwamba vipengele tofauti tofauti vya ibada vinaendana pamoja kimaana. Mazoezi yanamuruhusu kiongozi wa ibada kwa uongozi wa Roho Mtakatifu wakati wa ibada badala ya kukalia kufanya mziki kuwa sawa.

**G. Maandalizi ya Kimaombi**

Kabla ya ibada, kiongozi wa kuabudu, na wengine wanaohusika kwenye ibada ya kuabudu wanatakiwa wakutane na kuomba pamoja. Kuikabidhi ibada kwa Bwana, muombe kwamba imbariki, na kwamba Roho Mtakatifu ataongoza na kuelekeza ibada. Omba kwa ajili ya wokovu kwa yeyote asiyeamini ambaye anaweza akawa amehudhuria, kwamba mioyo yao itavutwa kwenye toba na imani katika Kristo. Omba kwa ajili ya waumini kuvutwa karibu kwa Kristo. Omba Bwana alinde mda wa kuabudu kutoka kwenye mashambulizi yoyote ya yule mwovu.

## IV. FANYA MAZOEZI YA UPANGAJI IBADA YA KUABUDU

Hatua zifuatazo zinaweza kukusaidia kupata uzoefu katika upangaji wa ibada ya kuabudu na timu yako ya upandaji kanisa. Katika darasa lako la mafunzo, gawanyika katika makundi madogo. Jadili kila moja ya hatua zifuatazo na tumia karatasi ya mfano wake kupanga ibada. Shirikisha mpango wako wa ibada na makundi mengine.

### A. Hatua 1: Chagua Kisa

Nini kitakuwa kisa cha ibada ya kuabudu? Mda mwingi wazo kuu la mahubiri linafaa kwenye hitaji hili. Kwa mfano, katika somo la mahubiri katika mafunzo haya umeandaa mahubiri kwenye fungu la Waefeso 5:15-21. wazo kuu la fungu hili ni: "Mungu anatutaka tujazwe na Roho kwa sababu ni busara na inaletea maisha yenye furaha." Kisha kwa hiyo kisa cha ibada ya kuabudu kinaweza kuwa: "*Ujazwe na Roho.*" Kama siku hii ni siku maalumu, jumapili ya pentekosti, Krismas, Pasaka, kisa chako pengine kinakuwa kama vichwa hivyo.

### B. Hatua 2: Chagua Nyimbo/Mziki na Matukio Maalumu

Ni nyimbo zipi na sifa utatumia katika ibada ya kuabudu? Chagua zile ambazo zinaendana na kisa na ambazo ni za kisasa na za kimapokeo. Pia, Uwe na uhakika kuwa mapigo ya mziki yametofautiana—yote yakionyesha kusherehekea na fikira. Utakuwa na mziki wowote maalumu, kama vile sauti au solo ya vyombo? Kutakuwa na maigizo yanayoelezea sura ya mahubiri? Utakuwa na ushuhuda wowote? Uwe na hakika shuhuda unazochagua zinaendana na kisa.

### C. Hatua 3: Weka Mtiririko wa Ibada ya Kuabudu

Uwe na mda halisi wa kuanza na kumaliza. Husisha kila sura ya ibada ya kuabudu—nyimbo, mahubiri, matukio maalumu, maombi, kusoma Biblia, n.k. kielelezo 17.1 kina mfano wa karatasi ya upangaji wa ibada ambayo unaweza kutumia au kuirekebisha kuweka mtiririko wa ibada. Karatasi hii ya kupanga kisha inaweza kutumika na kiongozi wa kuabudu na mchungaji kama marejeo ya kuongoza halisi kwa ibada.

### D. Hatua 4: Orodhesha Vyombo Vinavyotakiwa

Tengeneza orodha ya vyombo utakavyohitaji kwenye ibada ya kuabudu, kama vile vitabu vya nyimbo au karatasi za nyimbo, kifaa chochote maalumu cha kuigizia, n.k. Onyesha nani atawajibika kukusanya na kuandaa vyombo kabla na wakati wa ibada.

### E. Hatua 5: Onyesha tarehe za Kufanya Mazoezi ya Nyimbo

Amua lini utafanyia mazoezi ya ibada ya kuabudu. Uwe na hakika kwamba wahusika wote wanatambulishwa na kuweza kuhudhuria mazoezi ya kuimba.

### F. Hatua 6: Chukua Mda Kuomba Kwa Ajili ya Ibada ya Kuabudu

Muombe Mungu kuongoza na kuelekeza ibada ya kuabudu. Omba kwa ajili ya mioyo ya watu kutayarishwa kumwabudu Bwana. Omba kwa ajili ya wasioamini wanaoweza kuhudhuria kwamba mioyo yao iweze kufunguka kwa ajili ya Bwana. Baadhi ya makanisa wana timu za maombi zinazoombea ibada ya kuabudu wakati ikiwa inaendelea. Makanisa mengine yana makundi ya kuomba wanaokuja kanisani asubuhi sana na kuchukua mda kuomba kwa ajili ya ibada na kimya kimya kuomba kwa ajili ya hao wanaoingia sehemu ya kuabudia.

### G. Hatua 7: Tathimini Ibada ya Kuabudu

Baada ya ibada chukua mda kuitathimni. Mtiririko ulikuwaje na anga la kuabudu? Nini kinahitaji kubadilishwa? Nini kitumike tena? Mungu amekutana na kusanyiko lako kwa namna ya ajabu? Kulikuwa na watu hasa walioguswa wakati wa ibada ya kuabudu? Kulikuwa na yeyote aliyeokoka? Shirikisha unachojifunza kutoka kwenye tathimini yako kwenda kwenye ibada ijayo ya kuabudu.

**Kielelezo 17.1 Mfano wa Karatasi ya Kupangia Ibada ya Kuabudu**

## MFANO WA KARATASI YA KUPANGIA IBADA YA KUABUDU

**Utaratibu wa Ibada ya Kuabudu**

**Tarehe**________ **Jina la kanisa:**________________________

| Mda | Shughuli za Kuabudu | Mtu anayewajibika |
|---|---|---|
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |

### SULUHU

Kumwabudu Mungu kwa pamoja ni moja ya kazi kuu na nafasi ya kanisa. Kuongoza kuabudu ni kazi muhimu ambayo haitakiwi kuchukuliwa kirahisi. Viongozi wa kuabudu wenye ujuzi ni kipawa cha Mungu kwa kanisa. Wanatakiwa kufahamika, kuwezeshwa na kutolewa kwenye huduma. Maombi yanayofaa na uongozaji wa ibada ya kuabudu kunaweza kuongeza ufanisi wa uwezo wa kusanyiko kumwabudu muumbaji wao. Kuchukua kisa , kuangalia nyimbo/mziki na matukio maalumu, na kuonyesha mtiririko wa ibada ya kuabudu vyote ni sura muhimu za kuunda mazingira ya ibada yenye ufanisi.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kuna miundo ya kuonyesha iliyotumika mara kwa mara katika utamaduni wako ambayo inaweza kushirikishwa kwenye ibada yako ya kuabudu (mf. mashairi)? Jinsi gani unavyoweza kutumia miundo ya kuonyesha katika ibada ya kuabudu?
- Kwa nini ni muhimu kuchukua mda kupanga kwa ajili ya ibada ya kuabudu?
- Nini linatakiwa liwe jukumu la mchungaji katika kupanga ibada ya kuabudu? Nini linatakiwa liwe jukumu la kiongozi wa kuabudu?
- Elezea mtiririko wa ibada ya kuabudu ambayo ilileta maana kwako hasa hasa? Ni mambo yapi katika ibada yalikuwa na ufanisi zaidi? Nini unachoweza kujifunza kutoka katika ibada hii cha kukusaidia katika upangaji wa ibada ya kuabudu kwenye kanisa lako lililopandwa?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Panga na andaa ibada ya kuabudu. Baada ya ibada, tathimini ufanisi wake. Nini kilifanya kazi? Nini unachihitaji kubadili? Shirikisha matokeo haya kwa mkufunzi wako au mshauri.
- Kama ikiwezekana, tembelea makanisa mengine kwenye au karibu na eneo lako unalolenga. Chunguza ibada ya kuabudu na tambua mifumo ya kuabudu. Nini unachoweza kujifunza kutoka kwenye uchunguzi wako cha kutumia katika jengo lako mwenyewe la kanisa?

## VYANZO


- Robinson, Martin and David Spriggs. *Church Planting: The Training Manual.* Oxford, England: Lynx Communications, 1995.
- Rowlands, Gerald. *I Will Build My Church! (Volume Two).* Singapore: I.C.M. Publications, 1995.

KANISA

SOMO LA 18

# Kanisa la Mtaa na Mwili Mkubwa wa Kristo

## KUFANYA KAZI PAMOJA KATIKA USHIRIKIANO

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kusaida washiriki kujifunza kanuni kwa ajili ya ushirika wenye ufanisi na ushirikiano na mwili mkubwa wa Kristo, mf. Makanisa mengine, madhehebu, mashirika ya kanisa, n.k.

☞ **Wazo Kuu**

- Kiwango cha shirika kinatofautiana kufuatana na kazi iliyopo na tabia ya kundi linalohusika.
- Kuna angalau sifa kumi za ushirikiano wenye ufanisi.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa. . .

- Kuelewa jinsi ya kuanzisha ngazi yenye ufanisi ya shirika na ushirikano wa malengo mbali mbali ya huduma.
- Kujua kanuni za kuanzisha ushirikiano wenye ufanisi.
- Kushiriki katika kuanzisha ushirikiano kwa upana wa huduma ya upandaji makanisa

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Kutumia mchanganyiko wa mazungumzo na majadiliano ya darasani. Wafanye washiriki kujadili swala la mzunguko wa uhusiano wa waliojiunda . Tunatumia hasa njia hii katika maisha yetu binafsi?

### I. KADHIA YA USHIRIKIANO

Kuna sababu mbili za lazima kwetu kushriki na makanisa mengine na mawakala katika eneo au katika nchi ambao ni mzunguko wa wajibu wetu. Moja ni kitheolojia na lingine ni mazoezi.

#### A. Swala la Kitheolojia

Sababu ya kitheolojia ni muungano wa muhimu wa mwili wa Kristo. Hao wote ambao wamezaliwa kutoka hapo juu wamerithiwa kwenye familia ya Mungu (Yn 1:12, 13). Familia hiyo pia inaitwa mwili na ni mmoja, siyo nyingi (Efe 4:3-6). Katika maombi yake ya uwakili mkuu Kristo aliomba kwa ajili ya umoja wetu ili kwamba ulimwengu upate kuamini kwamba baba amemtuma (Yn 17:20-21). Hakika, maajabu ya injili ni kwamba Mungu ameumba watu wote kuwa mmoja katika Kristo, akivunja mipaka ambayo iliwatenga (Efe 3:2-6; Gal 3:26-28). Mgawanyo na mashindano miongoni mwa wajumbe tofauti wa kanisa wamekuwa kizuizi cha kuendelea kwa injili, kikwazo kwa wasio waumini, na chukizo kwa umoja wa wajumbe wa Mungu.

Kama sisi, na mapana yetu yote na utofauti, ni sehemu ya mwili wa Kristo, tunatakiwa kuanza kutenda kama ilivyo. Ulimwengu utaona umoja wetu na upendo na kuvutwa kwa kuamini kwa Yesu Kristo.

**B. Swala la Kimazoezi**

Katika nchi ambako watu wa kiinjili ni chini ya asilimia 2, haionyeshi sana kama dhehebu lolote au wakala anaweza kutimiza Utume Mkuu katika taifa hili mwenyewe. Ujazaji wa taifa kwa ushirika wa waumini unaoshuhudia itachukua kuhusika kwa watoto wote wa Mungu katika Taifa.

Zaidi ya hayo, kama tutafanya utafiti wa uangalifu, tutakuta kwamba mawakala tofauti na makanisa yana rasilimali zinazohitajika kwa wengine. Baadhi ya makanisa yamechapisha nyenzo zinazosaidia ufuasishaji. Mengine yameanzisha vipindi vya kanisa vya mafunzo, na wengine kuchagua mziki wa kisasa wa kuabudu. Baadhi ya mawakala wanachagua kufanya vyombo vya utangazaji, wengine katika kazi za vijana, kufikia watu kwa mchezo wa mpira, mkanda wa senema ya Yesu, n.k. Kuchangia vyanzo hivyo kunastawisha mwili mzima.

Kama tunaomba kwa pamoja, kufanya utafiti pamoja, na kuchangia rasilimali zetu, tunaweza kukuta kwamba Bwana Mungu amefanya kila kinachohitajika kwetu kuwepo kukamilisha kazi. Hii siyo kusema kwamba madhehebu tofauti yanatakiwa kuibuka au kupanda makanisa kwa kila moja. Yanaweza kutunza tofauti zao na kupanda makanisa yanayofata mapokeo yao. Kwa jinsi hiyo, Inawezekana kwao kufanya hilo wakati mda huo huo kushiriki na makundi yenye tofauti.


*Mtindo wa Mazoezi*

Wengi wameuliza jinsi gani ni rahisi kufanya ushirikiano na makanisa mengine au mawakala walio na tofauti za kupambanua bila kanisa lao au wakala kupoteza haki yake na kupatanisha mafundisho au mapokeo wanayothamini.

Inasaidaa kufikiria mapana ya aina moja yafuatayo yaliyoonyeshwa katika kielelezo 18:1. kati kati ya duara tuna kanisa letu la mtaa, au timu ya upandaji kanisa, au wakala. Kuwa sehemu ya kundi hilo, wajumbe wanahitaji kukubaliana kwenye maswala ya msingi au kiini cha kuwa ulinganifu katika maisha na huduma. Kwa jinsi hiyo, inawezekana kushiriki na miili mingine ya kiinjili katika eneo la utafiti, maombi, kushirikishana rasilimali, na mafunzo ili kueneza eneo kwa makanisa. Makundi haya tofauti yanashirikiana katika ngazi fulani bila kuachilia kupambanua kwao wakati wakiruhusu makundi mengine kutunza za kwao.

Inawezekana pia kushirikiana na makundi yasiyo ya kiijili katika uanzishaji ambao unafaidisha taifa. Mfano hapa utakuwa kutenda kazi na makundi ya kikristo yasiyo ya kiinjili yanayobishania serikali ya mtaa kupitisha sheria ambazo zinalinda maadili ya jumuia na thamani za Biblia. Mfano mwingine unaweza kuwa kushirikiana kutoa misaada kwa waliokumbwa na majanga.

**Kielelezo 18.1 Uhusiano wa Mzunguko Wa Mahusiano**



### C. Mchanganuo wa Ushirikiano

Wapanda kanisa kutoka madhehebu tofauti huko Urumi wanaanzisha makanisa kwa ajili ya madhahebu yao wenyewe. Kwa jinsi hiyo, wanashirikiana kimadhehebu kwenye maeneo yafuatayo:

- Maombi
- Utafiti
- Mafunzo ya upandaji kanisa
- Mikakati ya kiwilaya

Kila dhehebu linatunza kupambanua kwake lakini linafaidi kutoka kwenye ushirikiano katika kuchangia mawazo na rasilimali (kwa ajili ya mafunzo, matukio ya kufikia nje, n.k.). madhehebu yote yanapata uzoefu mkuu wa ukuaji na kuzidi kama matokeo ya kufanya kazi katika ushirikiano.

## II. KIWANGO CHA KUJITOLEA KATIKA USHIRIKIANO

Kuna ngazi tofauti za ushirikiano zinazowezekana katika kueneza uanzishaji wa upandaji kanisa, kila moja yenye mafanikio inahitaji ngazi kuu ya kujitolea kuwa mshiriki. Hakuna iliyo nzuri wala mbaya. Kila ngazi ya ushirikiano inafaa kwa hali maalumu. Kwa hakika, mara nyingi ni vyema kwa wanachama mashuhuri kuanza hatua ya kupatanisha na, wanapoelewa na kuwa na kujenga ujasiri, kunaongeza ngazi kwenye ushirikiano. Kwa kuwa ushirikiano unatokana na mahusiano, kama unaanza kwenye ngazi ya ushirikiano unaweza au usiweze kuwa na mahusiano unayohitajika kusalimisha harakati wakati wa siku ngumu ambazo zitakuja.

### A. Ngazi 1: Kutokujua (Hakuna Ushirika)

Katika ngazi ya kwanza ya kutokujua, ambayo zaidi mara nyingi ni hali ya kawaida. Huduma za kikristo zinafanya bega kwa bega katika baadhi ya miji, kutokufahamu kwamba wengine wenye imani hiyo hiyo na maono wanahudumu katika eneo hilo hilo. Uanzishaji wa upandaji kanisa unaweza kupishana kwenye jumuia fulani na zingine kutokujaliwa kabisa. Migogoro isiyo ya lazima inaweza kutokea.

### B. Ngazi 2: Kufahamu

Wakati makanisa tofauti au mawakala kwenye eneo moja wanapofahamiana na kutambua wengine kama kikundi halali cha kikristo, hisia za jumuia zinaanza kuendelea.

### C Nagzi 3: Kushaurisha

Kushaulisha kunatokea wakati makundi tofauti kwenye eneo yanapokutana mara moja moja kutaarifiana kuhusu shughuli zao za upandaji kanisa na kujitoa kuombeana.

### D. Ngazi 4: Ushirika au Mtandao

Hili linatokea wakati shirika la kudumu la kushirikisha habari na maombi linapoanzishwa. Washiriki kisha wanakubaliana kushirikiana kwenye miradi maalumu kwa kipindi cha mda mfupi. Kwa mfano, hii inaweza kuwa juhudi za utafiti wa upana wa mji (Kupima ramani ya kiroho) au siku ya maombi na kufunga wakikazia kwenye maeneo ya nyumba yasiyo na kanisa.

### E. Ngazi 5: Ushiriki au Ushirikiano

Kama makundi ya kanisa na mawakala wanaamua kushirikiana katika kuvurumisha kipindi cha mafunzo ya wapanda kanisa au Shule ya Biblia ya mwingiliano wa madhehebu ambayo kila kundi litachangia, ushirikiano uko njiani. Kwa kuchangia rasilimali kila dhehebu litaona makanisa mengi yameanzishwa na kuenea kukua kwa ufalme wa Mungu.

## III. SIFA KUMI ZA USHIRIKIANO WENYE UFANISI

Kielelezo 18.2 kina mchoro unaotambulisha sifa 10 za ushirikiano wenye ufanisi. Uaminifu miongoni mwa washiriki pengine ndiyo sifa muhimu zaidi ya ushirikiano wenye ufanisi. Vile vile, ushirikiano usio na maono wazi au malengo mara nyingi haudumu. Ushirikiano tunaotaka ni ule wa waliojitolea kuona eneo lote limeenezwa kwa washirika waumini wanaoshuhudia.

Katika uzoefu wako mwenyewe wa kufanya kazi katika ushrikiano, ni sifa zipi zilikuwa ngumu zaidi kuzipata kwenye ushirikiano? Kama umekutana na ushirikiano ulioshindwa, ni ipi kati ya sifa ilikuwa inakosekana, ambayo ilichangia kwenye kushindwa kwa ushirikiano?

**Kielelelezo 18.2 Sifa Kumi za Ushirikiano Wenye Ufanisi**

### SIFA KUMI ZA USHIRIKIANO WENEYE UFANISI

1 **Ushirikiano wenye ufanisi unajengwa kwenye kuaminiana, uwazi na kujali kwa wote.**
Ushirikiano ni zaidi ya ulinganifu, upangaji, mikakati na maarifa.

2 **Ushirika wa kudumu unahitaji mwezeshaji au mpangaji**
Huyu ni yule ambaye kwa ridhaa amepewa jukumu la kuleta ushirikiano kwenye kuishi na kutunza moto ukiwaka.

3 **Ushirikiano wenye Ufanisi unaanza ili kukamilisha maono maalumu au kazi.**
Ushirikiano wenye mafanikio unakazia kwa kile (makusudio) badala ya jinsi gani (muundo). Mfumo kawaida unafata kazi.

4 **Ushirikiano wenye ufanisi unaanza kwa kugundua mahitaji miongoni mwa watu wanaofikiwa na kuhudumiwa.**
Huanza kwa kuanza kuandika maelezo ya kawaida ya kitheolojia. Kutokana na mahitaji haya, vipao mbele vya ufalme, vizuizi vya kufanikiwa kiroho, na rasilimali zilizopo au zinazohitajika, vipao mbele vinavyotarajiwa kwa utendaji lazima vichujwe na kukubaliwa.

5 **Ushirikiano ni utaratibu, siyo tukio.**
Kuanza, upelelezi na hatua ya kujengea ushirikiano mara nyingi inachukua mda mrefu. Hata mkutano wa kupelelezea wa mapema zaidi unaweza kuua uwezekano wa ushirikiano. Hatimaye, kuaminiwa kwa mtu kunatakiwa na hilo linachukua mda mrefu kujenga.

6 **Ushirikiano hata unatia changamoto zaidi kutunza kuliko kuanzisha.**
Kuhakikisha kuwa maono yanabakia kuwa hai, mkazo wazi, mawasiliano mazuri, na matokeo ya kutimiza yanachukua mkazo mkubwa na kujitolea kwa mda mrefu.

7 **Ushirikiano wenye ufanisi unajengwa na huduma ya washiriki wenye kutambulika wazi na maono.**
Washiriki wote wanatakiwa kuwa na maelezo wazi ya misheni yao na kuishi kwao kwa hiyo. Vinginevyo, hawataelewa kamwe jinsi "wanavyofaa humo." Kuchangia kwenye picha kwa ujumla, au kufaidika kutoka kwenye juhudi za pamoja.

8 **Ushirikiano wenye ufanisi unatambua, hata kusherehekea, tofauti katika historia zao za ushiriki, maono na uhudumu.** Lakini hatimaye, ushirikiano lazima ukalie kile walichonacho kwa pamoja, kama maono na thamani, na makusudio ya huduma, badala ya tofauti zao.

9 **Ushirikiano wenye ufanisi unakaa umekazia kwenye hatima ya malengo na maono.**
Hawakatishwi na uhitaji wa utendaji wa siku kwa siku. Mara nyingi ni rahisi kukazia kwenye "njia" badala ya kwenye "mwisho."

10 **Ushirikiano wenye ufanisi unatarajia matatizo na kupanga mapema kwa ajili yake.**
Muwe na hakika utaratibu umejengwa kwenye ushirikiano kwa ajili ya kushughulika na mabadiliko, uwezekano, kukatishwa tamaa, wajibu usiokamilishwa, na kwa kifupi yasiyotarajiwa.

*Tambua: "Sifa Kumi" zilizotolewa kutoka kwenye ujumbe na Phil Butler wa mwingiliano wa maendeleo*

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni kwa njia zipi unaweza kuanza kuanzisha ushirikiano na kujenga imani na waumini katika makundi mengine katika eneo lako?
- Ni njia zipi maalumu ambazo wapanda kanisa kutoka katika madhehebu tofauti kwenye mji wanaweza kufaidi kutoka kwenye ushirika kwenye kuzidisha makanisa?
- Ni upi mtazamo wa Mungu wa mashindano kati ya makundi ya kikristo ya kiinjili?
- Jinsi gani wakiinjili wahusiane na wajumuia zisizo za kiinjili katika maeneo yao, hasa hasa makanisa yaliyoanzishwa kama vile Orthodox na Romani Katoliki.

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Fikiria ni makanisa yapi au mawakala katika eneo lako wanaofaa katika mzunguko wako, mzunguko wa pili, wa tatu.
- Fanya marudio ya utafiti (kupima ramani kiroho) kwenye eneo lako na orodhesha makanisa au huduma zilizo hai pale.
- Fanya mawasiliano ya binafsi na viongozi wa makundi katika mzunguko wa kwanza na wa pili na anza kuanzisha uhusiano nao. Anza kuwauliza nini maono yao kwa ajili ya eneo.
- Fikiria kuvurumisha ushauri, mtandao, au ushirikiano unaokazia kwenye kueneza eneo lako kwa makanisa.

## VYANZO

Butler, Phil. *Effective Partnerships*. Seattle, WA: INTERDEV, 1990.

# TABIA YA KIROHO

TABIA YA KIROHO

SOMO LA 14

# Huduma ya Upatanisho

## KUTATUA MIGOGORO

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwaandaa wakristo kwa ajili ya kazi yao ya kuingilia migogoro kwa neema na ujasiri ili kwamba waweze kuifanyia kazi bila kukwaza wengine au kuua uhusiano.

☞ **Wazo Kuu**

- Migogoro ni ya kawaida na haitakiwa kuwa ya kugawanya.
- Utatuzi wa migogoro ni swala la injili.
- Upendo ni sifa kuu ambayo ni ya lazima kutatua migogoro.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo kwenye somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kujua jinsi injili inavyogusa hali zetu za migogoro.
- Kujua jinsi ya kupenda watu katika hali ya migogoro.
- Kushiriki katika utatuzi wa migogoro katika njia ya kibiblia na ya afya.

☞ **Ushauri kwa wakufunzi**

Wakati wa kipindi hiki, tutafanya marudio ya migogoro katika mandhali ya injili ili kwamba tuone njia mpya ya kuikabili. Hili linaweza kuanzisha majadiliano mengi na maswali. Washiriki wanaweza kutaka kujadili jinsi gani na lini unatakiwa kuwatoa watu kutokana na migogoro isiyotatuliwa. Somo hili halizungumzii swala hilo; badala yake linashghulika na vitu vya kufanya kutatua migogoro.

Sura katika somo hili inaweza kuelezewa vizuri zaidi kwa mifano halisi. Itakuwa vyema kushirikisha baadhi ya uzoefu wako mwenyewe, kama inawezekana.

**UTANGULIZI**

Tunaishi katika ulimwengu usio kamili kama wenye dhambi waliokombolewa. Maandiko yanatuambia kwamba "…hakuna anayeishi kwa haki mbele zako (Mungu)" (Zab 143:2). Kwa kiwango chetu, hatuko wakamilifu, kupitia katika utaratibu wa kubadilishwa kidogo kidogo kwenye kivuli cha Yesu Kristo (2Kor 3:18). Katika utaratibu huu, tunasema na kufanya mambo—mda mwingi bila kufahamu—kwamba yanakwaza wengine. Kujisikia na kuibua migogoro kunaumiza. Wakati migogoro ikiwa inatarajiwa katika ulimwengu wote ulioanguka, ukweli ni kwamba kama hatufanyi kazi ya kutatua tutaishia kuharibiana. Kama Paulo anavyosema kwa Wagalatia, "*Kama mkiumana na kulana angalieni msije mkaangamizana,"* (Gal 5:15).

Kipindi hiki kinashughulika na kuchukulia migogoro ambayo inaibuka kati ya watu pekee, kawaida kwa sababu ya upendeleo wa binafsi, na siyo kwa sababu ya baadhi ya dhambi iliyo wazi. Migogoro inaweza kuwa kwa sababu ya matokeo ya dhambi, au haiwezi kutatuliwa na watu pekee waliohusika, inaweza kuwa lazima kwa kanisa kuingilia. (Tazama Somo la Kanisa la 15, malezi ya Kanisa.)

Kama mpanda kanisa, ni muhimu kwako kutunza uhusiano mzuri. Ingawa kipindi hiki kinashughulika na kutatua migogoro, kiuwazi ni vyema kama migogoro inaweza kuzuiliwa. Sehemu ya kwanza ya 'agano' katika kielelezo 15.1 inatoa baadhi ya hatua za kivitendo za kuepuka migogoro.

Jinsi gani tunaendea kuwaleta wengine kwenye mapatano na mmoja kwa mwingine na Mungu? Kama tutakavyoona katika kipindi hiki, Mungu ametupa wajibu na njia ya kushughulika na migogoro.

Uwe na hakika kufanya maombi ya mafunzo haya. Kisha utaweza kuwasaidia wengine kwenye "huduma ya kupatanisha" (2Kor 5:18).

## I. MAWAZO YA MWANZO KUHUSU UTATUZI WA MIGOGORO

### A. Migogoro Haiepukiki Kwa Sababu ya Kutokuwa Kamili Kwetu

Isipokuwa mtu mkamilifu tu angeweza kupita katika maisha haya bila migogoro ya aina fulani (Yak 3:2). Kila mmoja wetu pengine anaweza kusimulia hadithi za migogoro tuliyowahi kuwa nayo na wengine. Wakati tukikubaliana *kitheolojia* na wagalatia 5:24—*"Na hao walio wa Cristo Yesu wameusulubisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake,"*—*kiuzoefu* tunajua tunapungukiwa sana na maisha yasiyo ya dhambi. Kwa hiyo hatutakiwi kuchukuliwa na kushangaa wakati matatizo yanapoibuka. Wakati huo huo, tusingetakiwa kuikubali migogoro kigeni kama sehemu ya lazima ya mtimdo wa maisha yetu kama wakristo. Tungejifunza jinsi ambavyo Kristo angependa tutatue migogoro na kupatana na mmoja kwa mwingine.

### B. Ugumu wa Kukabili

Baadhi ya migogoro inaweza kutatuliwa kwa kukiri kosa, kuomba msamaha kwa mtu mwingine, na kufanya mabadiliko yanayofaa. Migogoro mingine inaweza kuhitaji kukabili. Nini kinakuja akilini mwako unaposikia neno 'kukabili?' Kawaida, tunafikiria kitu fulani mabacho ni 'kinyume.' Dhana zifuatazo za kawaida kuhusu kukabili siyo za kweli hasa, lakini zinawafanya watu kutoshughulika na wengine wazi wazi:

1. Kukabili kawaida kunakatisha.
2. Unapokuwa umehusika katika kukabili, kitu cha muhimu zaidi ni kushinda.
3. Nguvu na kukabili vinashinda mwishoni mwa migogoro.
4. Kukabili na migogoro kunaharibu mahusiano.

Hakuna moja ya maelezo hapo juu yaliyo ya kweli. Lakini kwa sababu mara nyingi tunafikiri kuwa ni ya kweli, yanatuzuia kutokushughulika na matatizo ya kutoka mda hadi mda.

Wakati sisi kama wakristo tunapozungumzia kukabili katika mandhali ya kutatua migogoro, tunazungumzia kumkabili mtu mwingine ambaye tuna migogoro naye kwa roho ya upendo na haja ya kupatanisha. Hii haimaanishi kwamba tunatakiwa kutambaa kuzunguka ukweli na kuepuka mzizi wa swala. Tunatakiwa kusema ukweli kwa mmoja kwa mwingine kwa sababu wote ni wajumbe wa mwili mmoja (Efe 4:25). Tunatakiwa "kutoruhusu mazungumzo yasiyo kamili kutoka midomoni mwetu, lakini kile kilicho msaada wa kujenga wengine na kufuatana na mahitaji yao…" (Efe 4:29).

### C. Matokeo ya Kuepuka Kutatua Migogoro

Ukataaji kuhusika katika utatuzi wa migogoro katika kanisa, nyumbani, kazini, au na marafiki kunaweza kukawa sumu kabisa. Pengine umefundishwa kwamba ni vyema kukaa kimya, lakini hilo linapotokea, hasira zinajijenga ndani na kuanza kula kama kidonda ndugu. Waefeso 4:26-27 inatushauri "kutokuruhusu jua kuchwa ukingali na hasira." Kama tunakuwa nazo "…tunampa shetani kupata kukandamiza."

***Mfano #1***

Mtu katika kanisa lako mpya ana baadhi ya tabia ambazo si rahisi kuishi nazo. Anajaribu kupita katika kanisa lote akijaribu kufanya urafiki bila kuwa na mafanikio. Hatimaye, anajua kuwa hatakiwi na pengine kusimama kushiriki katika kanisa au kuhamia jingine.

***Mfano #2***

Mwanamke katika kanisa ana tatizo la kiusafi. Alitaka mtu wa kuongea naye kuhusu hili. Wakati hao wa kanisani kwake mwishoni walipomkabili, ilikuwa ngumu na kulikuwa na hatari iliyokuwepo katika kulifanya hilo. Mwanamke angekuwa na hasira sana na kuaibika vibaya sana. Lakini lilifanyika kwa upendo na aliweza kulichukua. Upendo ulimaanisha kukabili mwanamke huyu ili kumsaidia, siyo kumsukumia mbali.

*Chukua dakika chache kuelezea jinsi ambavyo ungekabili mtu kwa kila moja ya maelezo hapo juu.*

## II. UTATUZI WA MIGOGORO NI SWALA LA INJILI

### A. Injili Inatuweka Huru Kushughulika na Migogoro

Injili inatuweka huru kukabili watu wengine kuhusu maswala ambayo yametuathiri. Kupata uhuru kikamilifu, lazima kwanza tuelewe udhaifu wetu wenyewe na hofu. Tunapoyaelewa maswala ambayo yametuathiri, tunaweza kukabiliana na kukabili bila vitisho.

Zifuatazo ni sababu za kawaida kwa nini watu wanaepuka hali za migogoro. Hofu zetu kuhusiana na migogoro zinapoonekana, zinakuwa wazi jinsi injili ilivyo swala halisi.

- Kuogopa Kukosa
- Kuogopa kushindwa katika mapambano
- Hofu ya kukataliwa
- Hofu ya wengine watakachofikiri
- Hofu ya kurudishiwa kukabiliwa

> Kuelewa nafasi yako katika Kristo kunaweza kukupa ujasiri kuwakabili wengine wazi wazi.

Unaweza kujihusisha kwenye hofu yoyote kati ya hizi? Kama ni hivyo, kisha pengine tatizo ni lile unalofikiria mwenyewe. Mtu mwenye hofu zilizo hapo juu anaweza kupenda kuhudumu…lakini anakuwa anasumbuliwa na kuhusu sifa njema au hisia za binafsi. Kama, kwa jinsi hiyo, mtu anafikiria kuhusu injili, kisha anaelewa kuwa Yesu ndiye pekee anayetoa haki na sifa njema. Katika jambo kama hilo, hofu hapo juu siyo swala hasa. Usalama wetu na sifa njema ziko ndani ya Kristo. Tunavutwa na haja ya kuhudumu na kupenda , siyo kwa hofu, kuadhibu, au kuonekana vizuri. Watu wanajisikia usalama sana na watu wengine ambao hawaangalii zaidi sifa zao njema wenyewe. Kuelewa nafasi yako katika Kristo kunaweza kukupa ujasiri kuwakabili wengine wazi wazi.

### B. Injili inatoa Kipande cha Kutatua Migogoro

Katika kuliandikia kanisa alilopanda Efeso, Paulo alielezea migogoro iliyokuwepo kati ya Wayahudi na Mataifa vile vile na upatanisho unaopatikana kwa msalaba (Efe 2:11-16). Asili halisi ya injili yenyewe inatuonyesha jinsi ya kupendana hata katika migogoro.

Unapokuwa katika mgogoro na mtu mwingine kiasili tunafikiri, “niko sahihi na wewe una makoso.” Tunapofanya hili tunaegemea kwenye haki zetu wenyewe na kuonyesha upofu wetu kwa upungufu wetu na dhambi zetu. Kwa kifupi hatutaki kukubali kutokupungukiwa kwetu au hitaji letu la msamaha.

Kinyume cha tabia ya “nina haki na wewe una makosa”, ujumbe wa injili unatoa mfano wa tofauti za kuendea migogoro. Katika kutatua hatima ya mgogoro kati ya mwanadamu na muumbaji wake, Yesu aliachilia haki zake, akachukua tabia ya kunyenyekea (Flp 2:5-8) na kuteseka (1 Pet 3:18), kufanya usuluhishi kuwezekana.

Ingeonekanaje kama tungechukua tabia hii kwa wengine? Kutatua migopgoro kusingekuwa rahisi kama tungekuwa tayari zaidi kuchukua nafasi ya unyenyekevu badala ya kulinda kiburi chetu? Hii ni tabia aliyonayo Yesu kwetu. Mfano wake unatuongoza kwenye maisha ambayo tunaweza kuachilia “haki zetu kuwa haki” na kufikiri mahitaji ya wengine zaidi ya yetu (Plp 2:2-3).

## III. MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA JUU YA KUTATUA MIGOGORO

### A. Mathayo 18:15-17

Yesu anatoa picha wazi ya kile anachotarajia kwa wafuasi wake kuhusiana na kutatua migogoro. Soma fungu hili na tambua kanuni Kristo anazotoa za kutatua migogoro.

- Orodhesha kanuni zilizopatikana katika fungu hili
- Tambua kwamba katika mfano wa kondoo aliyepotea unatangulia katika fungu na mfano wa mtumishi asiye na rehema unafata maelekezo haya juu ya migogoro. Nini unachofikiri mandhali haya yanachosema kuhusu mistari ya 15-17?

Kundi moja la wakristo wanaofanya kazi Ulaya wameandika maagano yafuatayo ya uhusiano kutokana na fungu hili. Ni mtindo unaweza kutumika katika kanisa lako.

**Kielelezo 15.1 Mfano wa Agano kwa Utatuzi wa Migogoro**

Sisi, wajumbe wa ____________________ , kuchukulia bila mzaha maelekezo ya maandiko kuishi katika mapatano na makaka na madada na kuuonyesha ulimwengu upendo wa Kristo kupitia upendo wetu kwa mmoja kwa mwingine, kufanya agano na mmoja kwa mwingine ifuatatvyo:

1. Nitakuwa mwangalifu kulinda uaminifu na heshima za wajumbe wengine wa timu kwa kutokubali au kushiriki katika kuzusha kuhusu wajumbe wengine wa timu.
2. Nitatia moyo na kutoa mchango unaofaa kuhusu wajumbe wengine wa timu.
3. Nitafanyia kazi mafundisho ya kibiblia kuhusu kutatua migogoro (Mt 18:15-17a) na msamaha (Mt 6:12; Efe 4:32).
4. Nitakumbusha na kutia moyo aliye na mchango wowote usiofaa kwenda kwa mtu kwa maswali na kutafuta kutatua mgogoro miongoni mwao.
5. Kijuhudi nitatafuta suluhu na kurejesha kwa kila ambaye anaweza kuasi agano hili, na kutarajia kwamba hilo hilo litafanyika kwangu kama nikishindwa.

Kanuni za kibiblia za kutatua migogoro zimetolewa katika Mathayo 18:15-17a kwa dhambi iliyofanywa na mjumbe dhidi ya mwingine:

1. Kila migogoro inapaswa kushughulikiwa kwa mising ya mmoja kwa mwingine. Hakuna mmoja, akiwemo kiongozi wa timu, atakayesikiliza malalamiko mpaka hapo mtu huyo kimaombi amejaribu kutatua mgogoro na mtu mwingine.
2. Hao tu walio kwenye ‘mduara wa kukwaza’ wanatakiwa kuhusishwa kwenye utaratibu wa kusuluhisha.
3. Kama mgogoro haukutatuliwa kwa misingi ya mmoja kwa mwingine, kisha kiongozi wa timu anatakiwa kushaulishwa. (kama kiongozi ni sehemu ya mzunguko wa kikwazo, kisha mjumbe mwingine wa timu , lakini siyo mwenzi wa hao waliohusika, atachaguliwa na hao waliohusika kuamua.)
4. Kama mgogoro bado haujatatuliwa, kisha utaletwa mbele ya kiongozi wa timu na mashahidi wengine wawili (lakini siyo mwenzi).
5. Kama suluhisho bado halijapatikana, kisha jambo litaletwa mbele ya timu yote kwa ajili ya uamzi.

### B. 2 Wakorintho 5:17-21

Tunatakiwa kuendea migogoro kwa njia mabazo kabisa ni tofauti na za kiulimwengu. Kama tulivyosema mapema katika somo hili, Yesu alichukua dhambi zetu ili kwamba tuwe na haki yake (2Kor 5:21). Tambua maneno ya Paulo kwa Wakorintho katika mandhali hiyo.

*Hili lote linatoka kwa Mungu, aliyetupatanisha sisi na yeye mwenyewe kupitia Kristo na kutupatia huduma ya upatanisho: Kwamba Mungu alikuwa akiupatanisha ulimwengu na yeye mwenyewe katika Kristo, bila kuhesabu dhambi dhidi yao. Na ametutolea kwetu ujumbe wa upatanisho. Kwa hiyo tu mawakili wa Kristo, kana kwamba Mungu alikuwa akikata rufaa kupitia sisi. Tunakusihi sana badala ya Kristo: Upatanishwe na Mungu”*(2Kor 5:18-20).

Inafurahisha kuona kwamba mara baada ya Paulo kuelezea upatanisho tulio nao katika Kristo na Mungu, anafanya kujulikana kwamba Kristo ametupatia *huduma ya upatanisho* na kwamba tu *mashahidi wa Kristo*. Kwa kutumia msemo huu, Paulo anamaanisha kwamba tunafanya kwa wengiene kile ambacho Kristo amefanya kwetu.

## IV. KUWAPENDA WENGINE

Unapoangalia kwenye hali ya migogoro, ni muhimu kufanyia kazi kuelekea kwenye kurejeza uhusiano. Kukabili ni nafasi ya kuwasaida watu. Dhumuni siyo kuadhibu au kuharibu. Tabia ya upendo kwa watu tunaofanya nao kazi ni ya lazima.

Mathayo 5:40-41 ni sehemu ya ajabu kuona nini Yesu anasema cha kufanya kwa watu wanaokupinga. Tunawapenda adui na kuomba kwa ajili ya wale wanaotutesa (Mt 5:44). Tumeambiwa kufanya vitu vinavyowashangaza watu, kama vile kutembea maili mbili badala ya moja (Mt 5:41), au kuwapa watu zaidi ya vile wanavyoomba (Mt 5:40). Hiki ni kikwazo cha upendo Yesu anachotuambia kufanya. Hizi ni silaha ambazo anatupatia kufanyia mapambano nazo.

Katika Warumi 12:14-21, tunaona mawazo hayo hayo yakiwa yameonyeshwa na Paulo kama tulivyoona katika maneno ya Kristo. Tabia ya mkristo ya kuonyesha anapokutana na mazingira makatili ni moja ya baraka, kujilinganisha na hao wanaomzunguka, kuishi kwa mapatano na wengine, siyo kulipa kisasi, akifunika mabaya kwa mazuri.

> **Mfano**
>
> Daktari kijana alikuwa akifanya huduma ya jamii ya mwaka mmoja kwenye hospitali ya serikali. Wasimamizi wake wote hawakuwa wakristo na walimpa mda mgumu. Baada ya miezi kadhaa, alikuwa tayari kuacha na kurudi nyumbani. Aliposhauriwa kuhusu jinsi ya kutatua migogoro, aliambiwa kushinda ubaya kwa kufanya wema kwa hao waliokuwa wakimtesa. Suluhu yake rahisi ilikuwa kuoka keki na kuipeleka kwa msimamizi wake kama zawadi. Kubuni huko kudogo, kuongezea na maombi, kulivunja upinzani wa msimamizi wake. Miezi yake iliyobaki ya kuhudumia jamii ilikuwa tofauti na ya nyuma. Siyo hali zote zitatatuliwa kirahisi hivyo. Lakini lazima tuamini kwamba kuna utatuzi katika kila hali, kwa Yesu Kristo ni mwenyezi dhidi ya ulimwengu huu.

## V. MSAADA WA VITENDO KWENYE KUTATUA MIGOGORO

### A. Jinsi ya Kuendea Migogoro

1. *Tambua nia yako binafsi*

   Ni ya lazima kuangalia kwa kile unachofikiria wakati unapokuwa katika mgogoro na mwingine. Je hili limevutwa na kiburi au haja ya kupenda kuhudumu? Kamwe hutakuwa na nia safi, lakini ni muhimu sana kwamba unajua tatizo hili na kumuomba Mungu kuliweka wazi katika maisha yako kabla hujaenda na kuzungumza kwa mtu mwingine kuhusu tatizo hili. Kumbuka kibanzi na boriti (Mt 7:3-5).

2. *Usidhani tu kuwa unaelewa hali yote.*

   Dhana tu ni kitu kibaya zaidi katika mgogoro. Usidhanie tu kuwa unalijua kabisa na usikilize upande mmoaja tu. Dhani tu kuwa hujui hasa historia yote na ni muhimu kwamba unatafuta kujua. Kusikiliza na kuuliza maswali ni kwa lazima hapa.

   > **Mfano**
   >
   > Jumapili moja asubuhi katika jengo mpya la kanisa Ulaya kulikuwa hakuna ubao wa kuonyeshea maandishi. Kila mmoja alidhani kuwa ulikuwa umeibiwa. Miziki yote ilibidi ibadirishwe na ibada ilicheleweshwe. Mwishoni, mmoja wa wajumbe alikuja nao. Viongozi kiasili walidhani kuwa alikuwa ameuazima na walimkasirikia kwa kutorudisha kwa mda unaotakiwa. Baadaye, waligundua kuwa huduma nyingine iliyotumia jengo hilo hilo walikuwa wameazima ubao huo na kuukabidhi kwake alipokuwa akiingia kwenye jengo ili kwamba wasipatwe na hali ya aibu!

3. *Anza na wewe mwenyewe*

   Kama tatizo lipo kati yako na mtu mwingine, ni vizuri kudhani kuwa umefanya kitu fulani kuumiza mtu mwingine. Kama unaielewa injili na ilichofanya Kristo kwako, kisha hauko juu kufanya hili. Itakuwa msaada kutafuta jinsi ulivyowaumiza ili kwamba uweze kulisahihisha. Tambua mzizi uliosababisha mgogoro. Hali ya kawaida ni kuangalia katika uwazi, sehemu inayoonekana ya mgogoro. Kwa mfano, ngoja tudhani kuwa tumemteta

mtu mwingine bila yeye kuwepo, na neno limemrudia mtu huyo…na mtu huyo sasa ametukasirikia. Kitu cha wazi ni kwamba tumemteta, pengine kwa kurudia baadhi ya vitu ambavyo havikuwa kweli. Lakini swala halisi, mzizi wa swala, ni ukosefu wa uaminifu kwa mtu huyo wa kutunza heshima yake. Kutokuwa na uaminifu huko ndicho tunachotakiwa kushughulika nacho. Inawezekana tumekuwa wa kutatiza katika kuteta kwa sababu tulikuwa na wivu na mtu huyo na kutaka kuona akingolewa chini kutoka kwenye nafasi yake. Tena, wivu ndiyo kinachotakiwa kushughulikiwa, kukiri na kuomba toba kwa ajili yake.

4. *Anza kwa kutia moyo*

Ni vema kuanza kwa kutia moyo unapokuwa unaleta upinzani kwa mtu mwingine. Lazima kutakuwa na vitu amabavyo ni vizuri kuwahusu, na unahitaji kulainisha unachotaka kusema kwa baadhi ya vitu vizuri vile vile. Kutia moyo ni kuzuri kwenye moyo (Mit 15:30; 25:11).

**B. Kuchukulia Upinzani  Kutoka Kwa Wengine**

1. *Kuliangalia kimakusudio.*

Upinzani mwingine ni nzuri na mwingine ni mbaya. Baadhi unasaidia na mwingine ni sumu. Usichukulie upinzani kwa kadiri ya uso. Ushikirie mbele yako na uchunguze kwa ajili ya ukweli. Kawaida kuna kibunda cha ukweli katika upinzani wote. Chukua vipande ambavyo ni msaada na vitumie kwenye maisha yako na vingine vilivyobaki vitupe.

2. *Usiweke moyoni mpaka inapothibitishwa.*

Angalia upinzani na wengine kabla hujauchukulia bila mzaha. Uliza watu wanaoaminiwa kama wanakubaliana na uchunguzi wako.

3. *Sikiliza kwa kutazama, “Ninafurahi tu kwamba hawajui chochote kabisa."*

Elewa injili inarahisisha kuishi na upinzani. Tunajua maisha yetu yako ndani ya Kristo na tunajua tu wenye ‘dhambi.’ Kuona dhambi si kitu cha kushangaza sana kwetu. Wakati mwingine inaumiza kuona jinsi dhambi zetu zinavyoumiza wengine, lakini kuziona na kuzitubia kunaleta utukufu zaid kwa Yesu, na hilo ndilo tunalotaka. Injili ina maana kwamba upinzani siyo kitu cha kufisha, wala siyo kisichotarajiwa. Ni njia ya ukuaji katika neema anayotoa Kristo.

## SULUHU

Mgogoro usiotatuliwa unaweza kuwa moja ya kitu cha kuharibu kwenye maisha ya binafsi na maisha ya mwingiliano. Kama una mgogoro ambao haujatatuliwa na muumini mwingine, mfanyakazi mwenzako au mmoja katika familia, chukua hatua sasa kutafuta kupatana. Na tupate ujasiri wa kuwapenda wengine kama Yesu anavyotupenda.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

### KWA NINI WATU WANASITA KUKABILI WENGINE?

- Lini kukabiliwa na mtu mwingine kumekuwa baraka hasa?
- Ni kwa njia zipi inaweza kuwa sumu  kuepuka kukabili kaka au dada katika Kristo kuhusu kikwazo?
- Ni vitu gani vingine unaweza kufanya kuweka kukabili kuwa rahisi kuchukua?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Mazoezi yafuatayo yatakusaidia kufanya mazoezi ya utatuzi wa mgogoro katika mahusiano yako binafsi:

- Fanya marudio ya mahusiano yako na ona kama kuwa watu ambao umekwaza—au waliokwaza na wewe.
- Tambua mzizi inayosababisha migogoro—na shughulika na swala la mzizi.
- Ongea na mtu na tafuta kupatana na utatuzi kwenye mgogoro wenu.

TABIA YA KIROHO

SOMO LA 15

# Unyoofo wa Maadili ya Wapanda Kanisa

## KUSHUGHULIKA NA PESA, JINSIA NA UWEZO

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwatia moyo wapanda kanisa kufurahia vitu vizuri Mungu alivyowapa, wakati wakiwa na tahadhali ya mitego Shetani anayotega ya kutumia pesa zetu vibaya, jinsia na uwezo.

☞ **Wazo Kuu**

- Waumini waaminifu wanatakiwa wakubali shauku zao za kushindwa katika unyoofu wa maadili.
- Shetani kawaida anashambulia maeneo ya fedha, jinsia, na uwezo.
- Bila usafi wa asili, unaopatikana kwa neema ya Mungu, hatuwezi kuwa wazuri.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa baadhi ya shauri la Shetani ambalo linamfanya kutokufurahia utoaji wa muumbaji wetu.
- Kujua kanuni za msingi za kufanya kwa juhudi unyoofu wa maadili katika maeneo ya kusikilizana kwa wote

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Ingeweza kuwa rahisi kuangukia katika kipande cha kusimulia mambo mengi ya kejeli za kushindwa kunakojulikana kwenye taifa au kulinganisha uovu wa siku zetu. Kufanya hivyo kunaweza kukosesha wazo. Tumeshajua vya kutosha kuhusu jambo la aibu; kinachotakiwa ni utatuzi. Chagua endapo kuinua kielelezo cha hakika cha maandiko NA kutoka katika uzoefu wa maisha yako na huduma.

### UTANGULIZ I

Shetani ni mbunifu sana. Fikiria kushindwa kimaadili katika huduma ya kikristo; mengi zaidi yanahusiana na pesa, jinsia au uwezo. Mungu amewapa watoto wake vipawa vizuri, lakini matamanio yetu ya dhambi, kujipatia binafsi au fahari, mara nyingi kunapelekea kwenye utumiaji wa fujo wa utoaji wake. Tunaweza kuishiwa kirahisi na unyoofu wa maadili. Bado, tunapokazia kwenye utukufu wa Mungu, rasilimali zetu, tamaa za mwili za kibinadamu, na mguso vyote vinaweza kuwa huduma nzuri kwenye ufalme.

> Uongozi kawaida ndiyo uchaguzi unaolengwa. Adui wa imani zetu atatafuta kubonyeza mguso wetu au kutuondosha kutoka kwenye uongozi kwa kutupa majaribu matamu ya fedha, jinsia na uwezo.

Lusifa anaelekea kutukandamiza kufikiri kwetu sisi, tulio chini kidogo kuliko maalaika (Ebr 2:6,7) kuwa tutashiriki katika hukumu yake. Mdanganyifu wa nafsi zetu anatutaka kuwa na mashaka juu ya umuhimu wa unyoofu wa maadili. Yeye aliyetaka kuiba utukufu wa Mungu anaendelea kuzungumzia kuiba enzi na uchaji ambao utainuka kwa Mungu kutokana na jumuia kumwabudu ambako tutasaidia kuanzisha. Uongozi kawaida ndiyo uchaguzi unaolengwa. Adui wa imani zetu atatafuta kubonyeza mvuto wetu au kutuondosha kutoka kwenye uongozi kwa kutupa majaribu matamu ya fedha, jinsia na uwezo. Njia zake siyo mpya.

Unyoofu wa maadili wa wapanda kanisa kinguvu unaathiri huduma kimapana na marefu. Watu wanavutiwa kwenye injili na wanafuaswa kwenye ukomavu na huduma—ni mitindo ya namna gani watafuatisha? Tabia ya wapanda kanisa siku zote itaweka alama yote katika majengo ya kanisa la mtaa na kwenye sifa njema ya mapana ya eneo au juhudi za taifa. Tu wadhaifu, lakini mkuu ni aliye ndani yetu kuliko huyo aliye ulimwenguni (1Jn 4:4).

## I. MATATU YANAYOPENDWA; PESA, JINSIA NA UWEZO

### A. Mali

Tunapozungumzia mali, tunarejesha siyo tu pesa lakini pia ni kwa vitu vyote au rasilimali, endapo ni vyetu wenyewe, au hizo za kanisa. (Tazama pia Somo la Uwakili Mwema katika Mwongozo wa Nne.)

#### 1. *Tahadhali*

Kutokea mwanzoni, mwanadamu alikuwa ameelekezwa kumiliki na kutawala dunia. Vyote vilikuwa vimetolewa na muumba kwa mwanadamu, aliyeumbwa wa juu kupita viumbe hai vyote. (Mwa 1:28-30). Tunatakiwa kuwa na mali na kuziangalia kama mawakala kwa Mungu. Pesa, mali na rasilimali, kwa ujumla, vinapatikana na tunatarajiwa kuvitumia kihekima. Tatizo ni kwamba mara chache tunafikiri kuwa tuna vya kutosha; tunatilia shaka hekima ya Mungu. Kupenda pesa kunaitwa mzizi wa maovu yote (1Tim 6:10). Uchoyo, wivu, tamaa na dhambi nyingine zinawashwa na tamaa inayoonekana ya kutotosheka ya macho. Kwa hiyo, mafundisho ya Yesu katika Biblia ni pamoja na marejeo mengi ya fedha kuliko kitu kingine—hata zaidi sana kuliko wokovu. Mwokozi wetu anajua mahangaiko ya mwanadamu na ametupatia tahadhali ya kutosha kuhusu hatari ya kurithi katika kutafuta mali. Mungu alikusuidia utoaji huu kuwa mzuri (na UNAWEZA kuwa) lakini mara nyingi tumefungua mlango kwa Shetani kuutumia kwa madhara.

#### 2. *Tabia*

> ... mahali mioyo yetu ilipo ndipo kutakuwa na mali zetu. Tunahitaji kushangaa kwa nini baadhi ya mioyo yetu ni baridi kama ulivyo muguso wa chuma cha thamani?

Wakati Yesu alipokuwa amejaribiwa nyikani, kutoshereza mahitaji ya mwili lilikuwa jaribu la kwanza (Mt 4:1-11). Akitiwa changamoto ya kubadili jiwe kuwa mkate, Bwana alijibu kwamba haikuwa kwa mema tu kwamba mtu angeishi, lakini kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu. Kutafuta chakula, pesa na mali havitakiwi kuwa kipaombele chetu. Kizuizi dhidi ya mazoea ya kutafuta maarifa na kufanya njia za Mungu. Kila moja ya vitu hivi ni muhimu. Wanafunzi walikwenda kuvua kwa ajili ya chakula na kipato. Yesu aliwatia moyo wafuasi kulipa kodi yao, na mali zilizokuwa zinachangiwa katika kanisa la zamani. Lakini swali ni kipao mbele; mahali mioyo yetu ilipo ndipo kutakuwa na mali zetu. Tunahitaji kushangaa kwa nini baadhi ya mioyo yetu ni baridi kama ulivyo muguso wa chuma cha thamani?

Mfanya kazi anastahili ajira yake (Lk 10:7), na yule ambaye hatunzi familia yake ni mbaya zaidi kuliko kafiri (1Tim 5:8). Mtawala tajiri kijana anaweza akawa aliamini na kudhani alikuwa akizifanyia kazi kanuni hizo (Lk 18:18-30). Kwa jinsi hiyo, Yesu akiitikia kwenye swali lake kuhusu uzima wa milele, alimwambia kijana tajiri kuuza kila alichokuwa nacho kuvisambaza kwa masikini. Kiongozi kijana tajiri asingefanya hivyo—kipao mbele chake kilikuwa hakifai.

*Vipao mbele vyetu lazima vipatikane kutoka kwenye ukweli kwamba kila tulichonacho ni cha Bwana. Tumenunuliwa kwa bei ya thamani na siyo vyetu wenyewe.* Zaka na sadaka ni njia za kurudisha sehemu kufanya umoja wa kazi za kikristo. Hata hivyo sisi sote, hasa viongozi ambao ni vielelezo, wanatakiwa kuwa wasimamizi wa Mungu wa pesa zote, mali na rasilimali walizonazo. Kuhamisha matumizi ya hazina iliyotolewa kwenye huduma ya kikristo kwa nafasi za viongozi wote; kuwa wakili mwenye hekima ni pamoja na kuwahusisha hao waliotoa rasilimali au wengine wanaoshiriki wajibu kwenye matumizi yake. Tabia ya uwakili mzuri inatakiwa kutumika endapo kiasi ni kikubwa au kidogo. Kwa hiyo, fimbo nzuri ya kupimia wakati unaangalia viongozi wanaoibuka ni; "Umekuwa mwaminifu kwa vichache; nitakuweka msimamizi wa vitu vingi" (Mt 25:21).

## B. Usafi wa Kijinsia

Tunamaanisha hali ya jinsia ya mwanadamu na kusherehekea ukweli kwamba Mungu ameumba mwanaume na mwanamke. Tuko tofauti na tumekusudiwa kwa mmoja kwa mwingine. Utatu wa Mungu kichwa mwenyewe anaonyesha uzuri wa utaratibu wa mahusiano. Kwa sababu tumeumbwa kwa ajili ya ushirika, inaleta maana kwamba tunatarajia vipande vya kimungu kwa ajili ya mahusiano Yetu katika Kristo, endapo kama upo kati ya mme na mke, binti na baba , mwanamke na mwanaume. Tunatarajia kuvutia kwenye mahusiano; hii ni sehemu ya uumbaji wa Mungu. Tutafikiria hali ya kijinsia ya mwanadamu kama mung'ao wote—kutoka kwenye utambuzi mwepesi wa tofauti kwenda kwenye ukaribu zaidi wa uhusiano wa kimwili.

*1. Tahadhali*

Bustani ya Edeni ilishuhudia Adamu na Eva wakitembea wao kwa wao na muumbaji wao; jinsia zao zilikuwa nzuri sehemu inayokubaliwa na mpango wa Mungu. Kwa mpango wa Mungu, mwanamke alikuwa ametokana na mwanaume na alikuwa mshiriki ambaye uzuri ulikuwa unakubaliwa sana na mwanaume. Lakini dhambi ilipoingia ulimwenguni kwa kutokutii, hofu na aibu ilifatia iliyopelekea Adamu na Eva kujifunika jinsia zao.

> Mungu anatarajia na anatia moyo hatua nyingi za mahusiano... lakini pia ... kuzuia ukaribu zaidi wa uhusiano wa shauri moja kwenye ngazi ya juu zaidi ya kujitolea.

Mungu anatarajia na anatia moyo hatua nyingi za mahusiano kati ya wanadamu, lakini pia anatoa kanuni kwenye mahusiano hayo na kuzuia ukaribu zaidi wa uhusiano wa shauri moja kwenye ngazi ya juu zaidi ya kujitolea. Viongozi wa kikristo hawajatolewa udhuru kutoka kwenye tamaa kali ya mwili. Kibinadamu, katika kuvutwa na uasi kwamba sisi, na siyo Mungu, tunajua zaidi, kwa kujivuna tunararulia mbali hayo majani ya mtini, tukitafuta kufunua na kuendekeza kwa kile kisicho chetu. Mungu hadhihakiwi; njia zake ni kamili.

*2. Tabia*

Kama Yesu angeruhusu majaribu ya Shetani kukubali utajiri wote wa ulimwengu, kisha angewajibika kwenye ufahari—dhambi ya fahari mwenyewe kama hatima ya kusudi la maisha. Kristo alikataa kufanya "kinachoonekana kizuri" na kurudisha kwa maandiko, "kaa mbali nami Shetani! Kwa kuwa imeandikwa: "Mwabudu Bwana Mungu wako, na mtumikie yeye tu '" (Mt 4:10).

Kama wapanda kanisa, tu viongozi na maono—tunajua tunakoelekea. Kwa hiyo ni kwa kuendeleza na kutunza tabia ya maadili. Fikiria mfano wa jasiri wa Agano la Kale—Yusufu alikubali viwango vya Mungu. Alikuwa mwaminifu, hata alipofanyiwa kama mwana anayependelewa au mtumwa aliyefungwa (Mwa 37). Aliepuka hali za kujaribu (Mwa 39). Yusufu alikataa kujitia katika dhambi.

Sehemu kuu ya kuweka jinsia ya mwanadamu katika hali inayofaa, sehemu bora ni kushughulika na hao wenye jinsia tofauti katika mtindo unaofanana na Yesu; kwa heshima. Mahusiano yanayofaa ni pamoja na tabia ambayo inapelekea kwenye kufanya maamzi. Heshima ni kipawa cha neema. Kinadhihirisha, kupitia sisi, thamani anayompa mtu Mungu. Inamuonyesha mtu mwingine kwamba unamthamini. Heshima ni kitu fulani tunachompa mtu bila wao kukifanyia kazi na haitegemei kujisikia kwetu au kutoa kwao heshima kwetu. Waefeso 5 inatuelekeza kushughulika na wenzi kwa njia Kristo anazoshughulika na kanisa—kwa heshima. Hakika, kuonyesha kama huko kwa thamani ya juu ambayo tunatakiwa kuonyesha kwa hao walio na jinsia tofauti, kwa hakika, ni usafi unaosaidia kulinda shauku ya kibinadamu na kuchukua nafasi. Kwa kuwabariki wanawake au wanaume kwa njia hii, tunaweza kujilinda dhidi ya kutumia vibaya kipawa cha jinsia ambacho Mungu ametupatia.

Kwa hakika, watu wengi wanatathamini wengine kufuatana na tabia zao. Uzinifu ni jaribu kuu la tabia kwa mwanaume au mwanamke yeyote. Kigingi kikuu cha ndoa zetu ni kikwazo kizuri—kufanya uhusiano wa upendano. Lakini, maelekezo siyo tu kwa hao walioana, kwa sababu majaribu ni dhahiri kwa wote waliooana na mabachela wapanda kanisa.

### C. Mamlaka na Nafasi

Kama kiongozi katika ngazi fulani, kwa mamlaka na/au nafasi, tuna mguso mahali fulani na kwa namna fulani. Kujitokeza kwa mguso huu ni uwezo. Lakini ni kiburi ambacho kawaida kitaonyesha cha nani ni kizuri—changu au cha wengine—kwamba uwezo huu utatumika. Uwezo unaweza kuwa msukumo wa uovu au nguvu za mazuri. Kama wapanda kanisa, tunatamani kwamba mguso wetu uwe wa nguvu na wa kutumika kwa ajili ya kuwezesha kimungu wengine kuwa yote ambayo Mungu aliyowakusudia.

1. *Tahadhari*

Mwaka 1986, wakati Duvalier, mtawala wa mabavu wa Haiti, alipokimbilia Kisiwa cha Karibiani, raia na utatu wa jeshi walikubaliana kutumika kipindi cha mpito na kupanga uchaguzi wa kidemokrasia. Maelezo zaidi ya kitakwimu ya ubadhilifu wa madaraka yanaweza kupatikana kwa uhaba sana. Katika miezi iliyofuata, kwa kifupi generali wa jeshi mwenye sauti nyororo aliyevikwa madaraka alishamili. Kila alipoonekana hadharani alikuwa na medali zaidi pamoja na utepe kwenye unifomu na uso wake uligeuka kuwa ulioumbuka kwa kusaga meno. Ubadhilifu wa madaraka ulikuwa unamvamia; nafasi ya kugusa kwa ajili ya haki na uhuru ilikuwa imetolewa kwenye mimbari ya kiburi na kujipatia binafsi.

> ... uwezo ni upanga wenye ncha mbili; unaweza kufungua mapito kwa ajili ya kazi ya Kristo au, kuibadhirisha, unaweza kukata ncha kujinufaisha.

Hakuna mpanda kanisa anayefanya uinjilisti, ufuasishaji au kuandaaji kwa ajili ya huduma anayetumaini kitu chochote zaidi ya nafasi ya mguso wa kuaminiwa kwao kwa wema, kwa ajili ya Bwana wetu. Tunajaribia aina hii ya uwezo, kwa kuwa tuko tunachukua kuongoza. Lakini uwezo ni upanga wenye ncha mbili; unaweza kufungua mapito kwa ajili ya kazi ya Kristo au, kuibadhirisha, unaweza kukata ncha kujinufaisha. Kawaida ni hatari kwa kiongozi anayevuka mipaka na anayetumia uwezo kuwasha kiburi cha maisha.

2. *Tabia*

Ibilisi alimfanyia hila kadhaa Bwana wetu, peke yake mwanzoni mwa huduma yake. Akimjaribu kujirusha kwenye mnara na kujaribu kama baba angetuma malaika wa kumwokoa, Ibirisi alitaka Yesu kuwa fidhuli kabisa kabisa, na asitumie imani yake. Kama Yesu angejitoa kwenye dhambi ya ufidhuli, kusingekuwa na msalaba au wokovu. Ufidhuli, ambao unasaidia kwa mda tu, ni uharibifu kwa mda mrefu ujao. Kristo alijibu kwa maandiko, akimkemea Shetani kwa kumuweka Mungu kwneye jaribu. Sisi wapanda kanisa tunajaribiwa mara kwa mara kwa lijamu zetu za madaraka, kufanya kila kinachoonekana kuwa bora kwa kipindi kifupi; kufanyia mazoezi ufidhuli. Bado wazo letu la uongozi ni tofauti kabisa kutoka kwenye kipande cha ulimwengu cha kutawala. Uchukuaji madaraka kimungu unaoana moja kwa moja kwenye kuelewa kwetu na kufanyia mazoezi uongozi unaofanana na wa Kristo (cf. Somo la Uongozi, “Uongozi wa Kitumishi” katika Mwongozo wa 4).

Maono yaliyo ya kiwango cha Kimungu kwa ajili ya wakati ujao na mkazo kwenye matokeo yanayotarajiwa yanatakiwa kuwafanya wapanda kanisa kumtegemea sana Mungu. Ni nguvu yake peke yake inayoweza kutuandaa kwa ajili ya mwendo. Na pale tulipo, kama viongozi, na tukusanye utii utupasao kutoka kwa wafuasi tofauti tofauti, ni muhimu sana kwetu kuelekeza utii wao, na wetu, wa kifalme kwa Kristo. Viumbe hai hawakuumbwa kusaidia uhudumu na madaraka yaliyotolewa sasa kimfululizo kipekee kwa wanadamu viongozi. Kuhakikisha kwamba hatutumii madaraka isivyopasa, ni lazima tushirikishe huduma na kuanzisha kuwajibika katika juhudi zetu za upandaji wa kanisa.

## II. KANUNI ZA JUMLA KWENYE UNYOOFU WA MAADILI

Tunatakiwa “kwanza kutafuta ufalme wa Mungu na haki yake” (Mt 6:33). Labda tuwe tumeweka vitu vya kwanza kuwa vya kwanza, vitu vya pili havitafata. Bila kuwa na usafi wa kimungu, usafi wa kawaida unashindwa. Bila *neema* ya Mungu, hatuwezi kuwa wazuri. Bila *upendo*, haki inageuka kuwa usugu. Bila *tumaini* ujasiri unageuka kukata tamaa kipofu. Bila *imani,* hekima ya kiulimwengu ni ujinga kwa Mungu. Ngazi mbili, za kikawaida na za kimungu, zinaning’inia pamoja (Kreeft, pp. 72,73).

Majaribu yako wazi, lakini tunatakiwa kutokukatishwa tamaa; ushindi unapatikana. Tuna ukweli wa kutegemea na ushindi wetu dhidi ya majaribu ni ushuhuda wenye nguvu kwa wote wakristo na wasio wakristo. Ngoja tuwe wafuatishaji wa Kristo, ambaye "alijaribiwa katika kila tabia kama kwa mwanadamu ...na hakufanya dhambi " (Ebr 4.15).

Kuwajibika kwa wengine kumethibitisha usaidizi unaozuia kushindwa na ni chanzo cha kutia moyo kwa walio wengi. Uwajibikaji kama huo unaweza kuwa kati ya mmoja au zaidi ya marafiki walio karibu au wafanyakazi wenzio. Wakati mwingine, kundi dogo linalokazia katika hili, pamoja na maombi, ushirika au mafunzo ya Biblia, pia inasaidia. Baadhi wanapendelea mfumo wa kawaida wa kuwajibika na wengine wanatumia njia yenye mfumo kidogo, lakini kanuni inabakia kuwa ile ile; "wawili ni bora kuliko mmoja" (Ecc 4:9,10). Kwa kuwajibika, tunalazimika kwenye mapambano yetu ya unyoofu wa maadili..

Mbio zinashindwa na hao wanaovuka msitari. Ustahimilivu ni muhimu sana kwa kuwa viongozi wengi wanaokimbia vyema lakini wachache wanaomaliza vyema. Biblia yenyewe inatoa maelezo ya kutosha juu ya hili. Ngoja tukimbie mbio za ushindi. Tunafikiria maisha ya Yakobo na kuamua kuangalia zaidi ya misuko suko yetu kwa wakati ujao. "Lakini anaijua njia ninayochukua; atakaponijaribu, nitatokeza nje kama dhahabu" (Yak 23:10). Kustahimili huko kunatoka katika:

- kuangalia ***unyoofu wa ndani***; "na tuweke kando kila mzigo mzito na dhambi ituzingayo kwa wepesi, na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu" (Ebr 12:1).
- kuangalia ***uimara kwa juu***; "Tukimtazama Yesu mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu" (Ebr 12:2).
- kuangalia ***huduma kwa nje***; "Tafuta kwa bidii kuwa na amani na watu wote na huo utakatifu; ... Mkiangalia sana mtu asiipungukie neema ya mungu" (Ebr 12:14,15).
- Kuangalia ***kwa mbele kwa matumaini***; "Kwa kuwa tunapokea ufalme usioweza kutetemeshwa, ngoja tuwe na shukurani, na kwa hiyo tumwabudu Mungu kwa ibada inayokubalika pamoja na unyenyekevu na kicho" (Ebr 12:28).

## III. FAIDA ZA UNYOOFU WA MAADILI

### A. Maisha ya Amani

Wakati matendo yako yanapoamsha kuamini kwako, unapata amani ya ndani. Kutokuwa na usingizi usiku na hisia za kujisikia maumivu kwa ndani kunaweza kuwa matokeo ya kupatanisha unyoofu wa mtu mwingine.

### B. Maisha Yaliyolelewa Vyema

Hakujawahi kamwe kuwa na kiongozi mfanisi ambaye hakuwa na kujiheshimu mwenyewe. Unyoofu ni jiwe la ufunguo ambao sehemu yote ya maisha iliyobaki inapumzika. Mpanda kanisa aliyelelewa vya kutosha kuweza swala KUU la unyoofu wa maadili atakuta kwamba malezi yanayohitajika kushinda maeneo mengine yote ya maisha yanapatikana kiurahisi zaidi.

Mpanda kanisa aliyelelewa vya kutosha kuweza swala KUU la unyoofu wa maadili atakuta kwamba malezi yanayohitajika kushinda maeneo mengine yote ya maisha yanapatikana kiurahisi zaidi.

### C. Kufuatwa kwa Ajili ya Kuheshimiwa

Wapanda kanisa wafanisi wanajua na kuelewa kwamba heshima na mvuto unakua kutokana na unyoofu. Unyoofu ni ufunguo wa kutegemeza uongozi kwa kipindi kirefu.

### D. Urithi wa Hakika

Wapanda kanisa wanaoacha urithi wa unyoofu wa maadili wanaweza kuacha zawadi kupita yote ya waliyokamilisha wakati wa kuzalisha kusanyiko la mtaa.

## IV. UNYOOFU WA MAADILI UNAWEZA KUWA WA GHARAMA

Wapanda kanisa, bachela au waliooana, peke yao au katika timu, siyo lazima kwamba watakuta bara bara ya unyoofu wa maandili ikiwa imesakafiwa vyema. Baadhi ya mapambano makali zaidi yanaweza kuwa chombo ambacho Kristo anatumia kutusafirisha kwenye tabia iliyoimarika kwa undani zaidi au ushuhuda unaoonekana zaidi kwa ajili yake na njia zake. Tumehakikishiwa uwepo wake na nguvu zake tunapotembea naye katika shauri moja. Lakini hatujahakikishiwa mafanikio kwa nje. Hatujui kama Zakayo kamwe alipata tena utaili wake wa kwanza (Lk 18:18). Yusufu alitumikia mda wa kifungo, kwa uongo akashitakiwa, baada ya kukimbia badala ya kudanganya na mke wa Potifa (Mwa 39.12-20). Na akaendelea kuwa mtoro baada ya kukataa kuchukua madaraka na “kugusa mpakwa mafuta wa Bwana” Alipokuwa na nafasi rahisi ya kumuua Mfalme Sauli Pangoni (1Sa 24).

Pengine umewindwa na dhambi zako, kutoka mda ulipoharibu unyoofu wa maadili. Kiukweli ni tunu na inayozaa mema. Na tuungame dhambi zinazotuzinga kwa wepesi (Ebr 12:1) na kumshika Mungu katika maneno yake. Ni mwaminifu na wa haki kutusamehe dhambi zetu (1Yn 1:9). Lakini tunaweza kuwa na madeni ya kulipa, magonjwa ya kutibu, au mahusiano ya kutengeneza. Ngoja na tuwajibike kwa yetu yaliyopita lakini bila kuruhusu jana kuonyesha utii wetu wa leo na kesho. Kutoka sasa na kuendelea, unyoofu wa maadili unaweza kuwa alama ya uongozi wetu na juhudi zetu za upandaji kanisa zinaweza kuvuna faida ya tabia ya nyoofu.

### SULUHU

Wapanda kanisa, tusidanganywe. Tunaweza tusiwe Noa, lakini ulimwengu unawacheka waumini. Wasio wakristo wanaendelea kushaua tabia ya dhambi. Maadili ya ulimwengu ni kama meli ambayo imepoteza usukani (unyoofu wa maadili umetoweka) na kilicho kibaya zaidi, hawataweza kujua mwelekeo kama hawatapata usukani (ukweli umekataliwa kabisa). Tuna misheni ya kuokoa maisha na kufanya hili kutataka tabia ya kufanana kwetu kidogo na Kristo na unyoofu wa maadili. Neno la Mungu, Biblia, inatuonyesha mwelekeo. Makanisa ya mtaa ni usukani wa kuendesha jamii kwa chumvi na nuru—kuashiria nyuma kwenye unyoofu wa maadili na kuwa baraza la ushirika wa kimungu. Kila mtu pekee anayemfata Kristo, anayefanya kazi ya uinjilisti, anawaita wenye dhambi kupatana na Mungu, na hivyo kwa kila mmoja

Mpanda kanisa, u wa kimkakati kwa misheni ya Mungu duniani. Kumbuka u mali ya nani, na ufanye kama yeye. Unyoofu wa maadili kwa wapanda kanisa ni msingi wa lazima.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Jinsi gani kushindwa binafsi katika unyoofu wa maadili kunadhuru huduma ya hadharani? Vipi kuhusu ufahamu wa kisiri wa dhambi ya mtumishi mwingine?
- Kama watu wakishindwa katika eneo moja kuna uwezekano wa kushindwa kwenye eneo jingine? Jinsi gani kipande cha nguvu cha Kimungu katika eneo moja kinasaidia kuhakikisha unyoofu katika maeneo mengine?
- Kutunza maadili mema kunakuwa rahisi kadiri unavyokaa mda mrefu katika huduma?
- Jinsi gani uwajibikaji imara kwa waumini wengine unasaidia kuendeleza na kutunza unyoofu wa maadili?
- Wakati jamii ikisisitizia kubadili sheria kuhusu unyoofu wa tabia unaofaa, nini tunachoweza kufanya ili kufanya mapatano yanayoendelezwa ya wakristo kuelekea kuwa na thamani kidogo?
- Kimsingi tumeligusia tatizo la fedha, jinsia na madaraka. Fikiria na jadili uwezekano unaoendana kati ya haya na maeneo mengine ya unyoofu wa maadili: ukweli, uaminifu, uwiano, huruma, umoja, kujilinda, furaha, uaminifu, na ustahimilivu.

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Muulize mwenzi wako/au rafiki mmoja au wawili wa karibu, “Ni eneo lipi moja la unyoofu wa maadili ambalo wengine wanachunguza mara chache katika maisha yangu?”
- Kufuatana na ulichojifunza, (AU kufuatana na kile Mungu anachokuongoza baada ya kuuliza kwa uaminifu sehemu yako) omba na panga kwa ajili ya mkakati mfupi ambao ni pamoja na malezi maalumu kuimarisha kile ambacho kinatambulika kidogo cha tabia yako. Pengine hili linaweza

kuwa eneo la kushindwa kwako, lakini halitakiwi; badala yake inaweza kuwa moja ya unayofanya kisiri ambayo hayajawavuta wengine bado.

- Malizia mkakati wako angalau wakati wa wiki mbili. Hili halihitaji kuwa la utata, lakini linatakiwa kuwa imara.
- Toa taarifa kwa mwenzi (kama umeoa) na angalau kwa rafiki mmoja au wawili ya ulichofanya na ulichojifunza kwenye utaratibu.
- Fanya yote hapo juu kati kati ya miezi miwili ya hasa hasa ulipojifunza somo hili.

## VYANZO


- Dyer, Charles. *The Power of Personal Integrity*. Wheaton, IL: Tyndale House Publishers, 1997.
- Hendricks, Howard, ed. *A Life of Integrity*. Sisters, OR: Multnomah Books, 1997.
- Kreeft, Peter. *Back to Virtue*. Fort Collins, CO: Ignatius Press, 1992.
- Searcy, Nelson, Chad Hall and Kelley Edwards. "Integrity; Searching for Cracks." *SmartLeadership Mag-Ezine* (October, 1998): www.SmartLeadership.com.

# MOAMBI

MAOMBI

SOMO LA 10

# Kuwezesha Maombi kwa Harakati za Upandaji Kanisa

## KUSAIDIA WENGINE KUOMBA KWA AJILI YA KUENEZA UPANDAJI KANISA

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwapa wapanda kanisa mawazo juu ya jinsi ya kuhamasisha maombi katika kusaidia harakati za upandaji kanisa.

☞ **Wazo Kuu**

- Harakati za upandaji kanisa zinahitaji kwamba raslimali za maombi ziandaliwe kuelekea kwenye "Z."
- Viongozi wa maombi lazima watambulike na kuendelezwa kuandaa harakati za maombi.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kujua jinsi ya kuhamasisha wengine kwa ajili ya maombi kusadia juhudi za upandaji kanisa.
- Kushiriki katika matukio ya maombi ya harakati za upandaji kanisa ambayo ni ya kimusingi kwenye ukubwa wa mji, ukubwa wa eneo au ukubwa wa taifa.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Tumia hili kama kiongozi cha mazoezi kwenye kujadili jinsi ya kuwezesha maombi yanayopelekea kwenye kueneza upandaji kanisa. Wafanye wafunzwa au wengine kushirikisha uzoefu waliopata kutokana na maombi ya pamoja, au kuhamasisha maombi kwa ajili ya mji au mkoa. Wafanye wafunzwa kujadili ni hatua zipi kila mmoja anaweza kuchukua kuhamasiha maombi kwenye madhehebu yao, kwenye miji yao, mkoa au taifa.

Shirikisha wafunza raslimali zozote au habari za mawasiliano kuhusiana na haarakati za maombi ambazo tayari zinatokea katika mji, mkoa au nchi.

### UTANGULIZI

Mwanzoni mwa mafunzo haya, katika maombi somo la 3, "Jinsi ya Kuwezesha maombi" (Mwongozo wa Kwanza), Tumejadili jinsi mtume Paulo alivyoona maombi kama sura nyeti ya uinjilisti na upandaji kanisa. Tumejadili mikakati kadhaa ya kuhamasisha maombi katika kusaidia huduma yako mwenyewe ya upandaji kanisa. Ili kwa harakati za upandaji kanisa kutokea kwenye upana wa mkoa, mji au taifa, maombi lazima yahamasishwe kukazia kwenye uinjilisti na upandaji kanisa kwa kiwango kikubwa. Mkakati wa maombi kwa kueneza upandaji wa kanisa lazima ukazie kwenye kitovu ambapo inamaanisha—kila kijiji na ujirani wa kila mji na jiji la taifa lako na miongoni mwa kila kundi la watu ambao hawajafikiwa.

Kuna upana wa njia mchanganyiko ambao watu wanaweza kuandaa maombi ya pamoja kwa ajili ya jiji au taifa. Huko Korea, siyo kawaida kwa makanisa kutumia usiku wote kwenye maombi, kwenda kwenye milima ya maombi kwa vipindi vya kufunga na kuomba, au kuamka saa 11 asubuhi kila asubuhi kwa ajili ya maombi. Marekani, wakristo watakusanyika kwa ajili ya siku za maombi maalumu, kama vile siku ya maombi kitaifa. Watu wanaweza kutenga saa kwenye siku hiyo kuomba maalumu kwa ajili ya taifa. Ulaya, timu za watu wametembea njia hizo hizo kama wahubiri

hadharani—kutoka uingereza mpaka Istanbulu—na kuomba kwa ajili ya upatanisho na kukata shauri kwa Kristo kwenye majiji na vijiji vilivyo njiani.

Maombi ya kimkakati kwa kiwango kikubwa yanahitaji vitu fulani vya ufunguo: utafiti, kutupa maono, mafunzo na ufadhili na viongozi wa maombi ya mtandao. Katika somo hili tutajadili vitu hivi vinavyohitajika kwa ajili ya uhamasishaji maombi kwa ajili ya harakati za upandaji kanisa kwenye jiji, kimkoa au kitaifa.


## I. UTAFITI (KUCHORA RAMANI YA KIROHO)

Kwa sababu ni haja ya Mungu kupatanisha watu na yeye mwenyewe na kutangaza utukufu wake kati ya mataifa, inaonekana kwamba Roho Mtakatifu ameshawahi kuwa anawapa watu mzigo wa kuomba kwa ajili ya ujirani, mkoa, jiji au taifa. Hatua ya kwanza katika kuhamasisha maombi kwa kiwango cha mapana ni kuwatafuta watu walio na mzigo wa maombi. Katika baadhi ya mataifa haya ni makundi ya wanaume, wanawake, kama vile ushirika wa Lidia yaliyopangwa kwa hali ya juu. Katika sehemu zingine yanaweza kutokea kwa watu pekee waliotawanyika wanaoomba wenyewe kwa ajili ya kuendelea kwa injili.

Mkakati unaoanzisha na kuweka kwa ajili ya kuhamasisha maombi utategemea juu ya kile utafiti wako unachodhihirisha. Kama unakuta idadi ya vikundi vya maombi na mitandao, kazi yako inaweza kukazia katika kuunganisha makundi hayo na uinjilisti na huduma za upandaji kanisa ili kwamba maombi yaweze kukazia kwenye kuendelea maalumu kwa injili. Mara nyingi, vikundi vya maombi au mitandao vimejitenga kutoka kwenye uinjilisti na juhudi za upandaji kanisa na kwa hiyo kupotea kwa raslimali iliyopotelea kwenye juhudi hizo. Mkakati wako kimsingi utakazia kupanga ushirikishaji wa taarifa kati ya juhudi za maombi na uinjilisti na juhudi za upandaji kanisa. Mkakati wako pia unaweza kuwa pamoja na kutia moyo na kushauri makundi haya ya maombi au viongozi wa mtandao katika kuhamasisha maombi katika sehemu nyingine za jiji, mkoa, na taifa. Sehemu nyingine ya mkakati wako unaweza kuwa kuleta makundi haya ya maombi na makanisa yao pamoja kwa vipindi kwa ajili ya maombi makubwa ya pamoja. Kwa sababu maombi ya pamoja yanakaziwa kwenye sifa na kumwambudu Mungu na katika kuenea kwa injili, ni mazuri katika kusaidia kuamsha umoja miongoni mwa wakristo, wakifurahia upana wa mwili, na yanaweza kuwa mahali pa kuanzia kwa ajili ya juhudi za ushirikiano ujao.

Kwa upande mwingine, kama utafiti wako unadhihirisha shughuli kidogo kwenye njia ya maombi yalioandaliwa, mkakati wako utakazia katika kuuliza Bwana kukuongoza kwa viongozi maarufu wa maombi.

**Kielelezo 10.1 Matokeo ya Utafiti**





## II. UTUPAJI MAONO—NINI MUNGU ANATAKA KWA SEHEMU HII?

Ukosefu wa maono mara nyingi unaota kutokana na ukosefu wa maombi. Watu wanatoa mda na juhudi kwa vitu ambavyo wanaamini ni muhimu au kwa vile ambavyo wana shauku ya ndani. Kitu cha ufunguo kwa kuhamasisha maombi ya kueneza upandaji kanisa ni kuwapa watu maono ya nini Mungu anataka kuona kinatokea katika jiji, mkoa, na taifa. Watu lazima wachochee ndani yao shauku ya moyo wa Mungu—yaani, haja yake ya kupatanisha mtu mwenye dhambi kwake,

kumkomboa mwanadamu kutoka kwenye kifungo cha dhambi na kumrejesha mtu kwenye ushirika na yeye kupitia Yesu Kristo. Mungu amechagua watu wa Mungu kuwa mawakili wa habari hiyo njema ya upatanisho wa waliopotea na ulimwengu unaokufa (2Kor 5:18-20). Wakristo wanapopata upya hisia za wito wao kama mawakili wa Kristo, kiasili watataka kuhusika kwenye makusudi ya Mungu.

Sehemu nyingine ya kutupa maono ni kuwapa watu picha ya "Z"—miji yao, mkoa na taifa litafananaje baada ya kuwa limefuaswa? Hayo yatakuwa makanisa mangapi? Nini asilimia ya wakazi watakuwa wakristo? Linganisha "Z" kwenye hali halisi yao leo. *Ni makanisa mangapi kwa sasa yapo? Kuwa asilimia kama ngapi wakazi ni wakristo walio hai?* Kisha jipe changamoto, ni makanisa mangapi yanahitajika kupandwa ili kuona jiji hili, mkoa au taifa likiwa limefuaswa? Watu wangapi wanahitaji kumwamini Kristo? (Rejea kwenye Somo la maono ya KUM, "Z" kufikiri, na somo la kanisa, "Kusudi la Kanisa").

**Kielelezo 10.2 "Z"-Kufikiri**




Kitu cha tatu cha kutupa maono ni kuwasaidia watu kuona jukumu la mkakati wa maombi katika uinjilisti na upandaji kanisa. Kuwafanya wao kugundua maombi ya mtume Paulo na vitu ambavyo aliombea, watakamata maono ya jinsi gani maombi yao yalivyo muhimu kwenye kuendeleza injili katika maeneo yao. (Rejea Somo la Maombi la 3, "Jinsi ya Kuwezesha Maombi.")

## III. FUNZA NA ANDAA WATU KUOMBA KWA AJILI YA KUENEZA UPANDAJI WA KANISA

Mara watu wanapokamata maono ya nini Mungu anataka kwa ajili ya ujirani wao, jiji, mkoa na taifa, na jukumu la maombi katika kuendeleza injili, watataka kupewa mawazo ya vitendo na msaada wa jinsi ya kushiriki kimaombi katika kuendeleza injili. Unatakiwa uweze kutoa mafunzo ya vitendo kwa njia tofauti za kutia moyo maombi, ikiwemo:

- Maombi ya utatu
- Maombi ya kutembea
- Kuanzisha timu ya msaada wa maombi kwa juhudi za upandaji kanisa
- Vita vya kiroho
- Kushirikisha habari kati ya makundi ya maombi na uinjilisti na juhudi za upandaji kanisa
- Kongamano la Maombi
- Siku ya maombi ya taifa
- Maombi na kufunga

Mengi ya aina hii ya mafunzo yatazaliwa kutokana na uzoefu wako binafsi wa maombi katika huduma yako ya upandaji kanisa. Masomo yote haya yameshafanyika kwenye miongozo ya mafunzo. Kumbuka kwamba maombi yanakamatwa zaidi kuliko kufunmdishwa. Watu wanapotumia mda wao hasa katika maombi, Mungu atawaonyesha jinsi ya kujipanga wenyewe na kuwapa njia za kiubunifu za kuhamasisha maombi katika mduara wao wenyewe wa mvuto.


## IV. TAFUTA NA WEKA MTANDAO WA VIONGOZI WA MAOMBI

Ili kwa harakati yoyote kufanikiwa, inahitaji viongozi. Unapofanya utafiti na kutupa maono, muulize Mungu kukuongoza kwa wanaume na wanawake walio na mzigo maalumu kwenye uongozi na ujuzi wa uongozi. Waombeaji hawa wanatupa maono, kutoa mafunzo na kukazia maombi kwenye maswala yanayohusiana na kuendeleza injili kwenye jiji, mkoa, au taifa. Wanahitaji kukaa wanajulishwa juu ya uinjilisti na juhudi za upandaji kanisa ili kwamba waweze kuhamasisha maombi ya kusaidia juhudi hizi. Chini kuna baadhi ya tabia unazotakiwa kuangalia kwa viongozi wa maombi:

- Uwe na tabia ya utiifu na unyenyekevu kwa uongozi wa kanisa. Hawatakiwi kujifikiria wenyewe kuwa muhimu zaidi kuliko viongozi wa kanisa.
- Kuwa wawezeshaji wazuri wa mikutano ya maombi. Kuweza kutunza mkutano wa maombi ukikazia na kuweza kuzuia kuomba kusikofaa au kusikosaidia.
- Kuwa na kujitoa kwa nguvu kwa Kristo na kuwa waaminifu kwenye malezi ya kiroho, kama vile usomaji wa Biblia, maombi ya mtu binafsi, ushirikiano, n.k.
- Kuwa na mahusiano mazuri na watu na sifa njema miongoni mwa waumini kwenye makanisa yao.
- Kuwa na uwiano nzuri kihisia. Viongozi wa maombi wamejifunza kutawala kubadilika kwa hisia zao na hawaruhusu hisia zao kutawala uombaji wao.
- Wasiozoelea udaku; wanaoweza kutunza siri.
- Kuwa na kuelewa na maono ya kueneza upandaji wa kanisa. Wanaoweza kuwakilisha maono haya kwa wengine.
- Kuweza kupangilia mtiririko wa habari kati ya makundi ya maombi na uinjilisti na juhudi za upandaji kanisa.

Viongozi wa maombi watafanya kazi katika ngazi tofaut katika harakati za maombi. Baadhi watakuwa viongozi wa vikundi maalumu vya maombi—pengine katika kanisa la mtaa, au na wajumbe kutoka makanisa kadhaa ya mtaa kwenye jumuia. Wengine watakuwa viongozi wa mitandao ya maombi—vikundi vidogo au watu pekee kwenye mkoa wote, jiji au taifa, waliounganishwa kwa mzigo wa kuombea kuenea kwa injili katika maeneo au miongoni mwa kundi la watu maalumu. Madhehebu yanaweza kutiwa changamoto kuteua wapangiliaji ambao wanaweza kuwajibika kwa kusaidia makanisa katika dhehebu hilo kuendelea na kuweka mikakati ya maombi.

**Kielelezo 10.3 Viongozi wa Maombi Huwezesha Maombi**




Viongozi wa maombi kitaifa wanaitisha maombi kwa ajili ya maswala na yanayowasumbua ambayo yanaathiri nchi nzima. Pia wanachochea maombi kwa hao wanaotumika katika serikali, jeshi, n.k. Wanategemesha mitandao ya maombi katika nchi nzima kwa ajili ya juhudi maalumu za maombi na wanaweza kupangilia shughuli, kama vile siku ya maombi ya taifa. Viongozi hawa wa maombi ya kitaifa wanaweza kuunganishwa kwa viongozi wa maombi ya kitaifa kutoka nchi zingine ulimwneguni.

**Mfano**

Huko Urumi, Dalili za kwanza za harakati za maombi zinaweza kuonekana. Kutoka Alba Iulia, Urumi, kundi la wanawake watatu walianza kuombeana na kuombea waume zao. Waliendelea kuomba kwa ajili ya makanisa yao, mikoa yao, kwa ajili ya taifa na kwa makanisa mapya kuweza kupandwa. Ushirika huu ulikua kufikia zaidi ya makundi 30 na wastani wa wanawake 150 waliohusika katika maombi. Ulienea mpaka Bucharest ambapo kitabu kidogo kwa ajili ya Urumi kilianzishwa na kutumika taifani kote na nje ya nchi. Katika Sibui makanisa mawili yasiyo ya dhehebu moja yanaomba pamoja. Huko Cluj kuna mkusanyiko wa maombi ya kila mwezi ya wanawake yaliyo wazi kwa makanisa yote, na mara nyingi wanawake wasiokata shauri wana hudhuria na baadhi wanakuwa waumini kupitia ushirika huu.

## SULUHU

Kutia moyo maombi na uanzishwaji wa maombi siyo wazo jipya. Badala yake, tunaungana na Mungu katika kazi yake. Kutoka mda wa wakristo wa kwanza, maombi yalifikiriwa kama sehemu nyeti ya uinjilisti na upandaji kanisa. Bila kujali kama maombi yako kwenye ngazi ya mtaa, jiji, kimkoa au kitaifa, lengo la kuwezesha maombi na harakati za maombi ni kuona Kristo akiwekwa kati, makanisa yanayokua yakifikika kwenye kila eneo ili kwamba kila mtu aweze kusikia na kuona injili katika njia ambayo inaendana nao na hali zao.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni uzoefu gani binafsi umekuwa nao katika kuhamasisha maombi au kueneza upandaji kanisa?
- Unajua mitandao yoyote ya kitaifa, kimkoa au jiji ya maombi?
- Ni kwa njia zipi nzuri umetunza mawasiliano mazuri kati ya timu yako ya maombi na huduma yako ya upandaji kanisa?
- Unajua mtandao wowote wa kitaifa au kieneo au kimji?
- Ni kwa njia zipi ambazo umetunza mawasiliano mazuri kati ya timu yako ya maombi na huduma yako ya upandaji kanisa
- Katika darasa chukua mda kujadili jinsi nyie kama wapanda kanisa mnaweza kushirikisha maono kwa kueneza upandaji kanisa na maombi kwa makanisa mengine na kati kati ya dhehebu lako.
- Umewahi kuhudhuria maombi ya kujirudia au kusanyiko la maombi? Ilikuwaje? Jinsi gani unaweza kupanga kusanyiko la maombi katika jiji lako au mji?
- Ni nini mapenzi ya Mungu kuhusiana na maombi katika maisha yako? Maombi, kama kipao mbele, swala ambalo si la kutokujadiliana kwa viongozi?
- Kwa nini maombi siyo sehemu nyeti sana ya maisha yetu na huduma?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Fanya marudio ya sura mbali mbali za maombi ya kuhamasisha ya kueneza upandaji kanisa. Amua ni katika hatua zipi unaweza kuchukua kusaidia kuhamasisha maombi kwa ajili ya jiji lako, mkoa, au nchi.

## VYANZO


- Livingston, Glenn. *Prayer that Strengthens and Expands the Church*. South Holland, IL: The Bible League, 1999. (This *Alliance for Saturation Church Planting* publication is available from The Bible League, 16801 Van Dam Road, South Holland, IL, 60473 USA. tel 1-800-334-7017. E-mail: BibleLeague@xc.org).
- Mills, Brian. *DAWN Europa Prayer Manual*. England: DAWN Europa, 1994.

MAOMBI

SOMO LA 11,12

# Kongamano la Maombi

## KUMSHUKURU MUNGU KWA UAMINIFU WAKE

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kusherehekea wema na uaminifu wa Bwana kwenye vipindi vyote vya mafunzo.

☞ **Wazo Kuu**

- Kumshukuru Mungu kwa uaminifu wake
- Kuomba baraka zake kwenye huduma zetu zijazo

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Mwishoni mwa somo hili, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kutiwa moyo wanaporejea baadhi ya baraka za Bwana wakati wa miezi ya mafunzo.
- Kutiwa changamoto kumtumaini Mungu hata kwa mambo makubwa katika maisha yao wenyewe na huduma.
- Kutiwa changamoto kuanzisha au kushiriki kwenye ushirika wa wapanda kanisa kwa ajili ya usaidizi unaoendelea na kutia moyo baada ya kumaliza zana hizi za mafunzo.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Masaa haya mawili ya maombi ya pamoja yanatakiwa kufata somo la maombi na yanatakiwa yawe ya mwisho ya kufungia mafunzo ya wapanda kanisa. Panga kiuangalifu kuufanya mda kuwa wa kutia moyo, baraka na kusherehekea. Chagua watu wawili au wanne wa kushirikisha jinsi Bwana alivyobariki juhudi zao za upandaji kanisa. Kisha gawanyika katika makundi madogo kuwapa watu mda zaidia wa kushirikisha. Mwishoni, kutaneni tena kwa mada wa sifa na kuabudu.

Uwe na ramani ya nchi na orodha ya makundi ya watu wasiofikiwa kuitumia wakati wa maombi ya pamoja. Vile vile, Somo la Kanisa la 18, kwenye historia ya ukristo katika nchi inaweza kutumika kama chanzo cha sifa kwenye kichwa cha uaminifu wa Mungu kwa watu wa nchi hii na haja yake ya kujaza taifa kwa utukufu wake.

Tambua: Zaburi 67 ni zaburi bora kutumia kama kisa kwa kongamano hili la maombi.

### I. MSIFU MUNGU KWA KUWA MUNGU MWAMINIFU

Imba pamoja idadi ya nyimbo au pambio ambazo zinakazia kwenye kutoa shukurani kwa Mungu kwa ajili ya uaminifu wake.

Waulize wafunzwa kufikiria sehemu yoyote ndogo ya maandiko ambayo yanahusiana na uaminifu wa Mungu, na kuyasoma kwenye kundi yanapokuja akilini.

### II. KUMBUKA BARAKA ZA BWANA ZILIZOPITA

#### A. Kwa kila mmoja Wetu Kipekee

Shirikisha ushuhuda mdogo wa jinsi Bwana alivyofanya kazi katika wokovu wako binafsi na ukuaji.

**B. Kwa Familia Zetu**

Shirikisha shuhuda za kazi ya Mungu katika familia yako.

**C. Katika Huduma Yako ya Upandaji Kanisa**


- Uwe na watu binafsi watatu au wanne wa kushirikisha kundi lote njia ambazo walimuona Bwana akibariki huduma yao ya upandaji kanisa au masomo ambayo Bwana aliwafundisha wakati wa mzunguko wa mafunzo.
- Katika makundi madogo, ruhusu kila mmoja anayetaka kushirikisha baraka kutoka kwa Bwana.

**D. Kwa Kanisa katika Taifa Lako**

Somo la Kanisa la 18, "Historia ya Ukristo katika___," Linajadili msingi wa ukristo katika nchi yako. Tumia hili kama kiongozi kwenye maombi.

- Mshukuru Mungu kwa wamishenari wa kwanza walioleta injili katika nchi yako.
- Mshukuru Mungu kwa kuandaa mioyo ya waumini wa kwanza kupokea injili.
- Mshukuru Mungu kwa wafia dini—hao waliokufa kwa ajili ya imani yao nchini kwako.
- Mshukuru kwa ajili ya wamishenari ambao wametumwa nje kutoka nchini mwako kwenda sehemu nyingine za ulimwengu.
- Msifu Mungu kwa Uchungaji wake wa kanisa katika historia.

**Kielelzo 12.1 Mshukuru Mungu kwa . . .**




## III. OMBA KWA AJILI YA KAZI INAYOENDELEA YA UPANDAJI KANISA

Katika makundi madogo, wafanye wafunzwa waombe kwa ajili ya kila mmoja wapo. Kuomba kwa ajili ya kuendelea kwa ufalme wa Mungu kwenye majiji na mikoa ambapo wapanda kanisa wanafanya kazi. Omba kwa ajili ya amani na ujasiri wa kutangaza injili.

Kwenye kundi kubwa, omba kwa ajili ya taifa lote. Muombe Mungu kwa ajili ya ukuaji ulioendelezwa na upanuzi wa ufalme wake kupenye sehemu zote za taifa. Omba kwamba injili itapenya kwa makundi ya watu wasiofikiwa. Tumia ramani ya nchi na orodha ya makundi ya watu wasiofikiwa kusaidia mda huu wa maombi.

## IV. SHEREHEKEA WEMA WA BWANA KWA WIMBO NA KUABUDU

Kumbuuka: katika kufunga, unaweza kutaka kufanya mipango kwa ajili ya ushirika unaoendelea wa wapanda kanisa ambao wanaweza kukutana kimkoa kwa mda (kila mwezi au nusu mwaka) kwa ajili ya maombi, kushirikishana, kuendeleza elimu na kutia moyo wapanda kanisa katika huduma zao.

# UONGOZI

UONGOZI

SOMO LA 11

# Utoaji Viongozi

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kusisitiza umuhimu wa kutoa viongozi kwenye utendaji kamili katika huduma, badala ya kuteua majukumu kwao tu.

☞ **Wazo Kuu**

- Kutoa kunakwenda zaidi ya kuteua—maana yake kuwaruhusu viongozi wapya kuendeleza huduma zao.
- Tunahitaji kuendelea kuwasiliana na viongozi wapya tuliowatoa kwenye huduma.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kujua tofauti kati ya kuteua na kutoa.
- Kujitolea kwenye huduma ya kuwezesha na kuwatoa wengine.

**UTANGULIZI**

Zana hii imeshajadili umuhimu wa kuteua kazi kwa watu wengine wanaoweza, ili kwamba kiongozi asifanye kazi zote. Viongozi wengi wamejifunza kwamba kwa hakika wanaweza kuongeza ufanisi wao wanapotumia mda zaidi wakifundisha na kuandaa wengine kwa ajili ya huduma, badala ya kujaribu kufanya zote wenyewe. Kwa jinsi hiyo, kuna hatua nyingine muhimu kwenye utaratibu wa mafunzo ambao unakwenda zaidi tu ya kuteua kazi kwao. Hii ni hatua ya *kutoa*. Tunapowatoa viongozi wapya kwenye huduma tunawaruhusu kutenda kikamilifu kama viongozi bila *uthibiti wetu*. Wanafanya maamuzi yao wenyewe na kupanga shughuli zao. Kwa maneno mengine, kutoa viongozi kunamaanisha kwamba tunawaruhusu *kuchukua huduma zao wenyewe* badala tu ya kutusaidia kufanya zetu. Huu ni utofautishaji nyeti.

> kutoa viongozi kunamaanisha kwamba tunawaruhusu *kuchukua huduma zao wenyewe.*

## I. WAPANDA KANISA LAZIMA WATOE WENGINE KWENYE HUDUMA

Viongozi wa kupanda kanisa wanazidi wenyewe kupitia kuainisha na kuendeleza wengine. Viongozi wengi wanajaribu kujenga huduma zao wenyewe kuwazunguka, lakini mungu anatuita kuwafuasa na kuwafunza wengine (2Ti 2:2). Kwa jinsi hiyo, lengo linatakiwa liwe kuona viongozi wapya wakiongoza huduma zao wenyewe.

### A. Mfano wa Yohana Mbatizaji

Pengine mfano bora wa ‘kutoa kiongozi’ ni Yohana Mbatizaji. Alitokeza mbele ya Yesu, na kupata wafuasi wengi (Mk 1:5). Alikuwa na nafasi ya kuteua wafuasi wa kwanza kwa Yesu (Yn 1:35-36). Kwa historia hii kichwani, fikiria kuitikia kwa Yohana wakati huduma ya Yesu ilipoanza kuzidi hiyo ya Yohana. Soma Yohana 3:22-30 na jibu maswali yafuatayo:

- Ni tatizo gani liliwaudhi wanafunzi wa Yohana katika mstari wa 26?
- Kwa nini unadhani walikuwa wamesumbuka?
- Jinsi gani unafikiri walitarajia Yohana kuitikia? Kwa nini?
- Ni neno gani Yohana anatumia katika mstari wa 29 kuelezea tabia yake kuhusu hali hii?

- Unafikiria nini kuhusu ufupisho wa Yohana katika mstari wa 30? Alikuwa na moyo mweupe? Ni aina gani ya hisia unadhani alijisikia alipofanya maelezo hayo?
- Jinsi gani kuitikia kwa Yohana ni sawa au tofauti kutoka kwenye tabia ya kawaidia ya viongozi wakristo ambao umewajua wakati huduma ya mtu fulani ilipoanza kuzidi zao?

Ni kweli kwamba Yohana Mbatizaji alikuwa na shauku kuhusu kuona mafanikio ya Yesu. Kwa hakika Yesu haweza kufanya kosa lolote katika huduma. Lakini vipi hatari ya kutoa mtu fulani ambaye anaweza asihudumu 'kikamilifu' kama tunavyofanya?

**B. Mfano wa Paulo**

Paulo pengine alikuwa mfano bora wa kiongozi aliyefunza na kutoa wengine kwa ajili ya huduma. Agano Jipya lina orodha ndefu ya watu waliosafiri na au kujifunza kutoka kwa Paulo, na kisha kuendeleza kazi ya kanisa. Kwa nyongeza ya viongozi zaidi wanaojulikana vizuri kama vile Timotheo, Tito, Sila, Prisila na Akwila, tunaweza kupata orodha ya wengine kwenye kufunga barua nyingi za Paulo. Paulo kikawaida alikaa mda mdogo sana katika kila moja ya kanisa aliloanzisha—popote kuanzia caribu na wiki na upeo wa karibia miaka miwili.

Jinsi gani Paulo angeweza kutumia mda huo mdogo kuwafunza viongozi, na kisha kuendelea na kuwaacha wakiwa wasimamizi? Hakuwa na hofu kama wangefanya kitu fulani kimakosa? Kiuhakika Paulo alikuwa akisumbuliwa na uwezekano huu. Na kwa hakika, kulikuwa na matatizo. Kanisa la Korintho, kwa mfano, lilikuwa ni uchafu. Lakini kunaonekana kuwa vigezo viwili vilivyomsaidia Paulo kushughulika na wasi wasi wake.

*1. Kipao mbele cha kufikia mataifa kwa injili*

Utume Mkuu unatuamuru kufanya wanafunzi wa mataifa yote. Hii ni kazi ya ajabu, lakini siyo ya uchaguzi. Lazima tuifanye. Kuelewa hilo, Paulo alilifikiria kuwa muhimu zaidi kuufikia ulimwengu kwa injili ya Kristo badala ya kuwa na wasi wasi kuhusu ukweli kwamba viongozi wengine hawatafanya vitu kwa njia ambayo tungependa. Wanaweza hata wakafanya makosa, au kuharibu kwingine. Soma Wafilipi 1:15-18 na kasha jibu maswali yafuatayo:

> Ni muhimu zaidi kuufikia ulimwengu kwa injili ya Kristo badala ya kuwa na wasi wasi kuhusu ukweli kwamba viongozi wengine hawatafanya vitu kwa njia ambayo tungependa

- Elezea aina mbili za mahubiri ambayo wengine walikuwa wakifanya wakati Paulo akiwa gerezani, kufuatana na mstari wa 15-17. Unajisikiaje kuhusu aina hizi za huduma? Kwa nini?
- Nini kilikuwa kitu muhimu sana kwa Paulo, kufuatana na mstari wa18?
- Nini Paulo alichofanya kwenye kuhubiri kutoka katika nia ya kweli?
- Nini Paulo alichofanya kuhubiri kutoka kwenye nia ya uongo?
- Unafikiri nia zilikuwa muhimu kwa Paulo?
- Jinsi gani unadhani Paulo aliweza kuitikia kwa njia hii?
- Nini utakachofanya wakati mtu mwingine akihubiri injili kwa njia ambayo hukubaliani nayo, au unapokuwa na maswali juu ya nia zao?

Tafadhali elewa kwamba hatuweki madai ya kuhubiri kutoka kwenye nia za uongo. Hata Paulo hakuwa na maana hiyo. Zaidi ya hayo, Paulo alikuwa akifurahi kwamba injili ilikuwa imehubiriwa kwa njia yoyote, kitabu cha Wagalatia kinaliweka wazi kwamba lazima iwe injili ya wokovu kwa neema kupitia imani katika Kristo—siyo injili ya uongo. Kwa Paulo, maswala mengine yalikuwa madogo kwenye umuhimu wa kuihubiri injili.

*2. kanisa ni la Bwana*


Kigezo cha pili ambacho kinaonekana kuwa kilimsaidia Paulo kutoa viongozi kwa haraka katika huduma ilikuwa ujasiri wake kwamba kanisa ni la Bwana, na kwamba ameahidi kulijenga (Mt 16:18). Kama wapanda kanisa au viongozi wa kanisa, hatimaye hatuwajibiki kwenye ukuaji wa kanisa. Paulo analifanya hili wazi wazi katika 1 Wakorintho 3:5-7. Mungu anaweza kutumia idadi ya watu kulileta kanisa kwenye ukomavu, kama tu alivyomtumia Paulo na Apolo.

Ujasiri huu hautupi udhuru kutokufanya kiwango chetu bora kuwa viongozi waaminifu. Kwa jinsi hiyo, inaondoa wajibu wowote wa kuhukumu huduma ya wengine. Mungu mwenyewe atahukumu nia zao na matendo yao (1Kor 4:5). Ukweli huu unatakiwa uturuhusu kuwatoa hao tuliowafunza kwenye huduma, na kisha kustarehe na kumwacha Bwana kuongoza na kuwatumia kama anavyotaka.

## II. MATATIZO YA UTOAJI

Kuwatoa viongozi kwenye huduma maana yake kuondoa mikono yetu kwao na kumuruhusu Bwana kuongoza njia ambazo wanamtumikia yeye. Wakati wa hatua ya kuteua ya mafunzo, uliruhusu kiongozi mpya kuwa na wajibu wa maeneo machache ya huduma yako wakati ukimtathimini na kumuongoza. Kwa jinsi hiyo, ulirejeza utawala wa maeneo mengi, na hatimaye alikuwa anawajibika kwenye huduma uliyotoa kwake. Kutoa ni hatua inayofata, ya juu kutoka kuteua, na kujitwalia kwamba kiongozi mpya ameshahakikishwa tayari uaminifu wake na uwezo. Na sasa ni mda wa kumusaidia kutafuta huduma yake mwenyewe, na kumtoa kuifanya. Kielelezo 11.1 kinatofautisha kuteua na kutoa.

**kielelezo 11.1 Kutoa dhidi ya kuteua**




Unapotoa kiongozi mpya, unaweza kwa kifupi kumukabidhi baadhi ya huduma ambayo ulikuwa ukiifanya. Kwa jinsi hiyo, katika kutofautisha kuteua, sasa anawajikika kwenye huduma hiyo mbele ya Bwana—siyo mbele yako. Mfano wa utoaji huu unaweza kuwa mpanda kanisa kukabidhi kanisa mpya kwa kiongozi wake mwanafunzi, na kuendelea kuanzisha kanisa jingine. Hii ni aina ya utoaji ambayo imeonyeshwa katika kielelezo 11.1. katika hali zingine, kiongozi mpya anaweza kuanza huduma yote mpya. Kwa mfano, mpanda kanisa anaweza kubakia kwenye kanisa mpya kama mchungaji, lakini akamfundisha mpanda kanisa mpya ambaye atakwenda nje kuanzisha kanisa jingine—kikawaida kwa usaidizi wa kanisa 'mama'.

Utaratibu wa utoaji siyo rahisi kama unavyosikika. Kumtumaini Mungu kufanya kazi katika maisha ya watu ambao mtu anawaongoza kunakokwenda kinyume cha asili ya binadamu na kuwa na changamoto mbili za bila mzaha kwa kiongozi yeyote.

### A. Hofu Kwamba Kiongozi Atafanya Kazi Nzuri

Kukosa huku kujizuia kunaweza kutishia kiongozi anayeogopa kwa ajili ya heshima yake au nafasi.

Watu wanapokuwa wamefunzwa na kutolewa kwenye huduma, baadhi yao kuna uwezekano wa kuonyesha vipawa vikubwa na vipaji kuliko kiongozi. Wanaweza pia kuanza kuwa na kuelewa kwa undani wa maono ya kiongozi na kutaka kufanya mabadiliko. Kukosa huku kujizuia kunaweza kutishia kiongozi anayeogopa kwa ajili ya heshima yake au nafasi. Kiongozi wa kiroho lazima aondoe kikwazo kinachokatiza kwa kwa ukuaji wake mwenyewe kiroho na kwa ukuaji wa kanisa

Kikwazo hiki kinachokatiza kinaweza kushindwa tu kwa imani na matumaini katika Mungu. Kiongozi anayejiamini katika kuwa yeye ni nani ndani ya Kristo anaweza kutumaini kwamba kwa kuwa tu Mungu yuko anatenda katika maisha yake mwenyewe, Anatenda katika maisha ya watu anaowaongoza. Kwa hiyo, kama Mungu anawaita watu wake kwenye huduma, ni kazi yake hasa na heshima iliyoko kwenye nguzo na siyo ya kiongozi. Kiongozi anahitaji kuwa jasiri kwamba anatembea katika utii kwa Bwana katika kuwezesha na kutoa watu wake kwenye huduma na kukabidhi duku duku zake na hofu kuhusu heshima yake mwenyewe na madaraka kwa Bwana (Flp 4:6-7, 1Pet 5:7).

Kama wakristo, haja yetu inatakiwa isiwe kwa heshima yetu na utukufu, lakini badala yake kwamba Mungu aweze kutukuzwa katika maisha yetu, huduma zetu, na ulimwenguni. Badala ya kuwa wenye wivu wa vipawa na vipaji vya wengine, viongozi wa kikristo wanatakiwa kufurahia katika kuona Mungu akiinua wengine wanaoweza kuendeleza alichoanzisha Kristo zaidi na zaidi kuliko wao wenyewe.

> viongozi wa kikristo wanatakiwa kufurahia katika kuona Mungu akiinua wengine wanaoweza kuendeleza alichoanzisha Kristo zaidi na zaidi kuliko wao wenyewe.

Kama tulivyoona matukio kadha wa kadha, mtume Barnabas ni mfano bora wa kiongozi anayejiamini. Alipokuwa Antiokia, aligundua kwamba vipawa vya Paulo vingeweza kutumika kwenye kanisa pale. Barnabas angeweza kukaa kimya na kutofanya chochote. Badala yake, Barnabas alisafiri umbali mkuu kwenda Tarsisi kumtafuta Paulo na kumrudisha Antiokia (Ac 11:25-26). Kuliko kujaribu na kulinda "ngome yake" huko Antiokia, Barnabas alichukua hatari na kumrudisha Paulo kwenye huduma pamoja naye. Tunaona kwamba hatimaye, Paulo alimzidi Barnabas katika huduma zilizosifika, kwa utukufu mkuu wa Mungu na kuendelea kwa ufalme wake.

### B. Hofu Kwamba Kiongozi Atafanya Kazi Mbaya

Kwa upande mwingine, watu waliotolewa kwenye huduma wanaweza wasiwe wajasiri kama kiongozi na wanaweza wasifanye vitu jinsi ambavyo kiongozi anatarajia vifanyike. Kiongozi anayejiamini anaamini kuwa Mungu yuko kazini kinguvu na kwa watu anaowaongoza, na yuko huru karibia kukaribisha hatari.

Kiongozi anayejiamini anaelewa pia kwamba *kushindwa ni sehemu muhimu ya kujifunza na kukua.* Mfano kutoka malezi ya mtoto: Mtoto anayejifunza kutembea ataanguka mara kadhaa kabla hajaweza kutembea mwenyewe. Mtoto anapoanguka, mzazi anamuinua, na kumpa maneno ya kumfariji, na kumwacha ajaribu tena. Hampigii kelele, "umeshindwa! Umeninitia aibu hasa! Usitembee tena!"

Wakati Yesu alipowafundisha wanafunzi, mara nyingi alitumia kushindwa kama tukio la kufundishia. Kukana kwa Petro ni mfano wa kutazamisha. Yesu aliruhusu kushindwa, na kuahidi kwamba kungepelekea Petro kuweza kuwaimarisha wapendwa (Lk 22:31-32). Wakati wa utaratibu wa mafunzo, Mungu alikutumia kusahihisha na kutia moyo kiongozi mwanafunzi wako. Mungu ataendelea kufanya naye kazi—ingawa inaweza au isiweze kuhusisha kuhusika kwako. Mtumaini Bwana kukamilisha kazi aliyoanzisha (Flp 1:6).

## III. KANUNI ZA UTOAJI

Kuna idadi ya kanuni zinazotumika katika hali nyingi za kuachilia. Wazo la jumla ni kwamba ni lazima uwe na uhusiano mzuri unaoendelezwa na kiongozi mpya, lakini utaepuka kumtawala na kumsonga.

### A. Anzisha na Tunza Uhusiano wa Ndani

Uhusiano wa karibu ni njia ya kawaida ya kuhudumu kwa wengine. Kuachilia ni kwa asili wakati watu wanapokuwa wameanzisha kifungo cha kuamini. Yesu alisafiri, alifanya kazi, alikula alicheka na kuomba na wanafunzi wake. Katika utaratibu, alijenga uhusiano wa karibu nao. Aliwaachilia wanafunzi wake akiwa na ujasiri kwamba wangechukua kazi kikamilifu. Baada ya yote, walikuwa "naye" (Mk 3:14-15).

> Kuachilia ni kwa asili wakati watu wanapokuwa wameanzisha kifungo cha kuamini.

Paulo vile vile anashirikisha jinsi miongoni mwa Wathethalonike aliwawashirikisha injili vile vile na *maisha* yake na wathethalonike (1The 2:8). Paulo pia anamwelezea Timotheo kama 'mtoto' wake na kusema kwamba Timotheo alijua "yote kuhusu mafundisho yangu, njia yangu ya maisha, kusudi langu, imani, uvumilivu, upendo na ustahimilivu" (2Tim 3:10). Lazima liwe lengo la mpanda kanisa kujenga aina hiyo hiyo ya urafiki wa karibu na hao anaotaka kuachilia.

### B. Hakikisha Viongozi Wajao Wanaendelea Kumiliki Maono

Viongozi wengi kimakosa wanadhani kuwa wengine wanaowazunguka wana maono waliyonayo. Lakini kuchukulia hili kimchezo kunaweza kuwa kosa kubwa. Ingawa maono yanaweza kuelezewa kiufundi mara nyingi, na hata kuweza kurudiwa na viongozi wa mbele inaweza isitoshe. Tunza maono mbele ya kiongozi mpya. Kama maono yakichoma mioyoni mwao kama ilivyo kwako, utasisimka kwa matokeo watakayopata.

### C. Usisubiri Sana Kuachilia

Watu wanajifunza kwa kufanya. Upesi unavyomuweka kiongozi mpya kwenye huduma, ndivyo watakavyofikia haraka umaarufu wao. Biblia inatuonyesha kuhusu kuwaagiza viongozi mapema zaidi (1Tim 3:6), lakini kinyume chake pia ni kweli. Katika Agano la Kale, mtume Sauli alijiletea balaa mwenyewe na familia yake kwa kujaribu kumzuia Daudi kutokujitwalia jukumu Mungu alilokuwa amempa.

### D. Tarajia Makosa

> Kama kuna nafasi ya kushindwa, watu wanaonekana zaidi kunapendelea kujaribu vitu vipya.

Wakati watu wanapochukua hatari, mara nyingi wanashindwa. Kama kuna nafasi ya kushindwa, watu wanaonekana zaidi kunapendelea kujaribu vitu vipya. Wakati hao uliofunza wanapofanya makosa, lazima wahakikishiwe tena kwamba una ujasiri nao. Uwe mwenye neema na mvumilivu ukitumia kila kosa kama nafasi ya kufundisha. Wakati wanafunzi walipokuwa hawawezi kuondoa mapepo, Yesu alichukua nafasi kufundisha umuhimu wa imani katika huduma ya kufungua (Mt 17:19-21). Somo katika utoaji au utii huenda lingekuwa limeangukia kwenye masikio ya kiziwi wakati huo. Lakini, kunaweza kukawa hakuna mashaka kwamba wanafunzi waliosikiliza kiusikivu kwenye somo hili kwa kuwa ilikuwa kikomo kwenye kushindwa walikokuwa wamekutana nako.

### E. Mtumaini Mungu Kutenda Kupitia Wengine

Mungu anaweza kufanya kazi kupitia wengine kama vile tu alivyofanya na wewe. Ni lazima uwakilishe hili kwa hao unaowafundisha. Kama watu hawaelewi kwamba unawaamini hawataweza kamwe kuchukua hatari na kwa hiyo kutokua. Yesu ana ujasiri kama huo kwa wanafunzi wake kwamba alieleza kuwa wangeweza kufanya kazi zaidi kuliko alizofanya (Yn 14:12). Tarajia huduma kuongezeka chini ya uongozi wa wengine.

### F. Epuka Kujitumainia

> Kuwepo kwa 'kiongozi mkuu' kunaweza kuzuia maendeleo ya viongozi 'wazuri'.

"Funza na Achilia", ili kwamba wengine kila mara wasikutegemee kama kiongozi. Jinsi gani Paulo angeweza kutumia mda huo kidogo akipanda makanisa haya? Alijua lini alihitajika kutoka nje ya njia. Alijua kwamba kulikuwa na kitu kuhusu kuwepo kwake kama 'kiongozi' ambacho kingezuia maendeleo ya viongozi 'wazuri'. Fikiria kama angekaa Listra kwa mda mrefu. Nani angehubiri wakati Paulo akiwa karibu? Huenda asingekuwepo mmoja isipokuwa Paulo, kwa sababu alikuwa mzuri katika hilo. Katika hali kama hiyo, kwa jinsi hiyo, wengine wasingekuwa na nafasi ya kuendeleza ujuzi wao wa kuhubiri. Paulo alitumia mda mdogo katika kila sehemu ili kwamba wengine watambue kuwa wasingetegemea juu yake kila kitu. Walitakiwa kufanya mambo wao wenyewe (Allen 1962:93).

Wakati mpanda kanisa fulani huko Ulaya alikuwa katika hatua hii angeweza kutangaza kwamba ansingeweza kuwa katika kanisa wiki ijayo kwa sababu ya mkutano kwenye mji mwingine. Wakati mwingine angepanga mikutano kiuchaguzi ili kwamba asiweze kuwepo. Wakati wa nyakati kama hizi wafunzwa wanalazimika na wanakua. Kama hufanyi mpango wa kukabidhi huduma, kisha wafunzwa watakutegemea kwa mda mrefu.

## IV. UTUNZAJI MAWASILIANO NA HAO ULIOTOA

Ingawa Yesu aliwaacha wanafunzi wake kimwili, aliwahakikishia kabla hajawakabidhi kwamba angemtuma Roho wake—wasingekuwa bila mvuto wake (Yn 14:16-18). Kama Yesu ambavyo hakuwaacha kabisa hao alioachilia, na hata kwetu ni hivyo, kuwasiliana na viongozi tulioachilia kunatakiwa kuendelezwe kwa ajili ya mashauri na uwajibikaji.

Mikutano yenye maana ni moyo wa uhusiano unaoendelea na viongozi wapya. Kwa mfano, kama viongozi wapya wanapanda kanisa binti, unaweza kuwa unakutana nao kwa mwezi au kwa wiki. Wakati wa mikutano hii chukua mda kufanya yafuatayo:

- Jadili maswala ya ujuzi, ufahamu na tabia ambayo wanashughulika nayo binafsi.
- Fanya marudio ya mahusiano yote muhimu katika maisha yao (familia, huduma).
- Jadili nao nini kimetokea kuhusiana na huduma tangu ulipokutana mara ya mwisho.
- Uliza huduma inakwenda wapi—Nini maono yao?
- Uliza kama kuna unaloweza kufanya kuwasaidia kufikia maono yao.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kwa nini kuachilia ni muhimu sana?
- Wangapi katika kanisa lako wana wajibu wa huduma?
- Kwa mda gani mtume Paulo kawaida alifanya kazi na waumini kabla hajahama na kuwaamini kuendeleza kazi ya kanisa mpya?
- Nini kinatokea wakati kanisa lako mama linapokataa kuachilia viongozi wapya kwenye huduma mpya?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Wakati gani na jinsi gani unapanga juu ya kuachilia kiongozi mwanafunzi? Unamuona akichukua baadhi ya majukumu yako ya zamani, au wakiendeleza huduma zao? Fanya mpango, na anza kufanya kazi kuelekea kuwaachilia kufikia umaarufu wao.

## VYANZO


- Martin, Robert W. *Mentoring Guidelines for Church Planters*. Budapest, Hungary: The Alliance For Saturation Church Planting, 1997. (This *Alliance for Saturation Church Planting* publication is available from The Bible League, 16801 Van Dam Road, South Holland, IL, 60473 USA. tel 1-800-334-7017. E-mail: BibleLeague@xc.org
- Steffen, Tom A. "Leadership: Ten Implications for Cross-Cultural Church Planters." N.p., n.d.
- Allen, Roland. *Missionary Methods - St. Paul's or Ours?* Grand Rapids, MI: Wm. B. Eerdmans, 1962.

UONGOZI

SOMO LA 12

# Uongozi wa Harakati

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la warsha hii ni kuonyesha kwenye aina ya uongozi unaohitajika kuongoza harakati za upandaji kanisa.

☞ **Wazo Kuu**

- Harakati za viongozi kiundani wanatamani maono ya Mungu kwa ajili ya kanisa na kiufanisi wanayawasilisha kwa wengine.
- Viongozi wa harakati wanavutia na kuwezesha wengine ili kusisimua harakati za upandaji kanisa.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo kwenye warsha hii yanapoeleweka kila mshiriki anatakiwa...

- Kujua aina ya uongozi ambao ni wa lazima kuanzisha na kusalimisha harakati za upandaji kanisa kwenye mandhali yao.
- Ajitolee kuomba kwamba Mungu atatoa uongozi unaotakiwa ili kuleta harakati za upandaji kanisa kwenye nchi yao.

☞ **Ziada**

12A Viongozi wa harakati

☞ **Ujumbe kwa Wakufunzi**

Hii ni warsha. Baada ya utambulisho mfupi gawanyika katika makundi madogo na kila kundi lianze kufikiri maswali yaliyotolewa.

## UTANGULIZI

Yesu, kiongozi wetu, mara aliposema, “nitalijenga kanisa.” Akiwa amefanya mkazo wake kujulikana, Yesu kisha aliendelea kutoa kielelezo cha kiongozi mtumishi kwa kuhudumu, kufundisha, na kutangaza mapenzi ya baba yake kwa wengine. Katika kufanya hili, Yesu aliamsha harakati za kanisa mpaka miisho ya dunia. Ni harakati hizi ambazo zinatuleta kwenye hatua tuliyopo sasa. Swali amabalo tunatakiwa tujiulize wenyewe ni “Ni aina gani ya uongozi kiufanisi zaidi unasisimua harakati za kanisa?”

Harakati za upandaji kanisa zinahitaji aina nyingi ya viongozi, kwa mfano waonaji, waelekezaji, wakufunzi, washauri, watia moyo, n.k. Ingawa wanatenda katika njia tofauti na katika ngazi tofauti, wana hili kwa wote: wote ni vyombo vya Mungu wanaotumia mvuto waliopewa na Mungu kuhamasisha mwili wa Kristo kuelekea ukamilishaji wa Utume Mkuu.

**Gawanyika katika makundi madogo. Katika kila kundi, fikiria yafuatayo:**

1. Jaribu Kufikiria harakati za upandaji kanisa katika nchi yako. Harakati hizo zitafananaje?
2. Unapofikia aina tofauti za uongozi zinazohitajika kwa ajili ya harakati za upandaji kanisa orodhesha ujuzi na sifa za lazima kwa viongozi katika ngazi tofauti.
3. Andika majina ya viongozi katika nchi yako ambao zaidi wanaelelezewa na hili

4. Unaposoma mifano ifuatayo kutoka ulimwenguni, jaribu kuainisha aina ya viongozi wa lazima kuona harakati kama hizo katika nchi yako.

**Mfano Kutoka Uruguayi:**

Jason Carlisle, mtoto wa mmishenari aliyebakia Uruguayi kama mmishenari, ni mwanzilishi wa mtandao wa vita vya kiroho. Mtandao huu unajaribu kuunganisha mwili wote wa Kristo katika maombi ya kimkakati. Washiriki wanatoka zaidi katika madhehebu ya kiinjili. Moja ya uanzilishi wa mtandao ni pamoja na kuchapisha vijitabu vya kuongoza maombi pamoja na maombi ya kila siku kwa taifa, maombi ya kusaidia matukio makubwa na maombi ya warsha katika makanisa.

*Orodhesha baadhu ya maeneo ya viongozi ambayo yanaweza kuwa ya lazima katika ngazi tofauti kama aina hii ya harakati za maombi ilikuwa zitokee katika nchi yako.*

**Mfano Kutoka Zimbabwe**

Maono ya kupanda makanisa 10,000 na kufundisha viongozi yalianza katika mwaka 1984-85 na Jim Montgomery na ted Olson (wamishenari kutoka nje waliokuja humo kutupa maono). Katika mwaka 1986 watu walikamata maono; utafiti wa kitaifa ulianza mwaka 1989 na kumalizika 1991. Katika mwaka 1992 waliendesha mkutano wa watu zaidi ya viongozi 500 kutoka makanisa tofauti. Mpaka kufikia mda huu, kumekuwa hakuna umoja miongoni mwa viongozi (taarifa kutoka kwa Xolisani Dlamini kwenye mkutano wa Ibero American DAWN ‘98).

Kutoka katika mfano huu, orodhesha baadhi ya vitu unavyojifunza kuhusu uongozi ambavyo ni vya lazima kwenye harakati kitaifa:

- Ni uongozi wa namna gani unaweza kuwa wa lazima kwa hili kutokea katika nchi yako?
- Unawajua watu ambao wanaweza kutiwa moyo kuchukua baadhi ya uongozi huu?
- Ni sehemu ipi unaweza kuwa katika hili?

**Mfano Kutoka Urumi:**

Huko Urumi, Timu ya KUM ya wamishenari wataalamu walisafiri nchi nzima kutafuta hao ambao Mungu amewapa mzigo kama huo kwa nchi nzima. Kwa kubuni mmoja kati ya kila viongozi 10 alishirikisha mzigo huo. Wasemaji waliwauliza kuwafundisha wapanda kanisa katika eneo lao la wajuzi wa KUM kufikiri. Wamenunuliwa kikamilifu kwenye maono ya KUM? Hapana, siyo asilimia 100. lakini mara nyingi walinukuru sura moja ya maono vyema sana, na walikuwa wameulizwa hasa hasa kufundisha kwenye eneo hilo.

Wataalamu wamishenari walishirikisha huduma katika kufundisha na kutupa maono na watu hawa, watu hao wenyewe walinyenyekea maono ya KUM Mungu mwenyezi aliwatunza watu hawa wakiendelea kuona mawazo ya KUM walipokuwa pia wakiendelea kuhamia kwenye ngazi mpya ya uongozi kati kati ya harakati. Walikwenda kutoka kuwa wapanda kanisa, kuwa wafundishaji wa wapanda kanisa, wafundishaji wa wafundishaji, wapangaji wa kazi ya KUM katika taifa.

Mda huo, wataalamu walijisikia kana kwamba watapaswa kuondoka nchini ili wasije wakaingilia Mungu alichokuwa akifanya kupitia watu hawa. Leo, watu hawa wanaongoza sura zao za harakati Mungu alizokusudia na kuanzisha Urumi.

- Jadili jinsi wamishenari wataalamu na vionongozi wa kitaifa walivyofanya kazi pamoja kuanzisha harakati Urumi.
- Jinsi gani jumuia hizi mbili wanaweza kufanya kazi pamoja kwa ukaribu katika nchi yako?
- Nani ni viongozi katika nchi yako wakiwa na baadhi ya maono ya KUM?
- Jinsi gani wanaweza kutiwa moyo kushiriki katika mafunzo?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Katika warsha yako, ulitambua baadhi ya mahitaji ya uongozi. Jitoe mwenyewe kuanza kuomba kwamba Mungu aweze kuinua viongozi wa kuwezesha harakati ambazo ni za lazima kufanya na kutunza harakati za upandaji kanisa katika nchi yako. Wakati huo huo, muulize Bwana kukuonyesha jinsi unavyoweza kufaa kwenye mpango wake wa kutimiza Utume Mkuu.

UONGOZI
*ZIADA*
12A

# Viongozi wa Harakati

## I. HARAKATI ZINAHITAJI AINA MAALUMU YA VIONGOZI

Kutokana na mda wa Mungu wa kuwahi kitakatifu, anawainua viongozi kuanzisha na kuendeleza harakati za upandaji kanisa. Viongozi hawa kisifa wanatofautiana kutoka kwa wengine. Wanavutwa na swali "Nipatie Scotland vinginevyo nitakufa!" ni mfano bora. Viongozi hawa kwa kifupi hawaanzishi vpindi au vyama, lakini kama tutakavyoona, wanavutia harakati ambazo zinahamasisha waumini kuelekea lengo lililoongezeka la kazi ya kanisa.

Harakati za upandaji kanisa kikawaida ni pamoja na kundi la viongozi wanaogusa ngazi kadhaa za maisha ya kanisa.

Kwa kifupi, viongozi wanaoamsha harakati za upandaji kanisa ni vyombo vya Mungu wanaotumia mvuto waliopewa na Mungu kuhamasisha mwili wa Kristo kuelekea ukamilishaji wa Utume Mkuu kupitia upandaji wa makanisa. Harakati za upandaji kanisa kikawaida ni pamoja na kundi la viongozi wanaogusa ngazi kadhaa za maisha ya kanisa. Baadhi ya viongozi hawa, kama John Knox, mfano uliotolewa hapo juu, vutia makanisa na mataifa kwa ajili ya upanuzi wa ufalme. Wengeine ((mchanganyiko zaidi) moja kwa moja wanagusa makusanyiko kwa mguso wa kimkoa. La mwisho na la kawaida zaidi, 'chimbuko' la viongozi wa mtaa wanawezesha waumini wenzao kuelekea kwenye uinjilishaji mkuu na upandaji kanisa. Viongozi hawa wa chimbuko wanaweza kuwa viongozi wa vikundi kiini, wapanda kanisa, mashemasi- wachungaji, au wainjilisti/wafuasishaji.

## II. VIONGOZI WA HARAKATI WANAWAKILISHA MAONO

Viongozi wanaochochea harakati ni waonaji. Mtu wa maono anaweza kuelezewa kama kuwa na tabia ya matarajio na matumaini, na mmoja anayeona kupita wakati uliopo kwenye wakati ujao katika mtazamo wa Mungu. Viongozi wa harakati za upandaji kanisa hawatungi maono yao, ingawa inaweza kusikika hivyo kwa wengine. Maono hasa ni maono ya Mungu. Viongozi wa harakati wanayagundua kwa kifupi kwa kuuliza, Nini Mungu anataka?"

Viongozi wa harakati za upandaji kanisa wanabeba mvuto unaoshurutisha ambao Mungu antaka kuona kanisa lake likianzishwa.

Viongozi wa harakati za upandaji kanisa wanabeba mvuto unaoshurutisha ambao Mungu anataka kuona kanisa lake likianzishwa kwa namna kwamba kila mwanaume mwanamke na mtoto anaweza kushuhudiwa injili. Viongozi wa harakati wanatambua umuhimu wa kuwakilisha maono haya kiushawishi kwa waumni wengine. Anabembeleza kujitolea kwenye maono kwa namna kwamba wengine wanajisikia kuwajibika kwenye mafanikio ya hilo.

Kila mwisho unaanza kwa wazo. Wakati mtu fulani anapojenga nyumba kwanza alianza kuwa na mchoro wa picha. Wakati mtu anapotaka kuanzisha biashara, kwanza kabisa anakuwa ameshatafsiri mpango ambao biashara itatoa na jinsi itakavyofanya kazi. Wakati mwana sanaa anapopaka rangi picha kwanza anakuwa amewaza au kuwa na hisia anazotaka kuelezea. Katika mifano yote hii kuna uumbaji wa aina mbili, kwanza picha akilini na kisha kitu kinachoonekana.

Baadhi ya maeneo yanakosa harakati kwa sababu mwili wa Kristo unakosa maono kwa ajili yake. Jinsi gani watu wanaweza kukazana kuelekea hicho ambacho hawawazii? Viongozi wa harakati wanapaka rangi picha ya haja ya Mungu. Wanatangaza 'Z' ikidhihirisha sababu ya kuhamasisha kote kote.

## III. VIONGOZI WA HARAKATI NI WAHAMASISHAJI

Viongozi wa harakati za upandaji kanisa wanatazama upanukaji wa kanisa kama ulivyo kiukweli, kama vita vya kiroho. Wakitambua kuwa hawawezi kupigana vita hii ya kiroho peke yao, wanalia kwa ajili ya kuhamasisha. Kama ulivyo wakati wa vita, wakati hisia ya uharaka na hitaji la kupona linapotawala kila kitu watu wanachosema na kufanya, ndivyo kanisa lililohamasishwa linavyofanya kazi pamoja kufikia kile Mungu anachotaka." Kuhamasisha' kwa kifupi maana yake ni kuweka wazi katika utayari kufuatana na uwezo wao katika kushiriki kwenye sababu kuu. Viongozi wa harakati wanaelewa kwamba wakati mwili wote wa Kristo utahamasisha kitahadhali kuzunguka sababu ya kushuhudia kwa ajili ya Kristo, Mungu atazidisha kanisa kuelekea kufikia lengo la kufanya wafuasi.

> Viongozi wa harakati za upandaji kanisa wanatazama upanukaji wa kanisa kama ulilvyo kiukweli, kama vita vya kiroho.

Inachukua mtu wa kiroho kuhamasisha makanisa katika vita hii ya kiroho. Inachukua yule anayemjua Mungu kujua kile Mungu anachotaka. Viongozi wa harakati wanaweza kutambua nyakati na kuhisi uongozi wa Roho kujua kile kanisa linachotakiwa kufanya. Kuendeleza undani huu wa kiroho, viongozi wa harakati wanatumia mda katika neno la Mungu, katika maombi na kufunga, wakiwa pamoja na mjenzi wa kanisa, Bwana na Mkombozi wetu, Yesu Kristo, kiongozi halisi wa harakati.

## IV. VIONGOZI WA HARAKATI NI WAWEZESHAJI

Kimapokeo viongozi wa kikristo wamekuwa wakifikiriwa kama wale "wanaofanya" huduma. Waefeso 4:11-12 inafundisha kwamba kazi ya uongozi kimsingi inatakiwa kuwaza na kuandaa wengeine kuwa na hakika kwamba huduma inafanyika. Viongozi wa harakati ni wawezeshaji, wale wanaofariji na kuwezesha wengine kutumia vipawa vyao. Wakati viongozi wa harakati wanaweza kuwa watu wenye juhudi sana, kawaida wakifanya kitu fulani, ni sahihi zaidi kuwaelezea siyo kama 'watendaji' lakini kama wale 'wanaosababisha vitu kufanyika. Wanatambulika kwa ajili ya kutia moyo wengine kimkakati kufanya kazi. Wakati viongozi wa harakati wanapokuwa kazini wengine wanaotaka kumtumikia Mungu watajiunga. Moja ya alama ya muwezeshaji mfanisi ni huduma iliyoongeza ufanisi wa wengine.

Kiongozi wa harakati ni kama mkulima anayepanda mbegu, anatifua udongo na kuumwagilia, lakini hana nguvu ya kufanya hasa mbegu kukua (1Kor 3:6-7). Kazi ya mkulima ni kulisha kile alichopanda, kuondoa vikwazo kwenye ukuaji wake na kutoa mazingira mazuri inavyowezekana kwa maendeleo yake. Hali ni sawa kwa kiongozi wa harakati. Kama alivyo mkulima ni 'mtendaji' anayesababisha vitu kufanyika.

**Kielelezo 12.1 Aina Mbili za Viongozi**



**Kiongozi Mwelekezi**

- ***Mtenda kazi* = "Kazi inafanyike!"**
- ***Mtendaji***
- ***Anayejaribu***
- ***Lengo* = "Fanya kazi ya huduma"**



**Kiongozi Mwezeshaji**

- ***Mtu wa watu* = "Ana husisha watu!"**
- ***Mteuzi***
- ***Mwandaaji***
- ***Lengo* = "Kuandaa kwenye"**

**SULUHU**

Alipomalizia kazi yake ya hapa duniani, Yesu aliwapa wanafunzi wake agizo kuongoza kama alivyofanya (Yn 20:21). Alikuwa amewaandaa vya kutosha ili kwamba kama wakitumia walichojifunza kutoka kwake, wangekuwa na mguso sawa (hata zaidi) (Yn 14:12).

Hao wanaomfata kiongozi leo wameamriwa kuongoza kama alivyofanya. Kumbuka njia ya kipekee ya Yesu. Aliishi kama mtumishi, kwa undani akiwapenda wafuasi wake aliowafundisha kuendeleza maono—huu ni uongozi katika ubora wake. Huyu ni kiongozi mkuu wa harakati anayegusa maisha na kubadilisha ulimwengu.

# VIKUNDI KIINI

VKUNDI KIINI

SOMO LA 12

# Vikundi Kiini Vinavyoenea Kupitia Makanisa ya Mtaa

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuelezea jinsi ya kupanga kwa ajili ya na kuweka huduma ya vikundi kiini katika kanisa lililopo.

☞ **Wazo Kuu**

Vikundi kiini vinaweza kutumika katika kanisa lolote linalotaka kukua na kutimiza Utume Mkuu.

☞ **Matokeo Yanayotaraji**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa kwamba vikundi kiini vinaweza kutumika kuimarisha kanisa lililopo katika maeneo ya ushirika, kufuasa, uinjilisti na maendeleo ya uongozi.
- Fikiria kuhusu mguso bayana na usio bayana ambao vikundi kiini vinaweza kuwa nao kwenye huduma iliyopo ya kanisa.
- Kuelewa hatua ambazo lazima zichukuliwe ili kupanga kwa ajili na kuweka matumizi ya vikundi kiini kwenye kanisa lililopo.
- Kuweza kuanzisha mpango wa msingi kuanza kutumia vikundi kiini kwenye kanisa lililopo.

## UTANGULIZI

Lengo la kuanzisha harakati za makanisa mapya ni kutimiza Utume Mkuu na hatimaye kufikia "miisho ya dunia" (Matendo 1:8) kwa habari njema ya Kristo. Ushirika, ufuasishaji na uinjilisti kwenye kikundi kiini unatoa matofali ya kujengea ambayo kanisa lililopo linahitaji ili kuanzisha makanisa mengi mapya kupitia makundi haya. Makanisa yaliyo na maono ya kuzidisha yanaweza kutumia vikundi kiini siyo tu kuanzisha makanisa binti mapya lakini pia kuleta kurejezwa na ukuaji wa makanisa yao wenyewe. Vikundi kiini kwa hakika siyo njia pekee ambayo hili linaweza kutokea, lakini ni njia ya ufanisi ya kuleta maisha mapya na mkazo kwenye huduma ya kanisa. Katika kutumia vikundi kiini, makanisa ya mtaa yaliyopo yanaweza kueneza "Yerusalemu" yao yaani majiji yao au mji, kwa ushuhuda unaoendana kwa ajili ya Kristo.

Unapoangalia faida katika huduma za vikundi, inakuwa wazi kwamba kuna sababu nyingi kwa nini kanisa la mapokeo litataka kutumia vikundi kiini pia. Vikundi kiini katika kanisa lililopo vinaweza kufanya kuwezekana kwa wajumbe kuendelea na kuimarisha mahusiano yao. Wanapotumia mda pamoja, wataanza kujifunza kuhusu furaha na mizigo ya mwingine, na wataweza kutimiza amri ya kiblia ya kupendana (Yn 13:34-35) na kubebeana mizigo (Gal 6:2).

Katika kutumia vikundi kiini, wajumbe wa kanisa wanaweza kujifunza kutambua vipawa vyao vya kiroho na kisha kuviendeleza na kuvitumia. Badala ya sehemu kubwa ya huduma kufanywa na viongozi wachache tu katika kanisa (mara nyingi kuzidiwa). Zaidi na zaidi ya wajumbe wataanza kuhusika katika huduma za kufuasa, kulisha neno na uinjilisti. Vikundi vitaweza kutoa kwa ajili ya maendeleo ya viongozi wapya katika kanisa kutoka miongoni mwa wajumbe. Kanisa litakua kwa matokeo ya uinjilisti kwenye vikundi.

Mda huo huo, matumizi ya vikundi kiini katika kanisa lililopo mara nyingi kunabadilisha baadhi ya nguvu ya huduma katika kanisa. Uongozi wa kanisa lazima ujitoe kwenye aina hii ya huduma na kuwa na jukumu bayana. Kuna maswala kadhaa ambayo lazima yajadiliwe na kuombewa kabla kikundi kiini hakijaanza kwenye kanisa. Mara uamzi unapofanyika kushirikisha vikundi kiini kwenye kanisa,

viongozi wa kanisa wanatakiwa kuanzisha mpango na kisha, uongozi wa Roho Mtakatifu, kuweka mpango huo katika kanisa.

## I. TATHIMINI

Ili kutumia vikundi kiini kwenye kanisa lililopo, kuna maswala ambayo lazima yapewe mawazo ya uangalifu. Kwa makusudi ya kujadili katika somo hili, tutadhani kwamba mpanda kanisa amekuwa akifanya kazi na vikundi kiini na atapenda kuvitambulisha kwenye kanisa lake anakotoka. Lazima atumie mda fulani na mchungaji (wa) na viongozi wa kanisa kuelezea sura na faida za vikundi kiini, vile vile kujadili nao baadhi ya maswala amabayo yataathiri majadiliano endapo kama watumie vikundi kiini katika kanisa.

Maswala ambayo lazima yajadiliwe na uongozi wa kanisa lolote ambalo linaazimia matumizi ya vikundi kiini ni kama yafuatayo:

### A. Maono

Ni maono yapi waliyonayo viongozi kwa ajili ya kanisa? Inawezekana kwamba vikundi kiini vitumike kusaidia na kutia moyo maono? Vikundi kiini vinaweza kutumika kama msingi wa mkakati wa huduma kubwa. Kwa kudhania kuwa uinjilisti na ukuaji unatokea katika makundi, jinsi gani makundi yanayozaliana yanaweza kutumia katika mkakati wa huduma kwa ujumla. Kanisa linataka kukua, linataka kuanzisha makanisa binti mapya, au linataka kutuma nje baadhi ya wajumbe kwenye timu ya umishenari kwenye miji mingine? Viongozi wa kanisa wanahitaji kuamua kwenye maono ya huduma na mkakati kwa vikundi kiini, kama inavyoendana na maono kwa ujumla ya huduma ya kanisa.

### B. Kujitoa

> Moja ya vigezo muhimu vinavyoweza kuonyesha mafanikio au kushindwa kwa vikundi kiini kwenye kanisa lililopo ni kiwango cha kujitoa miongoni mwa viongozi wa kanisa.

Moja ya vigezo muhimu vinavyoweza kuonyesha mafanikio au kushindwa kwa vikundi kiini kwenye kanisa lililopo ni kiwango cha kujitoa miongoni mwa viongozi wa kanisa. Wanahitaji kuelewa faida, na malengo ya huduma ya kikundi kiini. Wanahitaji kuelewa kwamba kikundi kiini siyo tu kikundi kidogo mahali ambapo watu watakutana pamoja kujifunza Biblia. Ndiyo, Kujifunza Biblia itakuwa sehemu ya vikundi, lakini siyo kusudi kuu. Kusudi kuu ni kuona mwili wa Kristo kwenye utekelezaji: wakimwabudu Bwana, wakiadilisha waumini, na kuwainjilisha waliopotea. Viongozi wako tayari kujitolea kwenye msisistizo huu kwenye huduma ya vikundi? Kutahitajika kuwa na baadhi ya ulaini kwenye sehemu ya uongozi wa kanisa uliopo ili kuweza kuratibisha baadhi ya mabadiliko ambayo vikundi kiini vitatambulisha kwenye kanisa.

### C. Huduma Zilizopo

Matumizi ya vikundi kiini katika kanisa yatasaida na kutia moyo huduma za uinjilisti, ufuasishaji na maendeleo ya uongozi. Kutafakari kwa uangalifu lazima kutolewe kwenye matokeo ambayo vikundi kiini vinaweza kuwa nayo kwenye huduma zilizopo katika kanisa. Katika baadhi ya makanisa, huduma ya vikundi kiini inaweza kukamilisha ambayo imeshakuwepo. Kwa jinsi hiyo, vikundi kiini vinaweza pia "kushindana" au kuingilia huduma iliyopo kwenye kanisa. Wakati mwingine huduma ya vikundi kiini inageuka kuwa ya ufanisi zaidi kuliko huduma iliyokwisha kuwepo. Kwa mfano, kama kanisa limekuwa likifanya uinjilisti kwa kufanya kampeni za nje ya mlango, idadi ya watu wanaoitikia kawaida inaweza kuwa kidogo sana. Kama uinjilisti wa kimahusiano unaotokea katika vikundi unafanyakazi vema sana, kiongozi wa huduma ya uinjilisti iliyopo anaweza kujisikia "kutishiwa" na vikundi kiini. Hili linaweza kupelekea kwenye matatizo kati ya hao wanaofanya huduma "kwa njia ambayo kawaida imekuwa ikifanyika" na hao wanaofanya huduma katika vikundi kiini.

Jadili matumizi ya vikundi kiini na kila kiongozi wa huduma katika kanisa, na ona jinsi anavyojisikia kuhusu hiyo. Kuna maeneo yenye migogoro maarufu? Baadhi ya huduma zilizopo zinaweza (Mf. Ufuasishaji) kuhitaji kubadilishwa au kuondolewa kama vikundi vinatumika? Maswali haya lazima yaulizwe kabla vikundi kiini havijaweza kutumika katika kanisa.

### D. Mapokeo dhidi ya Mawazo Mapya

Kwa baadhi ya watu kwenye kanisa lililopo, sura ya vikundi kiini inaweza kuwa kitu kigeni na kwa namna fulani cha kutisha. Wanaweza kupinga matumizi ya vikundi, hasa hasa kama hawajawahi kamwe kuwa katika huduma ya kikundi. Wakati mwingine watu wanapinga huduma ya kundi kwa sababu wamekuwa sehemu ya kundi kwa hatua fulani nyuma, na kundi halikufanya kazi vizuri. Mda wa kutosha na nguvu lazima vitumike ili kuwasaidia wajumbe wa kanisa kuelewa makundi na kuona faidia zake kwenye kanisa.

Kutegemeana na kanisa, kanuni zinazoambatana za kufanya uinjilisti wa kimahusiano kwenye vikundi inaweza kuwa vigumu kwa baadhi ya wajumbe wa kanisa kuzikubali. Kama hawajawahi kamwe kufanya uinjilisti wa kutosha, kama wameufanya kitofauti, au kama hawakuridhika na wazo la kufanya marafiki na wasioamini, wanaweza kuwa na mda mgumu wa kukubaliana na hitaji la vikundi kiini ambao uinjilisti wa kirafiki ni kipao mbele cha juu.

### E. Mahali

Haijalishi ni makundi mangapi yameanzishwa mwanzoni, kila kundi litahitaji kuwa na sehemu mahali ambapo watakutana pamoja kila wiki. Katika baadhi ya tamaduni, kukutana majumbani au kwenye kuta kunakubaliwa na hili halitakuwa tatizo. Katika tamaduni zingine, tatizo la wapi pa kukutania linaweza kuwa vigumu kulitatua. Kiongozi lazima afikiri wapi kundi la kwanza litakutana, hasa katika mwanga wa kuanzishwa kwa vikundi vingine zaidi kwa mda wa kipindi cha miaka kadhaa. Kwa kudhani kuwa makundi yanakua na kuzidi, wapi kundi jipya litakutana? Hili linatakiwa lijadiliwe kabla vikundi kiini havijaanzishwa ili kwamba lisiwe tatizo baadaye, kundi linapokuwa tayari kuzidi.

### F. Uongozi

Kwa kuanza, kila uongozi wa kanisa unahitaji kuamua nani ana sifa na anapatikana kuwa viongozi wa vikundi kiini vya kwanza (Tazama Mwongozo wa 3, Somo la Vikundi Kiini, “Kufunza Viongozi Wapya wa Vikundi Kiini”). Watu hawa lazima wapewe mafunzo na maandalizi ili kuweza kuongoza vikundi vyao kiufanisi. Mafunzo haya yanatakiwa yawe pamoja na somo kutoka katika miongozo hii kwenye vikundi kiini, na njia za kujifunza Biblia. Masomo mengine kutoka katika miongozo hii yanaweza kufundishwa kulingana na mahitaji na uzoefu wa viongozi wajao.

Mfumo wa kiusimamizi unatakiwa upangwe na kuwekwa katika sehemu kutoka mda ambao vikundi kiini vya kwanza vinaanzishwa (hili litajadiliwa kwa undani katika somo la 13, “Kusimamia Viini”). Mtu mmoja lazima ateuliwe kama mshauri wa viongozi wa vikundi kiini hivi na lazima awe tayari kukutana na viongozi angalau mara moja kwa mwezi, vile vile na kutoa mafunzo yanayoendelea na kutia moyo. Mshauri anaweza kuchagua kuanzisha kikundi kiini cha viongozi kuwapatia msaada unaoendelea, mafundisho na kutia moyo.

Kumbuka kwamba huwezi kuwa na vikundi mwanzoni kuliko ulivyo na viongozi kwa vikundi hivyo. Baadhi ya makanisa yanaamua kugawanya kusanyiko lote kwenye vikundi, wakati wengine wanaanza tu na watu walio na nia ya aina hii ya huduma. Kama viongozi wa kanisa wanatoa mwaliko wazi kwa yeyote anayetaka kuhusika, wanaweza kujikuta kwenye matatizo kama watu wengi wanaitikia kuliko viongozi waliopo.

Kumbuka kwamba huwezi kuwa na vikundi mwanzoni kuliko ulivyo na viongozi kwa vikundi hivyo.

Maswala yote hapo juu lazima yachukuliwe kwenye hesabu wakati kanisa linapofikiria kutumia vikundi kiini. Baada ya viongozi wa kanisa kujadili matumizi ya vikundi kwenye kanisa lao, mda lazima utolewe kwenye kuomba juu ya endapo au la kuendelea na aina hii ya huduma. Uamzi huu utakuwa na mguso imara kwenye maisha ya wajumbe wa kanisa na halitakiwi kuchukuliwa kirahisi. Kama Roho Mtakatifu anadhihirisha matumizi ya vikundi kwenye kanisa, kisha uongozi wa kanisa lazima upange jinsi vikundi vitakavyoanzishwa na kuwekwa.

## II. UPANGAJI NA UWEKAJI

Kila mpango unaoanzshwa kwa ajili ya huduma ya kikundi kiini katika kanisa utakuwa tofauti na utaonyesha utofauti na tabia ya kanisa hilo. Ingawa mchanganuo utatofautiana kutoka mpango hadi mpango, kuna hatua fulani ambazo lazima zipangwe na kisha kuwekwa ili kutambulisha huduma ya vikundi kiini kwenye kanisa lililopo.

### A. Hatua 1 – Anzisha Maono ya Huduma Ambayo ni Pamoja na Vikundi Kiini

Wachungaji na uongozi wa kanisa lazima waelewe lengo la huduma ya kikundi kiini. Vile vile wanatakiwa kuelewa kazi za vikundi kiini, pia na jinsi huduma inavyotokea katika kikundi kiini. Wanatakiwa waweze kuelezea faida za kikundi kiini kwa yule ambaye havielewi. Lazima wahakikishe na kutia moyo vikundi kiini kwenye kanisa.

Mkakati wa jumla wa huduma lazima ufikiriwe kimaombi. Jinsi gani vikundi kiini vitaingia katika maono na malengo ya kanisa? Vikundi vitatumika kwa kifupi kusaidia ukuaji na ufuasishaji katika kanisa? Kanisa linataka kuanzisha moja au makanisa binti zaidi? Kanisa linataka kutuma nje timu za wamishenari kuanzisha huduma ya vikundi kiini kwenye maeneo mengine? Mkakati wa jumla utaongoza na kuelekeza huduma ya vikundi kwa namna kwamba wataanzisha na kuingiliana na mmoja kwa mwingine.

### B. Hatua 2 – Anza Kushirikisha Maono kwa Kusanyiko

Wachungaji na viongozi wa kanisa wanatakiwa kuanza kushirikisha maono na faida ya kutumia vikundi kiini na kusanyiko. Wanahitaji kuonyesha jinsi vikundi vinavyoingia kwenye malengo ya kanisa, na jinsi vikundi vitakavyoimarisha kanisa na huduma yake. Vile vile wanatakiwa kuelezea faida kwa kila mmoja wa wajumbe wa kanisa.

### C. Hatua 3 – Chagua Viongozi na Wafunze

Onyesha hao katika kanisa wanaoweza kuwepo na wenye sifa ya kuongoza kikundi kiini. Tumia mda pamoja nao kuelezea malengo, faida, mawazo, n.k. ya vikundi kiini. Waulize kimaombi kufikiria kuongoza moja ya kikundi.

> "Uongozi" wa kikundi kiini unaweza kutumika kuandaa viongozi wajao.

Amua juu ya mfumo wa usimamizi kwa viongozi wa vikundi kiini. Angalau mtu mmoja lazima awajibike kushauri viongozi, kuwafanya kuwajibika, na kutoa msaada unaoendelea pamoja na matatizo na maswali. Njia moja ya kushauri viongozi ni kuanzisha kikundi kiini cha mwanzo na viongozi wa kikundi kiini kijacho kama wajumbe. Kundi hili linatakiwa likutane kwa miezi kadhaa kabla vikundi kiini vingine vyovyote havijaanzishwa katika kanisa. Hili litawapa viongozi yote mafunzo na uzoefu katika huduma ya vikundi kiini. Mtu anayeongoza "uongozi" huu wa kikundi kiini anatakiwa awe yule yule atakayeshauri viongozi wapya. Uongozi huu wa kiini unatakiwa uendelee kukutana mara moja moja (pengine mara moja kwa mwezi) baada ya vikundi vipya kuanzishwa. Huu unatakiwa uwe mda wa ushirika, mafundisho, na kujadili matatizo na maswali kwenye vikundi.

Funza Viongozi wajao wa vikundi kiini kwenye sura zote za huduma ya kikundi kiini. Kwa kiwango cha chini, wanatakiwa wapokee mafunzo kutoka kwenye Masomo ya Kikundi Kiini, Masomo ya Kujifunza Biblia, na Masomo ya Uongozi kwenye miongozo hii.

### D. Hatua 4 – Anzisha Vikundi Kiini Vipya

Baada ya miezi kadhaa ya kukutana katika "uongozi" wa kikundi kiini, viongozi wanatakiwa kuanzia kupanga kwa ajili ya kuanzisha vikundi kiini vyao. Lini kila kundi litakutana (yaani ni siku ipi na mda gani)? Wapi kila kundi litakutana? Ukidhani kuwa baadhi ya watu katika kusanyiko wameonyesha shauku ya kuwa sehemu ya kundi, jinsi gani itaamuriwa ni kundi lipi watajiunga?

Kuna kiasi kikubwa cha maandalizi ya awali ambayo lazima yatokee kabla kundi la kwanza kabisa la kikundi kiini kukutana (katika mwongozo wa 2, tazama Somo la Vikundi Kiini la 2, "kanuni za Uongozi wa Kikundi Kiini" na somo la 3, "kuanzisha Kikundi Kiini"). Mshauri wa viongozi wa vikundi kiini anatakiwa kusaidia na kutia moyo kila kiongozi kujiandaa kwa ajili ya mkutano huu muhimu wa kwanza.

Inaweza kuwa msaada kuweka tarehe ya kuanzia kwa vikundi kiini vipya na kushirikisha hili kwa kusanyiko, ili kwamba wawe wanaomba kwa ajili ya huduma hii mpya, vile vile na kutazama mbele kwenye nyakati ambazo vitaanza. Hili litasaidia kuamsha msisimko na shauku kuhusu vikundi vipya.

### E. Hatau 5 – Toa Tathimi Inayoendelea na Marekebisho Kwenye Huduma ya Kikundi Kiini

Uongozi wa kanisa unatakiwa, mda hadi mda, kutathimini maendeleo ya vikundi kiini. Kama ilivyo kwa aina yoyote ya huduma, marekebisho yanaweza kuhitaji kufanywa kwenye mipango na mawazo ya awali. Uwe wazi kwenye uongozi wa Roho Mtakatifu, na kwa kuendelea kuomba kwa ajili ya vikundi na viongozi wake, kwamba Mungu atawatumia kujenga kanisa na kulisaidia kutimiza malengo yake na makusudi.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Kwa kufikiria faida zote za vikundi kiini kwenye maeneo ya ushirika, kufuasa, uinjilisti na maendeleo ya uongozi, kwa nini kila kanisa lisitumie vikundi kiini?
- Ngoja tudhani kwamba kanisa limeamua kuanza kutumia vikundi kiini. Jinsi gani unaweza kuepuka "ushindani" kati ya huduma zilizopo za ufuasishaji na uinjilisti na huduma hizi sawa kwenye vikundi kiini?
- Kwa nini ni muhimu kuwa na mshauri kwa viongozi wa vikundi kiini katika kanisa? Nini wajibu na majukumu yake?
- Kwa nini "uongozi" wa kikundi kiini unatakiwa kuanzishwa miongoni mwa viongozi wa vikundi kiini wajao katika kanisa kabla kikundi kiini chochote kuanzishwa? Ni nini faida za kuwa na uongozi wa kanisa uliohusika katika huu "uongozi" wa kiini?
- Ni nini lengo la jumla la kutumia vikundi kiini katika mfumo wa kanisa lililopo?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Fikiria kuhusu kanisa unalidhania kuwa kanisa lako la "nyumbani". Ni nini maono ya kanisa? Ni malengo yapi lililo nayo? Inaweza ikawezekana kutumia vikundi kiini kusaidia kufikia malengo haya?
- Katika kanisa hili hili, nini matatizo au ugumu ungeweza kuwepo kama vikundi kiini vingetumika?
- Anzisha mpango mfupi, ulioandikwa kwa kutumia vikundi kiini katika kanisa hili (au katika kanisa lolote ambalo unalijua). Jinsi gani unaweza kuweka mpango huu?
- Fikiria makanisa unayoyajua ambayo yangefaidi kutoka katika huduma ya vikundi kiini. Jinsi gani unaweza kuyaendea kuhusu kutumia vikundi kiini kuimarisha kanisa na kulisaidia kufikia malengo yake? Unaweza ukawa tayari kuyasaidia kuanzisha huduma ya kikundi kiini katika kanisa? Lipe hili uangalizi wa makini na maombi.

VIKUNDI KIINI

SOMO LA 13

# Usimamizi wa Viini

## UANGALIZI NA UPANGILIAJI KWA AJILI YA VIONGOZI WA KIKUNDI KIINI

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hli ni kuchochea kila mfunzwa kuanzisha mfumo wa kiusimamizi ili kuvutia na kuwezesha ukuaji katika huduma yake ya kikundi kiini.

☞ **Wazo Kuu**

- Wajibu wa wapangaji na waangalizi wa viini.
- Lazima kuwe na kuendea kulikoundwa kwa kusimamia huduma ya kikundi kiini.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa . . .

- Kuelewa faida za na hitaji la aina fulani ya mfumo wa usimamizi kwenye huduma ya kikundi kiini.
- Kujua wajibu na majukumu ya kila mtu kwenye mfumo wa kiusimamizi na jinsi vinavyochangia kwenye ukuaji na mafanikio ya kiini.
- Anzisha msingi wa mpango wa kuweka aina fulani ya mtindo wa kiusimamizi katika huduma yake mwenyewe ya kikundi kiini kama hakipo kimoja kilichowahi kuwepo.

☞ **Ziada**

13 Vikund: Hatua ya Mwisho

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Katika "Utekelezaji wa Azimio, wafunzwa wameulizwa kusoma ziada 13A "Vikundi Kiini: Hatua ya Mwisho" na kuunda msingi wa mpango kwa ajili ya mtindo wa kiusimamizi kwenye huduma zao za vikundi kiini. Kwa kuwa hili ni somo la mwisho la kikundi kiini, uwe na hakika kuwa mpango huu umefanyiwa marudio ama na wewe au na mshauri/mkufunzi mwingine.

**UTANGULIZI**

Timu ya wamishenari wawili (Petro, Sandra and Michael) wamekuwa wakifanya kazi katika jiji lenye karibu watu 35,000 kwa miaka mitatu iliyopita. Wote wameanzisha vikundi kiini kadhaa, na baadhi ya vikundi hivi vimeongezeka mara kadhaa zaidi. Kama mtu angeangalia kwenye idadi ya watu wanaokutana na idiadi ya watu waliookoka, ingeweza kuonekana kwamba huduma yao imekuwa na mafanikio hata hivyo.

Kwa jinsi hiyo, vikundi vinaendelea kukua na kuzidi, Petro, Sandra and Michael wanachanganyikiwa zaidi na zaidi. Kila mmoja wao amekuwa na matatizo na maswali katika kujaribu kuanzisha kiongozi mwanafunzi mpya, na hakuna mmoja wa kuendea kwa ajili ya ushauri. Wote wana kazi nyingi ambazo hata inakuwa mara chache kuonana wao kwa wao. Na inaonekana kana kwamba wote wamechukuliwa katika huduma zao tofauti. Wakati Petro, Sandra and Michael walipoanza kufanya kazi kwenye jiji, Petro alikuwa na maono ya kuanzisha makanisa kadhaa kwa kutumia vikundi kiini. Hivi karibuni, ingawa, kila mmoja ana kazi nyingi na kikundi chake mwenyewe kiasi kwamba hakuna mmoja anayezungumzia hilo tena

Kile ambacho Petro, Sandra and Michael hawajui ni kwamba vingi kati ya vikundi kiini kadhaa vipya vinakutana na matatizo ambayo baadhi ya viongozi wenye uzoefu zaidi wangeweza kusaidia, lakini hakuna aliyewaambia au kuwapa msaada. Vikundi viwili kati yake vinapanga kuendesha kufikia nje

kiuinjilisti kwenye eneo hilo hilo la jiji, wakati eneo kubwa la mji linabakia kutokuwa na aina yoyote ya ushuhuda kwa ajili ya Kristo. Petro anafurahi kuwa viini vinaendelea kukua na kuzidi, lakini inaonekana kwake kwamba kwa jinsi fulani wanaweza kukamilisha zaidi kama wangepata njia ya kufanya kazi kwa umoja na ya mmoja kwa mwingine.

Ambacho Petro hatambui katika muonekano huo ni kwamba kuna sura ya kiuongozi ambayo inakosekana kutoka kwenye huduma yake ya kikundi kiini. Mtu fulani anahitajika kutoa usimamizi kwa ajili ya viini ili kupanga na kupangilia juhudi zao wanapokuwa wakifikia nje kwenye jiji lao.

Hata hivyo, kwa watu wengi waliohusika katika huduma, neno "utawala" linaleta akilini kivuli cha kazi ya makaratasi na kukatishwa kusiko kwa lazima. Wakati mwingine, "utawala" hata kumaanisha madaraka, utaratibu na kutawala, na kwa hiyo ni kitu fulani ambacho watu wanataka kuepuka kwenye huduma zao. Kwa jinsi hiyo, utawala ambao unaendelezwa kisawa sawa na kutumiwa kunaweza kusaidia kufanya uwezekano wa matumizi ya raslimali za Mungu.

> Utawala bila shaka ni wa lazima ili kuleta harakati za upandaji kanisa kupitia matumizi ya vikundi kiini.

Utawala ni kipengele cha lazima cha huduma ya kikundi kiini, na bila shaka ni cha lazima ili kuleta harakati za upandaji kanisa kupitia matumizi ya vikundi kiini. Utawala katika mfumo wa mtindo wa kiusimamizi ni kipengele muhimu cha maono ya huduma kubwa, hasa hasa vikundi kiini vinapoanza kukua na kuongezeka mara dufu.

## I. USIMAMIZI WA VIKUNDI KIINI

Katika wazo la jumla, "msimamizi" ni mtu anayeangalia kazi ya mtu mwingine. Anawajibika kuhakikisha kuwa kazi inafanyika vyema na kwa mda unaotakiwa. Katika huduma ya vikundi kiini, kuna hitaji la "wasimamizi" wa kusaidia viongozi wa vikundi kiini na "kazi" zinazotokea katika kikundi kiini. Wasimamizi hawa "hawatawali" na kulazimisha viongozi wa vikundi kiini kufanya vitu jinsi wanavyotaka; badala yake wanatoa maarifa, hekima na ushauri wa vitendo kwa viongozi, ili kwamba vikundi kiini vifanikiwe katika huduma zake.

### A. Umuhimu wa Usimamizi

Haijalishi vikundi kiini vimetumikaje katika huduma, kutafakari lazima kutolewe kwa jinsi gani viini vitasimamiwa kwenye mandhali hayo maalumu ya huduma. Kuna sababu kadhaa kwa nini aina fulani ya usimamizi unahitajika kwenye huduma ya vikundi kiini:

**Mipangilio:** Vikundi vilivyosimamiwa vina mtindo wa uongozi ambao unaweza kupanga juhudi za kikundi pekee kwa mwanga wa mkakati wa jumla wa huduma. Kadiri viini vinavyohudumu kipeke yake, kuna mpangilio ili kwamba juhudi za kila kundi zinachangia kwenye ukamilishaji wa kazi ya huduma kubwa. Mpangilio ni matokeo ya kuweza kuona "picha kubwa" ya nini (au kinachoweza kuwa) kinatokea nje ya kikundi kiini pekee.

Kwa mfano, ngoja tuseme kuwa lengo la jumla la huduma ya kikundi kiini fulani ni kuinjilisha mji wote au kijiji na kuanzisha makanisa matatu mapya. Kama juhudi za viini zinapangwa, kundi linaweza kuenea kwenye mji wote na bila "kupitana" na kila mmoja. Utafiti utafanyika kuonyesha meneo tofauti yanayokusudiwa kwenye mji, na kila kikundi kiini kitachora "mzunguko wa kuwajibika" kuzunguka eneo ambalo kitafikia. Katika njia hii viini vinaweza kushuhudia kwa ufanisi kwenye mji wote. Mda unapofika wa kuanzisha makanisa mapya, mipangilio kati ya viini inatoa uwiano na njia inayoridhisha ya kupanga katika vikundi viini kwenye makanisa.

**Kuelekeza:** Wakati aina fulani ya mtindo wa kiusimamizi upo mahali unapotakiwa, kila kiongozi wa kikundi kiini ana mtu ambaye anaweza kugeukia kwa maswali, matatizo na magumu. Kuna mazingira yaliyopangwa ambayo viongozi wa kikundi kiini wanaweza kujifunza kutoka mmoja kwa mwingine, vile vile na kujifunza kutoka kwa viongozi wenye uzofu zaidi. Badala ya viongozi wa vikundi kiini kuhangaika na matatizo au maswali yao wenyewe, wanakuwa na mtu fulani wa kugeukia kwa ajili ya msaada na ushauri.

> Moja ya sura muhimu ya usimamizi ni kwamba inatoa uangalizi na kulisha neno kwa viongozi wa vikundi kiini.

Viongozi wa vikundi kiini wanajikuta wao wenyewe kwa kuendelea wakihudumu kwenye mahitaji ya watu kwenye makundi yao, lakini hakuna anayewahudumia wao. <u>Moja ya sura muhimu ya usimamizi ni kwamba inatoa uangalizi na kulisha neno kwa viongozi wa vikundi kiini</u>. Njia moja ya vitendo ambayo hili linaweza kutokea ni kuunda "uongozi" wa kikundi kiini,

ambao viongozi wa vikundi kiini wanakutana kuhudumiwa na kujifunza kutoka kwa mmoja kwa mwingine.

**Kuwajibika:** Kila kikundi kiini kitakuwa na malengo yake ambayo yanachangia kwenye mkazo wa jumla wa huduma. Viongozi wa vikundi kiini wanahitaji mtu fulani ambaye watawajibika kwake kufikia malengo hayo. Malengo ya kila kundi yanaweza kwa vipindi kutathiminiwa na kurekebishwa, kama ni lazima. Hili hasa hasa linasaidia kwa makundi mapya na viongozi, kuwasaidia kuomba na kufikiria kuhusu mapenzi ya Mungu kwenye makundi yao na kuwasaida kuweka malengo yanayowezekana kwa ajili ya kundi. Kuliko tu "kusubiri vitu vitokee," kiongozi wa kikundi kiini aliyechukua kuwajibika atakazana kusaidia kundi lake kukamilisha kile ambacho Mungu amepanga mbele yao kama lengo.


**Unyooofu:** Moja ya faida ya kufanya huduma katika vikundi ni kwamba waumini wapya wanafuaswa na viongozi wapya wanaendelezwa kati kati ya viini. Kwa jinsi hiyo, kukosekana kwa ukomavu, kukichanganyika na jitihada zilizopita kunaweza wakati mwingine kuwa mchanganyiko hatari. Inawezekana kwa kikundi kiini kutoka nje ya njia na kuanza kutafsiri vibaya na/au kutumia maandiko vibaya. Mtindo wa kiusimamizi unaweza kutoa "utazamaji" ambao unahitaji kutokea katika kila kikundi kiini chochote ili kwamba uzidishaji, upitilizaji, na hata mafundisho potofu kutokuwa tatizo. Kundi lililoachwa lenyewe linaweza kuishia kutafsiri kwa kimakosa mafundisho ya neno la Mungu.

## B. Muundo wa Kiusimamizi

Haijalishi jinsi gani vikundi kiini vimesimamiwa, sura ya msingi inabakia kuwa ile ile: lazima kuwe na njia iliyoundwa ya kupanga na kusaidia viongozi wa vikundi kiini wanapokazana kuendeleza watu na huduma katika viini vyao. Wasimamizi wanamshikilia kiongozi wa kikundi kiini kuwajibika kwa kazi na malengo kwenye kikundi, na kuchunguza mafundisho na maendeleo ya kiroho ya wote kiongozi na wajumbe kwenye kikundi.

Mfumo unaofanana hasa wa kiusimamizi wa vikundi kiini kawaida una ngazi mbili: Tutaiita ngazi ya kwanza *wapangaji,* wanaofanya moja kwa moja na viongozi wa kikundi kiini. Tutaiita ngazi ya pili *waangalizi,* kimsingi wanaofanya kazi na wapangiliaji. Wote wapangiliaji na waangalizi wana wajibu maalumu na majukumu kusaidia kuendeleza viongozi wa kikundi kiini na huduma kati kati ya vikundi kiini:

*1. Mpangaji*




Kwa kuwa jukumu la mpangaji kimsingi ni kuelekeza na kufundisha viongozi wa kikundi kiini, Mpangaji anatakiwa atumie mda kama kiongozi wa kikundi kiini kabla hajateuliwa kwenye nafasi hii. Viongozi wa kikundi kiini wanahitaji kuwa na mtu atakayewashauri kama huduma yao itakuwa yenye ufanisi. Yafuatayo ni maeneo ambayo mpangaji anahitaji kuhusishwa katika maisha na huduma ya kiongozi wa kikundi kiini:

- Matatizo katika kundi – Mpangaji anakutana na viongozi wa kikundi kiini mara moja moja. Katika huduma zingine ni mara kwa mara kama mara moja kwa wiki, na wakati mwingine inaweza kuwa mara moja kwa mwezi tu. Huu unaweza kuwa mkutano usio wa kawaida, au mpangaji anaweza kuchagua kuunda "uongozi" wa kikundi kiini. Wakati wa mda huu wa mikutano, viongozi wa kikundi kiini wako huru kuuliza maswali, kujadili matatizo, na kujifunza kutoka kwa mmoja kwa mwingine katika uzoefu wao wa vikundi kiini.

- Ukuaji wa mtu wa kiroho – Mpangaji pia anatakiwa alifanye kiini cha kutumia mda kipekee na viongozi wa kikundi kiini na familia zao, kupata kuwajua vyema na kuelewa vyema nini kinachotokea katika maisha ya kila kiongozi. Hii inatakiwa kuwa mida isiyo ya kawaida ya kushirikishana na kuwa na ushirika, kama vile kuwa na milo pamoja au pengine kupata chai tu/kahawa nyumbani kwa kiongozi.

- Kuendeleza viongozi wanafunzi – Moja ya maeneo magumu ya huduma kwa kiongozi wa kikundi kiini itakuwa kuendeleza mwanafunzi wake kiongozi. Viongozi wengi wapya wa vikundi kiini hawajawahi kamwe kufanya kazi kwa juhudi kuendeeleza mwingine kama kiongozi, na watakuwa na maswali mengi na matatizo katika eneo hili. Mpangaji anaweza kushirikisha njia za vitendo ambazo aliendeleza kiongozi mwanafunzi kwenye vikundi kiini vilivyopita.

- Upangaji na uwajibikaji – Mpangaji anawajibika kuwasaidia viongozi wa kikundi kiini kuendeleza malengo na mipango kwa ajili ya huduma na kuwawajibisha kupata malengo haya. Hii ni pamoja na kuchora “mduara wa kuwajibika” na kila kundi kuwasaida kuelewa wapi watakuwa wanafanya kazi (katika maeneo gani ya kijografia), na kwa mkato gani wa wakazi watawafikia. Mpangaji pia lazima asaidie viongozi wa kikundi kiini kuanzisha mpango wa kuzidisha na kufanya mpango huo. Kwa nyongeza, kila kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa kuwa na mipango ya pekee kwa maendeleo ya kiroho ya kila mjumbe wa kundi, na mipango kwa ajili ya uinjilisti na shughuli nyingine za kikundi. Kufanyia marudio na kurekebisha mipango hii na viongozi wa kikundi kiini ni muhimu kwa ukuaji na mafanikio ya kila kikundi kiini.

- Ujuzi wa vitendo wa huduma – Mpangaji anatakiwa pia kutoa mafunzo na mafundisho yanayoendelea kwa viongozi wa kikundi kiini, kuendelea kuwaandaa kwa huduma yenye matunda. Mpangaji anatakiwa kukazana kutoa mafundisho ambayo yatakidhi mahitaji ambayo kwa wakati huo yapo kwenye maisha na huduma za viongozi wa kikundi kiini. Mafundisho yanatakiwa yatoe njia za vitendo kusaida katika matatizo halisi ya maisha na hali ambazo viongozi wanakutana nazo.

> Kila kiongozi wa kikundi kiini anatakiwa kuwa na mpango wa pekee wa maendeleo ya kila mjumbe wa kikundi.


- Kutia moyo – Ni wazo zuri kwa mpangaji kutembelea vikundi kiini mda hadi mda, na anatakiwa awe na kuelewa wazi nini kilichojifunzwa na kufundishwa kwenye kikundi. Kila mandhali ya huduma ni tofauti, lakini mpangaji anatakiwa kutunza mwelekeo wa wajumbe wangapi walio katika kila kundi, na wageni wangapi wanakuja kwenye kundi, wapi makundi yanakutania, na tatizo ambalo halijatatuliwa ambalo viongozi wanakabiliwa nalo.

- Maombi – Mpangaji lazima atumie mda katika maombi na viongozi wa kikundi kiini na anatakiwa awaombee viongozi wa kikundi kiini katika mda wake pekee wa maombi. Anatakiwa kuendelea kuangalia njia za kuwasaidia viongozi, ili kwamba huduma zao zifanikiwe na kwamba wanakua katika ukomavu na kufanana na Kristo.

Kwa sababu ya kiasi cha mda mwingi na nguvu ambazo mpangaji anatakiwa atoe kwenye uangalizi na maendeleo ya kila kiongozi wa kikundi kiini, anatakiwa awajibike siyo kwa zaidi ya vikundi kiini vinne au vitano.

2. *Mwangalizi*

Jukumu la mwangalizi linatofautiana na la mpangaji zaidi kwa ukweli kwamba mwangalizi haingiliani moja kwa moja na viongozi wa kikundi kiini – anafanya kazi kimsingi na wapangaji. Mwangalizi anatakiwa awe mwenye uzoefu kwenye huduma ya kikundi kiini, akiwa ameshakuwa kiongozi wa kikundi kiini na mpangaji yeye mwenyewe. Mwangalizi anapendelea katika maisha na huduma ya kila mpangaji, vile vile na kuelekeza hduma kwa jumla kwa vikundi kiini. Mwangalizi ni mshauri wa wapangaji kwa njia sawa mpangaji ni mshauri kwa viongozi wao wa kikundi kiini.



Mwangalizi anatakiwa akutane na wapangaji mara moja moja, siyo chini ya mara moja kwa mwezi. Wakati wa mida hii ya kukutana, wapangaji wanaweza kutoa taarifa za maendeleo na shughuli za kila moja ya kikundi kiini ambavyo wanawajibika kwavyo. Kwa makusudi ya kutunza maadiko, mwangalizi anaweza kuchagua kuanzisha aina fulani ya fomu zilizoandikwa ambazo kila mmoja wa wapangaji anaweza kujaza habari kuhusu viini.

Moja ya kazi muhimu za mwangalizi ni kushauri na kuendeleza juhudi zinazoendelea zilizopangwa miongoni mwa vikundi kiini. Mwangalizi anatakiwa atunze "picha kubwa" ya huduma akilini, na anatakiwa kuhakikisha kwamba kila mpangaji wazi wazi anaelewa jukumu la kila kikundi kiini kwenye mpango huo. Kwa mfano, lengo la kundi moja fulani la kikundi kiini ni kuanzisha makanisa mapya mawili kwenye eneo la mji. Wapangaji wawili wanafanya kazi na vikundi kiini viwili vya kujitegemea, wakati mpangaji wa tatu ana baadhi ya vikundi kiini vya kujitegemea vile vile na baadhi ya vikundi kiini ambavyo vilianzishwa kwenye kanisa lililopo. Ni wajibu na jukumu la mwangalizi kuwasaidia wapangaji kuelewa jinsi vikundi kiini vyote vinavyoweza kufanya kazi pamoja kuunda makanisa haya mawili mapya na hatua zipi zinahitaji kuchukuliwa ili kuona hilo linatokea.

Wakati kunapokuwa na matatizo kwenye vikundi, au kwenye maisha ya mpangaji, mwangalizi wakati wote anapatikana kusikiliza, kuomba, na kutoa ushauri. Anatakiwa atunze mda wa maombi ya mara kwa mara kwa kila mpangaji, vile vile na kwa hitaji la maombi lolote la dharura kati kati ya vikundi.

Baadhi ya huduma za vikundi kiini wanachagua kukusanya vikundi kiini vyote kukutana pamoja mara kwa mara (pengine mara moja kwa mwezi) kwa ajili ya kuabudu, kushirikiana na/au mafundisho. Wakati mwingine kukutana huku kunaeleweka kama mida ya "kusherehekea". Kama kukutana huku kunatokea, mwangalizi, anaweza akamuuliza mpangaji mmoja au zaidi kusaidia kwenye kuabudu au kufundisha.


Baadhi ya huduma za vikundi kiini wanachagua kukusanya vikundi kiini vyote kukutana pamoja mara kwa mara (pengine mara moja kwa mwezi) kwa ajili ya kuabudu, kushirikiana na/au mafundisha.

## II. MIUNDO YA KIUSIMAMIZI KWENYE VIELEZO TOFAUTI VYA HUDUMA YA KIKUNDI KIINI

Mara nyingi, matengenezo yanayoonekana na huduma ya kikundi kiini yataonyesha mfumo ambao muundo wa kiusimamizi utakaochukua. Somo la Kikundi kiini la 6, "Falsafa ya Huduma ya Kikundi Kiini," limeonyesha mitindo kadhaa tofauti ambayo inaweza kutumika katika huduma ya kikundi kiini.Yafuatayo ni marudio kwa ufupi ya kila moja ya mitindo hiyo, pamoja na aina ya miundo ya kiusimamizi ambayo inaweza kutumika katika kila hali:

### A. Kielezo 1: Vikundi Kiini Vinavyoanzisha kanisa la Mapokeo kwa Viini

**Kielelezo 13.2 Viini Vinavyoanzisha kanisa**





Katika hali hii, kikundi kimoja au zaidi ya vikundi kiini vya awali vinakua na kuongezeka mara dufu mpaka vinapokuwa vinaweza kuanzisha kanisa mpya la mapokeo. Kanisa hili litakutana katika eneo la kati kwa ibada ya kuabudu ya kimapokeo inayofaa kwa mandhali ya hapo na utamaduni. Kanisa litaendelea kutumia huduma ya vikundi kiini kwa ajili ya uinjilisti, ushirikiano, ufuasishaji na kukua kunakoendelea kwa kanisa. Linaweza pia kuchagua kuanzisha huduma ya kimapokeo "vipindi" kama vile shule ya jumapili, huduma ya wanawake, kuwafikia watoto siku za mapumziko, n.k. Kielelezo 13.2 kinaonyesha aina hii ya mtindo.

Katika hali hii, muundo wa kiusimamizi utahitajika mda mrefu kabla kanisa halijaanzishwa. Mtindo huu utahitaji angalau mpangaji mmoja kuanagalia huduma ya kila kiini pekee na kuwasaidia viongozi kupanga juhudi za kuanzisha kanisa mpya. Inashangaza kufahamu kwamba baada ya kanisa kuanzishwa na viini kuendelea kukua na kuongezeka, mpangaji anaweza kuitwa “shemasi” au “mzee” mkuu wa huduma ya kikundi kiini.

**B. Kielezo 2: Kanisa Lililopo Linaanza Kutumia Vikundi Kiini**

**Kielelezo 13.3 Viini Vilivyoongezwa Kwenye kanisa**





Inawezekana kwa kanisa lililopo kuanza vikundi kiini kwa ajili ya ushirika, uinjilisti, na ufuasishaji (tazama Somo la Vikundi Kiini 12). Uongozi uliopo katika kanisa lazima uamue ni vikundi vingapi vinahitajika/vinawezekana kufuatana na idadi ya watu katika kanisa wanaoweza kufundishwa kuwa viongozi wa vikundi kiini. Katika mda kanisa litakapoanza kukua kadiri vikundi kiini vinavyokua na kuongezeka. Mchanganuo huu unaonyeshwa katika kielelezo 13.3

Kikufanana, muundo wa kiusimamizi katika hali hii unatumia viongozi wa kanisa waliopo kutimiza wajibu wa mpangaji na mwangalizi. Mashemasi na wazee wanaweza kuwa wapangaji, na mchungaji (au timu ya uchungaji) anaweza kufanya maamuzi ya juu ya maana kushikilia nafasi ya mwangalizi. Kadiri kundi linavyokua na kuongezeka, mara nyingi sana viongozi wa kikundi kiini wataanza kutimiza wajibu wa mpangaji na hatimaye mwangalizi.

**C. Kielezo 3: Vikundi Kiini ambavyo Vinaanzisha kanisa la Kikundi Kiini**

**Kielelezo 13.3 Viini Vinaanzisha Kanisa la Kiini**





Kanisa la kikundi kiini linatofautiana kutoka kanisa la mapokeo kwa maana kwamba ama kuna jengo la kanisa ama ibada ya kuabudu ya kila mara jumapili asubuhi, na kanisa halipo kuanzisha na kutunza “vipindi” kanisani. Kanisa ni mkusanyiko wa viini vyenyewe, na kazi zote za kanisa zinatokea katika kila kiini, ikiwepo ubatizo na meza ya Bwana. Viini vinakutana pamoja mara moja moja (Mf. Mara moja kwa mwezi) kwa ajili ya mkutano wa kusherehea. Huu ni mda wa kutia moyo, ushirika, kuabudu na/au mafundisho. Viini vyote vinajifikiria vyenyewe kuwa sehemu ya kimoja, kanisa kubwa. Kielelezo 13.4 kinaelezea mtindo huu.

Mara nyingi, muundo wa kiusimamizi kwa kanisa la kikundi kiini ni rahisi na wa kimadaraja. Kila vikundi kiini vitano, vina mpangaji na kuna mwangalizi kwa kila wapangaji watano. Kama idadi inakua na kuwa kubwa, kuna hitaji la ngazi nyingine ya washauri, wakati mwingine wanaitwa “wachungaji wa Viini” wanaofanya kazi na waangalizi.

**D. Mtindo 4: Vikundi Kiini Kadhaa Vinakua, Vinazidi na "kulisha" Makanisa ya Mtaa Yaliyopo**

**Kielelezo 13.5 Viini Vinalisha Makanisa**




Siyo hitaji kwamba vikundi kiini moja kwa moja vinaanzisha makanisa mapya. Inaweza kuwa kimkakati zaidi kujenga na kuimarisha makanisa ya mtaa yaliyopo ambayo katika mda yataanzisha makanisa binti mapya. Vikundi kiini vinaanzishwa kikujitegemea kwa makanisa yaliyopo. Kadiri watu wapya wanavyoletwa katika vikundi kiini, wanatiwa moyo kuanza kuhudhuria kanisa la mtaa pia. Mara nyingi wataendelea kuwa sehemu ya kikundi kiini chao vile vile na kuhudhuria kanisa. Utaratibu huu unaonyeshwa kwenye kielelezo 13.5.

Katika hali hii, moja ya viongozi wa kikundi kiini anaweza kushika wajibu wa mpangaji, ili kusaidia kupanga juhudi za vikundi kujenga makanisa kwenye eneo hilo. Kama wakati mmoja au zaidi ya makanisa yaliyopo yanatamani kutumia vikundi kiini kwenye kanisa lao, muundo tofauti wa kiusimamizi utahitaji kufikiriwa na kutumiwa.

## III. MATUMIZI KWENYE HUDUMA YAKO YA KIKUNDI KIINI

Kichwa kinachochaguliwa kwa kila mtu kwenye muundo wa kiusimamizi kama vile "mpangaji" na "mwanagalizi" siyo muhimu. Katika mandhali ya huduma yako maalumu, unaweza kuchagua na kutumia kichwa chochote unachojisikia kinafaa na kueleweka. Kitu muhimu sana ni kwamba kuna watu wanaofanya <u>kazi</u> za wapangaji na waangalizi kwenye muundo wowote uliotolewa wa kiusimamizi. Hawa ni watu wanaohitajika kusaidia vikundi kiini kukamilisha malengo ambayo Mungu ametenga mbele yao.

Mandhali yako itaonyesha nani hasa anatimiza wajibu huu wa uongozi. Kama vikundi kiini vimeanzishwa kwa kujitegemea kwa kanisa lililopo, mara nyingi kiongozi wa kikundi kiini mwenye uzoefu zaidi anashika wajibu wa mpangaji mara kundi linapoanza kukua na kuzidi.

Pengine unatumia vikundi kiini katika kanisa la mapokeo ili kusaidia kanisa kukua (na hatimaye kuanzisha makanisa binti mapya). Katika hali hii unahitaji kutumia hekima na busara katika kuamua nani atajaza wajibu wa mpangaji na mwangalizi. Mara nyingi inapendeza kwamba watu hawa wamekuwa viongozi wa makundi wenyewe na wana uzoefu sana katika maisha ya vikundi kiini. Kwa jinsi hiyo, kwenye kanisa la mapokeo, matatizo yanaweza kuibuka kwa haraka kama viongozi waliopo wamepangiwa wajibu huu lakini wao wenyewe hawajawahi kamwe kuwa sehemu ya huduma ya kikundi kiini. Maombi ya kutosha na utambuzi vinatakiwa kutumika kama ukiwa kwenye hali ya namna hii. Kama huna uchaguzi lakini kutumia viongozi "wasiozoea - viini katika nafasi hizi, fanya kadiri uwezavyo kuwasaida kuelewa sura, faida na utofauti wa huduma za kikundi kiini. Kwa mda, viongozi kutoka kwenye huduma ya vikundi kiinii wanajitwalia nafasi hizi za uongozi kwenye muundo wa kiusimamizi.

> Muundo wa kiusimamizi hauhitajiki ili kutawala huduma za vikundi kiini, lakini kuandaa, kuwezesha na *kutoa* vikundi kiini kuhudumu.

Hata hivyo, moja ya vitu vya kwanza tunavyofikiria tunapoona aina yoyote ya muundo wa kiutawala ni dalili za mabavu. Ni muhimu kuelewa kwamba muundo wa kiusimamizi hauhitajiki ili kutawala huduma za vikundi kiini. Badala ya kutawala vikundi kiini, kila kiongozi kwenye utawala wa chama anatakiwa kuwa anafanya yale yote anayoweza kuandaa, kuwezesha na *kutoa* vikundi kiini kuhudumu kwa njia iwayo yote ambayo Roho Mtakatifu anawaongoza. Harakati za kikundi kiini chini ya uelekekezi wa Roho Mtakatifu hasa hasa "hautawaliwi" kwa namna ya kuingilia kwa mwanadamu. Ni utii wa uaminifu wa watu wa Mungu wa kujitoa kikamilifu kutumia maisha yao, mda na vipaji wanapohudumu ndani na kupitia vikundi kiini.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Elezea hitaji la baadhi ya mahitaji ya muundo wa kiusimamizi unapofanya kazi na huduma ya kikundi kiini. Kwa nini usiviache viini kufanya vyovyote wanavyotaka? Ni faida zipi za kuwa na kuwepo kwa muundo wa kiusimamizi?
- Kwa maneno yako mwenyewe, kwa kifupi elezea kazi za kiuongozi ambazo zinatakiwa zitokee kwenye huduma yoyoye inayoendelea ya kikundi kiini.
- Kama kwa sasa unahjihusisha katika huduma ya vikundi kiini na hakuna mmoja bado anayeshikilia wajibu wa mpangaji, nani unaweza kumwendea kuhusu kuwa mpangaji? Unaweza kujifikiria kushika wajibu huu wakati fulani mbeleni?
- Jinsi gani wajibu wa mwangalizi ni tofauti na wa mpangaji?
- Inawezekana kwa wapangaji na waangalizi kuendelea kuwa viongozi wa vikundi kiini?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Soma Ziada 13A "Vikundi Kiini: Hatua ya Mwisho." Kimaombi fikiria nini Mungu anataka kwa ajili ya huduma yako ya kikundi kiini kabla hujaanza kupanga kwa ajili ya aina fulani ya muundo wa kiusimamizi katika huduma yako.
- Halafu, anzisha mpango rahisi wa aina ya muundo wa kiusimamizi ambao ni wa lazima katika mandhali ya huduma ya kikundi kiini chako maalumu. Fikiria juu ya vichwa utakavyoweza kutumia kwenye wajibu wa mpangaji na mwangalizi. Hata kama una vikundi kiini kadhaa wakati huo, nani wanaoweza kushika wajibu wa mpangaji kwa vikundi hivi? Roho Mtakatifu anavyoendelea kufanya kazi na kundi lako linakua na kuzidi, jinsi gani utaamua nani watakuwa wapangaji na waangalizi wa mbeleni? Wapi watatoka, na aina gani ya mafunzo au uzoefu watahitaji ili kuwaandaa kwa aina hii ya huduma? Ni aina gani ya muundo wa kiusimamizi unaohitaji kutunza na kuchochea ukuaji na haja za Mungu kuona ikitokea katika vikundi kiini vyako? Ni aina gani ya muundo wa kiusimamizi utaendana vema zaidi na mtindo wa huduma unayofanya nayo kazi? Chora katika mpango wako mchoro wa mtindo unaotumia na jinsi muundo wa kiusimamizi uliochagua unafaa katika mtindo huu.
- Fanya marudio ya mpango wako kwa ajili ya muundo wa kiusimamizi na mshauri wako au na mkufunzi wa somo hili.

VIKUNDI KIINI
*ZIADA*
13A

# Vikundi Kiini: Hatua ya Mwisho

## I. MOYO KWA MATAIFA

Tunapojifunza Biblia, ni wazi kwamba Mungu anataka kujifanya mwneyewe kujulikana miongoni mwa mataifa yote ya dunia. Katika Kutoka 19:5 Mungu anamwelekeza Musa kuwaambia watu wa Israeli kwamba *"Kama mkinitii kikamilifu na kutunza agano langu, ndipo mtakapokuwa tunu kwangu kuliko makabila yote ya watu, maana dunia yote pia ni mali yangu, nanyi mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani na taifa takatifu."* Mpaka atakapokuja Kristo, taifa la Israeli lilikuwa chombo kilichochaguliwa na Mungu kuwa mashahidi wake kwenye ukuu wake na utukufu. Zaburi 96:2-3 inasema, "*Mwimbieni Bwana, libarikini jina lake; tangazeni wokovu wake siku kwa siku. Wahubiri mataifa habari za utukufu wake, na watu wote habari za maajabu yake."*

Yesu alipokuja, Alikamilisha sheria ya Agano Jipya (Rum 10:4), Alilianzisha kanisa (Mt 16:18) na aliwaamuru wanafunzi wake kuwa mashahidi wake (Mdo1:8) mpaka "miisho ya dunia." Kanisa liligeuka kuwa chombo ambacho kupitia hicho Mungu anataka kufanya upendo wake na neema kujulikana kwa watu wote.

Mvuto wetu wa kuanzisha makanisa mapya ni kutimiza amri ambayo Kristo alitupatia kwenye Utume Mkuu. Tumegundua kwamba vikundi kiini ni njia moja ambayo inasaidia kuanzisha makanisa yanayokua, yenye afya na yanayozaliana. Tumetumia mda wa kutosha kujadili kwa undani na kufanya kazi kwa huduma ya vikundi kiini.

> Tumegundua kwamba vikundi kiini ni njia moja ambayo inasaidia kuanzisha makanisa yanayokua, yenye afya na yanayozaliana.

Ni muhimu kujua na kuelewa umaalumu wa huduma ya kikundi kiini. Kazi kwenye kikundi kiini zinaonekana katika mfano wa kanisa la kwanza Yerusalemu (Mdo 2:42-47). Vikundi kiini ni njia moja ya kuiga na kutoa njia kwa kazi hizi hizi zinazofanana kutokea katika makanisa yetu na huduma leo.

Kwa jinsi hiyo, ni muhimu kuweka akilini lengo la jumla, "picha kubwa" ya kile Mungu anachotaka kutoka katika juhudi zetu binafsi za huduma. Ni nafasi ipi vikundi kiini vinasimama katika utimizaji wa Utume Mkuu? Nini kinatakiwa kiwe kinatokea katika vikundi kiini vyenu ili kusogea karibu na karibu kuelekea lengo hilo? Inatosha kuanzisha vikundi kadhaa na kuviona vikianza kuzidi, au Mungu anataka zaidi? Nini ni hatua ya "mwisho" kwa vikundi kiini kuchukua katika kusaidia kutimiza amri ambayo Kristo alitoa zaidi ya miaka 2000 iliyopita?

## II. KUZIDISHA KWA IMANI

Moja ya tabia kuu za vikundi kiini zinazotofautisha ni kwamba vinazaliana. Kuzaliana lazima kutokee kama kundi litabakia "hai" – bila hilo hatimaye vinadumaa na kufa. Kuzidisha siyo mvuto wa kichocheo cha uinjilisti katika vikundi kiini, lakini unaruhusu uinjilisti unaoendelea na wa juhudi kutokea. Kawaida kuna "nafasi" kwa wasioamini zaidi na waliokata shauri wapya katika kuzidisha vikundi kiini.

Kila mmoja wetu anaelewa na kukubaliana na hitaji la kuzidisha kwenye huduma ya kikundi kiini. Kwa jinsi hiyo, ni mara ngapi "tunapunguza" nguvu na ukuu wa Mungu kwa vipingamizi vyetu wenyewe vya imani na maono? Tunapoangalia huduma ya vikundi kiini vyetu wenyewe kwa macho sawa na ambavyo Mungu anaviangalia? Kama tungeliona huduma zetu kama Mungu anavyoziangalia, ni vipingamizi gani na vizuizi vitatakiwa kuondolewa? Nini kitakuwa tofauti? Jinsi gani tutaelewa umuhimu na umaarufu wa vikundi kiini vyetu?

Tunapoanza mara ya kwanza kufanya kazi na vikundi kiini, ni vigumu kufikiria zaidi sana kuliko kufanya vikundi hivyo vya awali kuendelea, kufundisha viongozi wanafunzi na kufanya kazi kuelekea kufanya kuzidisha kutokea. Tunajifunza zaidi kuhusu vikundi kupitia makosa, matatizo na furaha za kuwa viongozi wa vikundi kiini. Mara tunapogundua hitaji la kuwa na vikundi tofauti vinavyofanya kazi pamoja kwa umoja na ushirikiano kimoja kwa kingine ili kukamilisha malengo ya huduma kubwa. Katika mda tunapoanza kufikiria aina fulani ya muundo wa kichama ambao unahitajika kusaidia kupanga juhudi za vikundi kiini vingi.

Isaya 40:26 inasema, "Inua macho yanu na mutazame mbinguni: *nani aliyeziumba zote hizi? Yeye aletaye nje jeshi lao kwa hesabu; aziita zote kwa majina. Kwa sababu yeye ni hodari kwa nguvu zake, hakuna moja isiyokuwapo mahali pake."* Katika huduma zetu za vikundi kiini, tunahitaji pia "kuinua macho yetu na kuangalia mbinguni." Tunapoangalia pengine lakini si kuelekea kwa Mungu, tunafikiria kile tu ambacho kinaweza kufanyika kwa uwezo wetu. Lakini tunapoangalia kwa Mungu, tunaanza kuelewa uwezo na nguvu zake, na anachoweza kufanya kupitia sisi.

Kama tungekuwa na macho yanayoona kile Mungu anachoona, tungeweza kuwa na shauku, kuogopeshwa au pengine yote? Kukosa kwetu imani wakati mwingine kunapunguza uwezo wetu wa kutumiwa na Mungu katika kipimo kamili cha mapenzi yake kwa maisha yetu na huduma? Imani inatuwezesha kuota ndoto kubwa na kujaribu vitu vikubwa kwa ajili ya Mungu, tunapotambua kuwa nguvu zake zinapatikana kuwezesha juhudi zetu.

Imani haijijali yenyewe kwa upungufu wetu wote na kutotosheleza. Badala yake, imani inakazia kwenye utoaji na uwezo wa Mungu mwenyewe kukamilisha kile ambacho anataka. Imani inaona kinachoonekana kutokuwezekana, lengo lisilofanyika, na kisha kuwa tayari kujitokeza na kutumiwa na Mungu katika kupata kile ambacho kibinadamu kilikuwa kazi "isiyowezekana" nje. Imani haielewi sawasawa jinsi ya kukamilisha lengo fulani au kazi, lakini inaelewa kwamba Mungu anaweza kukamilisha kazi hiyo kwa na kupitia watu waliotayari kutumiwa bila kujali hali zao na misuko suko.

Tumetaja kuwa viongozi wa vikundi kiini wanatakiwa wakazane *kuyatoa* makundi hayo kuhudumu kwa nguvu za Roho Mtakatifu na chini ya uelekezi wake. Wakati vikundi kiini vinapokuwa na wajumbe ambao kwa utii wamejitoa maisha yao, mda na vipaji kwa Bwana, Roho Mtakatifu ana watu ambao anaweza kufanya nao kazi na kupitia wao ataweza kutoa matunda

> Viongozi wa vikundi kiini wanatakiwa wakazane *kuyatoa* makundi hayo kuhudumu kwa nguvu za Roho Mtakatifu na chini ya uelekezi wake.

Kujitoa kikamilifu kwa Mungu kuna maana kuwa na imani ambayo itaturuhusu kuhudumu kwenye misukosuko migumu, kushinda vizuizi vinayoonekana kutowezekana, na kuacha kukubali vizuizi ambavyo ulimwengu utaweka juu yetu. Tunahitaji kuomba kwamba Mungu atupatie imani ambayo tunaweza kutumiwa kukamilisha kupitia vikundi kiini vyetu vitu vikubwa ambavyo alivyo navyo moyoni mwake.

## III. MAKANISA KWA AJILI YA MATAIFA

Kama lengo letu moja katika huduma ni kuwa na vikundi kiini vinavyozaliana vinavyoendelea kutoka katika makanisa, vingapi vitatosheleza? Vipi kama tungekuwa na vikundi kadhaa ambavyo viko hai katika jiji au mji wetu? Vipi kama vikundi 10, au vikundi 50, au hata 500?

2 Petro 3:9 inaonyesha moyo wa Mungu kuelekea waliopotea: "*Mungu hachelewi kutimiza ahadi zake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huwavumilia, bila kutaka hata mmoja kupotea, lakini kila mmoja kuifikia toba.*" Haja za mioyo yetu inatakiwa pia iwe kufikia "kila mmoja" kwa habari jema ya kuokoa ya Yesu. Tunahitaji vikundi vya kutosha ambavyo vitahudumu siyo tu kwa ujilani wote fulani au kijiji, lakini kote kote kwenye mji wote na mikoa ya nchi. Yesu alizungumza juu ya imani inayoweza kuhamisha milima (Mt. 17:20). Tuna imani ya kutosha kuona nchi nzima ikiwa imejazwa na vikundi kiini ambavyo vinawafikia waliopotea, kuadilisha waumini na kutangaza habari njema ya Yesu Kristo mpaka atakaporudi?

Wakati huduma zetu za vikundi kiini zinapoacha kukatishwa kwa ukosefu wetu wa imani na kuwa na mtazamo mfupi, kisha vinageuka kuwa vya kutumika katika mikono ya Mungu. Wakati vikundi vyetu vinapokuwa na maono siyo tu kwa wakati ulio karibu, lakini kwa wakati ambapo nchi nzima itakapoenea kwa makanisa, kisha Mungu ataanza kuvitumia kwa njia ambazo kamwe tusingeotea kuwa zilikuwa zinawezekana.

Hili kisha, ni hatua ya “mwisho” ambayo tunahitaji kuchukua kama vikundi kiini vyetu vitasaidia kukamilisha Utume Mkuu. Hatua hii ya mwisho ni utaratibu wa kutia moyo viongozi wote wa vikundi kiini na wajumbe wote wa vikundi kiini kuona kikundi chao kikiwa kinatumika kwa njia ambazo Mungu anataka kukitumia. Ni utaratibu wa kutoa picha pana ya maono, ya kutia changamoto viongozi wa vikundi kiini “kuinua macho yao” kuelekea mbinguni na kuona taifa lao likijazwa kwa utukufu wa Mungu. Ni utaratibu wa kufanya kazi kwa juhudi kuelekea lengo hilo ndani na kupitia vikundi kiini.

Wakati tu huduma za vikundi kiini vyetu vinapokuwa na macho ambayo yanaweza kuona na imani ambayo itainuka kwenye changamoto tutaweza kumuona Roho Mtakatifu anaanza kutumia vikundi hivyo kwa njia ya ajabu na ya kimuujiza. Tunapoomba tu bila kukomaa kwa ajili ya mataifa yetu Bwana ataanza kufanya kazi kuzidisha vikundi ambavyo vitakuwa na mguso kwenye mji wote, mikoa na nchi.

Hatua ya mwisho katika huduma yetu ya vikundi kiini kwa kifupi ni “Hatua ya Imani.” Ni hatua ya mwisho ambayo lazima ichukuliwe kama huduma zetu za vikundi kiini zitakwenda kutumiwa na Roho Mtakatifu wa Mungu kusaidia kuleta kuhusu ukamilishaji wa Utume Mkuu. Hatutakiwa kuogopa kushindwa. William Carey, mvumbuzi mmishenari huko India, mara aliposema, “Jaribu mambo makubwa kwa ajili ya Mungu; Tarajia vitu vikubwa kutoka kwa Mungu.”

> “Jaribu mambo makubwa kwa ajili ya Mungu; tarajia vitu vikubwa kutoka kwa Mungu.”
>
> - *William Carey*

Nguvu ni za Bwana—tunahitaji kuwa watumishi ambao kupitia nguvu hiyo itatiririka. Nguvu ni za Bwana—kwa kifupi tunahitaji macho ambayo yako tayari kuiona. Ukamilishaji wa kazi pia ni wa Bwana—tunahitaji kuamini kwa imani kwamba juhudi zetu zinaongozwa kwenye ukamilisihaji wa kazi ambayo Mungu mwenyewe ameahidi kukamilisha.

Mungu anawasubiri watumishi waaminifu kuchukua” hatua hii ya imani” pamoja naye. Utakuwa mmoja wao?

# KUHUBIRI

KUHUBIRI

SOMO LA 1

# Kuhubiri Kibiblia I

## KUUELEWA UJUMBE

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuelezea jinsi ya kutunga ujumbe ambao utakuwa mwaminifu kwenye kusudio la somo na kuwakilisha wazi wazi wazo kuu la kifungu.

☞ **Wazo Kuu**

- Ujumbe unatakiwa kuainisha na kuwakilisha ujumbe wa Biblia kuliko tu mawazo ya mzungumzaji.
- Kuna aina nyingi za miundo ya ujumbe zinazowezekana. Uchaguzi unaguswa na somo, wasikilizaji, na msemaji.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa jinsi ya kutumia kichwa na ujazo ili kufupisha na kuweka wazi wazo kuu la ujumbe.
- Kujua wazo kuu la kimuundo la ujumbe.
- Kujua baadhi ya aina kadhaa za ujumbe ambazo zinaweza kutolewa.

**UTANGULIZI**

Mahubiri ya kibiblia ni ya kimungu na utendaji wa kibinaamu. Katika kuhubiri, Mungu anazungumza kwenye akili na mioyo ya watu akiwaleta kwenye imani na ukomavu ndani ya Kristo, lakini anafanya hivyo kupitia mawasilisho ya wanadamu. Mawakala watatu katika utaratibu ni neno la Mungu, Roho Mtakatifu, na muhubiri. *Wajibu wa muhubiri ni kuhakikisha kwamba anawakilisha ujumbe wa Mungu kwa nguvu za roho Mtakatifu*.

Kusudi la jumla la ujumbe wa kibiblia ni kuwashawishi watu kuamini taarifa zilizotolewa na kuzitendea kazi. Kwa hilo kutokea, makusudio ya muhubiri ni kuwakilisha ukweli wa neno kwa njia ambayo:

- itasadikisha akili
- itaamsha uwezo wa kuwazia
- itasogeza kwenye mapenzi
- itachoma dhamiri
- itagusa hisia

Kuna vigezo vikuu viwili vinavyoathiri endapo au la makusudio haya yatafikiwa. Navyo ni 1) ujumbe, 2) wasikilizaji, na 3) msemaji. Ujumbe kiusahihi lazima uonyeshe Mungu anachotaka kuwasilisha. Wasikilizaji lazima waone kuendana kwa ujumbe kwenye maisha yao. Na msemaji lazima atoe ujumbe kwa namna inayoufanya wazi na kutoupunguza. Kila moja ya masomo haya kwenye njia hii litakazia kwenye moja ya sura hizi tatu.

Tunapofikiria uundaji na utoaji wa ujumbe kibiblia, tunafanya dhana fulani:

- Tunataka ujumbe kuendana na maana ya neno la Mungu, kuliko tu fikira zetu, au mawazo ambayo tunaweza tukawa tumeyasikia kutoka kwa wengine.
- Tumetumia njia ya kujifunza kwa kufata neno kuvumbua maana ya fungu ambalo litahubiriwa kwa wengine.

- Tuko katika hali ambapo mfumo wa 'njia moja' ya mawasiliano kama vile kuhubiri kutakuwa kwa ufanisi kuliko njia ya 'njia mbili' kama vile kuongoza mafunzo ya Biblia kwa kufata neno au kwa kifupi tu kuwa mazungumzo juu ya Bwana.

- Baadhi, lakini siyo wafunzwa wote watataka kutoa mahubiri katika mandhali ya kawaida ya kuhubiri. Kwa jinsi hiyo, kanuni za kuhubiri kuzuri kibiblia zinatumika katika maandalizi mengi: mkusanyiko wa kanisa, mikutano ya vijana, vikundi vya wanawake, mikutano ya kiuinjilisti n.k. Wanawake pia na wanaume wawakilishaji watafaidika kutoka kwao.

> Baadhi, lakini siyo wafunzwa wote watataka kutoa mahubiri katika mandhali ya kawaida ya kuhubiri.

## I. MAFUNZO YA BIBLIA KWA KUFATA NENO—MSINGI IMARA

Ujumbe wa kuzingatia kwenye mafunzo ya kufata neno ya kifungu cha kibiblia ni njia bora kuhakikisha kwamba tunatoa ujumbe wa Mungu na siyo fikira zetu wenyewe. Kwa hiyo, mafunzo ya fungu yaliyoongozwa kimaombi ni ya muhimu kama mhubiri atakuwa na hakika kwamba hakika anatoa ujumbe wa Mungu. Kumbuka kwamba tunajifunza Biblia kikufata neno ili kuweza kutambua azimio la mwanzo la mwandishi

Kile tunachoelewa kwa kiasi na kisha kuhubiri azimio la andiko, kisha tunahubiri neno la Mungu na siyo mawazo yetu wenyewe. Somo la Njia za Kujifunza Biblia la 2-7 katika Mwongozo wa Kwanza linaeleza jinsi ya kufanya mafunzo ya Biblia kwa kufata neno. Fanya marudio ya uchunguzi, ufafanuzi na matumizi kutoka kwenye masomo hayo.

## II. WAZO KUU LA UJUMBE

Uzi mmoja wa kawaida unashonwa kote kwenye majadiliano yanayohusiana na mazungumzo wazi ya hadharani ya ufanisi. Mzungumzaji mfanisi anajenga ujumbe wake kuzunguka wazo moja lenye maana. Hili limekuwa kweli kwa wafafanuzi wa juu, wataalamu wa mawasiliano ya kisasa na wahubiri watimilifu. Kwa sababu akili yetu inatafuta umoja na utaratibu, ni muhimu kwamba tunahubiri kwa namna kwamba tabia hizi zinakuwa wazi kwa wasilizaji wetu.

> Tunajenga ujumbe wetu kuzunguka wazo moja la kati, na kila kinachosemwa kinatakiwa moja kwa moja au kinyume kiunge mkono kisa hicho.

Tunajenga ujumbe wetu kuzunguka wazo moja la kati, na kila kinachosemwa kinatakiwa moja kwa moja au kinyume kiunge mkono kisa hicho. Kwa hiyo ni muhimu kuchagua fungu la maandiko ambalo lina wazo la kati. Kama fungu lako lililochaguliwa lina mawazo kadhaa ya kati, pengine lina ujumbe wa mahubiri kadhaa badala ya moja tu.

### A. Weka Wazi Wazo Kuu (Kisa)

Wakati wote inasaidia kusema wazo la kati la fungu kwa kuainisha mambo mawili muhimu: *Kichwa* na *ujazo*. Njia hii inafanana na kueleza kanuni za kibiblia kwenye hatua ya ufafanuzi ya njia ya kujifunza kwa kufata. Kwa jinsi hiyo, 'kanuni za kibiblia ambazo zinatokana na kujifunza kwa kufata mara nyingi zinakuwa kwa namna fulani ndefu na za kutatanisha. Kwa kuanza na kanuni za fungu, na kuainisha kichwa na ujazo, mara nyingi tunaweza kufanya wazo kuu kuwa fupi na rahisi kuwezekana katika ujumbe, wakati tukitunza maana ya manenno yenyewe ya andiko.

*Kichwa* kinaeleza jambo linalozungumziwa au somo ambalo fungu linazungumzia. Huyu kawaida ni mtu, sehemu, kitu, au wazo. Linaweza kuonyeshwa kwa jina rahisi, na kwa hiyo haliundi fikira kamili. *Kichwa* cha fungu fulani kinaweza kuwa upendo, ufuasishaji, Yesu, kanisa, toba, n.k. katika hali zingine, *kichwa* kinaweza kuwa fungu la maneno machache ambayo yanafanya kazi kama jina. Mfano, wa aina hii ya vichwa ni: "kumpenda Mungu," "Kuwasamehe wengine," "kujazwa na Roho Mtakatifu," au "haja ya kumpendeza Bwana kwa kila kitu."

*Ujazo* ni fungu la maneno machache ambayo 'yanakamilisha' kichwa kwa kuelezea nini fungu linasema 'kuhusu kichwa.' Ujazo pia unaweza usilete maana wenyewe, lakini unapokuwa umejumlishwa kwenye *kichwa,* unaunda fikira kamili au wazo linaloleta maana na ni rahisi kuwakilishwa.


**Table 1.1 Kichwa na Ujazo**

| Aya: | Kichwa: | Ujazo: | Wazo Kuu: |
|---|---|---|---|
| Mit 9:10 | Hofu ya Mungu | . . . ni mwanzo wa hekima. | Hofu ya Mungu ni mwanzo wa hekima. |
| Rum 8:32 | Mungu, aliyetupa mwana wake | . . . atatupa kila tunachohitaji. | Mungu, aliyetupa mwana wake, atatupatia kila tunachohitaji. |
| Ebr 10:14 | Kujitoa mara moja kwa Kristo | . . . ametufanya kuwa kamili milele | Kujitoa mara moja kwa Kristo kumetufanya kuwa wakamili milele. |
| Rum 1:16 | Injili | . . . ni uwezo wa Mungu wa kuokoa. | Ijili ni uwezo wa Mungu wa wokovu. |
| 1kor 15:55 | Kifo | . . . kimepoteza nguvu yake dhidi ya waumini. | Kifo kimepoteza nguvu yake dhidi ya waumini. |

**B. Amua juu ya kusudi la Ujumbe**

Mara unapogundua wazo kuu ambalo mwandishi wa Biblia alikuwa akijaribu kuwakilisha, kuwa na maana hasa karibu ambayo utaanzia mahubiri yako. Hatua inayofata ni kuonyesha kusudi la ujumbe. Unataka ujumbe kuwasababisha wasikiaji kuamini ujumbe na kuufanyia kazi. Uamzi maalumu unaotaka wasikiaji kuchukua ni kusudi la ujumbe wako. Unatakiwa usijaribu kuunda kuitikia huku kupitia juhudi zako mwenyewe—hiyo ni kazi ya Roho Mtakatifu. Kwa jinsi hiyo, kwa kuwa umetambua kuitikia ambako unaamini Mungu anataka kutoka kwenye kifungu, unatakiwa kujaribu kuunda ujumbe kwa namna kwamba unafanya kazi kuelekea kusudi la Bwana.

**Kielelezo 1.2 Vigezo Vitatu katika Kuhubiri**




Kielelezo 1.2 kinaelezea jinsi Neno, Roho Mtakatifu, na ujumbe vinavyotakiwa kufanya kazi pamoja kugusa wasikilizaji. Hili ni jambo wakati tu muhubiri anapokuwa makini kwa vyote maana ya aya na kwenye uongozi wa Roho. Msemaji ambaye ni mwaminifu kutafuta kwa maombi maana ya fungu anatakiwa kutarajia kwamba hili litatokea.

## III. MUUNDO WA UJUMBE

Ujumbe mzuri, kama anwani yoyote ya umma, kawaida utakuwa na sehemu kadhaa. Sehemu hizi ni kama matofari ya kujengea. Vipo karibu wakati wote, ingawa utaratibu au mpangilio wa umuhimu unaoendana wa kila kimoja unaweza kubadilika. Tena, hili linakaribiana kuendana na ujumbe wa muhubiri. Inachukua mazoezi kuamua jinsi gani ya kuvipangilia vizuri. Zaidi ni sanaa kuliko sanyansi.

### A. Utangulizi

Ujumbe unatakiwa uwe na aina fulani ya utangulizi, endapo au la imewekewa alama hivyo. Kama, kwenye utangulizi, hupati usikivu wa wasikilizaji, na haja yao kwenye ujumbe unaoutoa, hakika unapoteza mda wako kuhubiri. Miili yao inaweza kuwepo pamoja nawe kwenye chumba, lakini akili zao ziko mbali sana.

Utangulizi kwa hiyo unatakiwa ukamilishe mambo matatu:

1. *Kusalimisha usikivu wa wasikilizaji.*
2. *Kutoa kichwa cha mahubiri.*
3. *Kuhusisha kichwa na mahitaji wanayojisikia wasikilizaji.*

Wasikiaji wanaweza kuamua endapo wasikilize au wadharau msemaji kwenye wakati mchache wa mwanzo wa ujumbe. Utangulizi uliofikiriwa vizuri unaweza kwenda mbali kuelekea kuwashawishi kwamba una kitu cha kusema, na kwamba ingefaa kukusikiliza. Utangulizi hafifu unaweza kukamilisha kinyume chake. Utangulizi mzuri unahitaji kuwaelewa wasikilizaji. Hili litakuwa kichwa cha somo linalofuata.

> Wasikiaji wanaweza kuamua endapo wasikilize au wadharau msemaji kwenye wakati mchache wa mwanzo wa ujumbe.

### B. Mwili

Mwili wa ujumbe ni msingi wa yaliyomo. Wakati wa kipindi hiki maana ya kifungu cha maandiko kawaida yanaelezewa, vile vile na kuendana kwake kwa hali ya wakati huo ya wasikiaji. Hapa ni mahali unapotakiwa kuwasaidia wasikilizaji kugundua wazo hilo hilo kuu ulilopata wakati wa kujifunza kwako kwa kufata. Pengine kwa kuwa hakutakuwa na mda wa kutosha kupitia utaratibu wote au kuleta nje uchunguzi wako wote, utahitaji kuchagua kwa uangalifu machache ambayo ni ya muhimu zaidi. Kazania kwenye ukweli ambao kwa haraka na kiwazi wazi unaonyesha wazo kuu, na kufaa kwa kusudi unapouelewa.

Mwili ni moyo wa ujumbe. Unatakiwa utoke kwenye neno. Kama maandiko yamewezeshwa zaidi kwa maelezo, michango ya mtu, hadithi zilizonukuriwa, au kitu kingine tu, siyo ujumbe wa kibiblia. Tunza maana ya maneno yenyewe kuwa kati.

### C. Suluhu

Suluhu ni mda unapofupisha ulichosema kwenye ujumbe na kuita kwa ajili ya kujitolea au kuitikia. Hili halimaanishi kwamba wakati wote utasubiri kutumia ujumbe mpaka mwishoni. Unaweza kuleta matumizi unapokuwa umefika mahali popote. Kwa hakika, baadhi ya wahubiri wanajisikia kwamba ujumbe wenye ufanisi unaweza kuundwa ifuatavyo:

1. Waambie kile <u>unachokwenda kuwaambia</u> = Utangulizi
2. Waambie = Mwili
3. Waambie <u>kile ulichowaambia</u> = Suluhu

Kurudia rudia kunaweza kuwa mtambo wa kujifunza kwa ajabu kama kunatolewa kwa njia inayopendeza. Kwa jinsi hiyo, ujumbe wakati wote unatakiwa kuishia kwa maelezo ya kusudi linalotakiwa, endapo au la lilikuwa limetambulishwa mapema kwenye ujumbe. Hiki kinatakiwa kiwe kitu cha mwisho ambacho watasikia, na kitu cha muhimu zaidi ambacho wanachukua kwenda nacho majumbani baada ya ujumbe kumalizika.

Suluhu inatakiwa iwe na moja au zaidi ya vipengele vifuatavyo:

- Ufupisho wa wazo kuu.
- Kielelezo kinacholeta pamoja wazo kuu na wazo la kati.

- Madondoo yanayokamilisha kusudi sawa kama kielelezo.
- Swali.
- Maombi.
- Mwelekeo maalumu au kuitia kwa ajili ya utendaji.

### D. Vielelezo

Kielelezo kinakusudiwa kuweka mwanga au kulifanya wazo kueleweka zaidi, mafundisho au swala lililoamshwa kwenye ujumbe. Kinaweza kutumika wakati wowote kwenye ujumbe—utangulizi, mwili, au suluhu. Hasa hasa kinasaidia unapotaka kutoa msisitizo kwenye mafundisho au kuelezea kifungu kigumu. Lakini kumbuka: Vielelezo lazima vichangie kwenye kuelewa kwa ujumbe uliotolewa. Usihusishe vielelezo kwa ajili tu ya kutaka kuwa na kielelezo.

Kuna aina kuu tatu za vielelezo vya kutumia katika kuhubiri: vielelezo vya kibiblia, vielelezo visivyo vya kibiblia na masomo ya kitu.

1. *Vielelezo vya Kibiblia*

Biblia imejaa vielelezo wazi, vya ajabu. Wakati mwingine tunaweza kupata vielelezo vya kisasa ambavyo pia vinafaa au vizuri, lakini mara nyingi hatuwezi. Nani anaweza kukuza hali kwenye mfano wa kondoo aliyepotea, au mfano wa maua ya shambani, au mtu aliyejenga nyumba juu ya mwamba? Wakati vielelezo hivi vinapoongea wazi wazi, tunatakiwa tuvitumie. Mifano ya vielelezo vya kibiblia ni pamoja na:

- Maisha ya mtu aliyetajwa katika fungu. Kwa mfano tazama Wafilipi 2:19-30.
- Marejeo yanayoingiliana. Kamusi itakusaidia kupata vifungu vingine vya kibiblia ambavyo vinashughulika na somo hilo hilo na inaweza kukusaidia kulielezea. Kanuni hapa ni kutumia maandiko kutafsiri maandiko.
- Masimulizi ya kibiblia. Masimulizi mengi kutoka Agano la Kale inasaidia kuelezea kanuni zilizotajwa kwenye Agano Jipya. Kwa mfano, maisha ya Yona ni kielelezo kizuri cha kanuni ambazo Mungu anahitaji utii wetu mkamilifu.
- Ramani. Ramani ya sehemu mahali ambapo tukio linatokea mara nyingi inasaidia kuelewa kifungu cha Biblia.
- Taarifa zilizopatikana kutokana na mandhali. Nyenzo kabla na baada ya Waefeso 5:15-21 inatusaidia kuelewa sura ya kujazwa kwa Roho.

2. *Vielelezo Visivyo vya Kibiblia*

Usiogope kutumia vielelezo ambavyo havitoki kwenye maandiko, ikiwa kiufanisi vinaunda maana ile ile. Mara nyingi, vielelezo hivi vitaungana zaidi na wasikilizaji wako. Hili hasa ni kweli ikiwa wasikilizaji hasa hasa hawaifahamu Biblia. Katika hali kama hizi, maana ya vifungu vingi au mifano ingewapotea, na ni vizuri kuchagua kitu fulani wanachoelewa. Mifano isiyo ya kibiblia ni pamoja na:

- Matukio ya hivi karibuni. Ukweli wa kibiblia haumailizi mda. Kwa jinsi hiyo, inaeleweka zaidi wakati tukio la hivi karibuni linapovielezea. Mara nyingi nakala kwenye gazeti na vijitabu vinatumika.
- Uchunguzi wa maisha ya kila siku.
- Uzoefu wa binafsi. Uzoefu wa binafsi mara nyingi ni vielelezo vyenye nguvu, kwa jinsi hiyo, tahadhari kujifanya kila wakati mshindi.
- Vielelezo kutoka katika asili. Picha ya shakwe kwenye amani, akisimama kwenye jiwe na mawimbi yakimzunguka, ni kilelezo kizuri cha mkristo aliyesimama kwenye jiwe lake, Bwana Yesu Kristo.
- Hadithi za nyuma. Ni muhimu kujua kuhusu maisha yasiyo ya maadili ya mji wa Waefeso kuelewa kikamilifu kusumbuliwa kwa Paulo kwenye sura ya 5 ya Waefeso.

3. *Masomo ya Kitu*

Masomo ya kitu ni zana yenye mafanikio katika mawasiliano kwa sababu yanatokana na kanuni kwamba kujifunza wazo mpya ni sura inayofanya rahisi wakati daraja linapojengwa kati ya kinachojulikana na kisichojulikana. Kitu ambacho ni cha kawaida kwenye uzoefu wa wajifunzao kinaonyeshwa na kuelezewa. Kisha kulinganisha kunafanywa kati yake na wazo mpya ambalo limetolewa. Kitu siyo hasa hasa kama wazo lililotambulishwa, isipokuwa kwa njia nyingine kinafanana na hilo. Anayejifunza kisha ataelewa baadhi ya wazo la ukweli mpya na kuwa tayari kushukuru kwa mawazo mengine mapya.

Moja ya faida kuu za masomo ya kitu ni kwamba yana ufanisi katika kusalimisha usikivu wa anayejifunza. Kristo mara nyingi alitumia masomo ya kitu katika huduma yake ya kufundisha. Yote ya asili kwake yalionyesha ukweli kuhusu Mungu. Baadhi ya masomo ya kitu aliyotumia ni kama ifuatavyo:

- Maji ya mwili na maji ya uzima (Yn 4:7-15, mwanamke kisimani)
- Mtoto na ufupisho wa imani (Mt 19:13-15)
- Ulishaji wa watu elfu tano na "mkate wa uzima" (Yn 6)

Baadhi ya mawazo mengine kwa masomo ya kitu ambayo tunaweza kutumia ni:

- Ramani ya njia (Yn 14:6)
- Glasi ya maziwa (1Pet 2:2, Ebr 5:12,13)
- Kipande cha sabuni (1Yn 1:9)
- Glasi ya maji na mkate (Yn 4, 6)
- Mshumaa au tochi (Yn 8:12)
- Mlango au lango (Yn 10:1-10)
- Picha ya kondoo au aliye halisi (Isa 53:6; Ps 23)
- Upanga (Ebr 4:12)
- Kipande cha fedha na zawadi iliyofungwa (Rom 6:23)
- Caseti isiyochomekwa kwenye umeme—isiyowekwa kwenye chanzo cha nguvu zetu za kiroho hatuwezi kufanya lolote (Yn 15:5)

## IV. AINA ZA UJUMBE

Kuna aina nyingi za ujumbe. Msemaji mzuri anatakiwa kuweza kutumia kadhaa kati yake kadiri mahitaji yanavyoibuka. Ni kama zana mkononi mwa muhunzi. Kila moja inafaa kwa hali fulani ya kazi. Muhubiri, kama muhunzi, anahitaji kujua lini na wapi kila moja inapoweza kuwa ya ufanisi zaidi kutumika. Mifumo iliyoorodheshwa hapo chini siyo ya kuchosha. Mabadiliko ni mengi kuweza kuyaorodhesha. Pia, ujumbe unaweza kiufanisi kuunganisha mfumo zaidi ya mmoja.

### A. kuelekeza

Aina hii ya ujumbe hasa hasa inatoa ukweli. Unatumika hasahasa kuelezea mafundisho. Ni ya ufanisi sana wakati kusudi kuu la ujumbe ni *kujulisha.* Inaweza kusaidia kuleta mabadiliko katika *kuelewa.* Nyaraka nyingi za Agano Jipya ni mtindo wa kuelekeza. Zinalinda kusisitizia kwenye maana na sababu.

### B. Kiibada

Ujumbe wa kiibada unakazia zaidi kwenye muitikio wa kiroho kuliko ukweli au ufahamu. Kama ujumbe wa kueleleza unakusudia zaidi kwenye 'kichwa' ujumbe wa kiibada unakusudia kwenye 'moyo' wa msikilizaji. Aina hii ya ujumbe inasisitizia hisia, na mara nyingi pamoja na vielelezo vya kihisia zaidi. Zaburi ni mfano mzuri wa kitabu cha kiibada.

### C. Kimasimulizi

Ujumbe wa kimasimulizi unajengwa juu ya hadithi moja au zaidi. Hadithi hizi zinaweza au zisiweze kuwa za kibiblia. Ukweli wa neno unachanganywa kwenye hadithi. Hadithi inatumika kama kiunzi kinachosaidia wasikiaji kupangilia na kuelewa ukweli uliofundishwa. Ujumbe kama huo unaweza kuwa wa kukumbukwa. Kwa hakika, uangalifu lazima ufanyike ili kwamba hadithi hazizidi nguvu ya ukweli wa neno, na kuwa mamlaka. Vitabu vya kihistoria vya Biblia ni vya kimasimulizi.

### D. Ki-kuuliza

Wakati ujumbe mwingi unakazia kwenye kutoa majibu, mtindo wa kuuliza unaweza pia ukawa wa ufanisi. Mara nyingi, wahubiri wanajibu maswali ambayo hakuna anayeuliza, na kwa hiyo haja yake ni ya chini. Kama mzungumzaji anaweza wazi wazi kuweka dhahiri maswali yanayoendana ambayo yanawasibu wasikilizaji, wanaweza kuhusika zaidi kwenye ujumbe. Kuliko kuwa tu 'wasikilizaji' kutendewa wanaweza kuanza kutarajia na kutafuta majibu ya maswali yaliyotolewa na ujumbe. Wanapogundua majibu kwenye neno kupitia ujumbe, matokeo yanaweza kuwa ya hakika.

### E. Wa Kimzunguko au Kimstari

Ujumbe mwingi wa magharibi ni wa kimistari katika kuendelezwa, na kwa hiyo maana nyingi ya maneno katika kuhubiri inasisitizia vifupisho au kuanzisha mahubiri kiutaratibu. Katika nchi nyingi, kwa jinsi hiyo, aina ya ujumbe wa kimzunguko unaeleweka vizuri zaidi. Ujumbe wa kimstari unashughulika na naama moja, na kuhamia kwa nyingine. Kutoa suluhu kwa kimzungukoo, kwa kutofautisha, kwa kujirudia kunarudi kwenye maana ile ile kutoka katika kona tofauti au namna tofauti ya kuendea. Aina hizi mbili zinaweza kulinganishwa na kuchunguza sana katika nyumba ya kumbukumbu. Kusogea kikuendela kutoka upakaji rangi hadi upakaji ingeweza kuwa njia ya kimstari. Lakini kutembea kuzunguka sanamu ya kuchekesha na kuiangalia katika mitazamo tofauti kadhaa inaweza kuwa njia ya kimzunguko. Aina zote zina thamani, kutegemeana na somo chini ya uangalizi na haja ya wasikilizaji.

## SULUHU

Neno la Mungu ni "hai na lina nguvu" (Ebr 4:12). Mahubiri kibiblia wazi wazi yanawakilisha neno la Mungu kwa namna kwamba nguvu yake itabadirisha wote wanaosikia. Muhubiri ana wajibu mkubwa kuhakikisha kwamba anawakilisha ujumbe wa Mungu na siyo mawazi yeke mwenyewe. Kuelewa neno la Mungu kupitia mafunzo ya kiuangalifu na ya kimaombi ni hatua ya kwanza katika kuandaa mahubiri. Uwe na hakika kuchukua mda wa unaohitajika kujifunza na kuelewa neno la Mungu unapolihubiri.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Fikiria kuhusu mmoja wa wahubiri bora uliowahi kusikia. Nini tabia ya mtindo wa kuhubiri kwao au yaliyomo yaliyofanya kuwa ya ufanisi? Watu waliitikiaje kwenye mahubiri yao?
- Kwa nini mahubiri yatokane na kujifunza Biblia kwa kufata neno?
- Nini kazi ya mahubiri kibiblia? Kuna mifumo tofauti ya kukamilisha kazi hii?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Chagua moja ya kitabu cha injili, na unapokuwa unakisoma, fanya orodha ya vielelezo au somo la kubisha unaloona limetumika.
- Chagua chumba katika kota yako au nyumba na angalia kuzunguka ndani yake kwa vitu ambavyo vinaweza kuwa vya masono ya kitu ya ukweli wa kiroho. Uwe mbunifu. Chunguza hata vitu rahisi vinavyoweza kuelezea kwa nguvu mawazo magumu ya kibiblia.

KUHUBIRI

SOMO LA 2

# Kuhubiri Kibiblia II

## KUELEWA WASIKILIZAJI

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kusisitizia umuhimu wa kuelewa wasikilizaji wanaokusudiwa wakati wa kuandaa ujumbe.

☞ **Wazo Kuu**

- Yesu, Petro na Paulo walirithi ujumbe wao kutoka kwa wasikilizaji.
- Wakati wasikiaji wanapogundua ukweli kwenye maneno wao wenyewe, inakuwa na nguvu zaidi ya kukumbukwa kuliko wanapoambiwa tu.
- Ujumbe mzuri utaonyesha 'msingi wa wote' ambao wahusika wa kibiblia na wasikilizaji wa sasa wanachangia.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa jinsi wahubiri wa Agano Jipya walivyotofautisha ujumbe wao kufuatana na wasikilizaji.
- Kujitolea kusaidia wasikilizaji kugundua maana ya fungu lililohubiriwa kwao.

**UTANGULIZI**

Katika sehemu ya njia za kujifunza Biblia ya zana hii, tumesisitiza umuhimu wa kugundua maana ya maandiko, kuliko tu kusoma fikira zetu na mawazo kutoka humo. Kwa jinsi hiyo, katika hatua ya matumizi, tumekazia kwamba ni muhimu kulinganisha mandhali ya kibiblia ili kuelewa tunachotakiwa kufanya. Wakati njia ya kujifunza kwa kufata inapotumika kwa mafunzo ya binafsi, tunaweza tukadhani kuwa tunajua mandhali yetu. Inapotumika katika kujifunza Biblia katika kikundi kidogo, tunatarajia pia kila mmoja wa washiriki kuwa makini na mandhali yao wenyewe, na kuweza kufanya matumizi yanayofaa kwenye maisha yao wenyewe.

> Mda wa maana katika maandalizi ya ujumbe unatakiwa utolewe kwenye kufikiri kuhusu nani atakuwa anasikiliza ujumbe.

Tunapoanzisha mafunzo ya kufata kwenye mahubiri au ujumbe, tunatakiwa tusidhani kuwa tunaelewa wasikilizaji. Badala mda wa maana katika maandalizi ya ujumbe unatakiwa utolewe kwenye kufikiri kuhusu nani atakuwa anasikiliza ujumbe, na nini mahitaji yao yanaweza kuwa. Kwa kipindi kirefu, hali ya kanisa imara, hili kwa namna fulani ni rahisi, kwa kuwa mchungaji kawaida anajifunza kuhusu watu wake kwa mda. Katika hali ya upandaji kanisa, kunatakiwa kuwe na mfereji wa mawasiliano mapya ya kila mara ya walioalikwa kusikia neno, na kuhusu hao tunaoweza kuwa tunawajua kidogo. Kwenye mkutano wa kundi kubwa wa kiuinjilisti, tunaweza tusijue karibia chochote kuhusu wengi wa wasikilizaji. Inachukua juhudu kufanya utafiti wa mahitaji ya jumla ya mtu yule yule kwenye wasikilizaji wetu wanaokusudiwa, na hata zaidi kujifunza kuhusu mahitaji binafsi ya kila anayehudhuria. Faida yake, kwa hiyo, ni mahubiri au ujumbe wenye ufanisi zaidi.

### I. MAHUBIRI YA AGANO JIPYA

Tunapoangalia kwenye kuhubiri katika Agano Jipya, tunaona kuwa hawakuhubiri tu kitu kile kile kwa kila tukio. Isipokuwa walirekebisha ujumbe wao kulingana na mahitaji na kiwango cha kiroho kwa wasikilizaji.

## A. Mahubiri ya Yesu

Yesu pengine ni mfano bora wa muwakilishaji mjuzi ambaye ulimwengu umewahi kuona kamwe. Yeye, akiwa Mungu, alikuwa na kufahamu kwa undani kwenye mahitaji ya wasikilizaji wake kuliko tunavyoweza kutumaini kuwa nako. Lakini kanuni ya kurekebisha ujumbe kukidhi mahitaji bado inatumika. Fikiria jinsi Yesu alivyosema kitofauti kwa Mafarisayo kuliko kwa wanafunzi wake. Kwa Mafarisayo waliokataa kusikiliza, alitoa maonyo makali ya hukumu (Mt 23). Kwa wanafunzi, ujumbe wake ulikuwa zaidi wa kukaribisha na kutia moyo (Yn 14).

Yesu pia alitoa ujumbe wake katika kiwango cha kueleweka. Kwa mwanamke kisimani, alizungumzia maji (Yn 4). Lakini kwa Nikodemu mfarisayo, alitambulisha maana ya kuzaliwa upya kutoka juu (Yn 3). Katika mathayo 13:10-15, Yesu alielezea kwa wanafunzi wake kwamba amehubiri hasa kwa umati kwa mifano *ili kwamba wasiweze kuelewa* ukweli ambao hawakuwa tayari kutii. Kwa jinsi hiyo, alielezea kikamilifu kila kitu kwa wanafunzi wake (Mk 4:33-34).

## B. Mahubiri ya Petro

Petro alijifunza kutoka kwa muhubiri mtaalamu—Yesu. Pia alikuwa mwangalifu kurekebisha ujumbe kwa wasikilizaji. Ulinganisho mmoja unaweza kuelezea ukweli huu. Fikiria tofauti kwenye mahubiri Petro aliyohubiri kwa umati wa Wayahudi siku ya Pentekosti, na kwa Mataifa huko nyumbani kwa Korneli. Kwa kusanyiko la Wayahudi, alianza mara moja kunukuru manabii wa Agano la Kale Yoeli (Mdo 2:17-21). Wangekuwa walikuwa wanafahamu fungu, na kuthamanisha maandiko ya Agano la kale. Katika mahubiri yake mafupi, aliweza kufanyia kazi nukuru zingine mbili kutoka Zaburi ya Daudi. Wazi wazi, ujumbe huu ulikuwa wa kueleweka kwa Wayahudi, na ulipelekea toba kuu.

Kuzungumzia kwa Petro Mataifa nyumbani kwa Korneli kulikuwa tofauti sana. Hakukuwa na kunukuru kutoka Agano la Kale. Badala yake, Petro alianza kwa maelezo ya jinsi Mungu asivyo wa sehemu, lakini anakubali watu kutoka mataifa yote (Mdo 10:34-35). Hili lingegonga kuitikia kwa pamoja kwa kundi hili lililokuwa limeangaliwa kwa chini na Wayahudi. Wakiwa wameshindia kujaliwa kwao, Kisha Petro mara moja anahamia kwenye huduma na kufa kwa Kristo. Tena, matokeo yalikuwa ya ghafla.

## C. Mahubiri ya Paulo

Mchoro 2.1 Unalinganisha mahubiri ambayo Paulo alitoa kwenye makundi tofauti wakati wa huduma yake ya upandaji kanisa katika kitabu cha Matendo.

**Mchoro 2.1 Mahubiri ya Paulo**

| *Aya* | *Wasikilizaji* | *Utangulizi* | *Ujumbe* |
|---|---|---|---|
| Mdo 13:16-41 | Wayahudi wasioamini Pisidian Antiokia | • Historia ya zamani ya Waisraeli na nukuru za Agano la Kale | • Hitaji la toba<br>• Kristo |
| Mdoa 17:22-31 | Mataifa wasioamini huko Atheni | • Madhabahu yao ya ndani | • Kuwepo wakati wote kwa Mungu<br>• Kufufuka kwa Kristo |
| Mdo 20:18-35 | Wazee wa kanisa la Waefeso huko Mileto | • Maisha ya Paulo miongoni mwao | • Haja ya Paulo ya kuhudumu<br>• Wajibu wao kwenye kundi |
| Mdo 22:1-21 | Mob Myahudi asiyeamini huko Yerusalemu | • Historia ya Paulo kama Mfarisayo na mtesaji wa kanisa | • Kukata shauri kwa Paulo (ushuhuda)<br>• Misheni ya Paulo kwa Mataifa. |
| Mdo 26:2-23 | Mfalme Myahudi asiyeamini herodi Agripa huko Kaisaria | • Shukurani kwa Agripa<br>• Maisha ya Paulo yaliyopita | • Maisha ya Paulo ya nyuma<br>• Kukata shauri kwa Paulo<br>• Msamaha kupitia Kristo |

Mringanisho unagusia ukweli kadhaa.

- Kwanza, tunaona tofauti inayoonekana kati ya ujumbe wa Paulo kwa waumini wanaoamini kutoka Efeso na kwa wengine tu. Paulo aliwazungumzia kuhusu kujitolea na wajibu wao kumtumikia Bwana kwa kuchunga kundi. Kwa makundi mengine, kwa jinsi hiyo, Paulo alikazia kwenye hitaji la toba na kwa Kristo—hii ina maana, kwenye injili.
- Pili, Paulo mara nyingi alitumia ushuhuda wake binafsi kwa aina zote za makundi. Kushirikisha safari yake ya kiroho ilikuwa kipao mbele cha Paulo bila kujali nani alikuwa anazungumza naye.
- Tatu, Pauo alifanya kila juhudi kujilinganisha na kundi fulani na kupata nia zao katika kusikiliza ujumbe wake. Hili lilienda mpaka katika kutumia miungu ya uongo huko Atheni kama kielelezo cha mahubiri.

## II. KUKUSUDIA KWA WASIKILIZAJI WAKO UNAOLENGA

Mara nyingi sana, wahubiri wanatoa ujumbe wao kwa fikira kidogo kwa wasikilizaji wao. Mara ngapi umesikia mtu fulani akihubiri ujumbe wa 'moto wa jehanamu na kibiriti kiwakacho' wa toba ya wokovu kwa kundi la kanisa ambalo si pamoja na asiyeamini mmoja anayejulikana? Kwa kuzidi upande mwingine, wahubiri mara nyingi wanatumia mda mwingi sana wakihubiri ujumbe juu ya maadili ya kikristo na kuishi kwa wasioamini wasio tayari kwa chochote isipokuwa injili.

> Mara nyingi sana, wahubiri wanatoa ujumbe wao kwa fikira kidogo kwa wasikilizaji wao.

Katika kuhubiri kwetu kunafanana sana na kwa Agano Jipya, Tuanahitaji kukazania kwenye tabia za wasikilizaji, na kutoa ujumbe ambao unaendana nao na wa kueleweka. Kuna tabia nyingi ambazo tunatakiwa kufikiria.

### A. Tabia Muhimu za Wasikilizaji

Tabia ya wasikilizaji ambayo inaweza kuwa muhimu inatofautiana sana kutoka kundi hadi kundi. Orodha hapo chini ni sehemu tu. Mda na uzoefu utakusaidia kujua swali gani la kuuliza.


- Umri – Watu wazee na vijana wanaangalia maisha kitofauti, na kupenda kusikiliza aina tofauti za ujumbe. Ni muhimu kurekebisha yote yaliyomo na kutoa ujumbe kufuatana.
- Hatua ya kiroho – watu wanahitaji kuwa na yaliyomo ambayo yanaoana na ngazi yao ya ukomavu kiroho, na kuwasaidia kusogea kwenye ngazi ya juu. Tunatakiwa tusipoteze ukweli wa kutatanisha kwa wasioamini (Mt 7:6). Wala kuwalemeza na ukweli kwa hao ambao wanaweza wakawa wanakua (Ebr 6:1-3).
- Elimu—ni muhimu kutokuongea kwa tabia ya utata sana au kirahisi sana. Mara nyingi, ngazi ya kieleimu ya wasikilizaji inatupa wazo la ngazi halisi.
- Mapendeleo– kama unataka kupata usikivu wa kundi, zungumzia vitu ambavyo wanavipendelea. Hili linawezekana tu unapokuwa unajua nini wanapendelea.
- Habari za nyuma za kikabila—watu wa habari za nyuma za kikabila wanaona vitu kupitia macho ya mtazamo wa ulimwengu wao, ambao unaweza ukawa unatofautiana kutoka kwa ule wa mzungumzaji. Ni muhimu kujua tofauti hizo ni nini.
- Habari za nyumba za kidini—mapokeo ya kidini yanakwenda kwa ndani zaidi, na hatuwezi kuyadharau. Kitu fulani kinachomaanisha kitu kimoja kwetu kinaweza kuchukuliwa kwa jumla kwa njia tofauti kwa mtu anayeangalia kupitia muunganiko wa dini nyingine.
- Nafasi ya Familia—watu mabachera, waliooana, walioachika au wajane na akina bibi wana mahitaji tofauti yanayoendana na hali za familia zao. Tunahitaji kuwa na hakika ujumbe wetu unatimiza mahitaji hayo.
- Ajira—profesa au nafasi ya kazi pia inagusa mahitaji yetu na mapendeleo yetu.
- Jinsia – Wanaume na wanawake wanaangalia kitu sawa kwa njia tofauti. Nani walioko katika wasikilizaji wako?

### B. Nini Mahitaji ya Wasikilizaji Wako

Inaweza ikawa hatari kuweka kwa jumla, lakini tunaweza kupata baadhi ya kuelewa tunaporejea nyuma kwenye mfano wa mahubiri ya mtume Paulo. Alihubiri injili kwa wasioamini, lakini akiitolea kwa wanaoamini. Hili linaonekana rahisi, lakini mara nyingi linaangaliwa kimakosa. Baadhi ya ukweli wa kiroho ni mugumu kuelewa kuliko mwingine. Mtu asiyeokoka anaweza kuelewa tu injili Roho Mtakatifu anapomthibitishia. “Nyama” ya maandiko inakuwa imepotezwa kwake. Kwa njia sawa, waumini wengi mara nyingi sana wanalishwa mlo wa kawaida wa “maziwa” na kwa hiyo kubakia dhaifu na kutoandaliwa kwa ajili ya huduma. Kielelezo 2.2 kinaeleleza ukweli kwamba kila kundi linahitaji mlo “sawasawa” wa neno ambalo ni haki kwao.

Kutoka katika kielelezo , ni wazi kwamba injili ni kwa wasioamini, na ukweli kuhusu kujitolea na kuishi kikristo ni waumini waliokomaa. Wakati wasikilizaji wanapokuwa wamechanganyika, ujumbe pia unatakiwa uendane na upana huo.

**Kielelezo 2.2 Mlo Unaofaa**




Inaweza pia ikatambulika kuwa wakati mtu anapomtumaini Kristo, mara moja au ghafla hayuko tayari kwenye ukweli mgumu wa kiroho. Kuna kipindi cha kawaida cha ukuaji kwa muumini mpya wanapoendelea kuhitaji injili kuingizwa na kuelezewa, lakini wanapojifunza na kukua, wanatakiwa waweke ‘nyama’ zaidi na ‘maziwa’ kidogo kwenye mlo. Kwa hiyo, unapopanga ujumbe wako, utahitaji pia kufikiria siyo tu uwiano wa waumini kwa wasiowaumini, lakini pia wasikilizaji wako karibu na kwenye hatua ya ‘nyama’ au maziwa’.

## III. KUSAIDIA WASIKILIZAJI KUGUNDUA

> Wasikilizaji wa lazima waingiliane na maandiko wao wenyewe.

Haijarishi wapi katika kipimo cha ukuaji wasikilizaji wako wanaweza wakawa, mahubiri yako yatakuwa yenye nguvu zaidi ya kukumbukwa kama yanafungua neno kwao na kuwafanya kugundua ukweli ndani yake. Haitoshi kwao kwa kifupi kujifunza tu kutoka *kwako,* au kusikiliza vitu *unavyosema.* Lazima waingiliane na maandiko wao wenyewe. Kwa njia hii, mahubiri kibiblia yanafanana na msisitizo juu ya kugundua tulikoona tulipojifunza njia ya kujifunza Biblia kwa kufata neno.

Fikiria mtu fulani anakutumia barua, na unakwenda posta kuipokea. Kwa jinsi hiyo, badala ya kukupa barua ya kusoma, karani wa posta anaifungua, na kuisoma kimya kimya, na kisha kukuambia kwa wastani ilichosema. Utaridhika? Hutasikia haja ya kuisoma wewe mwenyewe? Hili hasa ndilo wahubiri wanalofanya. Wanasoma neno kisiri, na kisha kusimama na kulifupisha kwa ajili ya wengine kwa kile wanachokumbuka kutokana nalo. Inatosha sana wakati muhubiri

anapofungua Biblia kwa ajili yetu, na kutuongoza kwenye kujifunza kwetu wenyewe kwa ukweli uliomo ndani yake.

> Muhubiri anatakiwa awasaidie kujenga daraja kati ya wasikilizaji na neno ili kwamba waweze kuligundua.

Kwa nini tujisumbue kuhubiri? Kwa nini tu tusiwape Biblia na kuwaacha waisome? Kwa sababu vitu vingi katika Biblia ni vigumu kuelewa. (Hata Petro aliona hivyo katika 2Pet 3:15-16.). Mtu fulani anahitaji kusaidia kuelezea maswala yenye utata, na kuonyesha jinsi ya kutumia ukweli kwenye maisha yao. Mahubiri ya kibiblia yanaweza kusaidia kuelezea kufanana kati ya mandhali ya kibiblia na mandhali ya sasa ya wasikilizaji. Inahitaji ujuzi na kuwa tayari kujua lini tunahitaji kuwasaidia kugundua, bila kuwa kigingi kati yao na Biblia. Kukamilisha hili kunahitaji kwamba tunachukua mda kuweza kujua wasikilizaji vyema, na kurekebisha ujumbe wetu kukidhi mahitaji yao.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Jinsi gani unafikiri Paulo alivyolichukulia swala la miungu katika kifungu cha Matendo 17? Jinsi gani ungekuwa umetoa ujumbe huo katika hali inayofanana?
- Ni njia ipi ni bora ‘kuwianisha mlo’ kwenye ujumbe kwa ajili ya kundi mchanganyiko?
- Vitu gani unafikiri ni ‘nyama’ na vitu gani ni ‘maziwa’?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Soma nyuma kwenye orodha za tabia kwenye sehemu ya 11. A. kisha tathimini kundi unalohudumu. Andika maelezo mafupi kufupisha kila maana kadiri inavyohusiana na kundi lako. Kuna tabia nyingine muhimu unayohitaji kuongeza kwenye orodha kuweza kueleza vya kutosha wasikilizaji wako? Nini unachohitaji bado kuendelea kujifunza kuhusu wao ili kuhubiri kwa namna ambayo inakidhi mahitaji yao?
- Inayofata, tathimini moja ya ujumbe ambao umehubiri hivi karibuni, au ulioandaa kuhubiri hivi karibuni. Unaendana na kundi hili? Kwa nini na kwa nini siyo? Jinsi gani unaweza kuurekebisha kuufanya kuendana zaidi, wa kuvutia na kutumika?

KUHUBIRI

SOMO LA 3

# Kuhubiri Kibiblia III

## KUJIELEWA MWENYEWE

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kumsaidia mfunzwa kuongeza utayarishaji wake na utoaji ili kukuza ufanisi wa ujumbe.

☞ **Wazo Kuu**

- Maisha, ushuhuda, na mtindo wa muhubiri unaweza kukuza utoaji sehemu kutoka kwenye mahubiri.
- Sauti, utabia, na umaridadi unaweza kudhibitiwa na kurekebishwa kupitia juhudi na matendo.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa hitaji la binafsi kujiandaa kiroho kwa ajili ya kuhubiri.
- Kuweza kutawala vyema sauti yake na utabia wakati wa kuhubiri.
- Kuwa na ufahamu wa ufundi zaidi wa usomaji wa ufanisi wa neno.

**UTANGULIZI**

Tumejadili ukweli kwamba kuelewa kwa muundo wa ujumbe na kuelewa kwa wasikilizaji ni ufunguo kwenye mahubiri ya kibiblia yenye ufanisi. Kigezo cha tatu ni msemaji. Kielelezo 3.1 kinaeleleza jinsi maneno ya msemaji yanavyoweza ama kusaidia kuainisha na kuelezea ujumbe wa neno kwa wasikiaji, au kuukatisha.

Muongeaji anaathiri upokeaji wetu wa ujumbe angalau katika hatua mbili. Ya kwanza, kila mara mtu anapoongea kwetu kwenye somo lolote, bila kuelewa tunachuja maneno yao kupitia maoni yetu kwa mtu huyo. Kama tunamdhania mtu huyo kuwa wa kutegemewa, mwenye akili sana, wa kuaminiwa, n.k., wanayosema yatakubalika zaidi kwetu. Kama, kwa upande mwingine, hatuwaamini au kutompenda msemaji, tutafanya kudharau au kutojali thamani ya ujumbe. Hilo linatoke kwenye ujumbe pia.

> Tunachoona kinaweza kutangua kile tunachosikia.

Kuna njia ya pili ambayo mzungumzaji anaathiri ujumbe. Hata kama ni mtu amabye tunampenda na kumuamini anapoongea, tunaweza tusipate yaliyomo katika ujumbe kama anafanya kitu fulani kinachokatisha, au kama 'lugha yake ya mwili' inapingana na anachosema. Pengine anatuambia kuhusu kitu fulani ambacho kilitokea, lakini anaonekana kukatishwa. Kiasili tutashangazwa nini hasa wanachofikiria kuhusu kuliko kukazania juu ya wanachosema. Pengine tunagundua mdudu anayetambaa kwenye kola ya shati lao, na kabisa kukosa kile wanachosema. *Tunachoona* kinaweza kutangua kile *tunachosikia*. Tena, hilo pia ni sawa katika kuhubiri.

Katika somo hili, tutajadili maeneo kadhaa muhimu ambayo yanamsumbua msemaji. Pengine maswala ni hali ya kiroho ya mzungumzaji, hali ya kihisia, na muonekano kimwili. Tutaangalia katika kila moja ya haya katika kurudia.

### I. MASWALA YA KIROHO

Kuhubiri ni shughuli ya kiroho. Tunamtegemea Roho Mtakatifu kuchukua maneno tunayosema na kuyatumia kwenye mioyo ya wasikilizaji. Ili kwetu tuwe na ujasiri kwamba hili litatokea, tunahitaji kuangalia kwa karibu maisha yetu ya kiroho.

**A. Kuwa Mwenyewe**


Watu wanaweza mara nyingi kwa haraka kuweka doa la 'kuigiza.' Na hata hivyo, hata wahubiri wenye kumaanisa sana mara nyingi wana 'kubadilika kwa hadhi zao' wanaposimama mbele za wengine kuongea au kuhubiri. Sauti zao na matamushi yanaweza kubadilika kighafla. Katika hali mbaya zaidi, wanaweza kuchukua kwa namna fulani 'utakatifu hewa' ambao unatarajiwa kuwashawishi wengine kwamba wanatakiwa wasikilize, lakini una madhara tofauti kama siyo kuafakali kwa kweli kwa maisha ya kiroho ya msemaji.

> Mungu ameumba kila mmoja wetu kwa namna ya pekee ili kwamba tuweze kumtumikia kama anavyopenda.

Katika hali halisi, Mungu ameumba kila mmoja wetu kwa namna ya pekee ili kwamba tuweze kumtumikia kama anavyopenda. Huu ulikuwa ukweli mgumu kwa Musa. Katika Kutoka 4:10-12, alielezea jinsi kuongea kwake taratibu kulivyorudisha nyuma ujumbe kwa Waisraeli utumwani Misri. Mungu alimkemea Musa. Alikuwa amemuumba Musa sawasawa na jinsi alivyotaka awe—ikiwemo kusema taratibu. Tunapofikiria kwamba tunataka kuwa kama mtu fulani tu, au kutenda kitofauti kuliko Bwana alivyotuumba ili kuwakilisha ujumbe wake, tunamfanyia kitendo cha dharau isiyo ya mzaha.

Hili, kweli, halimaanishi kwamba hatutakiwi kuongeza ujuzi wetu wa kuongea au kukua katika uhusiano na Bwana. Tunapaswa. Tunachosema ni kwamba tunapoendelea kukua, tunatakiwa tusijifanye kana kwamba tuko mbali njiani kuliko tulivyo. Ni muhimu kwamba wasikilizaji kuona kwamba tu wenye dhambi, tuliookolewa kwa neema, kama ilivyo. Tunatakiwa kuwa vielelezo vya ukuaji kiroho, siyo ukamilifu.

**Kielelezo 3.1 Kusaidia au Kurudisha Nyuma Ujumbe**




**B. Weka Usikivu Kwenye Kutembea kwako na Bwana**

Paulo alimshauri Timotheo kwamba ukuaji wake mwenyewe na kutembea kungeweza kuathiri huduma yake (1Tim 4:16), na ingeweza kuonekana kuwa kanuni ya kisheria kwa kila mmoja anayetamani kuhubiri neno la Mungu. Moja ya changamoto za ajabu kwenye Agano Jipya inapatikana katika Matendo 4:13. katika kurasa hizo, Petro na Yohana wanasimama mbele ya mwenye cheo kikubwa na mwenye mamlaka ya elimu za kidini zaidi katika siku zao. Bila kujali ukweli kwamba walikuwa wavuvi wasio na elimu, walionyesha ujasiri kwenye ujumbe wao. Kwa nini? Kwa sababu walikuwa wametumia mda pamoja na Yesu. Hata wajumbe wasioamini wa Sanhendrini walitambua ukweli huu.

Nia ya fungu hili siyo kuzunguzmzia kinyume cha elimu na mafunzo. Mtume Paulo pia alitumiwa na Mungu kiajabu, na alikuwa na mafunzo ya kidini ya juu iwezekanavyo. Isipokuwa, maana ya ujumbe ni kwamba *hata wasio na elimu* wanaweza kutumiwa kinguvu kama wana kutembea kiroho kunakotikisika. Haijalishi kiasi gani ulivyokuwa kabla na mafunzo uliyonayo. Mungu anaweza kukutumia katika kiwango chochote kama unakazania kukaa karibu naye. Hiki ni kigezo muhimu zaidi katika kuhubiri kwa kweli kibiblia.

## II. MASWALA YA KIHISIA

> Wahubiri, au wasemaji mashuhuri, wanapata shida katika moja ya mbili za kuupindukia kihisia.

Wahubiri, au wasemaji mashuhuri, wanapata shida katika moja ya mbili za kupindukia kihisia. Wengine wanafikiri kwamba hawataweza kufanya kazi nzuri, na wanatawaliwa na hofu. Hili linaweza kuwa na bila mzaha sana kiasi kwamba wanaweza kukataa kuongea, hata wanapokuwa na vitu muhimu vya kusema. Hali nyingine ya kupindukia ni kuwa na hakika sana kwa uwezo wetu ambapo tunaangukia katika kiburi.

### A. Hofu ya Kuzungumza Hadharani

Baadhi ya hofu ni nzuri. Ni hisia za kawaida Mungu alizotupa kwa kusudi. Kiasi kinachofaa cha hofu kinaweza kuwa:

- kunoa kuhisi kwetu
- kutuchochea kufanya tuwezavyo
- kutufanya kutambua utegemezi wetu kwa Mungu

Hata wahubiri wenye uzoefu mara nyingi wanajisikia “kutambaliwa” matumboni mwao, au badhi yao kutokuwa na hakika kabla hawajaongea. Kumuwakilisha Mfalme wa Wafalme ni kazi ya ajabu, ambayo hakuna mmoja wetu anayeistahili. Tunapokumbuka ukweli huu, inatusaidia kuepuka kiburi au kutegemea uwezo wetu wenyewe.

#### 1. *Kinachosababisha hofu*

Kuna vingi vinavyosababisha hofu. Vya kawaida vingi ni kama ifuatavyo:

- Hofu ya kushindwa. Mara nyingi tunaogopa kwamba tutafanya kitu ambacho ni bubu, na watu watatucheka.
- Hofu ya yasiyojulikana. Tunakwenda kuongea kwenye idadi ya watu na hatujawahi kufanya hivyo kabla.
- Hofu ya kukataliwa. Watanikubali?
- Hofu ya chuki. Jinsi gani watafanya kwa kile ninachokwenda kusema?
- Hofu ya kushindwa. Hili linaweza kutokea wakati tunapokuwa hatukujiandaa sawasawa.

#### 2. *Kutawala Hofu*

Kuna idadi ya vitu tunavyoweza kufanya kusaidia kudhibiti au kushinda kiasi cha hofu zisizo nzuri.

- Mpe ujumbe Mungu, ambaye yuko pamoja nawe na anakujari.
- Fanya kila kitu kwa ajili ya Bwana. Tunataka kukubaliwa naye, kuliko tu huko kwa watu wengine.
- Kumbuka kwamba ujumbe wako ni muhimu sana, ni neno la Mungu. Kazania katika ujumbe wako na kiasi gani wasikiaji wanahitaji ujumbe.
- Fanya mafunzo yako vema; jua ujumbe unaokwenda kutoa.

*3. Kutawala mkazo Unaotokana na Hofu*

Kuna mazoezi machache ya kimwili ambayo unaweza kufanya kila mara unapojiandaa kuongea ambayo yatasaidia kupunguza mkazo wowote unaohusiana na hofu unayoweza kujisikia.

- Kabla ya kuamka kuzungumza, jinyooshe. Jiweke katika hali ya kustarehe na kazania katika kuruhusu mishipa ya shingo lako, mgongo, miguu na mikono kupumzika.
- Tawala kupumua kwako. Kabla ya kuongea, vuta pumzi sana kujaza mapafu yako kwa hewa safi. Fanya hivi mara kadhaa. Wakati wa mahubiri, tulia mara kwa mara, jipe mwenyewe kuvuta pumzi. Usiongee haraka haraka.

**B. Kiburi**

Kinyume cha hofu ni kiburi. Kiburi ni tabia ya kawaida ya dhambi—hasa miongoni mwa hao wanahusika katika huduma za hadharani na kuzungumza. Paulo anamuonya Timotheo kwamba wakristo wachanga wanaweza kirahisi kuangukia katika mtego huu kama tunawatukuza wao kwenye nafsi za juu sana kwa haraka zaidi (1Tim 3:6). Kwa jinsi hiyo, karibu mkristo yeyote anaweza kutoa mifano ya viongozi wakristo wengi wenye uzoefu waliokutana na kushindwa kwa namna hiyo.

> Ukuaji wa kiroho wa kweli unakuja tu kupitia huduma ya Roho Mtakatifu katika moyo wa msikilizaji.

Hao wanaoruhusu wenyewe kutawaliwa na kiburi wanasahau kuwa ukuaji wa kiroho wa kweli unakuja tu kupitia huduma ya Roho Mtakatifu katika moyo wa msikilizaji. Msemaji mwenye uwezo, anayejigamba anaweza akawa wa kuchekesha, kukupendezesha au wa kufurahiwa kumusikiliza. Watu wanaweza kufurika kumsikiliza akiongea. Kwa jinsi hiyo, hana uwezo wa kusababisha ukuaji wa kweli wa kiroho. Kama ambavyo ufalme wa Mungu unahitaji, mahubiri yao au ujumbe ni upotezaji wa mda kwa kiwango bora, na dhambi kwa kiwango kibaya.

## III. MASWALA YA KIMWILI

Ingawa kuhubiri ni shughuli ya kiroho, ujuzi wa kuongea vizuri kwenye uma kunaweza kufanya ujumbe kusikilizwa. Kuongea hadharani ni ujuzi uliosomewa. Baadhi ya watu wana vipaji vya asili vya kuongea hadharani, lakini kwa kujifunza baadhi ya ufundi wa kusaidia, mtu yeyote anaweza kuwa mzungumzaji mwenye ufanisi wa hadharani. Ni kutangaza neno la Mungu kihadharani kwa wengine. Ni muhimu kwamba utabia wa muhubiri au kutawala sauti kusikatishe usikivu wa watu kutoka kwenye ujumbe.

Kuna idadi ya ufundi wa kuongea hadharani ambao unasaidia kwa muhubiri. Kwa kuweka usaidizi huu, na kupitia maandalizi thabiti na mazoezi, unaweza kuhubiri kiufanisi ili kwamba watu wako wakue katika kuelewa neno la Mungu na katika utii na kuimarisha uhusiano na Mungu.

**A. Kutawala Sauti**

Msemaji itakuwa rahisi kumsikiliza kama anajua jinsi ya kuwala sauti yake na kuirithisha kwenye kusikiwa kwenye chumba anachoongelea.

*1. Tabia za Sauti*

a. Uzito

- Badirisha uzito wa sauti yako kufata hisia na maana ya ujumbe wako.

b. Kusikika kwa Sauti

- Chagua kusikika ambako ama siyo kugumu au dhaifu.
- Ni vizuri sana kurekodi sauti yako kwenye kanda na kuisikiliza. Unaweza kubadilisha sauti yako kuifanya kuwa na kuendana kwa kusikika kwake.
- Usisemee katika kusikika kumoja kusikobadilika kwa sauti yako.

c. Matamshi

- Unapoongea hadharani, unatakiwa ufungue mdomo wako kwa upana kutamka maneno vizuri.

d. Wepesi na Haraka

- Unatakiwa usiongee ama haraka sana wala taratibu sana.
- Woga mara nyingi unatupelekea kusema kiharaka. Fanya mazoezi ya kutoa ujumbe katika ukimya wa chumba chako na fanyia kazi utoaji wa haraka.
- Wepesi wako au haraka lazima uweze kurithi wasilizaji wako. Lazima waweze kukufata na kukuelewa bila ugumu.
- Tumia kutulia kiubunifu, kama ambavyo ungefanya katika mazungumzo ya kawaida.

*2. Rithisha Sauti Yako Kwenye Kusikika kwenye Chumba*

Ili kuhakikisha kwamba kila mmoja kwenye chumba anaweza kukusikia, unatakiwa kusema mpaka kwa mtu wa mwisho kwenye chumba. Hili kiutendaji ni muhimu kama huna utaratibu wa kuzungumzia hadharani. Kama kusikika katika chumba ni hafifu, unaweza ukarekebisha kufuatana nako kwa njia zifuatazo:

- Zungumza taratibu zaidi
- Tengeneza mafungu mafupi na kutulia kati kati yake.
- Tamka maneno yako kiuangalifu.
- Tofautisha kusika kwa sauti.
- Sindikiza maneno yako kwa kujongea zaidi kwa mwili
- Tumia kusikika kudogo kwa sauti.

## B. Muonekano

Muonekano wa nje wa msemaji ni muhimu pia. Unapoongea, unatakiwa kufikiria maeneo yafuatayo.

*1. Umaridadi*

Muonekano wa kwanza ni muhimu. Hutakiwi kuvaa kupitiliza au kwa kiwango cha chini. Hutakiwi kujiwekea usikivu kwako mwenyewe, lakini kwa mungu. Kwa hiyo, vaa katika namna ambayo inafaa kwa ajili ya kundi ambalo unahudumia.

*2. Mkao*

Wasikilizaji wanatuona kabla ya kutusikiliza. Namna ambayo tunatembea kuelekea mimbarini tayari inawakilisha kitu fulani kwa wasikilizaji. Unapotembea kwenda kwenye mimbari, unatakiwa kuwafanya watu kujua kuwa una ujumbe kutoka kwa Mungu. Ni ujumbe muhimu. Kwa hiyo, simamisha kichwa chako, na mwili wako kwa adabu.

Unapokuwa mbele ya kundi, weka mikono yako nje ya mifuko, na usiegemee kwenye ukingo pamoja nao. Weka mikono yako kuwa huru kwa ajili ya kutoa ishara kwa kawaida unapowakilisha. Epuka mikao ifuatayo:

- Kijeshi - Mwili unanyooka na bila kupinda na mikono ikiwa imewekwa nyuma. Hii inapitisha ugumu na mkazo.
- Ulegevu – Epuka kuweka uzito wako wote kwenye mguu mmoja na mabega yako yakilegea juu yake. Hili linawakilisha uvivu na kukosa haja.
- Kikuhani – Kwa nafasi hii, tunajaribu kuonekana watakatifu kupita. Kunyooka bila kupinda na mikono yetu ikiwekwa katika mkao wa kuomba.
- Simba – hapa muhubiri anahama kutoka upande mmoja hadi mwingine kwenye mimbari kama simba navyofanya kwenye zizi lake.

Ruhusu mkao wako kujirekebisha wenyewe kwenye hisia ya ujumbe. Unaongea kwa wasikilizaji kwa sauti yako na mwili wako. Ruhusu mwili wako kubadilika kiasili na sauti yako. Mwili wako na sauti kisha vitafanya kazi pamoja katika mawasiliano, kuliko tu kinyume na kila kimoja

3. *Ishara*

Unapokuwa unazungumza kwa marafiki, unatumia ishara na kichwa chako, na mabega yako, na mikono yako, na miguu yako na uso wako. Mwili wako wote unatumika. Unapotoa mahubiri, unatakiwa kuwa kawaida kama unavyokuwa unapokuwa unaongea na marafiki zako.

- Ishara inatakiwa iwe kweli na ya kawaida. Inatakiwa isindikize ujumbe kama ambavyo ingesindikiza mazunguzo na rafiki.
- Siyo lazima kutabasamu kila wakati. Kwa hakika, hiyo inaweza kuwa lazima, kwa sababu baadhi ya ujumbe wako unaweza kuwa kuhusu juu ya kutubu. Muonekano wa uso wako unatakiwa uendane na hisia za kawaida za ujumbe wako.
- Unapokuwa unatoa kielelezo kuhusu maisha ya mtu binafsi, au kitu fulani ambacho mtu binafsi amesema, inafaa kuigiza kusikika kwa sauti, ishara, na kuonekana kwa uso kwa mtu binafsi ambaye unamwigiza. Kwa maneno mengine, inafaa kuigiza visa kutoka kwenye Biblia au maisha ya kila siku.
- Tunza mawasiliano ya macho na wasikilizaji. Unataka wajue kuwa unapendezwa nao binafsi. Unaweza kufanya hilo vyema kwa kutunza mawasiliano ya macho nao. Unataka kujua kama wanaitikia kwenye ujumbe wako. Unajua hilo kutokana na kusoma macho yao tu.

**C. Usomaji Kiufafanuzi**

Kabla ya kusoma kifungu cha kibiblia kwa wasikilizaji, unahitaji kuelewa mafunzo kuhusu ujumbe huo. Unatakiwa uelewe kwanza nini mwandishi anajaribu kuwakilisha, ili kwamba uweze kuwa chombo cha Mungu katika kumwakilisha kiufanisi.

- Soma fungu kwa uangalifu, angalau mara tatu.
- Tambua matamushi.
- Soma maneno. Kama kuna maneno yoyote ambayo huyajui, yaangalie kwenye kamusi.
- Tambua kisa cha fungu vile vile na mafundisho yake. Pia tambua jinsi kisa hicho kilivyoendelezwa.
- Tambua kusudi alilokuwa nalo ndani mwandishi ikiwemo kifungu hiki katika masimulizi ya kibiblia. Ili kufanya hivyo, ni muhimu kuangalia katika mandhali.
- Kama kuna watu wametajwa kwenye kifungu, tambua tabia zao.
- Kama fungu ni masimulizi ya kibiblia, fuatisha katika kusoma kwako maendeleo ya masimulizi kutoka kwenye utangulizi wake, kipeo, na suluhu. Jaribu kukamata hisia za masimulizi katika sauti yako mwenyewe kama ilivyoendelezwa.

Unasoma neno la Mungu, Kwa hiyo lisome kwa mvuto na shauku.

**MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Fikiria muhubiri mfanisi unayemjua. Nini kilikuwa katika mtindo wake wa kuongea ambacho kinamfanya kuwa mfanisi? Elezea matumizi ya sauti yake na lugha ya mwili.
- Ni mawazo yapi mawili ya msaada yaliyopatikana kutoka kaika somo hili ambayo yatakuza ufanisi wako mwenyewe wa kuhubiri?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Uwe na rafiki atumie kanda ya kurekodia (au video ya kamera, kama una moja) kukurekodi unapotoa ujumbe. Kisha unapokuwa unarudia kanda, tathimini matumizi yako ya sauti kufuatana na kubadilika badilika kulikotolewa katika somo hili. Kama unatumia video, jifunze muonekano wako na lugha ya mwili vile vile. Kama una kanda tu muombe rafiki yako anayerekodi aangalie vitu hivi na kukutathimini.

# FAMILIA

FAMILIA

SOMO LA 3

# Huduma kwa Familia

## WARSHA

☞ **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kutoa nafasi ya majadiliano wazi na ya kweli ya maswala amabyo yanaweza yakawa na mguso kwa mpanda kanisa na uwiano kati ya huduma na familia.

☞ **Wazo Kuu**

- Lazima kuwe na uwiano wa mda unaotumiwa katika huduma kwa familia na huduma kwa kanisa.
- Katika maisha na huduma ya mpanda kanisa, matatizo yataibuka ambayo yanahusiana moja kwa moja kwa mwenzi na watoto. Matatizo haya lazima yatambulike, kujadiliwa kiuwazi, na kujitolea lazima kufanyike sehemu ya mpanda kanisa kuyatatua kimaombi.

☞ **Matokeo Yanayotarajiwa**

Matokeo ya warsha hii, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa kuwa kama mpanda kanisa, uwiano na umoja katika uhusiano wa kijinsia vile vile na nyumbani ni sura ya kimsingi kwenye huduma yenye afya.
- Fanya mazoezi ya kujitoa kwenye kuelewa wajumbe wa familia ya mtu na jinsi maisha yao yanavyogushwa na kuwa na mguso kwenye huduma ya mpanda kanisa. Kazana kupata uwiano na umoja katika familia na ndoa.

☞ **Ushauri kwa Wakufunzi**

Mifano iliyotolewa hapa inatumika mara chache kusisimua majadiliano juu ya hitaji la kutafuta uwiano kati ya huduma ya mpanda kanisa na ndoa na familia. Tafadhali jisikie huru kutumia mifano yako mwenyewe na maswali ya majadiliano lakini hakikisha majadiliano yako yanagusia kwenye maswala kama vile uongozi wa kitumishi, utatuzi wa migogoro, kufanya majadiliano sahihi nyumbani, njia zinazofaa za kuonyesha upendo kwa mwenzi wa mtu, kukubali udhaifu wa mwenzi wako na uwezo, n.k. Kiuangalifu jiandae kwa ajili ya kipindi hiki kwa kusoma muonekano wa mambo na kisha anzisha mda wa somo lako kufuatana na maswala ambayo yanasumbua wafunzwa wako. Mfuatano wa mambo na maswali yaliyotolewa yanaweza au yasiweze kutosha kukidhi mahitaji ya mandhali yako maalumu. Katika hali hii, jisikie huru kuanzisha mifano yako mwenyewe na maswali.

### UTANGULIZI

Mara nyingi swali linaulizwa, “Nini cha kwanza, familia au huduma?” Jibu ni ama. Mungu anakuja wa kwanza. Kwa sababu tunampenda, tunamtumikia. Ametupatia kazi fulani za kufanya, ambazo zote ni sehemu ya huduma yetu kwake. Kujaribu na kutenga familia na huduma ni kama kujaribu kutenganisha maisha yetu ya kiroho kutoka kwenye huduma zetu. Haiwezekani, kwa sababu yanaingiliana. Familia zetu ni sehemu ya huduma zetu.

Ufunguo wa huduma yenye ufanisi katika kupanda kanisa na katika familia ni <u>uwiano</u>. Baadhi ya wapanda kanisa na wachungaji wanachukulia kujitolea kwao kwenye huduma katika kanisa kwa kupindukia, na kiufanisi wanadharau familia zao. Hili moja kwa moja linapingana na amri katika Biblia kwa baba kuelekeza na kutoa malezi kwa watoto wake (Kum 6:7, Mit 22:6). Jinsi gani baba atafanya haya kama kamwe haoni watoto wake au kutumia mda pamoja nao? Fikiria Eli kuhani, ambaye watoto wake wa kiume walikuwa wamelogwa Mungu akawaacha wakafa (1 Sa 2:34). Mungu

ametupa wajibu wa kulea watoto wetu kwa sababu anajua kuwa wao wenyewe, hawataweza kufanya maamzi sahihi.

Baadhi ya wapanda kanisa wanachukua kupindukia kwingine—wanazingwa na familia zao kupindukia, kwa kiasi kwamba hawatimizi wito wa Mungu aliowapa kama wachungaji/au wapanda kanisa. Inaweza ikawa rahisi kwa familia kuwa kitu fulani kinachochukua mda wetu wa sala mbali kutoka kwa Mungu. Yesu alionya katika Mathayo 10"37 kwamba yeyote anayeipenda familia yake zaidi kuliko Kristo hamfai.

Sifa za wote waangalizi na mashemasi katika 1 Timotheo 3 zinahitaji zaidi mtazamo wa uwiano—kiongozi katika kanisa anatakiwa awe mtu mwenye mke mmoja, anayedhibiti watoto wake na nyumba yake vyema. Kama tu watu binafsi wanaoshindwa maadili wanajiondoa wenyewe kutoka kwenye huduma. Kila mpanda kanisa aliyeoa lazima akazane kutunza uwiano wa kufaa kati ya mda anaotumia na mke wake na watoto, na mda anaotumia katika kanisa. Zote ni huduma, na zote ni wito wake.

**MIPAKA KWENYE WARSHA HII**

Mambo yafuatayo yanajadili hali na matatizo ambayo ni ya kawaida miongoni mwa wapanda kanisa. Unapofanyia kazi angalia kufanana katika maisha yako na huduma.

- Gawanyika katika makundi mdogo mwanzoni mwa mda wa somo. Kila kundi linatakiwa lishughurikie muonekano mmoja.
- Pata kanuni za kibiblia ambazo zingeweza kuwa zimetumika kwenye hali.
- Mwishoni mwa mda wa mda wa kikundi kidogo, kila mmoja wenu akusanyike kama kundi kubwa na kila kundi litoe yale liliyopata.

*Nakala kwa mkalimani: Tafadhali badilisha majina katika mchanganuo wa ufuatao kwa hayo yaliyo ya kawaida katika lugha yako.*

## I. MUONEKANO NAMBA MOJA—IGOR NA LUBA

Akiwa ametikiswa na kuyumba yumba kwa treni, Igor alipumzika chini kwa kukaribisha usingizi wa usiku. Wakati zimekuwa siku tano za kazi nyingi wakati wa semini ya mafunzo, alikuwa ametiwa moyo na kile alichokuwa amejifunza na ushirika wa wengine walio na haja sawa naye: kuanzisha makanisa mapya. Kumekuwa na umoja wakati wa semina. Kila mmoja alielewa mahangaiko yake na kusumbuliwa kwa kuwa wote walikuwa katika hatua ya awali ya kuanzisha makanisa. Mda wao wa maombi ulikuwa wa kiibada na kuwezeshwa.

Igor alipochukuliwa na usingizi, akinuia kuendelea kwa huduma yake ya upandaji kanisa, alijisikia amani safi na hisia zilizorejezwa za kuwepo kwa nguvu ya Mungu katika maisha yake. Asingesubiri mawazo yake mapya na timu yake ya upandaji kanisa na kuanza kuyaweka katika huduma yake.

Luba, karibia katika mda sawa ambao Igor alikuwa amechukuliwa na usingizi, alikuwa kati kati ya msiba mkuu wa familia nyingi tangu kuondoka kwa Igor. Alipowafungia yeye na mtoto mdogo wa Igor (mtoto wa kike wa miezi 8) alijisikia kuwa na wazimu. Homa ya mafua ikawa imewapiga watoto wote watatu kwa siku mbili zilizopita na sasa mtoto Katiya alikuwa na homa kali na amekuwa akitapika. Luba alikuwa amechoshwa. Kuendelea kwa hitaji la watoto wake na kusafisha kusikoisha kwa uchafu unaotokana na homa ya mafua kulikuwa kumemfikisha mwisho wa nguvu zake kimwili.

Lakini homa ilikuwa ya mwisho katika matatizo kadhaa tangu Igor alipoondoka. Tofauti na kazi za ziada ambazo zililetwa na kuondoka kwake, Friji yao ilikuwa imeharibika na kuvuja kwa dari kulikuwa kumeharibu baadhi ya ukuta wa sebureni wakati wa mvua kubwa ya mwisho.

Wakiwa wameishi katika mji huu mgeni kwa miezi michache, hakuwa na wa kukimbilia au hata kuongea naye. Alikuwa akikutarajia kurudi kwa Igor. Msaada wake ungekubaliwa, lakini hata zaidi ya hilo alitaka kuzungumza na mtu kuhusu mizigo ya moyo wake na nafsi inayohusiana na kuishi eneo la porini mbali na familia yake na marafiki na mtindo rahisi wa maisha.

Igor na Luba waliposalimiana katika mlango wa mbele walikuwa wamefurahi sana kuonana. Hakuweza kusubiri kuzungumzia kuhusu matukio ya wiki iyopita lakini kulikuwa na matatizo ya ghafla ambayo yalihitaji usikivu wa Igor..

MASWALI YA KUFIKIRIA

1. Ni vitu gani vya mara moja ambavyo Igor angefanya kufanya hali kuwa bora?
2. Jinsi gani Igor ataitikia kwenye hali anayokuta nyumbani?
3. Tafadhali eleza unachofikiri Igor atataka kuzungumzia wakati yeye na Luba watakapokaa chini kwa ajili ya mazungumzo.
4. Ni aina ani ya mzigo Luba anaweza akawa anabeba ambayo alitaka kushirikisha mtu mwingine?
5. Huduma ya Igor inamtaka kuwa mbali na nyumbani mara kwa mara- wakati mwingine kwa mda wa wiki nzima. Jinsi gani anaweza kuzuia kutokea kwingine kwa kuchosha kama huko?
6. Jinsi gani anaweza kumtia moyo kujiona mwenyewe kama mshiriki wake katika huduma?
7. Jinsi gani mpanda kanisa mwenye familia anavyoonyesha mda kiasi gani anahitaji kutunza/kuweka pembeni kwa ajili ya kuangalia mahitaji ya familia yake?

## II. MUONEKANO NAMBA MBILI —ANDREA NA TIBOR

Anjurea alikuwa akifurahia kuhusu baba mchanga ambaye mme wake, Tibor, alikuwa ndiyo amemuongoza kwa Bwana. Alikuwa na furaha sana kwa ajili ya Tibor kwa sababu alikuwa akitumiwa sana na Bwana. Katika miezi sita iliyopita kanisa mpya lilikuwa limekua kutoka familia ya wenzi mpaka familia 15. walikuwa wametiwa moyo katika huduma hii lakini Anjurea alikuwa bado na usumbufu unaojirudia na fikira. Alikuwa amemwambia Tibor juu ya hitaji lake la kuzungumza lakini ilionekana kana kwamba alikuwa na kazi nyingi sana mara zote na huduma yake kiasi kwamba hawakupata mda wa kuzungumza. Alirudi nyumbani kila jioni akiwa amechelewa sana na kuchoka sana. Alisema kuwa wangeongea wakati ambao atakuwa na usikivu, lakini tena alikuwa akiamka na kutoka nje ya nyumba asubuhi sana kwenda kwenye mikutano fulani au kuzungumza na mkata shauri mpya au kufundisha darasa katika moja ya mkutano wa vikundi kiini kwenye ujirani wao. Tofauti ya usumbufu wa awali, alikuwa anaanza kujisikia wivu. Huduma hii ya upandaji kanisa ilikuwa inageuka kumeza upendo wote wa Tobor ambao ulikuwa ukichukua nafasi yake katika maisha yake. Alikuwa akijisikia vitu ambavyo hakutaka kujisikia. Alitaka kuwa msaada kwa Tibor na huduma yake. Huko kulikuwa kujitoa kwake kwa Bwana na kwa mme wake. Lakini alijisikia kuachwa sana. Huu ulikuwa mji ambao haukuwa na kanisa kabla yao kuja na mpaka hivi karibuni kulikuwa hakuna waumini. Sasa kulikuwa na badhi ya wanawake waliokata shauri waliokuwa wakifuashwa lakini kamwe wasingeweza kuelewa maisha yake kama mke wa mchungaji. Alitaka kujisikia kana kwamba ni sehemu ya mchango kwa huduma ya Tibor, lakini mpaka kufikia hatua hii hakuwa amehusishwa na hakuwa ameombwa kuhusika. Atafanya nini kumfanya Tibor kupunguza vya kutosha kuzungumzia mizigo hii moyoni mwake?

MASWALI YA KUFIKIRIA

1. Kutoka katika ukweli wa hadithi inaonekana kwamba Tibor alikuwa akiwasiliana na Anjurea juu ya mahitaji yake kama mke na mama?
2. Unafikiri Tibor alikuwa akimuhusisha Anjurea katika huduma yake ya upandaji kanisa? Kulikuwa na ushirikiano na umoja katika maisha yao?
3. Katika njia zipi Tibor anashindwa kama mme?
4. Ni ushauri gani wa vitendo unaoweza kushauri ambao unaweza kumsaidia Tibor kuwa mzuri katika kuwasiliana na mke wake?
5. Nini unachoweza kusema kuhusiana na “uiwiano” katika ndoa hii?
6. Jinsi gani Tibor anaacha nje Waefeso 5:25-26?
7. Jinsi gani Tibor anaweza kumhusisha Anjurea kiufanisi katika huduma yake?

## III. MUONEKANO NAMBA TATU—NICU NA FAMILIA YAKE

Nicu alikuwa amekuwa na wiki ndefu. Alikuwa amefanya baadhi ya makosa makubwa kama mme na baba. Alikuwa amenyenyekezwa kwa njia zake mwenyewe za dhambi na sasa, baada ya kukiri na kutubu, maisha yalikuwa yakianza kuchukua mtazamo bayana kwa mara nyingine tena. Lakini kama mtu angemuuliza jinsi gani alikuwa akiendelea siku hizo, angekubali kuwa bado alikuwa na hasira. Hadithi yake hii hapa:

Siku moja kijana wake wa kwanza Razvan, mwenye umri wa miaka 18 alikuwa akiangalia mkanda kwenye deki yao nyumbani. Alikuwa ameuazima kutoka kwa mmoja wa marafiki zake. Nicu aliingia chumbani na kukaa na kuungana na Razvan. Mara baada ya Lina, mke wa Nicu, alipoingia chumbani na kuungana nao. Baada ya dakika chache tu iligeuka kuwa dhahiri kwa Lina kwamba picha hiyo haikuwa inafaa kwa wakristo kuangalia. Alifanya mtazamo wake kujulikana kwa Nicu na kisha kuondoka chumbani. Nicu alimfata na kuelezea kwamba Razvani alikuwa mkubwa vya kutosha sasa kufanya uamzi wake mwenyewe kuhusu anachoweza kuangalia na ambachao hangeweza kuangalia. Lina alibisha kwamba lilikuwa jukumu lao kama wazazi wakati mtoto yeyote alipokuwa bado anaishi katika nyumba yao kuonyesha nini kinatakiwa kiangaliwe, kusoma, au kuzungumzwa nyumbani kwao. Nicu alikuwa amemchukia Lina kwa kumkabiri kwa hili, hasa mbele za Razvan. Ilikuwa inatia haya kama kichwa cha nyumba kukabiliwa na mke wake. Kwa hiyo kwa namna fulani ya kikulipiza kisasi hakukubaliana na wazo lake na mtazamo na kumruhusu Razvan kumalizia mkanda wake.

Usiku huo walipokuwa tayari kwenda kulala, Lina alianzisha swala hilo tena lakini Nicu alikataa kung’atuka kutoka aliposimamia. Hata akawa na hasira na Lina na kukataa kuomba naye kabla ya kwenda kulala. Asubuhi iliyofata baada ya kulala vibaya, Nicu aliamka kufanya sala yake. Hakuweza kukazia mawazo kwenye usomaji wake wa Biblia, hakuweza kuomba kwa sababu alikuwa na hasira sana. Wakiwa kwenye meza ya kifungua kinywa, alitangaza kwa familia yote kwamba hakuna mikanda itakayoruhusiwa kuangaliwa katika nyumba yake tena na hapakutakiwa kuwa na ya kipekee. Mtoto mwingine hakujua nini kilikuwa kinaendelea lakini waliweza kujua kufuatana na sauti ya baba yao na machozi katika macho ya mama yao kwamba kulikuwa na kitu ambacho hakikuwa sawa kati yao. Nicu alikuwa amejisikia vibaya sana kuhusu hali nzima. Alikuwa mchungaji. Alikuwa amehusika katika kuanzisha kanisa mpya na kuwaambia watu kuhusu upendo wa Kristo na furaha ya maisha ya kikristo. Hakuwa na upendo na furaha katika maisha yake kutokana na tatizo hilo. Lakini kulikuwa na zaidi kuliko hilo. Alijua kuwa mke wake alikuwa sawa kuhusu wajibu wake wa kutenga mvuto wa kiroho nyumbani. Alikuwa na kiburi zaidi kukubali kushindwa kwake. Alijua pia kwamba alikuwa akiacha kuyatii maandiko kwa sababu alikuwa hampendi mke wake kama Kristo alivyolipenda kanisa. Hasira hizi alizokuwa nazo akijiasikia zilikuwa hasa hasira katika mwili wake kwa sababu walikuwa mwili mmoja. Alitakiwa kusahihisha hali. Wakati wa mlo uliofata, wakati familia yote ilipokuwa pamoja tena, aliomba msamaha kwa ajili ya vitu kadhaa alivyokuwa amefanya ambavyo vilikuwa makosa. Alifanya hivyo kwa kuvunjika na kwa machozi na kuomba msamaha kutoka kwa familia yake. Waliomba pamoja na majadiliano yenye uhai yalifata kuhusu sehemu ya mikanda katika nyumba yao.

MASWALI YA KUFIKIRIA

1. Razvan ana umri wa miaka 18, kijana! Kwa nini anajisikia huru kuonyesha mikanda isiyo sawa kwenye televisheni ya wazazi wake?
2. Kama ilivyodhihirishwa katika kuitikia kwa Nicu kwa Lina, ni sifa zipi za kikristo zinakosekana katika maisha yake?
3. Mda wa chakula wa familia ulikuwa mda wa “mkutano” unaofaa kujadili hili, au matatizo yoyote magumu ya familia?
4. Kwa nini kulikuwa na tofauti ya mapendekezo katika kufikiri kwa wenzi wakristo kwenye jambo wazi linalohusiana na sura ya maisha ya kiroho au maadili?
5. Nini unachoweza kusema kuhusu mawasiliano na kuelewa kati ya Nicu na Lina mpaka kufikia hatua hiyo?
6. Nicu anaweza akawa aliaibishwa na kukabiliwa kwake na Lina?
7. Jinsi gani kutokea kwa namna hiyo kunaweza kuzuiliwa wakati mwingine?

## IV. MUONEKAN0 NAMBA NNE—ANICKA AND MIREK

"Tutaonana hivi karibuni!" Anicka alisema huku akifunga mlango nyuma ya mgeni wa mwisho. Ilikuwa usiku wa manane uliopita, na alikuwa amekuwa na nguvu za kutosha kukusanya vikombe vya chai na kuviweka kwenye sinki kabla ya kuangukia kitandani mwake. Mme wake Mirek alikuwa tayari anajiandaa kwenda kitandani.

Simu ililia asubuhi sana iliyofata. Anicka aliikimbilia ili kwamba isikatize mda wa Mirek wa kujifunza. Alikuwa rafiki kutoka mji wanaopakana nao aliyekuwa akipita mjini. “Ninaweza kuwa nyumbani kwenu jioni ya leo?” aliuliza. Ingemaanisha kazi ya ziada kwake, lakini angewezaje kusema hapana?

Maisha yao yalikuwa yamebadilika hasa kati kati ya miezi sita tangu walipoanza upandaji kanisa. Anika hakuweza kukumbuka mda mwingine ambao umekuwa na kazi kiasi hicho. Walipokwenda nje kwenye ujirani, ilionekana kana kwamba ujirani ulikuwa ndani ya kota zao. Watu walikuwa wakifika kwa ajili ya kujifunza Biblia, ushauri, au mikutano karibu kila saa ya siku. Anicka hakuchukia hilo: Watu wengine walikuwa wakitambua kuwa alikuwa tayari ameshalijua—kwamba Mirek alikuwa na moyo wa kiuchungaji. Alijaribu kujiambia mwenyewe kwamba alitakiwa kuwa mke wa msaada . lakini kwa kuwa tu Mirek alitaka kuwa huru kuzungumza na watu na kuwasaida katika mahitaji yao, hilo lilimaanisha kuwa Anicka atachukua kazi zingine zote zilizobaki?

Anicka alifikiria nyuma mwezi wa sita, walipotumwa nje kama wapanda kanisa. Mchungaji wao alikuwa amewatia moyo kufanya kazi pamoja na kukalishana mmoja kwa mwingine. Mchungaji alijua kwamba kipawa cha Anika cha uinjilisti kingeweza kuwa muhimu katika upandaji wa kanisa. Ilidhihirisha kuwa kweli—waumini wa kwanza katika kanisa lao walikwa watu aliokutana nao Anika na kuwashuhudia. Lakini sasa, alikubali yeye mwenyewe, kuwa ana mda mdogo wa kwenda nje na kufanya alichopenda zaidi: Kuzungumzia wengine kuhusu Kristo. Kitu fulani kilitakiwa kubadilika, na kwa haraka.

MASWALI YA KUFIKIRIA:

1. Mtindo wa maisha wa Mirek na Anicka unashauri kuwa wana uwiano katika maisha yao? Elezea jibu lako.
2. Ni matarajio yapi ya Anika ambayo hayakuonyeshwa? Vipi kuhusu ya Mirek?
3. Jinsi gani Mirek angemsaidia mke wake kutumia vipawa vyake?
4. Inawezekana kwa wenzi kuwa sawa “washiriki katika huduma?" (Tazama Mdo 18:24-26).

## V. MUONEKANO NAMBA TANO—RENATA NA FAMILIA YAKE

Renata angeweza kuona kutokana na uso wa baba yake kwamba amefanya kosa. Je alikuwa amesahau kufanya kazi za kawaida, au hili lilikuwa kutokubali uamzi wake wa kumfata Kristo? Alijitahidi wakati wote kuwa mwangalifu kusaidia nyumbani kabla hajatoka kwenda kufanya kazi na timu ya upandaji kanisa. Baada ya yote, baba yake aliweka wazi kwamba alijisikia kana kwamba mtu wa miaka 26 ingekuwa vizuri kutumia mda wake kumwangalia mme wake kuliko kuongoza kundi la wanawake la ufuasishaji.

Jioni hiyo tu, kundi la kufuasa lilikuwa limekwenda vizuri. Mfanya kazi mwenzake Mathiasi alikuwa amemtia moyo kuendelea kufundisha wanawake jinsi ya kujenga kanisa na kumjua Kristo vizuri. “Sijui tutafanya nini bila msaada wako,” alisema. Hakuna namna mke wangu angeweza kuongoza kundi akiwa na watoto wawili nyumbani. Tunashukuru kwamba upo.”

Mama yake na Renata aliingia chumbani na kumwambia hali halisi. "Renata," alianza, “tunakuhitaji nyumbani kesho jioni.”

"Mama," Renata alijibu, "unajua jioni hiyo ndiyo ninayokutana na timu yangu."

"Ndiyo, “ mama yake alirudisha, kiuchungu, “watu muhimu katika maisha yako. Jinsi gani naweza kusahau?”

Renata alijaribu kutawala hasira yake na kwa haraka akatoka nje ya chumba. Alijua alitakiwa kuheshimu wazazi wake, lakini maneno aliyokuwa amejaribiwa kusema yalikuwa mbali kiheshima. Hisia zake zilikuwa mchanganyiko wa hasira na hatia. Kwa nini wakati wote aliitikia vibaya kwenye mchango wa wazazi wake? Kwa nini walipanga shughuli kikusudi kumfanya kutofanya kile Mungu alichomwitia?

Zaidi ya kitu chochote, alitamani angeweza kumdu kuishi yeye mwenyewe, lakini kazi yake kama mpanda kanisa ilimanisha kuwa angeweza kufanya kazi ya masaa machache tu kama mtunza Stoo. Kinyume chake, bado ilionekana kama kitu cha kigeni kwa kijana, mwanamke bachela kuishi nje ya nyumba ya familia ya wazazi wake.

Wakati mwingine Renata alijisikia kana kwamba aliishi katika ulimwengu wa aina mbili; kwenye timu ya kupanda kanisa alikuwa akisifiwa na kuthaminiwa kama mshiriki mzuri, nyumbani, alikuwa akipingwa na kufanywa kama mtumwa. Alijua ni ulimwengu gani alipendelea, lakini alijua hilo, angalau kwa sasa, ilibidi aishi hivyo.

MASWALI YA KUFIKIRIA:

1. Mzizi wa tatizo ulitoka kwa wazazi wa Renata, au anafanya kitu fulani kuchangia kwenye tatizo? Kama ni hivyo, Ni nini?
2. Jinsi gani anaweza kuwaheshimu wazazi wake wanapokuwa wanapinga jinsi anavyotumia mda wake?
3. Nini utakachomshauri Renata kama akija kwako kutafuta ushauri katika hali yake ya kuishi?
4. Ni vitu gani vya kipee lazima vifikiriwe wakati mwanamke bachela anapokuwa anasaidia kupanda kanisa? Jinsi gani wapanda kanisa wengine wanaweza kuwa waangalifu kwa vitu hivyo?